Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

## Kikao cha Thelathini na Nne - Tarehe 27 Julai, 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWAKILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE):**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamaati ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2011/2012 pamoja na

Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Nishati na Madini Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 270

### Fedha za Chenji ya Rada Katika Kuboresha Elimu

**MHE. ESTHER N. MATIKO (K.n.y. MHE. VINCENT J. NYERERE)** aliuliza:-

Serikali iliamua kutumia fedha za cheji ya rada katika kuboresha elimu ya msingi nchini:-

Je, ni kiasi gani ambacho kimeshatumika na kimetumika kwenye mambo gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU**) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Vincent Josephat Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utoaji wa elimu nchini unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ya upungufu wa miundombinu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Kwa kuzingatia hali halisi ya upungufu wa vitabu na madawati na umuhimu wake katika tendo la kujifunza, Serikali imefanya maamuzi ya kutumia fedha za fidia ya ununuzi wa rada shilingi bilioni 72.3 kuimarisha elimu ya msingi. Asilimia 75 ya fedha hizi sawa na shilingi bilioni 54.2 zitatumika kununua vitabu vya Kiada, Viongozi vya walimu, mihtasari na miongozo ya mihtasari na asilimia 25 sawa na shilingi bilioni 18.1 zitatumika kununulia madawati.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Serikali ipo katika hatua ya kukamilisha mchakato wa manunuzi hayo, hivyo hakuna kiasi chochote cha fedha kilichotumika. Aidha, utaratibu wa malipo utakaotumika ni kuwa malipo yatafanyika baada ya vitabu kuwasilishwa shuleni na shule husika kutoa taarifa kwa kutoa hati ya kukiri mapokezi ya vitabu hivyo.

**MHE. ESTER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza , kufuatia majibu ya Naibu Waziri.

(a) Kwa kuwa shule nyingi za Tanzania zina changamoto ya vitabu ni kweli, ningependa kujua ni vigezo vipi vimetumika kuweza kugawa hivi vitabu kwa shule au ni shule zote za Tanzania zinapatiwa hivi vitabu

na kama siyo zote ni vigezo vipi vimetumika maana yake kuna shule zingine zina hali mbaya?

(b) Nakumbuka wakati wa Bajeti ya Wizara hii, walisema kwamba mhusika ambaye atakuwa anachapisha hivi vitabu ndiyo atakuwa anawajibika kupeleka vitabu hivi mpaka katika shule zote kuhakikisha kwamba amevifikisha kwenye mashule. Nataka kuuliza hawaoni kwamba kwa kumwachia huyo muhusika kupeleka vitabu mpaka kwenye kila shule ni gharama zaidi kwa maana ya *distribution cost.* Kwa nini baada ya kuvichapisha wasingeweza kuweka *either* Mikoani au katika Wilaya halafu ndiyo vikawa *distributed* na Maafisa wa Elimu husika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa tunatambua kwamba shule zetu nchini zina matatizo makubwa ya vitabu na hasa kwa Shule za Msingi, vitabu hivi vitasambazwa kwa shule zote za msingi nchini Tanzania na kwa hiyo, hatukuwa na kigezo cha kutenganisha shule na kwa kuwa tunagawa shule zote sana sana itakuwa tu mahitaji ya shule na shule ndiyo ambayo yanaweza kutofautisha kwa maana ya mahitaji yale yatakuwa yamechanganuliwa kwa Halmashauri na Mkoa, halafu ni shule zote nchini.

(b) Mchakato huu ulivyoendeshwa wa kufuata shule wa hawa wachapishaji na wasambazaji kwa kuwapa majukumu yote mawili ni rahisi zaidi kuliko kugawa majukumu ya mchapishaji pekee yake na msambazaji pekee yake kwani hii gharama inamfanya huyu kupeleka moja kwa moja kwenye Halmashauri husika, gharama hiyo tumeiangalia pia hata tulipokuwa tunafanya mazoezi wenyewe ya kupeleka vitabu.

Zamani tulikuwa tunapeleka fedha, halafu Halmashauri zinanunua, tumegundua kwamba tunapoteza fedha nyingi. Badala yake sasa bora kufunga mkataba wa pamoja wa kufikisha kitabu eneo husika na kwa makubaliano yale na gharama yake ni nafuu zaidi kuliko yale ya msambazo kama ambavyo ilivyokuwa. Kwa hiyo, tuna imani gharama haitokuwa kubwa kwa kum-*assign* yeye kupeleka vitabu mpaka mahali husika.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kuniona. Kwa kuwa Serikali huwa inapeleka *Caption Grants* kwenye shule mbalimbali kwa ajili ya ununuzi wa vitabu na kwa kuwa hakuna fedha zozote ambazo zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa madawati, ni kwa nini Serikali sasa haikufikiria kupeleka pesa zote hizo katika ununuzi wa madawiti na kumaliza tatizo ambalo linakabili shule nyingi sana Tanzania?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba

kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunapeleka fedha za *Capitation* kwenye shule husika. Fedha hii ya *Capitation*, kazi yake ni yale matumizi ya kawaida pale shuleni, yanamsaidia Mkuu wa Shule kununua vitabu pale anapoona vina pungufu, kufanya matumizi mengine ya Utawala na yale yote ambayo shule kupitia Kamati zake kwa shule za msingi lakini kupitia Bodi zake kwa shule za Sekondari wanafanya matumizi wao wenyewe.

Mchakato wa madawati kupitia utaratibu huu, kwa kuwa tunagawa katika shule zote nchini, utaratibu wa namna ambavyo tutapeleka fedha hii kwenye Halmashauri ili wapate ya kununua madawati badala yak u-*centralise,* huo tutaupitia na tutaweza kufanya maamuzi ambayo yatawezesha pia kudhibiti hii isitoweke bila kufuata utaratibu wake.

Kwa hiyo, tofauti na *Capitation* kama ambavyo nimeeleza na namna ambavyo tumeratibu kupeleka madawati ili yaweze kununua kulingana na upungufu wa maeneo hayo ni kama ambavyo nimeweza kueleza.

Na. 271

**Nafasi ya Wazanzibari Kwenye Masuala ya Muungano**

**MHE. MARIAM SALUM MSABAHA** aliuliza:-

Wazanzibari wengi wanakerwa na matatizo ya Muungano kama vile mgao wa fedha za Miradi ya Maendeleo zinatolewa na wafadhili:-

(a) Je kwa nini misaada haitolewi kwa uwiano na wakati mwingine kutoka Zanzibar?

(b) Je ni Wazanzibari wanagapi wameajiriwa katika sekta za Muungano?

(c) Je ni Wazanzibari wangapi wamepatiwa ufadhili wa masomo ya juu ndani na nje ya nchi kwa mwaka 2010/2011?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Salum Msabaha Mbunge wa Viti Maalum lenye vipengele a, b na c kwa pamoja kama ifauatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa Zanzibar kwa kutumia *formula* ya gawio ya asilimia 4.5 wanapata mgao wake wa fedha na misaada ya kibajeti na zimekuwa zikipitia katika Fungu 31 Ofisi ya Makamu wa Rais na kuwasilishwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, takwimu za mgao huo kwa miaka mitano iliyopita ni kama ifuatavyo:-

Mwaka 2007/2008 ni bilioni 27.3, 2008/2009 ni bilioni 23 2009/2010 ni bilioni 50.2, 2010/2011 ni bilioni 38.8 na 2011/2012 ni bilioni 32.4.

Mheshimiwa Spika, nataka nikiri kwamba jibu (b) na (c) hakuna takwimu halisi au za pekee zinazoonesha idadi ya Wazanzibari walioajiriwa katika sekta za Muungano na idadi ya Wanzazibari walioko nchi za nje kwa masomo.

Takwimu zinazoweza kupatikana ni zile zinazoonesha idadi ya wafanyakazi wote katika taasisi za Muungano na idadi ya wanafunzi wote wa Tanzania walioko nchi za nje kwa masomo. Masuala haya yanashughulikiwa na sekta ya Utumishi wa Umma na Sekta ya Elimu ya Juu ndani ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na takwimu halisi kama zinavyoombwa na Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri wa Sekta za Utumishi wa Umma wa SMT na SMZ walishakubaliana kuwa Sekretarieti ya Ajira ifanye uchambuzi wa suala hili,na kazi hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa takwimu za elimu, Kamati ndogo ya ushauri kuhusu masuala ya Elimu ya Juu na Mafunzo (*Sub- Advisory Committee on High Education and Training SACHET)* yenye wajumbe kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar pamoja na

Idara ya Elimu ya Juu ya SMZ wataombwa kufanya uchambuzi wa takwimu za Elimu ya Juu nchi za nje ili takwimu zinazoombwa ziweze kupatikana. Ahsante sana.

**MHE. MARIAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri. Nataka nimwulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Zanzibar ni nchi kamili ina Rais, Baraza la Mawaziri na Wawakilishi, haioni sasa Zanzibar ipewe uhuru wa kutosha kutafuta misaada hiyo ya nje bila kungoja gawio kutoka Tanzania Bara?

(b) Kwa kuwa hizi nafasi za Muungano kama sekta ya ajira zimekuwa zikilalamikiwa sana na Wazanzibar wengi, endapo nafasi hizi zitatokea. Mheshimiwa Waziri haoni sasa ni kutangaza katika gazeti la Zanzibar Leo na redio ili Wanzazibari wengi wapate kujua nafasi hizi na kuondosha malalamiko ambayo yapo kwa sasa hivi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwamba Zanzibar kwa sasa hivi, takwimu nilizozitaja hapa ni ile misaada na mikopo ya kibajeti yani *GBS* ambayo inapita kupitia Fungu 31.

Lakini Zanzibar sasa hivi, wanaweza ku-*access* wenyewe misaada kutoka nje na hasa kwenye *Grants*, lakini kwenye mikopo inabidi ipate udhamini ni *signature* tu ya Hazina ya Tanzania. Lakini kwa *Grants* wanaweza waka- *access* wenyewe na wako huru kufanya hivyo na wanafanya na inakubalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa suala la ajira, Mawaziri wa Utumishi katika Sekta ya Umma au Sekta ya Utumishi wa Umma, wamekubaliana kwamba nafasi zinapotokea, zinawekwa magazeti yote, yale ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na vyombo vyote vya habari zinawekwa na wanapofanya *interview,* Sekreterieti za Utumishi wa Umma zinazofanya *interview* zinashirikiana.

Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa Mawaziri wamekubaliana kuondosha utata kama inavyolalamikiwa katika sekta hii.

**MHE. AMINA ABDALAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa hivi sasa nazungumza, tayari kuna magari yametoka Zanzibar kuja Dar es Salaam yanatakiwa yalipiwe ushuru mara mbili kama yanatoka nje na kawaida ilikuwa unalipa tofauti. Je, Serikali inasema nini kuhusu hili?

**SPIKA**: Swali tena hilo jipya sana maana wale walikuwa wanaulizia habari ya namna misaada

inavyogawana ndiyo maana akakupa zile hesabu. Lakini Mheshimiwa Waziri, hebu jibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Amour kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimepata malalamiko hayo yanayozungumzwa kwamba sasa hivi pale Bandarini Dar es Salaam, kuna magari yapatayo 500 ambayo yametoka Zanzibar na yamekwama pale, tatizo ni kwamba magari yale yametakiwa yaanze tena *process* upya ya ku-*evaluate* ushuri wa kulipia wakati Sheria ya ushuru inasema magari yakiingia *point* moja au bidhaa ikiingia *point* moja inachukuliwa kwamba imeshaingia Tanzania ila tu pale ambapo ushuru utakuwa umelipwa kasoro basi italipwa katika *point* ambayo kasoro ile imegunduliwa.

Sasa tatizo hili nimelipokea na nimewataka wafanyabiashara waniandikie ili nami nilifanyie kazi pamoja na Wizara ya Fedha na *TRA.*

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa matatizo haya ya mgao ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar imekuwa kama propaganda na watu wengi wanasema kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitoi chochote Zanzibar, ili kuondoa hayo wakati Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huwa inatoa na takwimu zipo na mgao unakwedna vizuri sana. (*Makofi*)

Je, Wizara sasa itakuwa tayari badala ya kutumia magazeti ambayo wananchi wengine Zanzibar hawashughuliki nayo, itoe takwimu hapa hapa ndani ya Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuondosha utata huu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sereweji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza taarifa hizi zipo na Zanzibar, tunashiriki katika mchakato wa kupatikana huo mgao wa *GBS, k*atika huo mchakato ambao unaitwa *Annual Review.*

Hizi taarifa zipo na zinatolewa, hasa zimo katika *Web Site* ya Wizara ya Fedha, *www.nof.go.tz.* Kwa hiyo, hata ukienda Wizara ya Fedha Zanzibar, naomba kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba, Wazanzibar wengi wamekuwa wakifanya *research* ya *AID* kwa Zanzibar. Na wanakwenda kule, wanapata taarifa zilizo kamili kama ambavyo zimeelezwa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, hizi Taarifa zipo na sio kama zinatolewa kwenye magazeti. Taarifa zipo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuwe tuna *access* hizo Taarifa. Kuna *website* ya Wizara ya Fedha, mbali ya Taarifa hizi basi kuna Taarifa ya migao ambayo inakwenda pia katika Halmashauri, migao ya

*OCs* katika Wizara na Taarifa nyinginezo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 272

**Upimaji wa Ardhi ya Vijiji**

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE** aliuliza:-

Wilaya ya Serengeti, ina migogoro mingi sana ya ardhi na hakuna utaratibu madhubuti wa kupima ardhi kwa wananchi, Vijiji nna Taasisi na kupewa Hati Miliki na Mpango wa *MKURABITA,* ulioanza upimaji wa Vijiji vitano vya mfano mwaka 2009, umesimama:-

(a) Je, Serikali, ina mpango gani wa kusaidia Wilaya kupima maeneo na kutoa Hati Miliki?

(b) Je, wimbi kubwa la uhamiaji haramu lililopo sasa maeneo mbalimbali, litadhibitiwa vipi ikiwa wananchi wanamiliki maeneo sio Kisheria?

(c) Je, Serikali, ina mpango gani wa kuelimisha wananchi, juu ta Sheria Na. 4 na 5 ya Mwaka 1999 juu ya Mipango na Matumizi Bora ya Ardhi?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali, ilikwishaanza utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura 114, ya Mwaka 1999 katika Wilaya na Vijiji mbalimbali nchini, kwa kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kupima mipaka ya Vijiji, ambapo katika Wilaya ya Serengeti, jumla ya Vijiji 61 vilipimwa na kutoa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji 41 *(Certificate of Village Land).*

(ii) Kutayarisha mipango ya matumizi ya ardhi, ambapo katika Wilaya ya Serengeti, jumla ya Vijiji 5 viliandaliwa mipango.

(iii) Kupima vipande vya ardhi na kutoa Hati Miliki za Kimila *(Certificate of Customary Right of Occupancy)*, katika Wilaya ya Serengeti, ambapo jumla ya Hati Miliki za kimila 148 zilitolewa.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya majaribio kwa kushirikiana na Benki ya Dunia na Wadau wengine, ilikamilika Juni 2012. Tayari, Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, imeanza kujengewa uwezo kupitia utekelezaji wa miradi ya majaribio.

Awamu ya pili, inatarajiwa kuanza mwezi huu wa Julai, itakayohusisha kuzijengea Halmashauri za Miji na Wilaya, zitekeleze Programu ya Kupima Mashamba na kutoa Hati Miliki za Kimila katika maeneo yao. Pamoja na kuwepo kwa mpango huo, Halmashauri za Miji na

Wilaya, zinatakiwa kutenga fedha kwa ajili, ya utekelezaji wa kazi hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Sheria za Ardhi, haziruhusu wageni kumiliki ardhi, isipokuwa wanaweza kupewa ardhi kwa madhumuni ya uwekezaji, chini ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya Mwaka 1997, inayosimamiwa na Kituo cha Uwekezaji. Hivyo, wimbi la Wahamiaji litadhibitiwa kwa Mamlaka zinazohusika kusimamia Sheria kikamilifu, kama Sheria ya Uhamiaji na Sheria za Ardhi. Kwa upande wa Sekta ya Ardhi, hatua zilizoanza kuchukuliwa ni pamoja na kutekeleza Mpango wa Taifa wa matumizi ya Ardhi, unaonza 2011 hadi 2031, ndipo hatua nyingine za upimaji wa kila kipande cha ardhi na kumilikisha mwenye haki juu yake, kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Serikali, imeanisha Sekta ya Ardhi, kuwa ni moja ya Vipaumbele katika Mipango yake ya Maendeleo. Inatarajiwa kuwa, ifikapo mwaka 2016, zaidi ya 42% ya ardhi ya Vijiji, itakuwa imeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi, kupimwa na kumilikishwa kwa mtu mmoja mmoja, taasisi au vikundi vya watu.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara, ilitayarisha Mpango Mkakati wa Elimu kwa Umma, kuhusu Sera na Sheria za Ardhi wa Mwaka 2005. Elimu ilianza kutolewa kwa kushirikiana na wadau wengine, zikiwemo asasi za kiraia. Kwa mwaka 2012/2013, kasi ya utoaji wa elimu kwa Umma itaongezeka kutokana na kuanzishwa kwa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kuharakisha utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi wa Mwaka 2011 hadi 2031, pamoja na kupima na kumilikisha wananchi ardhi waliyonayo, Halmashauri za Miji na Wilaya, zinashauriwa kujumuisha kwenye Mipango yao ya Maendeleo na kutenga fedha kwenye Bajeti, ili wachangie nguvu za Serikali Kuu, katika utekelezaji wa Mpango huo.

Aidha, natoa wito kwa Taasisi za Kidini na Asasi za Kiraia, kushiriki katika kutoa elimu kwa Umma, juu ya Sera na Sheria za Ardhi, kwa kuwa, Serikali peke yake, haiwezi kuwafikia wadau wote kutokana na ufinyu wa bajeti.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Mheshimiwa Spika, kwa sababu, katika swali la nyongeza, ukijaribu kuangalia *pace* ya upimaji katika Vijiji vya mfano hivyo 5, vikiwemo Rimng'olori, Pakinyigoti, Komwarobanda, nimepiga hesabu nimeona kama itachukua miaka 64 kukamilisha zoezi hilo la upimaji.

Sasa je, Serikali, ina mpango gani kuharakisha zoezi hili?

(b) Mheshimiwa Spika, pia katika mgogoro ambao upo wa ardhi kati ya Wilaya ya Serengeti na Bunda, hususan Kijiji cha Mikomariro Wilaya ya Bunda

na Kijiji cha Mngorori Wilaya ya Serengeti, ambako wananchi wanachukua mpaka pinde, kwa ajili ya kupigania mpaka. Taarifa hizi, Wizara ina taarifa na wako Watumishi pale Wizara ya Ardhi, ambao wameondoa Folio ya Ramani hiyo ya Mwaka 1979.

Je, Wizara, ina mpango gani wa kuingilia kati suala hili la mgogoro kati ya wilaya ya Bunda na Wilaya ya Serengati?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu Maswali Mawili ya Nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa swali la kwanza kwamba, Wizara yangu ina mpango gani wa kuharakisha upimaji; suala la msingi la kupima ardhi, kwanza ni la mmiliki wa ardhi, ndio jukumu lake hilo. Pili, jukumu la kupima Vijiji ni Halmashauri inayohusika. Wizara yangu, ni mwezeshaji tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge, ahimize Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, ihakikishe kwamba, upimaji wa ardhi, kwanza upangaji wa matumizi ya ardhi pamoja na kupima Vijiji na hatimaye kumilikisha wananchi, waingize katika Mpango wao wa Maendeleo. Katika bajeti zao zijazo, watenge fedha kwa ajili, ya kutekeleza kazi hiyo. Jukumu la Serikali Kuu ni kuwezesha. Nilishatamka hapa Bungeni, kwamba,

Wizara yangu iko tayari wakati wowote kusaidia kwa Wataalamu na vifaa pale ambapo Halmashauri, imepungukiwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Usuluhishi wa migogoro ya Vijiji; tumepokea ombi hilo. Tutashauriana na wenzetu wa *TAMISEMI,* ili tufanye taratibu za kuweza kupata taarifa za kutosheleza na hatima yake, tupate suluhisho la mgogoro huo.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, kazi ya upimaji ramani ni kazi ya Serikali Kuu. Je, Serikali, haioni kuachia Serikali za Mitaa, kazi ya kupima ramani na kutoa Vipimo vya vijiji na kuachia kwamba, itafute pesa, imeionea Halmashauri, ambayo sasa hivi hata kazi ya kuiendesha Ramani zenyewe ni kazi ngumu?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jukumu la Wizara yangu ni kusimamia Sera; hiyo ndio kazi ya kwanza, kutoa Sera na kusimamia utekelezaji wa Sera hiyo.

Jukumu letu vile vile ni kusimamia Sheria zilizopo, utekelezaji wake. Jukumu la kutekeleza ndio kazi ya Halmashauri, kutekeleza Sera hizo, ni moja ya wadau ambao wanapaswa kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, sasa, wao hawana fedha, ni jambo lingine ambalo wanaweza wakaomba, wakaingiza katika mpango wao na kuomba fedha kutoka Serikali Kuu, ili ikiwa Bajeti itaruhusu, waweze kutengewa fedha.

Lakini, si jukumu la Wizara yangu, kwenda kupima, kwa maana Bajeti hiyo hatuna. Isipokuwa, jukumu la Wizara yangu, kupitia kwa Idara ya Upimaji na Ramani, ni kuidhinisha hiyo michoro, kuhakiki na kuidhinisha ramani hizo ambazo zitakuwa zimeandaliwa na Wataalamu, walioko katika ngazi ya Halmashauri.

Na. 273

**Mikopo ya Ujenzi na Ununuzi wa Nyumba**

**MHE. KIDAWA H. SALEH** aliuliza:-

Watanzania wengi wanahitaji kuishi kwenye nyumba nzuri, lakini za bei nafuu; na mwaka 2010, ilianzishwa Kampuni ya Mikopo ya Nyumba *(Tanzania Mortgage Refinance Company (TMRC)* kwa madhumuni ya kutoa mikopo ya ujenzi na ununuzi wa nyumba:-

(a) Je, mikopo hiyo inatolewa kwa utaratibu gani?

(b) Je, hadi sasa ni watu wangapi wameshafaidika na mikopo hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, *Tanzania Mortgage Refinancing Company,* ni Kampuni binafsi iliyoanzishwa na Muungano wa Mabenki chini ya usimamizi wa Benki Kuu, ambayo kupitia Benki Kuu, ilipata mkopo wa dola milioni 30 kutoka Benki ya Dunia, ili kufanikisha upatikanaji wa mitaji ya mikopo ya nyumba nchini.

Mtaji huu, unatarajiwa kuongezesaka kutokana na mauzo ya hisa za kampuni hiyo, kwa benki za biashara. Hadi Mei 2012, Kampuni hiyo, ilikuwa imeongeza mtaji wake kwa kiasi cha shilingi bilioni 10 na milioni 45, kutokana na mauzo ya hisa zake katika benki 11 ambazo ni *CRDB* ambayo ilinunua hisa 11.48%, *AZANIA Bank* ina hisa 9.57%, Benki ya Uwekezaji kwa maana ya *Investiment Bank* hisa 9.57%, Benki ya *Exim* hisa 11.48%, Benki ya Watu wa Dar-es-Salaam hisa 10.53%, Benki ya *NIC* hisa 4.78%, Benki ya *ABC* hisa 9.57%, Benki ya Biashara kwa maana ya *NBC* hisa 9.57%, Benki ya Watu wa Zanzibar hisa 2.39% na *Bank of Africa* hisa 9.57%

Mheshimiwa Spika, Kampuni hiyo ya *TMRC,* haitoi mikopo ya nyumba kwa mtu mmoja mmoja, bali hutoa mikopo kwa mabenki yenye hisa katika Kampuni hiyo.

Benki zilizonunua hisa kutoka *TMRC,* ndizo zinazoweza kukopa katika kampuni hiyo na kukopesha wananchi wanaohitaji mikopo kwa ajili, ya kujenga, kununua ama kukarabati nyumba. Hivyo, wananchi wenye kuhitaji mikopo ya nyumba, hutakiwa kuwasilisha maombi yao kwenye mojawapo au baadhi ya Benki zenye hisa.

Mojawapo ya masharti ya kupata mkopo huo ni kuwa na dhamana ya mkopo ambayo ni nyumba itakayojengwa au kununuliwa au kukarabatiwa. Muda wa kurejesha mkopo pamoja na kiwango cha riba, ni makubaliano kati ya Benki husika na mkopaji, kutokana na uwezo wake wa kurejesha mkopo huo.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi 2012 ni Benki moja tu ya *AZANIA Bank* ndiyo iliyojitokeza kupewa mkopo na *TMRC,* wenye jumla ya shilingi bilioni 4.2. Benki hiyo, imetumia mtaji huo kutoa mikopo ya nyumba kwa wakopaji 95.

Aidha, pamoja na kuwa ni Benki moja tu imetumia fursa ya kupata mtaji kupitia *TMRC,* zipo pia benki nyingine za biashara zinazotoa mikopo ya nyumba kwa kutumia mitaji yao. Benki hizo ni *Commercial Bank of Africa, Stanbic Bank, Kenya Commercial Bank* pamoja na *Akiba Commercial Bank.*

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa Benki zilizokwisha nunua hisa kutoka *TMRC,* zianze kukopesha wananchi kwa kutumia mtaji huo kutoka *TMRC.* Aidha Benki ambazo hazijanunua hisa za *TMRC,* zinashauriwa

kufanya hivyo, ili kuweza kupata mtaji wa kutosha, kukopesha kwa ajili ya ujenzi, ununuzi au ukarabati wa nyumba.

**MHE. KIDAWA H. SALEH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili tu ya nyongeza. Moja, ni kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri, ametueleza Benki karibu 11 zimeshapata hisa kutoka Kampuni hii, lakini ni Benki moja tu ambayo ndio imeenda kuchukua mkopo.

Labda Mheshimiwa atueleze ni sababu zipi ambazo zimekuwa kikwazo kwa mabenki mengine kwenda kuchukua mikopo, ili kuweza kuwakopesha wananchi?

Mheshimiwa Spika, lakini mbili. Sharti moja la kupata mikopo ni kuwa na hisa kwenye hii Kampuni. Je, masharti mengine ni yepi, ambayo yanatakiwa, ili mabenki haya yaweze kupata mkopo? Pengine ni vikwazo vya masharti, ndio vimezuia kwenda kupata mkopo kule? Naomba tusaidiwe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu hilo swali kwa kifupi kwa sababu, jibu lako peke yake, limechukua dakika 5.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kidawa Hamad salehe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba, hatuna taarifa kama Serikali, juu ya kikwazo kipi kilichofanya Benki ambazo ni Wanahisa wa *TMRC* zisichukue mikopo hiyo. Pengine ni mipango ya ndani ya Taasisi hizo, ndizo ambazo kwamba, zimewachelewesha wao kufanya hivyo.

Lakini, tunayo matumaini kwamba, muda si mrefu na wao watachukua mikopo hiyo, ili kuwawezesha wananchi wetu wapate mikopo yenye masharti nafuu na waweze kukopa na kumiliki nyumba.

Mheshimiwa Spika, la pili. Masharti mengine ambayo yanatakiwa kwa mabenki haya; natumaini kwamba, kadiri tujuavyo sisi, hakuna masharti ambayo ni magumu yanayoshindikana kutimizwa na mabenki. Kama nilivyosema kwa swali la kwanza, ni kwamba, ni mipango yao ya ndani ya kwamba, kwa sasa hivi wanataka kufanya nini.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa, ni azma ya Serikali, kuhakikisha kwamba, wananchi wanaishi katika nyumba bora, lakini tatizo kubwa pamoja na kwamba, wanatoa mikopo, hizo benki, bado tatizo kubwa ni bei kubwa sana ya vifaa vya ujenzi. Je, Serikali, ina mkakati gani kuhakikisha kwamba, wanapunguza bei za bidhaa hizo za ujenzi, ili wananchi hawa waweze kunufaika na nyumba bora?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, bei ya vifaa vya ujenzi bado iko juu, lakini tukitazama sehemu kubwa ya vifaa hivi vinatoka nje ya nchi, ndio sababu, vinakuwa ghali. Kwa hiyo, mimi wito wangu, ili kuweza kupunguza bei ya vifaa ni tushawishi wawekezaji wajenge viwanda vya kuzalisha vifaa hivi hapa nchini. Waheshimiwa Wabunge, mnazo fursa hizo za kuweza kuwashawishi wawekezaji, mkaingia nao ubia, mkaanzisha viwanda vya kutengeneza vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na malalamiko kuwa kodi ni tatizo. Tunatambua kwamba, hilo ni tatizo, tunawasiliana na Wizara ya Fedha, ili kuona ni namna gani Serikali, inaweza ikapunguza kodi kwenye vifaa vya ujenzi, ili kupunguza bei yake. *(Makofi)*

Na. 274

**Fedha za Miradi ya Umwagiliaji wa Misozwe na Mashewa**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Wakati wa kupitisha Bajeti ya Mwaka 2011/2012, ilielezwa kuwa Halmashauri zilipokea shilingi bilioni 44 mwaka 2010/2011 na kutarajia shilingi bilioni 31 kwa ajili ya Mfuko Maalum wa Umwagiliaji:-

Je, Wilaya ya Muheza, imepelekewa kiasi gani kwa miradi ya Umwagiliaji ya Misozwe na Mashewa 2010/2011 na imepata kiasi gani 2011/2012?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2010/2011, Halmashauri zilipokea jumla ya shilingi billion 31.1 kwa ajili, ya Mfuko Maalum wa Umwagiliaji *(District Irrigation Development Fund (DIDF).* Kwa mwaka 2011/2012, zilitengewa jumla ya shilingi bilioni 32.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha hizi, ni kwa ajili ya kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji katika skimu mbalimbali za wakulima wadogo.

Aidha, kiasi kingine cha shilingi bilioni 10.945 zilizotengwa katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 ambazo zimetolewa na Serikali ya Japan kutoka kwenye mfuko wa *The Japan Policy and Human Resources Development (PHRD)* ni mahususi kwa ajili ya skimu 20 za mfano zilizoainishwa kuongeza tija katika uzalishaji wa kuongeza thamani *value addition* ya zao la mpunga.

Kutokana madhumuni ya matumizi ya fedha hizi kuwa tofauti na za kazi za ujenzi iliamuliwe zisipitie katika mfuko huo wa *DIDF.*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 skimu ya Misozwe haikupata fedha kutoka mfuko wa *DIDF* na mwaka 2011/2012 ilipewa shilingi milioni 450 kutoka *DIDF.* Katika mwaka huu tunaokwenda nao 2012 skimu ya Misozwe imetengewa fedha zaidi ya kiasi cha shilingi milioni 140 kutoka mfuko huo. Hivi sasa ujenzi wa bwawa kwa ajili ya skimu hii umefikia asilimia 98 na kazi za ujenzi katika skimu unatarajiwa kuanza baada ya mkandarasi aliyeteuliwa kusaini mkataba wa ujenzi.

Kwa upande wa skimu ya Mashewa haijafanikiwa kupata fedha kwa hii miaka miwili kutokana na ufinyu wa Bajeti. Hivyo tunaishauri Halmashauri ya wilaya Muheza kuendelea kuiombea fedha skimu hiyo kwa mwaka 2013/2014 kupitia mfuko wa wa umwagiliaji *DIDF* na sisi tunaahidi kuyafanyia kazi maombi hayo kulingana na uwezo wa kibajeti. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze Serikali sasa kwa kuendelea kupeleka fedha kwa wakati katika mradi huu. Lakini niwapongeze pia wasimamizi wa mradi huu na mkandarasi wanafanya kazi nzuri sana na mwenge ulikuwa pale tarehe 5 Julai, 2012.

Mheshimiwa Spika, kwanza nipende kukufahamisha kwamba mkandarasi ametia saini mkataba siku mbili zilizopita hivyo kazi inaweza ikaanza.

Lakini kazi kubwa ya ujenzi wa ile skimu haukuwa unaainisha kazi kubwa ambayo ni pamoja na kupima maeneo na kutifua zile skimu ili kuzigawa kwa wanachama zaidi ya 100 waliojiandikisha katika mradi huo.

Je, mpango huo wa kutifua na kugawa zile skimu utashughulikiwa sasa na Serikali?

Lakini swali la pili, ni kwamba wako wananchi ambao walikuwa wanakaa katika eneo hilo ambalo mradi umejengwa pale kwenye eneo la bwawa waliondolewa na walilipwa fidia. Katika eneo hili la skimu kuna hekta mia kuna wananchi pale wachache walikuwa wanamiliki eneo hilo. Wako tayari kuondoka kuwaachia mradi huo kufanya kazi.

Je, Serikali inashauri nini kuhusu uwezekano wa kutoa fidia kama walivyofanya katika eneo ambalo bwawa limejengwa sasa kwa hawa ambao wataachia hizi hekta 100 kwa ajili ya wanachama hao zaidi ya 100 za mradi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru kwamba ametambua kwamba hii kazi inakwenda vizuri mkandarasi amesaini na mimi naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge hii miradi ya umwagiliaji inakuwa kidogo ina songombingo kidogo ya hapa pale tutashirikiana mimi na yeye Wizara kwa maana na yeye Mbunge tufuatilie kwa karibu ili tupate utekelezaji ukamilifu wa mradi huu.

Hili suala la kupima maeneo na kugawa, kuna element hapa ya halmashauri kushirikiana na Wizara sasa mimi naomba kwamba nichukue jukumu hili niwasiliane na Halmashauri na yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge tukubailiane ili tujue katika ule mkataba wa awali wa kuanza kutengeneza hii skimu makubaliano yalikuwaje kuhusu hawa wananchi waliokuwa katika nje ya upande wa skimu siyo kwenye ujenzi wa mabwawa, makubaliano yalikuwaje, na kama kusema kweli utaratibu unaotakiwa wa sasa hivi kupata fidia mimi nadhani hilo ni jambo ambalo Wizara pamoja na Halmashauri tunaweza tukalifanyia kazi na tukalipatia ufumbuzi.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nilikuwa swali kidogo la nyongeza ambalo halitofautiani sana na mwuliza swali. Kwetu katika jimbo la Nkenge kuna Bonde la Nkenge ambalo zamani lilikuwa linatumia kilimo cha umwagiliaji, nilikuwa nauliza sasa Serikali ina mpango gani kwa ajili ya kufufua kilimo hicho ili wananchi waweze kujipatia chakula ukizingatia ndizi zimeanza kupata mnyauko na hatuna chakula cha kutosha?

**SPIKA**: Haya Nkenge tena.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba palikuwa na kilimo pale Nkenge kwa mujibu wa taarifa niliyokuwa nayo hii ya hali ya umwagiliaji nchini hii ambayo ninayo hapa.

Kutokana na ufinyu wa Bajeti tumejielekeza kwenye maeneo maalum kwa ajili ya uzalishaji wa mazao maalum. Lakini hasa katika hili alilosema kwamba kuna upungufu mkubwa wa chakula mkoa wa Kagera kwa sababu ya tatizo la unyaufu, mimi nadhani hili linawezekana kuangaliwa upya.

Naomba nikiri kwamba nitakaa naye ili tuangalie kwamba katika huo mfumo wa mbadala wa zao la ndizi tunapeleka nini ikiwa ni pamoja na kuboresha mfumo huo wa umwagiliaji wa Nkenge.

Na. 275

**Zao la Mchikichi**

**MHE. DAVID Z. KAFULILA** aliuliza:-

Michikichi ni zao muhimu kwa uchumi wa mkoa wa Kigoma na Taifa kwa ujumla:-

(a) Je, Serikali ya awamu hii ya nne imekwishatumia kiasi gani katika Bajeti zake kuliboresha zao hilo?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa wakulima hao wanajengewa uwezo wa teknolojia na biashara ili waweze kufaidika na thamani halisi ya kilimo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukubaliana na Mheshimiwa Kafulila kwamba michikichi ni zao muhimu kwa uchumi wa Mkoa wa Kigoma na Taifa kwa ujumla. Kwa kutambua umuhimu huo Serikali ya awamu hii ya nne, imekwishakutumia kiasi cha shilingi milioni 92 katika jitihada kuboresha na kuendeleza kilimo na biashara ya zao hili.

Aidha kiasi cha shilingi 36 zimetumika kununulia mashine nne za kukamulia mawese na mashine mbili za kusindika mawese katika kata Buhanda, Businde na Kagera katika manispaa ya Ujiji.

Mheshimiwa Spika, jumla ya shilingi milioni 56 kupitia mpango wa maendeleo ya kilimo cha wilaya ya *DADPS* zimetumika kwenye ujenzi wa soko la kuuzia bidhaa zitokanazo na zao la mchikichi katika vijiji vya Sunuka na Ilagala katika Halmashauri ya Kigoma vijijini.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati wa kuhakikisha wakulima wa michikichi wanajengewa uwezo wa teknolojia na biashara ili wafaidike na thamani halisi ya kilimo hicho. Serikali kwa kushirikiana na shirika la *TACARE* inazalisha mbegu bora na kuwapatia wakulima jumla ya miche 8,000 zimezalishwa na kugawiwa kwa wakulima wa chama

cha maendeleo ya Wakulima wa Michikichi wa Kigoma *(KIPAFADA).*

Pia Wilaya ya Kasulu ilianzisha jumla ya miche bora ya michikichi ilizalisha michikichi 9,000 na kuigawa kwa wakulima. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na shirika la Kimataifa la *UNIDO* imejenga kiwanda kikubwa cha kusindika michikichi na bidhaa zitakanazo na kijiji hicho katika kijiji hicho cha Ilagala ambacho kina wazalishaji wakubwa wa zao la michikichi.

Kiwanda hiki tayari kimekamilika na utaratibu wa kupata fedha za kunulia jenereta kubwa la kukiendesha kiwanda hiki unaendelea ili kianze uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa mwaka 2011/2012 Halmashauri ya Kigoma vijiji, kupitia mipango yake ya maendeleo ilitenga jumla ya shilingi milioni 40 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za kuingia na kutoka mashambani kuja viwandani katika kurahisisha zoezi zima la usindikaji wa michikichi kutoka kijiji cha Ilagala.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza majibu ya Serikali ya kutenga milioni 92 kwa miaka saba sawa sawa na wastani kama wa milioni 10 kwa mwaka ni matusi kwa watu wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa Serikali itambue kwamba Tanzania inaagiza asilimia 60 kutoka

nje, mpaka sasa kuna kampuni ya Malaysia ambayo ina *supply* mafuta nchi ya Msumbiji,

**SPIKA:** Na wasiwasi kama unahutubia.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Zambia, Kongo na Tanzania, napenda....

**SPIKA:** Mheshimiwa Kafulila.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Napenda kuuliza maswali mawili, ni lini hiyo jenereta kwa ajili ya hicho kiwanda itapatikana ni lini kwa sababu isiwe hadithi?

Ni lini Serikali itaingiza kwenye akili yake mkakati wa namna gani ya kufanya mkoa wa Kigoma u-*supply* mafuta kwa nchi ya Tanzania, Msumbiji, Kongo na Zambia badala ya ku-*import* kutoka nje?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumsihi Ndugu yangu Mheshimiwa David Kafulila, kwamba haya maneno ya Serikali haina akili sijui nini hayapendezi. Mheshimiwa hapa mkakati tunakaa tunazungumza kila siku na vyema vile vile unapozungumza ukawa kidogo na nani hii. Tumezungumza tumesema Serikali inaingiza *importation* ya i-*recrued define* ni tani laki mbili tumeshasema kwamba mkakati wa kitaifa ni kupunguza *importation* hizi tuna namna mbili za kupunga hamna kwa kuingiza kupitia mafuta ya alizeti ama kwa kuzalisha uzalishaji wa mafuta ya mawese.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mafuta ya alizeti kwa sasa hivi umetoka katika miaka mitatu kutoka tani laki saba mpaka tani laki moja na nukta moja *which means* uzalishaji wa alizeti ni mkubwa zaidi kuliko uzalishaji wa mawese uliotoka tani 17,000 hadi tani 28,000 na mahitaji yetu katika uwekezaji huu ni kwamba lazima sekta binafsi ishiriki.

Sasa mkakati wa haraka kwa sababu alizeti ni zao la msimu hadi msimu tumepeleka kwamba mwaka huu tutumbukize tumetoa ruzuku ya alizeti kutoka shilingi milioni 200 hadi bilioni mbili na ili kuongeza uzalishaji kwenye kanda ya mikoa ya Singida, Dodoma na kadhalika na kwa maana hiyo tunawasihi *CRDB* ambao mwaka jana waliwekeza bilioni 9 katika *processing* ya alizeti wawekeze zaidi kwa mkakati maalum wa kuondoa hii *dependence* kutoka Malaysia.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kweli kwamba watu wanahitaji *choice* baina ya mafuta ya alizeti na mafuta ya mawese lakini Serikali haitopanda mawese kwa ajili yako Mheshimiwa David Kafulila.

Serikali itatengeneza mazingira ya kuwawezesha wakulima wa Kigoma wapande mawese na naomba nimsihi Mheshimiwa David Kafulila na shemeji zangu wa Kigoma kwamba katika hili tumejipanga Serikali kwamba kutakuwa na uzalishaji wa wakulima wadogo na uzalishaji wa wakulima wakubwa na Serikali itatoa pesa kwa kiasi cha kutosha ili kuongeza uzalishaji wa miche bora tusitegeme ile miche ya kienyeji.

Mheshimiwa Zitto, ni hapo hapo Kigoma.

**MHE. ZUBERI K. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara jana ambapo shirika la *NDC* limeamua kuwekeza na kusindika mazao mbalimbali na naomba kunukuu vilevile…

**SPIKA:** Muda wenyewe mfupi uliza swali tafadhali.

**MHE. ZUBERI K. ZITTO:** Upembuzi yakinifu wa mazao ya muhogo mtamu na mchikichi ulifanyika na kuchagua mafuta ya mawese kama kipaumbele katika mazao hayo matatu. Juhudi za *NDC* kupata ardhi ya kuanzisha kilimo cha michikichi wilaya ya Kisarawe na Kibaha zinaendelea. Kwanini mchikichi ulimwe Kisarawe na siyo Kigoma ambao ndiyo asili ya mchikichi?

**SPIKA:** Kwanini usiseme Kibaha nayo tu na siyo Kigoma? Naomba ujibu swali kwa kifupi hili swali limechukua muda mrefu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanini zao la mawese lisimwe Kisarawe kwetu na Kibaha wakati zao la mawese ni zao la biashara ambalo lina *potential* kubwa sana kwa wakulima wake?

Tulichosema ni kwamba pamoja na kuilima Kigoma na kilimo kwa maana hiyo kuongeza kilimo kwa wakulima wadogo wa Kigoma na *commercial farming* ya mawese ile *priority* iko pale pale lakini na

wengine ambao wana *potential* wa kulima mawese na kuzalisha kwa mfano kule jimbo la Mheshimiwa Kandege kule tumekwenda juzi kule kwa Mheshimiwa Keissy wanataka kuanzisha kilimo cha michikichi. Tunataka *zone* nzima ile iwe na kilimo cha michikichi kwa sababu bado kuna *potential* ya kukidhi *demand* ya tani ya zaidi ya laki mbili kote tukilima michikichi na alizeti tukidhi mahitaji ili tuondokane na kuingiza mafuta haya kutoka nje.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea michikichi lazima ilimwe huko.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Kuhusu nini Mheshimiwa David Kafulila.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Hajajibu swali moja kuhusu ni lini jenereta Ilagala kwa ajili ya kiwanda hicho?

**SPIKA:** Mbona uliacha Zitto kapewa nafasi? Tunaendelea swali linalofuatia.

Na. 276

**Biashara ya Nguo za Mitumba Nchini**

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI (K.n.y. MHE. KHERI KHATIB AMEIR)** aliuliza:-

(a) Je, Tanzania imeagiza tani ngapi za nguo za mitumba kutoka nje na zina thamani gani?

(b) Je, biashara hiyo ya mitumba inaleta ajira kiasi gani kwa Watanzania wa kawaida kwa mwaka?

(c) Je, Serikali inaweza kutueleza ni hasara kiasi gani inayoletwa kutokana na biashara hiyo kwa viwanda vyetu nchini kuzorota uuzaji wa bidhaa zake kwa kipindi cha mwaka mmoja?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge namba 276 naomba nifanye masahihisho kidogo tu kwenye jibu langu ambalo nakala ilitangulia jana. Kwenye jibu (a) naomba nifanye masahihisho kidogo tu, nguo za mitumba zenye thamani ya jumla ya s hilingi ni milioni siyo bilioni hapo tu badala ya bilioni iwe milioni, halafu inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir Mbunge wa Matemwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2005 hadi mwaka 2011, jumla ya tani 452,356.57 za nguo za mitumba zenye thamani jumla ya shilingi milioni 354,101,480 ziliingizwa nchini. Aidha, takwimu zinazoonyesha zinaonyesha kuwa uagizaji wa bidhaa

hizo kutoka nje ya nchi umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009 mpaka 2011 jumla ya leseni ya biashara 292 za uuzaji reja reja wa mitumba zimetolewa na mamlaka za Serikali za mitaa hapa nchini.

Kuna jumla ya wafanyabiashara wakubwa 48 ambao hufanya biashara ya kuagiza mitumba kutoka nje ya nchi na kuuza mitumba hiyo kwa wauzaji wadogo. Hakuna takwimu ya kiasi cha ajira zinazotolewa kwa vile utafiti haujafanyika katika eneo hili la uuzaji wa nguzo za mitumba. Lakini inaonyesha wazi idadi kubwa ya vijana wanauza nguo hizo.

(c) Mheshimiwa Spika, je, hakuna hasara inayopatikana kwa viwanda vyetu kwa wafanyabiashara kuuza nguzo za mitambua nchini na kuongezekana kwa biashara kuuza mitumba nchi?

Kuongezeka kwa biashara ya nguo za mitumba hakuna athari ya moja kwa moja kwenye viwanda vyetu kutokana na ukweli kuwa viwanda vyetu vya nguo pamoja na kwamba ni vichache bado vimejikita zaidi katika uzalishaji wa khanga, vitenge, mashuka, vikoi na mablanketi. Baadhi ya viwanda vilevile huzalisha vitambaa maalum kwa ajili ya batiki na *tie and dye* na *T-shirts.*

Hata hivyo, fursa hiyo ya soko la mitumba inaweza kutumiwa na viwanda vya ndani endapo viwanda vitapanua wigo wao wa bidhaa za nguo zinazozalishwa na kwa gharama nafuu ili kuhimili ushindani.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona naomba kuuliza swali kama ifuatavyo kwamba sekta ya nguo na *Textile* kwa ujumla imekuwa mkombozi wa uchumi wa nchi nyingi ambazo zimeendelea leo hii. Ni vipi Tanzania inawekeza katika kuimarisha sekta hii ya *textile* kwa ujumla katika *value chain* ili kuweza kuikomboa nchi yetu na umaskini badala ya kutegemea mitumba?

Mheshimniwa Spika, kama Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Bishara alivyosema alivyokuwa anawasilisha hotuba yake jana Serikali ipo katika kukamilisha mkakati wa kuimarishsa sekta ndogo ya nguo ili kuweza kukabiliana na changamoto mbalimbali za kuingiza nguo zenye ubora hafifu na nguo za mtumba ambazo zina asili ya viwanda vyetu.

Katika kipindi hiki ambacho tunakitegemea cha mwaka 2012/2013 Wizara imejipanga vizuri katika kuboresha viwanda vidogo vidogo vya nguo ambavyo vitasaidia katika kupunguza tatizo la mitumba na wananchi wetu waweze kupata nguo zenye ubora badala ya kutumia mitumba.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na muda umekwisha lakini bado maswali matatu. Mheshimwa Ritha Kabati atauliza swali linalofuata.

Na. 277

## Eneo la EPZ – Iringa

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, katika Mkoa wa Iringa ni eneo gani limetengwa kwa ajili ya *EPZ?*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Iringa una maeneo mawili yaliyopendekezwa na kutengwa kwa ajiil ya miradi ya *EPZ* na *SEZ.* Eneo la kwanza ni lile l ililopendekezwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ambalo linakadiriwa kuwa na ukubwa wa ekari 500 katika kijiji cha Viwengi kilichopo katikati ya Vijiji vya Lundamatwe na Lugalo Wilaya ya Kilolo.

Eneo la pili lipo Kijiji cha Ndolezi, Kata ya Mafinga, Wilaya ya Mufindi ambalo linakadiriwa kuwa na ukubwa wa hekta 1,200.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuyaainisha na kutenga maeneo hayo kwa ajili ya mradi wa *EPZ* na *SEZ,* taratibu za kuyachukua maeneo haya zinaendelea kupitia Halmashjauri za Wilaya ya Kilolo na Mufindi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa

ikiwa ni pamoja na taratibu za ulipaji wa fidia kwa waliopisha mradi. *(Makofi)*

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake na pia napenda kuishukuru Serikali kwa kutenga maeneo ya Kilolo na Mufindi kwa ajili ya miradi ya EPZ. Lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mkoa wetu wa Iringa una rasilimali nyingi sana na kwa kuwa kuanza mapema kwa miradi hii ya *EPZ* na *SEZ* tungeweza kutatua tatizo la ajira kwa vijana wetu wa Mkoa wa Iringa. Naomba kujua Mheshimiwa Waziri afafanue kwa sababu katika jibu lake la msingi naona hajafafanua vizuri kwamba ni lini hasa?

Swali la pili, ninapendakujua vigezo vinavyotumika kutoa vipaumbele katika kuanza utekelezaji wa miradi hiyo katika maeneo ambayo yameshatengwa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo.

Swali la kwanza analotaka kujua ni lini, jibu ni kwamba pale ambapo maeneo haya ambayo nimesema mawili yatakapotwaliwa ndipo wakati ambapo miradi hii inaweza ikaendelea na fidia

itakapolipwa kwa wale ambao watapisha hapo napo mradi huu unaweza ukaendelea.

Mheshimiwa Spika, tatizo ni vigezo vipi, niseme kwamba kwa upande wa utaratibu wa *EPZ* ambao unaendelea hakuna suala la vigezo, suala ni fursa hii ni fursa kama ambavyo tunasema kwamba kila mkoa yaani mikoa yote ishirini *EPZ* ina nafasi ya kuwekeza kwa kutenga maeneo maalum.

Kwa hiyo, suala la vigezo hakuna bali hii ni fursa ambayo Wabunge wote ningeomba mchangamkie suala la vigezo hakuna vigezo ni maeneo tu kutengwa na Serikali inawekeza kwa kuweka miundombinu. (*Makofi*)

Na. 278

**Kuzuiwa kwa Wafanyabiashara Afrika Mashariki**

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR** aliuliza:-

Nchi za Afrika Mashariki zipo kwenye mchakato wa kuelekea kwenye ushirikiano wa kibiashara na hatimaye matumizi ya Sarafu moja.

(a) Je, Serikali ina taarifa ya kuzuiwa Wafanyabiashara wa Tanzania wenye magari yenye shehena za unga kwenye mpaka wa Kenya?

(b) Je, ni sababu zipi zinazosababisha wafanyabiashara hao kuzuiwa?

(c) Je, Serikali imefanya jitihada gani ya kuwasaidia wafanyabiashara hao?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda jibu swali la swali la Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mbunge wa Fuoni, lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na makubaliano yaliyopo katika Itifaki ya Umoja wa Forodha, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kuwa malighafi/bidhaa zinazotoka kwenye nchi hizo kwa ajili ya kuuzwa miongoni mwao, sharti zikidhi vigezo vya uasilia wa bidhaa ili zisitozwe ushuru wa forodha.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo taarifa ya kuzuiliwa kwa shehena ya unga wa Ngano kutoka Tanzania kuingia katika soko la Kenya bila kulipia ushuru wa forodha. Taarifa hizo ziliwasilishwa Wizarani kama malalamiko ya wafanyabiashara kutoka Tanzania. Malalamiko hayo yalihusiana na kuwa Mamlaka ya Mapato ya Kenya ilizuia uingizaji wa unga wa Ngano kutoka Tanzania kwa madai kuwa haukidhi vigezo vya uasili wa bidhaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea malalamiko hayo, Wizra yangu iliwasilisha malalamiko ya wafanyabiashara hao wa Tanzania katika

Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo iliunda timu iliyojumjuisha wataalamu kutoka nchi zote wanachama kwa ajili ya kuhakiki suala hilo. Taarifa ya timu ya wataalamu iliwasilishwa katika Baraza la Mawaziri la Kisekta la Biashara, Uwekezaji, Fedha na Viwanda kwa ajili yakujadiliwa na maamuzi, ambapo ilibainika kuwa shehena hiyo ya unga wa Ngano haikukidhi vigezo vya uasilia wa bidhaa zinazotoka ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, ili kuwasaidia wafanyabiashara hao, Wizara yangu iliwaandikia barua yenye Kumb. Na. DC. 95/378/01C/39 ya tarehe 5 Agosti, 2011 ikiwaomba wawasilishe Wizarani vielelezo vinavyohusu gharama ya utawala, kanuni ya ukokotoaji wa thamani ya uchakavu wa majengo ya kiwanda pamoja na mashine za uzalishaji *(depreciation formula and value).* Hata hivyo, vielelezo hivyo bado havijawasilishwa Wizarani kwa ajili ya mashaurianona utatuzi.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, je, ni taratibu zipi zinatumika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki pindi wafanyabiashara wanapopata vikwazo wakati wanapopeleka bidhaa zao?

Pili, Wizara inamkakati gani wa makusudi ili kuwasaidia wafanyabiashara wetu ili kulitawala soko la Afrika Mashariki?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, jibu la Mheshimiwa Zubeir ni kama ifuatavyo:-

Kwanza lazima nikiri mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba vikwazo visivyo vya Forodha ni suala muhimu sana na linatukwaza sana katika maendeleo ya Afrika Mashariki, lakini hatua muhimu sana zimejitokeza na zinafanywa ili kuviondoa vikwazo hivyo tusifikie hatika hali ya kutokufahamiana miongoni mwetu.

Mheshimiwa Spika, hali ya kwamba wananchi wachukue hatua gani pindipo inapotokezea matatizo wanaposafirisha bidhaa zao ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza wanatakiwa wawasilishe malalamiko yao katika Wizara yetu au kupitia katika *focal Person* ambao tumewapanga mipakani. Wakishafikisha kwetu sisi tunakaa Kamati maalum ya watu maalum ya watu wa ndani yaani wataalamu wa kwetu Wizarani pamoja na katika Sekta husika na kupeleka taarifa hizi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki Sekretarieti ambayo kunatengenezwa Kamati maalum ya nchi tano kwa ajili ya uhakiki wa suala hilo halisia.

Mheshimiwa Spika, kuna dhana ya kwamba bidhaa nyingi ambazo zinatoka Tanzania tu ndiyo ambazo zinakwama kwenda katika nchi za jirani, lakini niseme vilevile matatizo haya vilevile na sisi tumekuwa tunalalamikiwa hivyohivyo. Kwa mfano kulikuwa na mazao ya Kuku, Siagi, Sabuni na kadhalika, nayo pia

Tanzania iliona haikidhi haja ya uhalisia kwa hiyo nao tukawaambia hebu kaeni muhakiki ili sisi tukubali. Hivyo, haya ni mambo ambayo ni ya maelewano baina ya nchi mbili.

Suala la bei taratibu zipo nyingi sana za jinsi ya kuanzia tangu kuwekwa *harmonization* ya mitaala, kukaa na wananchi kuzungumza nao mnaona kwenye televisheni na vitini vyetu na katika maonyesho ya Sabasaba, yote hii ni kuwahamasisha wananchi ili waweze kusajihisha biashara zao.

Na. 279

**Changamoto za Ajira katika Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. ESTHER A. BULAYA (K.n.y. MHE. MARY P. CHATANDA)** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje na changamoto ya ajira katika Jumuiya ya Afrika Mashariki hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya Watanzania tuna tatizo la uwajibikaji na kujituma kwa moyo katika utendaji?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Ushirkiano wa Afrika Mashariki kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la kutojituma na kutowajibika ni la mtu binafsi na wala halina uhusiano wa Utanzania wala Utaifa wa nchi nyingine yoyote. Hii ni hulka ya baadhi ya binadamu. Kwa maoni yangu, Watanzania walio wengi, wakiwemo waheshimiwa Wabunge ni wenye kuwajibika na kujituma na ninawapongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi jibu kwa swali la Mheshimiwa Mary C. Chatanda, Mbunge wa Viti Maalum, ni kama ifuatavyo:-

(i) Serikali inahakikisha kuwa ufunguaji wa Soko la Ajira nchini unafanyika hatua kwa hatua kulingana na makubaliano yaliyomo katika itifaki ya Soko la Pamoja kwa kuzingatia Mkakati wa Taifa wa Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja;

(ii) Serikali imeendelea kuendeleza miundombinu (vifaa, mitaala, majengo) ya elimu na mafunzo ya ufundi, katika vyuo vya maendeleo ya wananchi na taasisi za mafunzo ya maendeleo ya jamii kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kujenga raslimali watu wenye ufanisi, weledi na ujuzi wa kukidhi mahitaji ya soko la ajira ndani ya nchi, na katika Jumuiya;

(iii) Nchi wanachama zimekamilisha mchakato wa kuwiainisha Mifumo ya Elimu na Mitaala ya mafunzo. Hivi sasa elimu inayotolewa katika shule na vyuo hapa Tanzania inalenga kuwawezesha wahitimu kuwa na nafasi kubwa katika soko la ajira;

(iv) Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imewezesha kupatikana kwa wataalamu maalum *(Focal Persons*) 140 kutoka Halmashauri zote za Wilaya ili waweze kuwahamasisha wananchi wote kuhusu fursa zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tunajua Tanzania kuna vituo vya ajira yaani *Labour Exchange Bureau* lakini jukumu la vituo hivi katika soko la ajira la Afrika Mashariki haviko wazi. Sasa nini jukumu la vituo hivi katika kuhakikisha Watanzania wanapata fursa kwenye soko la pamoja kupata kazi katika nchi wanachama?

Pili, kama tunavyojua hakuna vyuo duniani ambavyo vinafundisha kazi, lakini katika nchi za wenzetu wamekuwa wakiwapa *training* wahitimu na hiyo imekuwa ikigharamiwa na Serikali na baada ya kuwapa *training* vyuo hivi vimekuwa vikiwasaidia wahitimu vijana ambao ni wengi katika kuwatafutia ajira.

Je, Serikali haioni huu ni wakati muafaka wa kuviboresha vituo hivi ili viweze kutoa *training* na kuwasaidia wahitimu kupata ajira katika nchi za wanachama?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki

najibu swali la Mheshimiwa Esther Bulaya, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najibu ya swali la Mheshimiwa Ester ni kama ifuatavyo. Ni kweli kwamba kuna *exchange* centres ambazo kwa hivi sasa zinaitwa *TAESA* yaani *Tanzania Employment Service Agents.* Kwanza nawapongeza kwa kazi zao nzuri za kuweza kupokea mahitaji ya ajira na kuwaweka wananchi wanaohitajika katika ku-*allocate* katika sehemu zinazotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu kwa kushikiriana na Wizara ya Kazi, hivi sasa imeona kwamba hili ni jambo muhimu la kuweza kupokea na kupeleka maombi na kwa kweli tumebaini kwamba hata Ulaya, Qatar na Uarabuni wanatumia vitengo hivi. Kwa hiyo sisi kutumia na Mabalozi wetu tutashirikiana na Wizara ya Kazi ili hivi vitengo viwe vinatumika katika kutafuta ajira ndani ya Afrika Mashariki na kwa ajili ya wananchi wetu.

Lakini la pili ni kama lile jibu la awali nililolisema kwamba uwezeshaji wa wananchi upo na tunafanya katika mbinu nyingi kwa ushirikiano wa Wizara za Kisekta, lakini pia wananchi wenyewe pia tunataka wawe na ujasiri wa kuthubutu kuweza kuingia katika hili soko.

Mheshimiwa Spika, bila ujasiri wa kuthubutu tutashindwa kuingia katika soko la ajira na nichukue nafasi hii vilevile kuwapongeza wale wote ambao wako katika nchi za Afrika Mashariki Watanzania wanafanya kazi nzuri tunawasilisna nao na wao wawe

ni Walimu wa kuwavutia wengine kwenda kufanya kazi huko.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, wakati Naibu Waziri wa Kilimo anajibu swali la Mheshimiwa Kafulila ni kweli kwamba sehemu ya pili hakujibu lakini ni kweli pia kwamba Mheshimiwa Kafulila alisimama lakini mimi sikumwona bali nilimwona aliyesimama kwa swali la nyongeza.

Kwa hiyo, namwomba Naibu Waziri ajibu sehemu ile ambayo hakujibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Kafulila la nyongeza sehemu ya pili kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza namuomba radhi kwamba nilitereza kidogo sikuweza kujibu.

Mheshimiwa Spika, hili suala la *generator,* Ilagala kwa kuzingatia uzalishaji mkubwa wa Michikichi uliokuwepo, Serikali na *UNIDO* imetoa pesa kwa ajili ya kuanzisha kile kiwanda lakini kile kiwanda kinamilikiwa na wakulima wenyewe wa Michikichi wa Ilagala wana kikundi chao kinaitwa *Yataka Moyo Group.*

Kwa hiyo, kwa kuwa, hatua za kutengeneza kile kiwanda huwezi kuanza kununua *generator* wakati unajenga msingi chini, hapana! *Generator* ni katika vitu vinavyonunuliwa mwishoni. Sasa kwa kuwa pesa

ya awali iliwekwa na Serikali na *UNIDO* na wadau wengine ni ninyi wenyewe *Yataka Moyo Group* na Halmashauri.

Naomba kusema kwamba hatukuweka *generator* uzalishaji hauanzi. Kwa hiyo, sisi wenyewe tulioweka pesa hii kwa maana ya Serikali na *UNIDO* na ninyi wadau wengine mwaka huu wa fedha tutakamilisha zoezi hili ili uzalishaji uanze kulingana na matarajio na matumaini ya wananchi wa eneo la Ilagala na hasa wale wenye kikundi chao cha wakulima.

**SPIKA:** Mengine mtaongea nje. Muda umepita sana na sasa naomba niwatambue wageni waliopo Bungeni.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo ambao ni familia yake wakiongozwa na mke wake Bi. Detha Muhongo, karibuni sana. (*Makofi*)

Pia kuna wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene Naibu Waziri wa Nishati na Madini ambaye pia ni mke wake Mrs. Mariana Simbachawene, karibu sana. (*Makofi*)

Pia tuna mgeni mwingine wa Naibu Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Stephen Masele ambaye ni Madame wake Bi. Paulina Masele, yeye kaja na *Baby*, karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni kutoka Wizara ya Nishati na Madini ambao ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini Ndugu Eliakim Maswi, karibu sana. Naomba asimame alipo. Ahsante sana. (*Makofi*)

Haya ahsante. Maana ya makofi hayo mimi siijui. Basi hivyo hivyo itakavyokuwa. Lakini tunakupongeza sana kwa kushika Wizara hiyo.

Halafu tuna Wenyeviti wa Bodi, Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Naomba wote wasimame kwa pamoja popote pale walipo. Ahsanteni sana, tunawatakia kazi njema. (*Makofi*)

Tunaye Ndugu Michael Mujija Meneja Mkuu wa Uratibu wa Utaratibu wa uagizaji mafuta kwa pamoja *Petrolium Importation Coodination* asimame sijui kama nimetamka jina vibaya. Naomba asimame Mkurugenzi, ahsante sana. (*Makofi*)

Tunao Maafisa wengine wote kutoka Wizara ya Nishati na  Madini pamoja na Taasisi zake zote sijui kama mlisimama mwanzoni tena simameni  kama mpo.

Lakini tuna wageni  wa Waheshimiwa Wabunge, bahati nzuri safari hii wamekuja kama vikundi. Kuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla na Mheshimiwa  Selemani Zedi ambao ni Madiwani sita wakiongozwa na Mheshimiwa Patrick Ngululi Diwani wa Kata ya Izanzu Halmashauri ya Mji wa Nzega.

Naomba Waheshimiwa Madiwani popote walipo wasimame. Ahsante sana, Karibuni Waheshimiwa Madiwani. (*Makofi*)

Halafu tuna wageni 15 wa Mheshimiwa Ritta Kabati, ambao ni kikundi cha *maua Group* kutoka Jimbo la Iringa Mjini wakiongozwa na Mwenyekiti wao Bi. Rose Mwaikambo. Haya kikundi hiki cha wakulima wa maua. Ahsante sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni sita wa Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan ambao ni viongozi na Wamiliki wa Maduka ya Madawa Muhimu kutoka Dar es Salaam na hao pia wasimame. Ahsanteni sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni waliofika kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 80 pamoja na walimu wao kutoka shule ya Sekondari ya Maria De Mathias, Dodoma, hii ni shule mpya wako wapi, wasimame popote walipo na walimu wao, shule ipo karibu na *Saint Gaspar* pale, karibuni sana na msome kwa bidii bila ubabaishaji. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi wengine 59 pamoja na walimu wao kutoka shule ya Mtakatifu Anna ya Morogoro, naomba na hao wasimame. Tumefurahi sana kuwaoneni, karibuni sana na msome kwa bidii. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunao wanafunzi wengine 40 pamoja na walimu wao kutoka shule ya sekondari Malambamawili, Dar es Salaam wasimame popote walipo. Ahsanteni sana

karibuni sana. Wanafunzi wote tunaomba mtumie nafasi yenu ya kusoma ndiyo kazi mliyonayo kwa faida yenu na kwa faida yetu sisi wote kama Taifa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Edward Lowassa, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 8.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi namba 219.

Kuna tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Wabunge wa CHADEMA Mheshimiwa David Silinde, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa CHADEMA kwamba leo saa 7.15 mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi namba 231.

Halafu Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa *Bunge Sports Club* wanaocheza mpira wa miguu netiboli wanahimizwa kuhudhuria mazoezi kesho siku ya Jumamosi asubuhi ili kujiweka sawa kwa ajili ya mchezo wa kirafiki na *NMB* utakaochezwa kesho jioni hiyo hiyo.

Kwa hiyo, timu ya ushindi itapangwa uwanjani. Kwa hiyo, tafadhali wote wahudhurie asubuhi. Mojawapo wa viongozi wa timu ya ushindi ni Mheshimiwa Nimrod Mkono, sasa mtajua wenyewe.

Waheshimiwa Wabunge nina matangazo mengine mawili. Moja, Mheshimiwa Murtaza Ali Mangungu, nasikia yeye ni Mratibu anaomba niwaarifu Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka katika maeneo yanayochimbwa na kufanyiwa utafiti wa gesi na mafuta kuwa leo tarehe 27 Julai, 2012 saa 8.00 mchana watakutana kwenye Ukumbi wa Msekwa B kwa ajenda mahsusi.

Halafu Mheshimiwa Kapt. John Chiligati, yeye anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge waliosoma iliyokuwa *Alliance Secondary School,* baadaye kuwa Mazengo Sekondari wakutane saa 7.15 katika Ukumbi wa Msekwa C kwa mazungumzo mafupi na Makamu Mkuu wa Chuo cha sasa hivi *St. Johns.*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na kazi. Tumetumia muda mwingi sana, nusu saa. Naomba tutumie muda vizuri. Katibu tuendelee na shughuli zinazofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 - Wizara ya Nishati na Madini

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, napenda kutoa Hotuba fupi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/13.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka 2011/12 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka 2012/13.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutumia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani yake kubwa kwangu kwa kuniteua kuwa Mbunge na Waziri wa Nishati na Madini. Uteuzi huu ni dhamana kubwa na changamoto kwangu, hususan katika kuhakikisha kuwa Sekta za Nishati na Madini zinachangia ipasavyo katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Naahidi kuchapa kazi kwa ubunifu na ufanisi wa hali ya juu. Vilevile nitatumia ujuzi wangu na maarifa ambayo nimeyafanya katika nchi mbalimbali duniani, kuboresha maisha ya Watanzania. Naahidu kwa neema ya Mwenyezi Mungu, kuyatekeleza majukumu aliyonipa kwa uadilifu kwa kushirikiana na Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee namshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.), kwa miongozo na ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Nitumie nafasi hii pia kukupongeza wewe Mheshimiwa Anne Semamba Makinda (Mb.) na Naibu

Spika, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb.), kwa namna ya pekee mnavyosimamia shughuli za Bunge hili. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote walioteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. Pia, nawapongeza Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb.) na Mheshimiwa Stephen Julius Masele (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mawaziri wa Wizara ya Nishati na Madini. Katika kipindi kifupi nilichofanya nao kazi, wamenipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu na wameonesha uwezo mkubwa katika uongozi. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Musa Zungu Azzan (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge hili. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa jinsi wanavyosimamia majukumu yao. Kwa namna ya pekee, natoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi (Mb.), Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo (Mb.) na Wajumbe wote wa Kamati, kwa ushauri na ushirikiano unaolenga kuimarisha utendaji wa Wizara. Nakiri kuwa Kamati hii imefanya kazi kubwa ya kuchambua kwa kina mapendekezo ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2012/13 na kutoa ushauri wa msingi kuhusu Bajeti hiyo. Ushauri huo umetuwezesha kufika hapa tulipo leo na kutoa mwelekeo mpya wa namna bora ya kuendesha na kusimamia ustawi wa Sekta za Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 mwezi huu nchi yetu ilikumbwa na msiba mkubwa wa vifo vya Watanzania wenzetu kutokana na ajali ya kuzama kwa meli huko Zanzibar. Natoa pole kwa familia za wafiwa na Watanzania wote kwa ujumla; Mwenyezi Mungu, azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge, mtapewa Kitabu cha Hotuba yangu na naomba taarifa na hoja hizo ziwasilishwe kama zilivyoletwa hapa asubuhi hii. Mbali ya hicho Kitabu cha Hotuba, vilevile mtapewa viambatisho ambavyo ninavyo hapa. Hii ni ramani na mmesema kwamba Wizara ina mambo mengi ya siri, nataka kuwahakikishia kuanzia sasa hakuna mambo ya siri Wizarani kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watapokea ramani ambazo zinaonesha umeme uliowekwa vijijini, Miradi ya Umeme Vijijini kwa wakati huu na miradi iliyopangwa kutekelezwa kwenye bajeti ninayowaomba. Kwa kuwa muda huu ni mfupi, ninaomba Waheshimiwa Wabunge chukueni muda njooni ofisini kwetu, nyuma ya Dodoma hoteli, kusudi muweze kuonana na wataalam na ninawapatia siku tatu; Jumapili, Jumatatu na Jumanne, njooni Wizara kwetu pale ukiwa na maswali, ukiwa na majibu na kwa wale wanaopenda shutuma njooni tu. Ramani ya pili mtaona wachimbaji wa madini wote na vitalu

vilivyogawiwa. Ramani nyingine itawaonesha Gridi za Umeme za Taifa na Miradi ya Gridi zote zipo hapa. Ramani nyingine itawaonesha vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi na makampuni ambayo yanafanya kazi hiyo, vyote vipo hapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba mzitumie vizuri hizo ramani na mna mnakaribishwa ofisini kwa maswali ya aina yoyote na majadiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara kwa mwaka 2011/2012: Mwaka 2011/2012 ulikuwa wenye changamoto nyingi kwa Wizara ya Nishati na Madini ikiwemo kuondoa mgawo wa umeme nchini. Pamoja na changamoto hizo, Wizara imetekeleza majukumu yake kwa kiwango cha kuridhisha sana.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2011/12, Wizara ilipangiwa lengo la kukusanya jumla ya Shilingi 131,266,153,300. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 jumla ya Shilingi 138,094,409,550, sawa na asilimia 105 ya lengo zilikusanywa. Lengo hili limefikiwa kutokana na kuimarika kwa usimamizi na ufuatiliaji wa ukusanyaji wa maduhuli kutoka Sekta za Nishati na Madini kwa mujibu wa Sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2011/12, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 402,402,071,000 ili kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, Shilingi 76,953,934,000, sawa na asilimia 19.12 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 325,448,137,000,

sawa na asilimia 80.88 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hata hivyo, Bajeti hiyo iliongezeka kwa Shilingi 136,112,000,000 baada ya kufanyika uhamisho na kufikia Shilingi 538,514,071,000.

Mheshimiwa Spika, uhamisho wa fedha uliofanyika katika kipindi husika ulikuwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya dharura ya kufua umeme ikiwa ni pamoja na ununuzi wa mafuta mazito ya kuendesha mitambo ya kufua umeme; malipo kwa mkandarasi anayejenga mitambo ya kufua umeme wa MW 60 huko Nyakato, Mwanza; na ulipaji wa madeni ya *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, jumla ya fedha zilizopokelewa na Wizara kutoka Hazina hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni, 2012 zilikuwa Shilingi 453,223,402,600, sawa na asilimia 84.16 ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2011/12. Kati ya fedha hizo, Shilingi 297,708,810,730 zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, sawa na asilimia 65.69, ambapo Shilingi 267,326,750,000, sawa na asilimia 89.79 ya fedha za maendeleo zilizopokelewa zilikuwa fedha za ndani na Shilingi 30,382,060,730, sawa na asilimia 10.21 ya fedha za maendeleo zilizopokelewa ni fedha za nje. Aidha, Shilingi 155,514,591,870 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, sawa na asilimia 34.31 ya fedha zilizopokelewa katika Mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika Sekta ya Nishati: Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Mwaka 2011/12 katika Sekta ya Nishati ni pamoja na kuongeza ufuaji wa umeme; upanuzi na uboreshaji wa njia za kusafirisha umeme;

kuwezesha upelekaji wa umeme vijijini; kutekeleza Miradi ya *Tanzania Energy Development and Access Expansion Project (TEDAP);* kuimarisha na kupanua miundombinu ya gesi asili na mafuta; kuendeleza shughuli za utafutaji wa gesi asili na mafuta; kuendeleza nishati jadidifu *(renewable energies);* na kudurusu na kuandaa Sera za Nishati.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kazi zilizopangwa kwa Mwaka 2011/12, Wizara ilifanikiwa kuondoa mgawo wa umeme kwa kutekeleza Mpango wa Dharura wa Umeme nchini; kukamilisha ujenzi wa mtambo wa kufua umeme kwa kutumia gesi asili wa MW 105 Dar es Salaam *(Ubungo II);* kununua mitambo ya MW 18 ya Mtwara kutoka Kampuni ya Wentworth; kukamilisha ufungaji na uzinduzi wa jenereta za kufua umeme katika Wilaya za Kasulu, Kibondo, Ngorongoro, Songea na Sumbawanga; kuzindua ufuaji umeme kwa kutumia maporomoko madogo ya maji kW 300 – Mawengi (Wilaya ya Ludewa), mwezi Novemba, 2011 ambapo zaidi ya kaya 300 ziliunganishiwa umeme; kukamilisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kV 33 ya kuunganisha Mtwara na Msimbati; kukamilisha ujenzi wa njia za umeme za msongo wa kV 33 kwa maeneo ya Mgwashi (Tanga) na Mbwewe (Pwani) na kukamilisha Tathmini ya Matumizi ya Nishati Vijijini Mwaka 2011 inayoonesha kuwa hadi kufikia Disemba, 2011 kiwango cha asilimia 6.6 ya Watanzania waishio vijijini wameunganishiwa umeme, hii ni sehemu ya asilimia 18.4 ya Watanzania wote waliounganishiwa umeme kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kusainiwa kwa Mkataba wa Mkopo kati ya Serikali ya Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China tarehe 20 Juni, 2012 kwa ajili ya ujenzi wa mtambo wa kusafisha gesi asili katika maeneo ya Songo Songo na Mnazi Bay na ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asili kutoka Mnazi Bay kupitia Somanga Fungu hadi Dar es Salaam; kusainiwa kwa mikataba mitano ya uzalishaji na ugawanaji wa mapato ya mafuta na gesi asili katika maeneo ya Rukwa, Kyela, Kilosa, Pangani na Kitalu Na. 8 kilichopo Mashariki mwa Mafia; kugunduliwa kwa gesi asili katika maeneo ya Mtwara kisima cha Ntorya - I na visima vilivyopo kina kirefu cha bahari vya Zafarani – I, Jodari – I, Mzia – I; na Lavani - I (Lindi); na kuanza kwa utekelezaji wa Mpango wa Uagizaji wa Mafuta wa Pamoja *(Bulk Procurement)* mwezi Januari, 2012.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2011/2012, maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Sekta ya Madini ni kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli; kusimamia Sheria ya Madini ya Mwaka 2010; kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini; kuendeleza uchimbaji wa kati na mdogo ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo ya uchimbaji mdogo; kuimarisha Mfuko wa Wachimbaji Wadogo; kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo; kuendelea kuimarisha ukaguzi wa shughuli za migodi ili kuongeza usalama, afya na mazingira bora; kuimarisha Mfumo wa Usimamizi na Utoaji Leseni za Madini katika Ofisi ya Makao Makuu ya Wizara  na Ofisi za Madini za Kanda na Afisa Madini Mkazi ili kuongeza kasi ya utoaji  leseni; kuimarisha na kuwezesha Mashirika/Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni *STAMICO, GST, TMAA* na Chuo cha

Madini, Dodoma *(MRI)* kutekeleza majukumu yake ipasavyo; na kudurusu Sheria mbalimbali za Madini.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Madini ni pamoja na migodi mikubwa nchini yenye mikataba *(MDAs)* kuanza kulipa mrabaha wa asilimia nne ya mauzo ya madini kulingana na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010; kulipwa kwa shilingi bilioni 188.1 za kodi ya mapato Serikalini kutoka Kampuni ya *Geita Gold Mine Limited* na shilingi bilioni 37.2 kutoka Kampuni ya *Resolute Tanzania Limited* kulikowezeshwa na ukaguzi uliofanywa na Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania *(TMAA)* kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA);* kuanzishwa kwa vocha za mauzo ya madini ya ujenzi zilizowezesha kukusanywa kwa mrabaha wa shilingi milioni 350.59 ikilinganishwa na shilingi milioni 30 zilizokuwa zinakusanywa kwa mwaka katika kanda zote za madini; na kutolewa kwa leseni za madini 1,097 za utafutaji mkubwa wa madini, 19 za uchimbaji wa kati; na 9,997 za uchimbaji mdogo wa madini.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kusainiwa kwa makubaliano ya ubia kati ya *STAMICO* na *Tanzania American International Development Corporation (2000) Limited (TANZAM 2000)* na kuunda kampuni ya ubia, ambapo *STAMICO* inamiliki hisa asilimia 45 na *TANZAM* 2000 asilimia 55; na kusainiwa kwa makubaliano ya ubia kati ya *STAMICO* na *Obtala Resources Limited* na kuanzisha Kampuni ya ubia *(Stabtala Investments)* kwa hisa asilimia 50 kwa 50. Kampuni ya *Stabtala Investments* itaingia ubia na

Watanzania wenye leseni kwa ajili ya kufungua migodi ya dhahabu yenye ukubwa wa kati.

Mafanikio mengine ni kutengwa kwa eneo la Itandula la uchimbaji mdogo wa madini lenye jumla ya hekta 37 lililoko Wilayani Tarime na hekta 15,605 eneo la Mbesa Wilayani Tunduru; kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo 380 katika Mikoa ya Lindi, Kigoma, Singida, Morogoro, Manyara na Tabora; kubadilisha ramani 33 kutoka kwenye mfumo wa *analogue* kwenda kwenye mfumo wa *digital* na kuingizwa kwenye kompyuta *documents meta-data* zipatazo 1,206; kufanyika kwa uchoraji wa ramani za kijiolojia na kijiokemia katika QDS 194, 212, 230 na 148; na kukamilika kwa ujenzi wa Ofisi ya Madini ya Kanda ya Kati – Singida.

Mheshimiwa Spika, licha ya mafanikio yaliyopatikana, Sekta ya Nishati na Madini imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo kukidhi kasi ya ukuaji wa mahitaji ya umeme; uchakavu wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme; kufikia lengo la asilimia 30 ya Watanzania ambao wameunganishiwa umeme ifikapo 2015; kupunguza upotevu wa umeme; kuwa na miundombinu ya gesi asili inayokidhi mahitaji; upungufu wa umeme kutokana na ukame uliosababisha kupungua kwa maji katika mabwawa makubwa ya kuzalisha umeme; kupanda kwa bei za mafuta katika Soko la Dunia; na upatikanaji wa vifaa hapa nchini kwa ajili ya ujenzi wa Miradi ya Umeme.

Mheshimiwa Spika, changamoto katika Sekta ya Madini ni pamoja na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; kuongeza fungamanisho la Sekta ya Madini na sekta nyingine za uchumi; ukuaji wa kasi wa shughuli za uchimbaji usio rasmi; biashara haramu ya madini; upatikanaji wa masoko ya uhakika kwa bidhaa za madini; mtaji mdogo wa uwekezaji kwenye uchimbaji mdogo; kushughulikia masuala ya fidia na uhamisho kupisha shughuli za migodi; migogoro ya kimaslahi na mahusiano baina ya wadau wa Sekta ya Madini; na uharibifu wa mazingira katika maeneo ya migodi na mfumko wa madini.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Nishati: Katika Mwaka 2011/12, Wizara iliendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuboresha upatikanaji wa nishati ya umeme nchini. Hadi mwezi Juni, 2012 uwezo wa mitambo ya kufua umeme (*installed capacity)* ulikuwa MW 1,375.74 (gesi asili asilimia 40, maji asilimia 41 na mafuta asilimia 19). Uwezo huo ni ongezeko la MW 367 sawa na asilimia 36 ikilinganishwa na uwezo wa MW 1,013.74 uliokuwepo mwezi Juni, 2011. Mwaka 2011 kiasi cha umeme kilichoingizwa kwenye Gridi ya Taifa kilikuwa MWh 5,153,400 ikilinganishwa na MWh 5,189,320 Mwaka 2010. Aidha, mahitaji ya juu ya umeme kwa Mwaka 2011/12 yalifikia wastani wa MW 820.35, ikilinganishwa na MW 730 kwa Mwaka 2010/11.

Mheshimiwa Spika, suala la mgao wa umeme haliwezekani wala halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakumbukwa kuwa mwezi Julai, 2011 wakati Bajeti ya Wizara yangu

ilipowasilishwa katika Bunge hili, nchi yetu ilikuwa katika mgawo wa umeme. Mgawo huo ulitokana na upungufu wa umeme wa takriban MW 300 uliosababishwa na upungufu wa maji katika mabwawa kwenye vituo vya kufua umeme. Kufuatia hali hiyo, Serikali ililazimika kuandaa Mpango wa Dharura wa Kuondoa Mgawo wa Umeme nchini ulioridhiwa na Bunge hili. Katika Mpango huo, jumla ya MW 572 zilipangwa kuzalishwa na kuingizwa kwenye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Juni, 2012 uwezo wa ufuaji umeme kutokana na Mpango wa Dharura wa Kuondoa Mgawo wa Umeme ulifikia jumla ya MW 422. Mitambo hiyo inajumuisha Symbion MW 137, Aggreko MW 100; IPTL MW 80; na Mtambo wa Gesi Asili wa Ubungo - II MW 105. Kutokana na kukosekana kwa mitambo ya MW 150 ya Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* iliyokadiriwa kugharimu Dola za Marekani milioni 162, sawa na shilingi bilioni 259.20, lengo la awali la Mpango wa Dharura lilipungua kutoka MW 572 hadi MW 422.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni, 2012 lengo la kuondoa mgawo wa umeme lilifikiwa kwa asilimia 100. Kwa sasa hakuna mgawo wa umeme kwa kuwa upungufu uliokuwepo ulikuwa ni kati ya MW 260 na MW 300 ikilinganishwa na uwezo wa MW 422 uliyoongezeka.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2011/12, Serikali ilikamilisha ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa MW 105 *Ubungo II,* Dar es Salaam na kuzinduliwa rasmi

tarehe 1 Julai, 2012. Mradi huo uligharimu jumla ya Dola za Marekani milioni 125, sawa na Shilingi bilioni 200 kwa udhamini kutoka Serikali ya Norway. Sambamba na mtambo huo, kazi za ufungaji wa mtambo wa kufua umeme wa MW 60 Nyakato - Mwanza ziliendelea chini ya Kampuni za M/S SEMCO Maritime AS na Rolls Royce Marine AS zote za Norway. Gharama za Mradi huo ni Dola za Marekani milioni 75, sawa na Shilingi bilioni 120. Mradi huo ulipangwa kukamilika mwezi Juni, 2012. Hata hivyo, kutokana na kuchelewa kupatikana kwa fedha, Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba, 2011 *TPDC* kwa niaba ya Serikali ilisaini Mkataba wa Usanifu, Ununuzi na Ujenzi, yaani *Engineering, Procurement and Construction (EPC)* na *China Petroleum Technology and Development Corporation (CPTDC)*, kwa ajili ya ujenzi wa bomba na mitambo ya kusafisha gesi asili. Aidha, mwezi Juni, 2012 Serikali ilisaini makubaliano ya mkopo nafuu na Benki ya Exim ya China kwa ajili ya ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi asili na bomba la kusafirisha gesi asili kutoka Mnazi Bay - Mtwara na Songo Songo Kisiwani (Lindi) hadi Dar es Salaam. Gharama za Mradi huu ni Dola za Marekani milioni 1,225.3, sawa na Shilingi trilioni 1.96. Kati ya fedha hizo asilimia 95 ni mkopo nafuu kutoka Benki ya Exim ya China na Serikali itachangia asilimia tano, sawa na Dola za Marekani milioni 61.26 zitakazolipwa kwa awamu tatu.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizofanyika chini ya Mradi huo ni tathmini ya fidia ya mali katika mkuza

wa bomba iliyokamilika mwezi Mei, 2012; tathmini ya athari za kijamii na kimazingira *(ESIA)* iliyokamilika mwezi Aprili, 2012 na kuridhiwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC);* na kukamilisha taratibu za kumpata mshauri wa kusimamia utekelezaji wa Mradi.

Mheshimiwa Spika, mwezi Juni, 2012 Serikali ilipata udhamini wa fedha kutoka *Norwegian Export Credit Agency* kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Kinyerezi I- MW 150. Mradi huu utagharamiwa na Serikali kwa njia ya mkopo, ambapo Dola za Marekani milioni 166.3, sawa na Shilingi bilioni 261.3 zitahitajika. Aidha, Serikali kupitia *TANESCO* ilifanya majadiliano na Kampuni ya Sumitomo kwa ajili ya kujenga mtambo wa kufua umeme wa Kinyerezi - II MW 240. Gharama ya Mradi huu ni Dola za Marekani milioni 432, sawa na Shilingi bilioni 691.20. Asilimia 85 ya fedha za utekelezaji wa Mradi huu zitapatikana kupitia kwa mdhamini, *Export Credit Agency for Japan (ECA).* Fedha za mkopo zitatolewa na *Japan Bank for International Corporation (JBIC), Nippon Export and Investment Insurance, Sumitomo Mitsui Banking Corporation (SMBC)* za Japani na asilimia 15 itatolewa na *Development Bank of South Africa (DBSA).* Mkataba wa *EPC* ulisainiwa mwezi Juni, 2012.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Somanga Fungu MW 320 unatekelezwa na Kampuni ya *Kilwa Energy Limited* ya hapa nchini ikishirikiana na Kampuni ya *ETG Power* kutoka Dubai. *TANESCO* inajadiliana na Kampuni ya *Kilwa Energy Limited* kuhusu Mkataba wa Kuuziana Umeme *(Power Purchase Agreement - PPA).* Mradi huu unaendelezwa na mwekezaji binafsi na gharama yake

ni Dola za Marekani milioni 365, sawa na Shilingi bilioni 584.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kufua Umeme wa Mchuchuma MW 600 unaendelezwa kwa ubia kati ya *NDC* (asilimia 20) na Kampuni ya Sichuan Hongda ya China (asilimia 80). Mkataba wa ubia *(Joint Venture Agreement)* kati ya *NDC* na Kampuni ya Sichuan Hongda ulisainiwa mwezi Septemba, 2011. Kampuni hiyo inaendelea kufanya utafiti wa kuhakiki kiasi na ubora wa makaa ya mawe yaliyopo katika eneo hilo. Kwa sasa, eneo hilo linakadiriwa kuwa na mashapo ya makaa ya mawe kiasi cha tani milioni 454.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ngaka MW 400 wa kuzalisha umeme kutokana na makaa ya mawe unatekelezwa na Kampuni ya *Tancoal Energy Limited* ambayo ni kampuni ya ubia kati ya Serikali kupitia *NDC* na Kampuni ya *Intra Energy Limited*. Uchimbaji wa makaa ya mawe umeanza katika Mradi huo kwa ajili ya matumizi viwandani na kuuzwa nje ya nchi, hususan Malawi na Msumbiji. Mradi unatarajiwa kuzalisha umeme kiasi cha MW 200 kwa kuanzia ifikapo Mwaka 2015/16 na kuongezeka hadi kufikia MW 400 Mwaka 2017/18. Uwekezaji kwa ajili ya kufua MW 200 utagharimu Dola za Marekani milioni 400, sawa na Shilingi bilioni 640.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira MW 200: Katika Mwaka 2011/12 Serikali ilifikia mwafaka na Kampuni ya *Tan Power Resources Limited* ili irejeshe rasmi hisa asilimia 70 ilizokuwa inamiliki katika Kampuni ya *Kiwira Coal and Power Limited (KCPL).*

Aidha, wafanyakazi 398 wa mgodi huo waliachishwa kazi na kulipwa mafao yao ya jumla ya Shilingi bilioni 1.56. Hata hivyo, wamebakizwa wafanyakazi 48 kwa ajili ya kutunza mgodi. Mgodi umekabidhiwa *STAMICO* ili itafute mbia wa kuendeleza mradi kwa njia ya ushindani. Anayeutaka Mradi wa Kiwira aje ashindane sio kupitia nyuma. Eneo hilo linakadiriwa kuwa na tani milioni 35.5 za mashapo ya makaa ya mawe na mradi utagharimu takriban Dola za Marekani milioni 400, sawa na Shilingi bilioni 640. Hadi Juni 2012, *STAMICO* imepokea maombi kutoka Kampuni 16 zilizoonesha nia ya kuingia ubia kwa ajili ya kuendeleza mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kufua Umeme wa Ruhudji MW 358 awali ulikuwa unaendelezwa na Kampuni ya *Aldwych International* ya Uingereza. Hata hivyo, Kampuni hiyo iliamua kuungana na Kampuni ya *Sithe Global Power Ventures* kutoka Marekani mwezi Disemba, 2011 ili kuendeleza mradi huo. Aidha, Makubaliano ya Awali *(MoU)* kati ya Serikali na Muungano wa Kampuni hizo yalisainiwa mwezi Januari, 2012. Mradi utagharimu takriban Dola za Marekani milioni 900, sawa na Shilingi trilioni 1.44 na utaendelezwa kwa utaratibu wa *Public Private Partnership (PPP)* kati ya Kampuni hizo na *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kufua Umeme wa Rusumo MW 75: Taarifa ya upembuzi yakinifu na tathmini ya athari za mazingira zilikamilika mwezi Aprili, 2012. Taarifa hiyo, inaonesha kuwa umeme wa MW 90 ungeweza kuzalishwa ikilinganishwa na MW 63 ya tathmini ya awali. Hata hivyo, kutokana na fidia na athari kubwa za mazingira, nchi washiriki yaani

Tanzania, Burundi na Rwanda zimeamua mradi huo uendelezwe bila kuwa na bwawa kubwa *(run-of-the river scheme)* na kiasi cha MW 75 kifuliwe badala ya MW 90. Kutokana na uamuzi huo, Mshauri wa Mradi (Kampuni ya SNC Lavalin kutoka Canada) ameelekezwa kudurusu tathmini ya mazingira. Mshauri huyo atakamilisha kazi ya kudurusu mradi huo ifikapo mwezi Agosti, 2012. Jumla ya gharama za mradi huu ni Dola za Marekani milioni 100, sawa na Shilingi bilioni 160, ambapo mchango wa Serikali ni Dola za Marekani milioni 28, sawa na Shilingi bilioni 44.80.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kufua Umeme wa Murongo/Kikagati MW 16 unaendelezwa na Kampuni ya *Trond Energy* kutoka Norway. Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Uganda zimekubaliana kuingia mkataba wa ushirikiano *(Bilateral Agreement)* ili kuendeleza mradi huo. Majadiliano ya mkataba wa ushirikiano yanaendelea. Mradi huo umepangwa kukamilika ndani ya miezi 30 baada ya kufikiwa makubaliano ya mkopo. Mradi utakapokamilika, utawezesha kila nchi kupata MW 8. Mradi utagharimu takriban Dola za Marekani milioni 30.46, sawa na Shilingi bilioni 48.74.

Mradi wa Kufua Umeme wa *Stiegler's Gorge MW 2,100*: Mwezi Aprili, 2012 Serikali ya Tanzania ilikutana na Serikali ya Brazil kujadili utekelezaji wa mradi wa Stiegler's Gorge, ambapo mwekezaji binafsi kutoka huko anatarajiwa kuanza kudurusu mradi pamoja na tathmini ya athari za mazingira. Pamoja na ufuaji umeme, mradi huu utahusisha shughuli za uvuvi, utalii, kilimo cha umwagiliaji na kulipatia Jiji la Dar es Salaam

maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani bilioni 1.9, sawa na Shilingi trilioni 3.04. Mradi huu unasimamiwa na *RUBADA.*

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuboresha Mifumo ya Umeme katika Jiji la Dar es Salaam: Katika Mwaka 2011/12 Serikali iliendelea na juhudi za kuimarisha miundombinu nchini ikiwemo kukarabati njia ya umeme kutoka Ilala mpaka Kurasini kwa kubadilisha waya kutoka milimita za mraba 150 hadi 432, kufunga transfoma za ukubwa wa MVA 15 katika vituo mbalimbali vya kupozea umeme, ambapo kituo cha *City Centre* kazi imekamilika. Aidha, kazi hiyo inaendelea katika vituo vya Gongolamboto, Kigamboni, Kipawa, Kurasini Mbagala, Mbezi Beach na Ubungo. Kazi nyingine iliyofanyika na kukamilika ni kubadilisha nyaya chakavu katika maeneo hayo. Mradi utatekelezwa kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 75, sawa na Shilingi bilioni 120.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa TEDAP: Katika Mwaka 2011/12 Serikali iliendelea na ujenzi wa misingi ya nguzo kwa ajili ya njia ya umeme ya msongo wa kV 132 Jijini Dar es Salaam pamoja na vituo vya kupozea umeme, kV 132/33 vyenye uwezo wa MVA 50 eneo la Gongolamboto *(Factory Zone II)* na Kipawa *(Factory Zone III).* Aidha, ujenzi wa kituo cha kupozea umeme eneo la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Kilimanjaro (KIA) kV 132/33 chenye uwezo wa MVA 40 unaendelea. Miradi hii inatekelezwa kwa udhamini wa Benki ya Dunia. Gharama za mradi ni Dola za Marekani milioni 116, sawa na Shilingi bilioni 185.60.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mradi wa Iringa - Shinyanga kV 400 *(backbone),* mshauri amekamilisha upembuzi yakinifu wa kuvipatia umeme vijiji vitakavyopitiwa na njia mpya ya umeme. Aidha, Mshauri wa Mradi, Kampuni ya Fitchner ya Ujerumani anaendelea na kazi ya kusanifu njia ya usafirishaji umeme na vituo vya kupozea umeme. Mradi utakapokamilika utagharimu Dola za Marekani milioni 650, sawa na Shilingi bilioni 1,040.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2011/12 Serikali kupitia *TANESCO* ilidurusu usanifu wa Mradi wa Dar es Salaam – Chalinze – Tanga – Arusha kV 400 *(redesigning)* ili uanzie Dar es Salaam kupitia Chalinze hadi Arusha badala ya kuanzia Morogoro. Uamuzi huu ulitokana na Serikali kuridhia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bomba la gesi asili kutoka Mtwara na Songo Songo kupitia Somanga Fungu hadi Dar es Salaam.

Baada ya bomba hilo kukamilika, Dar es Salaam itakuwa kitovu kikuu cha ufuaji umeme nchini na hivyo kuhitaji upanuzi wa mfumo wa usafirishaji umeme. Mwezi Juni, 2012 *TANESCO* na mkandarasi Kampuni ya *TBEA* ya China walisaini mkataba wa marekebisho *(EPC addendum),* hivyo kuongeza uwezo wa kusafirisha umeme kutoka Dar es Salaam. Mradi huu utatekelezwa kwa mkopo wa takriban Dola za Marekani milioni 770, sawa na Shilingi bilioni 1,232 kutoka Benki ya Exim ya China.

Mheshimiwa Spika, mwezi Januari, 2011 Serikali ilisaini mkataba wa mkopo na Taasisi ya Fedha ya

*BADEA* ya Misri na *OFID* ya Saudi Arabia. Lengo ni kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Umeme ya kV 220 ya Bulyanhulu – Geita – Nyakanazi. Kazi ya kuandaa zabuni za kandarasi za ujenzi ilikamilika mwezi Juni, 2012. Mradi utagharimu Dola za Marekani milioni 53, sawa na Shilingi bilioni 84.8.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuwepo miradi mingi ya ufuaji umeme katika maeneo ambayo njia ya umeme kutoka Makambako mpaka Songea itapita kama vile Ngaka, Mchuchuma na Masigira, Serikali imeamua kudurusu Mradi wa Makambako - Songea kutoka kV 132 mpaka kV 220. Serikali kupitia *TANESCO* ilisaini mkataba na Kampuni ya *SWECO* ya Sweden mwezi Agosti, 2011 kwa ajili ya kuandaa zabuni ya kumpata mkandarasi atakayesanifu na kutekeleza mradi. Tathmini ya fidia kwenye maeneo ambayo njia hiyo itapita inaendelea. Mradi huu unagharimiwa na Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Maendeleo la Sweden (Sida) kwa kiasi cha Swedish Kroner milioni 500, sawa na Shilingi bilioni 112.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Upanuzi na Uboreshaji wa Mfumo wa Usambazaji wa Umeme, Mradi wa Electricity – V, unatekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* na utahusisha usambazaji wa umeme katika Vijiji, Miji Midogo na Makao Makuu ya Wilaya katika Mikoa ya Geita (Bukombe), Mwanza (Magu na Kwimba) na Simiyu (Bariadi) na kukarabati vituo vikubwa vya kupozea umeme kwenye Mikoa ya Dar es Salaam na Arusha. Kazi ya kujenga njia za umeme na vituo vya

kupozea umeme itaanza katika Mwaka 2012/13. Gharama za Mradi ni Dola za Marekani ni milioni 31, sawa na Shilingi bilioni 49.6.

Mheshimiwa Spika, Miradi iliyo chini ya Ufadhili wa *Millenium Challenge Account (MCA-T):* Mradi wa Kukarabati Miundombinu ya Usambazaji wa Umeme Kigoma na Kituo cha Kufua Umeme Malagarasi. Kazi ya ukarabati wa miundombinu ya kusambaza umeme inaendelea kutekelezwa na Kampuni ya *Symbion Power LLC* kupitia ufadhili wa *MCA-T.* Mradi huo unajumuisha ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa kV 11 na upanuzi wa njia za umeme ili kuunganisha umeme kwa wateja mbalimbali. Kazi ya ujenzi wa Mradi huu inatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2012. *TANESCO* ilikamilisha upembuzi yakinifu wa Mradi wa MW 42 katika Mto Malagarasi *(Igamba III)* mwezi Mei, 2012. Serikali inafanya majadiliano na Washirika wa Maendeleo na sekta binafsi kwa ajili ya kutekeleza Mradi huu, hivyo kuongeza uwezo wa kufua umeme katika Ukanda wa Magharibi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kujenga Njia za Kusambaza Umeme unahusu ujenzi wa njia za msongo wa kV 33 na kV 11 kwa ajili ya kusambaza umeme katika Mikoa ya Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Mwanza na Tanga. Utekelezaji wa Mradi unaendelea na umefikia kiwango cha asilimia 40, ambapo kilomita 349.09 kati ya kilomita 870.43 zimekamilika. Mradi mzima unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kusanifu na Kujenga Vituo 24 vya Kupozea Umeme unahusu usanifu na

ujenzi wa vituo 24 vya kupozea umeme kV 33/0.4 na kV 11/0.4 katika Mikoa ya Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Mwanza na Tanga. Ujenzi wa vituo 22 kati ya 24 ulianza mwezi Aprili, 2012. Mradi umepangwa kukamilika mwezi Machi, 2013.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Njia ya Pili ya Umeme kutoka Dar es Salaam kwenda Unguja unahusu usanifu na uwekaji wa njia ya pili ya umeme kutoka Ubungo hadi Ras-Kilomoni na uwekaji wa nyaya za umeme chini ya bahari *(submarine cable)* kutoka Ras-Kilomoni hadi Mtoni – Unguja. Njia hii itakuwa na uwezo wa kusafirisha MW 100 kwa msongo wa kV 132. Kazi ya kuweka nyaya za umeme chini ya bahari imeanza mwezi huu wa Julai, 2012 na itakamilika mwezi Agosti, 2013. Miradi ya *MCA-T* katika sekta ndogo ya umeme iliyotajwa hapo juu inakadiriwa kugharimu Dola za Marekani milioni 201.25, sawa na Shilingi bilioni 322.

Mheshimiwa Spika, Upelekaji wa Umeme Makao Makuu ya Wilaya na Maeneo ya Vijijini: Katika kipindi cha Mwaka 2011/12, Serikali kupitia TANESCO ilikamilisha ufungaji na uzinduzi wa jenereta za kufua umeme katika Wilaya za Kasulu, Kibondo, Ngorongoro na Songea. Gharama zilizotumika kukamilisha Miradi hii ni Shilingi bilioni 33.61, ambazo ni fedha za ndani. Serikali pia imekamilisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kV 33 kutoka Sumbawanga Mjini mpaka Namanyere - Nkasi. Kwa sasa mkandarasi, *M/s Rousant International* anakamilisha upanuzi na ufungaji wa vifaa katika kituo cha kupozea umeme cha Sumbawanga Mjini kwa ajili ya njia ya umeme kwenda Nkasi.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* umeendelea kuwezesha utekelezaji wa Mradi Kabambe wa kusambaza umeme vijijini katika mikoa 16 ya Arusha, Dodoma, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Mara, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Pwani, Rukwa, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga. Wateja wa awali wapatao 20,000 wataunganishiwa umeme Mradi utakapokamilika mwezi Disemba, 2012. Gharama ya Mradi huu ni Shilingi bilioni 100.75.

Mheshimiwa Spika, Miradi Midogo ya Nishati Vijijini: Serikali kupitia REA imeendelea kuhamasisha uendelezaji wa vyanzo vya nishati jadidifu katika maeneo ya vijijini yaliyo mbali na Gridi ya Taifa. Katika Mwaka 2011/12, Mradi wa Mawengi wenye uwezo wa kuzalisha kW 300 kwa kutumia maporomoko madogo ya maji uliyopo Wilayani Ludewa ulizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Novemba, 2011. Mradi huu unamilikiwa na Ushirika wa LUMAMA na unahusisha Vijiji vya Lupande, Madunda na Mawengi. Katika Awamu ya Kwanza ya Mradi, zaidi ya kaya 300 ziliunganishiwa umeme. Katika Mradi huu Serikali imechangia Dola za Marekani 571,500, sawa na Shilingi milioni 914.40 kwa ajili ya kuunganishia umeme wateja 1,143.

Mheshimiwa Spika, mwezi Juni, 2011 *REA* ilisajiliwa katika Mpango wa *Clean Development Mechanism-Programme of Activities (CDM-PoA).* Mpango huo unahamasisha uendelezaji wa nishati jadidifu na

matumizi bora ya nishati. Wakaguzi kutoka *United Nations Framework Convention on Climate Change (UNFCCC)* kwa kushirikiana na *REA* walikamilisha tathmini ya Mradi wa Mapembasi - Njombe (MW 10) mwezi Aprili, 2012. Utaratibu huu unamwezesha mwendelezaji kupata mapato ya awali kutokana na kiwango cha hewa ukaa alichopunguza katika mazingira na hivyo kupunguza gharama za uwekezaji katika Miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wakala pia uliendelea kusimamia utekelezaji wa miradi kumi chini ya *Lighting Rural Tanzania – 2010*. Mradi huo unahamasisha matumizi ya nishati yenye mwanga bora vijijini ili kupunguza matumizi ya mafuta ya taa na mishumaa. Mikoa inayonufaika na Mradi ni Iringa, Kagera, Manyara, Mara, Mbeya, Mwanza, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga na Singida. Gharama ya Mradi huu ni takriban Dola za Marekani milioni 1.0, sawa na Shilingi bilioni 1.60 na unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikamilisha tathmini ya usambazaji umeme kwa gharama nafuu. Tathmini hiyo iliyokamilika mwezi Disemba, 2011 ilionesha kuwa gharama za uunganishaji umeme maeneo ya vijijini zinaweza kupungua kwa asilimia 30 kwa kurekebisha viwango vya vifaa kama vipozea umeme na nyaya za umeme; kuwa na mfumo wa ununuzi wa pamoja wa vifaa; matumizi ya *ready boards*; na kutumia mfumo wa *single wire earth-return*. Miradi ya mfano itatekelezwa katika Wilaya ya Kilombero (Kituo cha Umeme Kihansi mpaka Gereza la Idete) na Wilaya ya

Mbozi (Vwawa mpaka Itaka). Wateja wa awali wapatao 15,000 wanatarajiwa kuunganishiwa umeme kwa utaratibu huu. Gharama ya Mradi huu ni Shilingi bilioni 16.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kutekeleza jukumu lake la kusimamia taasisi zilizo chini yake, imegundua kuwa *TANESCO* inakabiliwa na changamoto kubwa ya upotevu wa umeme wa kiufundi na usio wa kiufundi unaokadiriwa kufikia asilimia 21. Wizara imegundua kuwa sehemu kubwa ya upotevu wa umeme usiokuwa wa kiufundi *(non technical losses)* unasababishwa na wizi unaofanywa na wananchi kwa kushirikiana na baadhi ya Wafanyakazi wa *TANESCO* wasio waaminifu na mafundi wa mitaani wajulikanao kama vishoka. Aidha, wateja wengi wenye nyumba za biashara, za kuishi na viwanda katika Jiji la Dar es Salaam na baadhi ya Mikoa ya Tanzania wamekuwa wakitumia umeme kwa njia zisizo halali. Pia, baadhi ya Wafanyakazi wa *TANESCO* wamekuwa wakishiriki katika vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa mali za Shirika.

Mheshimiwa Spika, hali hii imeleta taswira isiyokuwa nzuri kwa Shirika na kurudisha nyuma juhudi za Serikali katika kuboresha huduma za umeme. Ili kuondoa tatizo hilo, katika Mwaka 2011/12 Serikali kupitia *TANESCO* imechukua hatua mbalimbali za kinidhamu zikiwemo kuwafukuza kazi watumishi 17 na kuwafikisha mahakamani wengine 7; na kung'oa miundombinu iliyojengwa na vishoka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo zilizochukuliwa, natoa rai kwa wananchi wanaopata huduma ya umeme kwa njia zisizo halali kujisalimisha katika Ofisi za *TANESCO* haraka iwezekanavyo. Hatua kali zitachukuliwa kwa wale ambao hawatatii rai hii zikiwemo kusitishiwa huduma ya umeme, kulipia gharama ya umeme kwa kipindi chote alichokuwa anapata huduma hiyo kwa njia zisizo halali pamoja na kulipa faini.

Mheshimiwa Spika, shughuli za utafutaji mafuta na gesi asili katika Bahari ya Hindi na nchi kavu zimeendelea kufanyika kwa kasi kubwa. Kwa sasa kuna kampuni 18 za utafutaji mafuta na gesi asili katika nchi kavu, baharini na kwenye maziwa na kuna jumla ya mikataba ya kugawana mapato *(Production Sharing Agreements - PSAs)* 26. Kampuni kubwa za Kimataifa zinazojihusisha na utafutaji wa mafuta na gesi asili katika kina kirefu cha maji baharini ni pamoja na *BG Group* na *Ophir* za Uingereza; *ExxonMobil* ya Marekani; *Dominion* ya Australia; *Mubadala* ya Umoja wa Falme za Kiarabu; *Petrobras* ya Brazil, Shell ya Uholanzi; na *Statoil* ya Norway.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2011/12, Serikali kupitia *TPDC* ilisaini mikataba mitano ya uzalishaji na ugawanaji mapato ya mafuta na gesi asili *(PSAs)* na Kampuni za Heritage (Ziwa Rukwa na Bonde la Kyela); Petrobras (Kitalu Na. 8 karibu na Mafia); na *Swala Oil and Gas (T) Limited* (Bonde la Kilosa na Pangani). Serikali inaendelea kuboresha usimamizi wa mikataba hiyo na kujenga uwezo wa kufanya ukaguzi. Lengo ni kuhakikisha kuwa kampuni zote zinazofanya utafiti na

uzalishaji wa gesi asili na mafuta zinatekeleza kazi zake kwa mujibu wa makubaliano yaliyomo katika mikataba.

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2012 Kampuni za *Statoil* na *ExxonMobil* ziligundua gesi asili kiasi cha futi za ujazo trilioni sita katika kisima cha Zafarani -1 na mwezi Juni, 2012 kampuni hizo pia ziligundua gesi asili kiasi cha futi za ujazo trilioni 3 katika kisima cha Lavani – 1. Aidha, mwezi Mei, 2012 Kampuni za *BG Group* na *Ophir* zilichoronga visima viwili na kufanikiwa kupata gesi asili kiasi cha futi za ujazo trilioni 3.4 katika kisima cha Jodari – 1 na kiasi cha futi za ujazo trilioni 4.6 katika kisima cha Mzia – 1.

Mheshimiwa Spika, pia katika mwezi huo wa Mei, 2012 Kampuni ya *Ndovu Resources (T) Limited* iligundua gesi asili kwenye Kitalu cha Ruvuma katika kisima cha Ntorya-1. Kampuni hiyo inaendelea na uchambuzi wa takwimu ili kuhakiki kiasi cha gesi asili kilichopo. Aidha, Kampuni ya *PanAfrican Energy (T)* ilichoronga kisima SS 11 katika kisiwa cha Songo Songo ili kuongeza kiasi cha gesi asili kinachovunwa. Kisima hicho kina uwezo wa kuzalisha futi za ujazo milioni 60 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, uvunaji wa gesi asili unafanyika katika maeneo ya Songo Songo (Kilwa) na Mnazi Bay (Mtwara) kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ndani. Gesi asili iliyopo *(reserve)* Songo Songo ni futi za ujazo kati ya trilioni 1.0 hadi 2.5 na Mnazi Bay ni futi za ujazo kati ya trilioni 3.0 hadi 5.0. Uwezo wa mitambo ya Songo Songo kusafisha gesi asili ni futi za ujazo

milioni 110 kwa siku na Mnazi Bay ni futi za ujazo milioni 2 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, visima vya Mkuranga na Kiliwani Kaskazini vilivyogunduliwa kuwa na gesi asili Mwaka 2007, bado havijaendelezwa. Ili kukidhi mahitaji ya gesi asili nchini visima vya Kiliwani Kaskazini, Nyuni na Ndovu vitaunganishwa na mitambo ya kusafisha gesi asili kisiwani Songo Songo.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utafiti wa mafuta na gesi asili unaoendelea hapa nchini, yanaonesha kuwepo kwa kiasi cha gesi asili kinachokadiriwa kuwa zaidi ya wastani wa futi za ujazo trilioni 26.99, sawa na mapipa ya mafuta bilioni 4.86 ikilinganishwa na kiasi cha awali cha futi za ujazo trilioni 5.0 katika maeneo ya Songo Songo na Mnazi Bay. Aidha, tafiti zaidi zinaendelea na inatarajiwa kuwa gesi asili nyingi zaidi itagundulika. Kiasi halisi cha gesi asili kilichopo kitafahamika baada ya kuchoronga visima vya utafutaji *(exploration wells)* katika maeneo husika. Fedha zilizotumika hadi sasa katika utafutaji huo ni Dola za Marekani milioni 919.90, sawa na Shilingi trilioni 1.47.

Mheshimiwa Spika, ili kudhihirisha manufaa ya gesi asili na mafuta kwa wananchi wa maeneo ambayo rasilimali hizo zinapatikana, mwezi Januari, 2012 Serikali ilianza utaratibu wa kuhakikisha kuwa kampuni za utafutaji mafuta na gesi asili zinalipa tozo ya asilimia 0.3 ya mgawo wa faida ya gesi asili kwenye halmashauri husika. Utaratibu huu umeanza kutekelezwa katika Halmashauri ya Kilwa na utaimarisha uhusiano kati ya wananchi na wawekezaji kwenye maeneo hayo,

katika kulinda miundombinu. Serikali pia inahimiza kampuni hizo ziongeze wajibu wa ushiriki katika masuala ya kijamii - *Corporate Social Responsibility*. Aidha, Kampuni ya Mauren and Prom imeelekezwa kuilipa Halmashauri ya Mtwara asilimia 0.3 ya *service levy.*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Januari hadi Mei, 2012 majadiliano kati ya *TPDC* kwa niaba ya Serikali na Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT),* yalifanyika kuhusu utekelezaji wa mkataba wa uzalishaji na ugawanaji mapato *(PSA)* kati ya pande hizo mbili. Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa ni uingizwaji kimakosa wa Dola za Marekani milioni 28.1 kwenye mahesabu ya mkataba kati ya *TPDC* na *PAT.* Baada ya uchambuzi kufanyika, Serikali ilibaini kuwa baadhi ya gharama zilizoingizwa kwenye vitabu vya *PAT* hazikuwa zimebainishwa kwenye mkataba. Kati ya fedha hizo, Dola za Marekani milioni 20.1 zingekuwa mgawo wa Serikali. Kimsingi, *PAT* imekubali kuwepo kwa kasoro hizo na kuzifanyia marekebisho. Kuhusu kurejesha Serikalini Dola za Marekani milioni 20.1, Uongozi wa *PAT* umewasilisha taarifa hizo kwa Kampuni Mama ya *ORCA* iliyopo nchini Uingereza kwa ajili ya uamuzi wa mwisho. Serikali imeelekeza *PAT* kuwasilisha uamuzi wake mwezi Agosti, 2012.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asili kutoka Ubungo mpaka Mikocheni. Bomba hili litakuwa na sehemu za kuchepusha gesi asili kuelekea taasisi na nyumba zilizopo karibu na Barabara ya Sam Nujoma. Taasisi hizo ni pamoja na Chuo cha Maji cha

Rwegarulira, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Ardhi. Mradi huo utakapokamilika, viwanda sita katika eneo la Mikocheni na nyumba 57 vitaunganishwa kwa ajili ya kutumia gesi asili. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa kutumia mkandarasi wa ndani (Kampuni ya BQ Contractors) kwa gharama ya Shilingi bilioni tano na utakamilika mwezi Agosti, 2012.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja *(Bulk Procurement)* ulianza rasmi mwezi Januari, 2012. Katika kipindi cha kuanzia Januari, 2012 hadi Juni, 2012 kiasi cha tani 1,808,958 za mafuta aina ya petroli ziliingizwa nchini. Aidha, mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya soko la ndani ni tani 1,191,780 na nchi jirani ni tani 617,178. Mafuta yanayoingia rasmi katika soko la ndani yameongezeka kutoka wastani wa tani 160,000 kwa mwezi Mwaka 2011 hadi kufikia tani 198,000 kwa mwezi kati ya Januari, 2012. Mfumo huo umepunguza idadi ya siku ambazo meli inalipiwa gharama za *demmurage* kutoka siku 15 hadi siku 3 na kuboresha upatikanaji wa takwimu za mafuta nchini. Hata hivyo, utekelezaji wa mfumo huo unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kuingizwa kwa mafuta yenye kiasi kikubwa cha *ethanol.* Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali iliziagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)* na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* kudurusu viwango vya kiasi cha *ethanol* kwenye mafuta yanayoingizwa nchini na kufanya marekebisho katika Kanuni za Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja na makabrasha ya zabuni.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanza utekelezaji wa Kanuni na Mwongozo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja mwezi Januari, 2012, kumekuwepo na malalamiko mbalimbali. Malalamiko hayo ni pamoja na usimamizi wa zabuni za uagizaji mafuta kwa pamoja; kutokuwepo kwa Menejimenti ya *Petroleum Importation Co-ordinator Limited (PIC);* na Bodi ya PIC kusimamia shughuli zote ikiwemo kushiriki na kufanya maamuzi ya ununuzi. Kwa kutambua hilo, hatua kadhaa zilichukuliwa ikiwa ni pamoja na mapitio ya Mwongozo yaliyofanyika mwezi Mei, 2012 kwa kushirikisha wadau ili kuuboresha; *PIC* iliunda Kamati ya Zabuni ili kusimamia shughuli za ununuzi badala ya Bodi; na *PIC* pia iliajiri Menejimenti na wataalamu mbalimbali ili kusimamia shughuli zote za mfumo huo. Hatua hizi zitaboresha Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta wa Pamoja na kuondoa mgongano wa kimaslahi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mafuta ya Mwaka 2008 inaipa *TPDC* jukumu la kuanzisha na kusimamia Hifadhi ya Taifa ya Mafuta nchini *(National Strategic Petroleum Reserve).* Ili kufanikisha uanzishwaji wa Hifadhi ya Taifa ya Akiba ya Mafuta, Serikali iliamua kubadili matumizi ya ghala la kuhifadhia mafuta la *TIPER* kuwa ghala la forodha. Aidha, mwezi Mei, 2012 *TPDC* ilipokea mapendekezo ya kutoka Kampuni ya kitaifa ya Falme za Kiarabu ya *Emirates National Oil Company (ENOC)* ya kuingia mkataba wa kuanzisha Hifadhi ya Mafuta hapa nchini. Serikali imeunda kikosi kazi kwa ajili ya kupitia mapendekezo hayo. Kikosi kazi hicho kinaundwa na Wajumbe kutoka Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati na Madini, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *Consolidated Holdings*

*Corporation (CHC), EWURA* na *TPDC.* Kikosi kazi kitakamilisha kupitia mapendekezo ya Kampuni ya *ENOC* mwezi Agosti, 2012. Kiasi cha fedha kinachohitajika ni Shilingi bilioni 98.

Mheshimiwa Spika, *EWURA* imeendelea kudhibiti bei na kusimamia ubora wa baadhi ya bidhaa za petroli, dizeli na mafuta ya taa yanayouzwa nchini. Ili kukabiliana na tatizo la uchakachuaji, *EWURA* iliendelea kufanya ukaguzi wa kushtukiza; kuweka vinasaba kwenye mafuta yanayouzwa nchini; kutumia maabara zinazohamishika na kudhibiti matumizi ya mafuta ya ndege katika uchakachuaji. Aidha, katika Mwaka 2011/12, kati ya sampuli 115 zilizochukuliwa kwenye vituo vya mafuta ili kuhakiki ubora, sampuli 96 sawa na asilimia 83.5 zilithibitika kuwa na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuendeleza vyanzo mbalimbali vya nishati jadidifu, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini imeendelea kutoa kipaumbele katika kusambaza umeme kwenye maeneo yanayotoa huduma za kijamii. Ili kutekeleza azma hiyo, tathmini ya gharama za ufungaji wa nishati ya umeme wa jua zimefanyika na kubainika kuwa kwa wastani gharama za ufungaji mifumo ya umeme wa jua ni Shilingi milioni 12.4 kwa zahanati; Shilingi milioni 33.5 kwa kituo cha afya; Shilingi milioni 3.9 kwa shule yenye madarasa nane; na Shilingi milioni 12.5 kwa bweni.

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2012 *Millenium Challenge Acount Tanzania (MCA-T)* ilisaini mkataba

na Kampuni ya *Camco International (T) Limited* wa kutekeleza Mradi wa Umeme wa Jua *(Solar Energy)* wenye uwezo wa kW 235.6 katika vijiji 25 Mkoani Kigoma. Utekelezaji wa Mradi huo umeanza na utakamilika mwezi Agosti, 2013. Gharama ya Mradi huu ni Dola za Marekani milioni 4.75, sawa na Shilingi bilioni 7.60.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuhamasisha matumizi ya upepo kwa ajili ya kuzalisha umeme. Hadi sasa kampuni zilizojitokeza kuanzisha miradi ya kufua umeme kwa kutumia upepo ni *Geo-wind Power (T) Limited* (Kititimo - Singida), ambayo ni ya ubia kati ya *NDC, TANESCO* na *Power Pool East Africa Limited* wanaotarajiwa kuzalisha MW 50 kwa kuanzia na hatimaye kufikia MW 300; *Wind East Africa Limited* (Kititimo - Singida), ambayo ni ya ubia kati ya Kampuni za *Six Telecoms, Aldwych* na *IFC* wanaotarajiwa kuzalisha MW 100 utakapokamilika; na *Sino Tan Renewable Energy Limited* (Makambako - Iringa), ambayo itazalisha MW 100.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2011/12 Kampuni ya *Geo-wind Power (T) Limited* ilikamilisha ulipaji fidia kwa wananchi watakaopisha uendelezaji wa Mradi. Kampuni pia inaendelea na majadiliano na Benki ya Exim ya China ili kupata mkopo wa masharti nafuu kwa ajili ya kuendeleza Mradi huo. Aidha, Kampuni ya *Wind East Africa Limited* inafanya mashauriano na wananchi kwenye maeneo ya Mradi ili kupata ardhi.

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji wa Joto Ardhi (Geothermal): Baada ya utafiti wa kijiokemia na kijiofizikia katika eneo la Ziwa Ngozi (Wilaya ya Mbozi) kukamilika,Wizara itawezesha kuanza kwa uchorongaji wa visima viwili katika eneo hilo. Katika Mwaka 2012/13, Wizara imetenga Shilingi bilioni moja ili kuanza kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2011/12, Wizara iliandaa Rasimu ya Sera Biofuel Kimiminika *(Liquid Biofuel Policy)* ili kuendeleza *biofuel* nchini. Pia, Wizara iliandaa Hadidu za Rejea kwa ajili ya kumpata mshauri atakayeainisha maeneo maalumu *(agro-ecological zoning)* ya uendelezaji wa *Biofuel* Kimiminika.

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza vyanzo vingine vya nishati, Wizara ilibainisha maeneo 12 ya maporomoko madogo ya maji kwa ajili kuzalisha umeme katika Wilaya za Kilombero, Kilosa, Morogoro Vijijini na Mvomero Mkoani Morogoro. Pia, Wizara iliwezesha ujenzi wa mitambo ya *biogas* 1,500 kwa ajili ya kupikia majumbani katika Kanda ya Kaskazini kupitia Programu ya *Biogas* inayofadhiliwa na Serikali ya Uholanzi.

Mheshimiwa Spika, Ukuaji na Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa: Kiwango cha ukuaji wa shughuli za Sekta ya Madini nchini kwa Mwaka 2011 kilikuwa asilimia 2.2 ikilinganishwa na asilimia 2.7 Mwaka 2010. Aidha, mchango wa Sekta hiyo katika Pato la Taifa kwa Mwaka 2011 ulikuwa asilimia 3.3 kama ulivyokuwa Mwaka 2010. Kupungua kwa ukuaji na kutoongezeka kwa mchango wa Sekta ya Madini kumetokana na sababu mbalimbali zikiwemo

kusitishwa kwa uzalishaji wa almasi katika shimo kuu *(main pit)* la Mgodi wa Mwadui kwa takriban mwaka mzima kutokana na ukarabati wa mitambo kwenye mgodi huo; na kupungua kwa uzalishaji wa dhahabu katika Migodi ya Tulawaka na Golden Pride ambayo inakaribia kufungwa.

Mheshimiwa Spika, thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 1,508.7 Mwaka 2010 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 1,980.2 Mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 31.3. Ongezeko hilo lilichangiwa na kupanda kwa bei ya dhahabu ambayo ilikuwa ya wastani wa Dola za Marekani 1,571.28 kwa wakia Mwaka 2011 kutoka wastani wa Dola za Marekani 1,224.53 kwa wakia Mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 28.3. Asilimia 95 ya mauzo ya madini yote nje ya nchi ilichangiwa na mauzo ya dhahabu, ambapo thamani ya mauzo yake iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 1,436.2 Mwaka 2010 hadi Dola za Marekani milioni 1,879.62 Mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 31. Asilimia kubwa ya dhahabu inayozalishwa na migodi mikubwa Tanzania inauzwa nchi za Afrika Kusini, China, Japan na Switzerland.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uzalishaji na mauzo ya madini katika migodi mikubwa nchini katika kipindi cha Julai, 2011 hadi Juni, 2012 jumla ya wakia milioni 1.3 za dhahabu, wakia 391,522 za fedha na ratili milioni 13.3 za shaba zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi kutoka migodi mikubwa ya Bulyanhulu, Buzwagi, Geita, Golden Pride, North Mara na Tulawaka. Jumla ya thamani ya madini hayo ni Dola za Marekani bilioni

2.2. Vilevile, jumla ya karati 59,894 za almasi na karati 613,851 za Tanzanite zilizalishwa na migodi ya Mwadui na *TanzaniteOne*. Aidha, karati 73,737 za *Tanzanite* iliyokatwa na gramu milioni 4.9 za *Tanzanite* ghafi zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 10.03 ziliuzwa nje ya nchi na mgodi wa *TanzaniteOne,* wakati karati 44,254 za almasi zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 10.01 ziliuzwa nje ya nchi na mgodi wa Mwadui. Jumla ya mrabaha uliolipwa Serikalini na wamiliki wote wa migodi mikubwa nchini katika kipindi hicho ni Dola za Marekani milioni 62.03.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha *TANSORT* pia kilithamini almasi za kampuni 17 zinazozalisha na kufanya biashara ya almasi nchini. Jumla ya karati 52,600 za almasi zilizouzwa nje ya nchi zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 13.03 zilithaminishwa. Almasi inayozalishwa katika Mgodi wa Mwadui inauzwa Antwerp nchini Ubelgiji na soko kuu la almasi inayozalishwa na migodi mingine ni Afrika Kusini, Dubai, India, Israel na Russia.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2011/12, Serikali iliahidi kukamilisha majadiliano na wamiliki wa migodi mikubwa yenye mikataba *(MDAs)* ili walipe mrabaha kulingana na viwango vilivyopo katika Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imetekeleza ahadi hii ambapo kampuni zote zinazomiliki migodi mikubwa ya dhahabu nchini zimeanza kulipa kiwango kipya cha mrabaha cha asilimia nne ya mapato kabla ya kutoa gharama *(Gross Value)* badala ya asilimia tatu ya *Net Back Value* kuanzia tarehe 1 Mei, 2012. Kampuni hizo ni

*African Barrick Gold* inayomiliki migodi ya dhahabu ya Bulyanhulu, Buzwagi, North Mara na Tulawaka; Kampuni ya *Resolute Tanzania* inayomiliki mgodi wa dhahabu wa *Golden Pride*; na Kampuni ya *Geita Gold Mining Limited* inayomiliki mgodi wa dhahabu wa Geita. Kutokana na migodi mikubwa kuanza kulipa kiwango kipya cha mrabaha, Serikali inatarajia kukusanya mapato ya ziada ya Shilingi bilioni 30 katika Mwaka 2012/13.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 inaelekeza kuundwa kwa Bodi ya Ushauri ya Madini kwa ajili ya kumshauri Waziri mwenye dhamana ya madini masuala mbalimbali kuhusu maendeleo ya sekta. Bodi hiyo inatakiwa kuhusisha wadau muhimu wa sekta wakiwemo, wawakilishi wa wachimbaji wadogo na wakubwa na pia wafanyabiashara wa madini. Napenda kulitaarifu Bunge lako kuwa, Bodi hiyo imeundwa na kuzinduliwa rasmi tarehe 5 Aprili, 2012.

Mheshimiwa Spika, shughuli za utoaji wa leseni za madini nchini zimeendelea kuimarishwa na kuboreshwa, ambapo leseni za uchimbaji mdogo na biashara ya madini zimeanza kutolewa na Maafisa Madini wa Kanda kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Hatua hiyo imesaidia kupunguza mrundikano wa maombi ya leseni za uchimbaji mdogo katika Ofisi ya Makao Makuu ya Wizara na unalenga kuongeza kasi ya utoaji leseni kwa ujumla. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini *(Mining Cadastral Information Management System – MCIMS)* kwa

kuongeza kasi ya mawasiliano ya mtandao wa kompyuta; kutoa mafunzo kwa watendaji; na kuboresha mfumo wa kuingiza takwimu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka 2011/12, jumla ya maombi 13,562 ya utafutaji na uchimbaji madini yalipokelewa na kuingizwa kwenye Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini, ikilinganishwa na maombi 5,921 katika Mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 129. Kati ya maombi yaliyopokelewa, maombi 11,245 yalikuwa ni ya leseni ndogo za uchimbaji madini; maombi 65 ni ya uchimbaji wa kati; na maombi 2,252 ni kwa ajili ya leseni za utafutaji mkubwa wa madini. Aidha, jumla ya leseni 11,113 zilitolewa, kati ya hizo leseni 9,997 zilikuwa ni za uchimbaji mdogo, leseni 19 za uchimbaji wa kati na leseni 1,097 kwa ajili ya utafutaji mkubwa wa madini. Maombi ya leseni 334 yalikataliwa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na utoaji wa leseni, Wizara imechukua hatua za kutoa taarifa ya makosa *(default notice)* kwa wamiliki wa leseni za utafutaji madini ambao hawatimizi masharti ya leseni. Utekelezaji wa hatua hiyo ulianza mwezi Machi, 2012 kwa kutoa taarifa kupitia kwenye matangazo magazetini, ambapo jumla ya leseni za utafutaji 888 zilihusika. Kwa mujibu wa matangazo hayo, wamiliki wa leseni walitakiwa kurekebisha makosa yao ndani ya siku 30 kabla ya hatua za kisheria kuchukuliwa. Katika kipindi hicho, wamiliki wa leseni 246 walirekebisha makosa yao na wamiliki wa leseni 642 walipewa taarifa ya makosa ya siku 60 kwa mujibu wa Sheria. Wamiliki wa leseni zilizopewa taarifa za makosa na

walioshindwa kurekebisha makosa yaliyobainishwa watafutiwa leseni zao na watatakiwa kulipa madeni husika. Maeneo ambayo leseni zitafutwa, yatagawiwa kwa waombaji wapya ili kuyaendeleza ama kutengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo ili kuongeza wigo wa kutoa ajira kwa vijana. Aidha, leseni zote za madini ambazo zimekuwa hazifanyiwi kazi kwa muda mrefu, zitafutwa ifikapo mwishoni mwa mwezi Disemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, katika siku za karibuni, kumejitokeza biashara haramu ya madini inayofanywa na watu wasiokuwa waaminifu kwa kutumia nyaraka zisizo halali ikiwemo leseni za biashara ya madini. Kufuatia hali hiyo, Serikali ilitoa matangazo kwa umma kuhusu biashara hiyo na kushauri wanunuzi wa madini kushirikisha Ofisi za Madini zilizo karibu nao wakati wanafanya biashara hizo. Aidha, kutokana na matukio hayo, kuanzia tarehe 1 Julai, 2012 Wizara yangu imeanza kutoa leseni za biashara ya madini zisizoweza kughushiwa kirahisi. Napenda kuutaarifu umma kupitia Bunge lako Tukufu kuwa, mmiliki wa leseni au kampuni, ambayo itajihusisha na biashara haramu ya madini kwa njia yoyote, leseni yake itafutwa mara moja na wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji mdogo ni mojawapo ya vyanzo muhimu vya ajira nchini, hususan, maeneo ya vijijini. Katika Mwaka 2011/12 Serikali ilitenga na kutoa leseni katika maeneo ya Itandula Wilayani Tarime lenye ukubwa wa hekta 37 na Mbesa Wilayani Tunduru lenye hekta 15,605 kwa ajili ya uchimbaji mdogo. Eneo la Itandula limegawiwa kwa vikundi vya wachimbaji wadogo vilivyoundwa. Vilevile,

Serikali iliendelea kubainisha maeneo mengine yanayofaa kwa ajili ya uchimbaji mdogo yakiwemo Mogabiri, Nyakunguru na Goronga-Gibaso yenye jumla ya hekta 287.70 yaliyopo Wilayani Tarime.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 56(d) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010, pamoja na mambo mengine, inahimiza kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata mikopo na mitaji kwa kuanzisha mifuko maalumu. Kwa kuzingatia maelekezo hayo, katika Mwaka 2011/12 Serikali ilitenga Shilingi bilioni 1.19 kwa ajili ya Mfuko wa Kuendeleza Wachimbaji Wadogo wa Madini. Fedha hizo zimetumika kwa ajili ya ukopeshaji na ukodishaji wa vifaa kwa wachimbaji wadogo katika maeneo ya Rwamugaza Wilayani Geita kupitia *STAMICO;* Londoni Wilayani Manyoni kupitia Kampuni ya *Tan Discovery Mineral Consultancy*; na Pongwe Msungura Wilayani Bagamoyo kupitia Kampuni ya Kilimo *General Supplies Ltd*. Kituo cha kuwaendeleza wachimbaji wadogo kitakachoendeshwa na *STAMICO* eneo la Rwamugaza Mkoani Geita kitanufaisha wachimbaji wadogo wapatao 1,300 wanaofanya kazi katika maeneo ya Rwamugaza, Nyarugusu na Nyakagwe.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kituo cha kuendeleza wachimbaji wadogo kilichopo eneo la Londoni Mkoani Singida kwa kushirikiana na *GST,* kimeratibu *magnetic survey* kwa viwanja 22 vya wachimbaji wadogo katika maeneo ya Londoni na Sambaru. Hii ni hatua ya awali na muhimu ya kuwasaidia wachimbaji wadogo ili kubaini mashapo yenye dhahabu katika maeneo ya leseni zao. Hali hii

inasaidia kufanya uchimbaji wao kuwa wa uhakika katika uzalishaji na kuwezesha kumudu gharama za ukodishaji wa zana. Lengo ni kuwanufaisha zaidi ya wachimbaji wadogo 13,400 katika maeneo ya Londoni na Sambaru.

Mheshimiwa Spika, Kampuni za *Gemstyle* na *CE Holdings* nazo zilipata mkopo kupitia Mfuko wa Kuendeleza Wachimbaji Wadogo kwa ajili ya kuendeleza mradi wa usanifu na uongezaji thamani madini. Vituo hivyo vinaendeshwa na vikundi vya wanawake. Kupitia mkopo huo, Kampuni ya Gemstyle imeongeza idadi ya mashine za kuongeza thamani kutoka tatu hadi sita na kutoa mafunzo kwa wachimbaji 30 katika shughuli za uongezaji thamani madini.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2011/12, Wizara yangu ilitoa mafunzo kuhusu Sera ya Madini ya Mwaka 2009, Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Kanuni zake, taratibu za umiliki wa leseni mbalimbali za madini na elimu ya ujasiriamali kwa wachimbaji wadogo wapatao 380 katika Mikoa ya Kigoma, Lindi, Manyara, Morogoro, Singida na Tabora.

Mheshimiwa Spika, tarehe 23 Juni, 2012 nilikutana na wawakilishi wa wachimbaji wadogo kutoka nchi nzima kwa lengo la kujadiliana namna ya kuendeleza uchimbaji mdogo nchini. Katika mkutano huo changamoto mbalimbali zinazowakabili wachimbaji wadogo zikiwemo ukosefu wa vifaa vya kisasa na maeneo ya kutosha kwa uchimbaji mdogo zilijadiliwa na kuwekewa mkakati wa kuzitatua. Wachimbaji

wadogo waliagizwa kuimarisha vyama vyao vya uchimbaji kuanzia ngazi ya Wilaya, Mikoa hadi Taifa. Aidha, Wizara iliridhia kukutana na wachimbaji wadogo mwezi Disemba kila mwaka kwa ajili ya kutathmini maendeleo na changamoto za wachimbaji wadogo. Mpango Kazi wa kuboresha uchimbaji mdogo nchini unaotayarishwa na Serikali kupitia *STAMICO* utajadiliwa na kikao cha wachimbaji wadogo cha mwezi Disemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, Uimarishaji wa Masoko ya Madini na Vito: Sera ya Madini ya Mwaka 2009 inasisitiza uboreshaji wa mfumo wa masoko ya madini. Ili kufikia azma hiyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Chama cha Wafanyabiashara wa Madini – *TAMIDA* iliandaa Maonesho ya Kwanza ya Kimataifa ya Vito na Usonara, mjini Arusha yaliyofanyika kuanzia tarehe 26 - 29 Aprili, 2012.

Mheshimiwa Spika, maonesho hayo yalihudhuriwa na jumla ya washiriki 777, wakiwemo wanunuzi 300 waliowakilisha kampuni 200 kutoka nchi 25; waoneshaji *(exhibitors)* 125; na washiriki binafsi wapatao 75. Kampuni za Kitanzania zilizoshiriki katika uoneshaji *(exhibition)* katika maonesho hayo zilikuwa 39 kati ya 45. Wafanyabiashara wa ndani walipata fursa ya kutangaza madini yanayopatikana nchini na pia kukutana na Wafanyabiashara wa Kimataifa. Katika kipindi cha siku tatu za maonesho hayo, madini yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 3.88, sawa na takriban Shilingi bilioni 6.21 yaliuzwa na mrabaha wa Shilingi milioni 271.57 ulilipwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kuhakikisha kuwa shughuli za uchimbaji madini zinaendeshwa kwa kuzingatia Kanuni za usalama, afya na utunzaji wa mazingira, kwa kipindi cha Mwaka 2011/12, Wizara ilifanya ukaguzi wa kina katika migodi mikubwa minane ya Bulyanhulu, North Mara, Geita, Williamson Diamond, Golden Pride, Buzwagi, Tulawaka na TanzaniteOne. Aidha, ukaguzi wa kina wa shughuli za utunzaji wa mazingira katika maeneo ya migodi ulifanyika kwenye migodi 34 ya wachimbaji wadogo na migodi 19 ya wachimbaji wa kati.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utunzaji wa mazingira, wamiliki wa migodi mikubwa yote wanatakiwa kuwasilisha mipango ya ufungaji migodi *(Mine Closure Plans)* kwa mujibu wa Kanuni za Usalama, Afya na Utunzaji wa Mazingira, ikiwa ni utekelezaji wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, inayowataka vilevile kuweka dhamana ya fedha za kukarabati mazingira *(rehabilitation bond)*. Hadi sasa wamiliki wa migodi minane wamewasilisha mipango yao ya ufungaji migodi ambayo inawezesha kufahamu gharama zinazotakiwa kwa ajili ya kuweka dhamana ya ukarabati wa mazingira. Migodi hiyo ni Bulyanhulu, Buzwagi, Geita, Golden Pride, Mwadui, North Mara, Tanzanite One na Tulawaka. Kamati ya Kisekta ya Kitaifa imepitia mipango hiyo na kuidhinisha mpango wa ufungaji wa mgodi wa Golden Pride. Migodi iliyobaki imeelekezwa kurekebisha mipango yake ya ufungaji migodi na kuwasilisha tena kwa Kamati hiyo kwa majadiliano.

Mheshimiwa Spika, madini ya urani yanapatikana maeneo mbalimbali nchini yakiwemo Mto Mkuju (Wilaya za Liwale, Namtumbo na Tunduru); Bonde la Bahi (Wilaya ya Bahi) na Manyoni (Mkoa wa Singida); Gallapo na Minjingu katika Bonde la Ufa. Hata hivyo, ni maeneo ya Wilaya za Namtumbo na Manyoni tu ambayo kwa sasa yamethibitishwa kuwa na kiasi cha kutosha kuweza kuchimbwa kibiashara. Mradi wa urani uliopo Wilayani Namtumbo utaendelezwa na Kampuni ya Mantra Tanzania Limited na kiasi cha mashapo tani milioni 101.4 za urani yamethibitishwa. Gharama za awali za uwekezaji katika mradi huo zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 450, sawa na Shilingi bilioni 720.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya eneo la Mradi wa Namtumbo ipo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya *Selous Game Reserve*, ambayo ni miongoni mwa maeneo ya urithi wa Dunia *(WHC).* Kutokana na sababu hiyo, Serikali iliwasilisha *UNESCO* maombi ya kurekebisha mipaka ya eneo la Urithi wa Dunia ili kuongeza eneo la mradi.  Katika kikao cha Kamati ya *UNESCO* ya Urithi wa Dunia kilichofanyika Saint Petersburg (Urusi) tarehe 2 Julai, 2012, ombi la Tanzania liliridhiwa.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na Kanuni za Madini ya Mionzi Ayonisha za Mwaka 2010 - *the Mining (Radioactive Minerals) Regulations, 2010* chini ya Sheria ya Madini, 2010 zinatumika katika kusimamia shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini ya urani nchini. Sheria na Kanuni zote zilizotungwa na zitakazoendelea kutungwa zinazohusiana na usimamizi wa madini ya urani pamoja na mambo mengine

zinalenga kuzingatia miongozo/taratibu za Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *(IAEA)* za usimamizi wa madini hayo zinazohakikisha kuwa uchimbaji hauleti athari kwa binadamu na mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2011/12 Wizara iliendelea kusimamia shughuli za uingizaji, usafirishaji, uhifadhi na ukusanyaji wa takwimu za baruti na matumizi yake katika Sekta ya Madini. Usimamizi huu umewezesha Wizara kupata taarifa sahihi za kiasi cha baruti kilichoingizwa na kutumika hapa nchini. Katika kipindi hicho, tani 26,865 za baruti ziliingizwa nchini na kutumika katika shughuli za migodi; vyeti vya kulipua baruti 163 na leseni 18 za maghala ya kuhifadhi baruti vilitolewa. Aidha, Wizara iliendesha mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya baruti katika Mikoa ya Lindi na Kigoma kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, Asasi ya Kimataifa ya Extractive Industries Transparency Initiative (EITI) huzitaka nchi zilizo katika hatua za awali za kujiunga kufanya tathmini kuonesha iwapo utekelezaji wa vigezo vya uwazi vimefikiwa. Katika kutimiza hitaji hili, Kamati Tekelezi ya *TEITI* iliajiri mhakiki *(validator)* mwezi Januari, 2011. Taarifa ya mhakiki iliwasilishwa kwenye Bodi ya *EITI* tarehe 15 Mei, 2011 kwa ajili ya kutolewa uamuzi. Bodi ya *EITI* ilionesha kuridhishwa na taarifa hiyo. Hata hivyo, vigezo vitano kati ya 18 havikukamilika kuiwezesha Tanzania kuwa mwanachama kamili.

Mheshimiwa Spika, vigezo hivyo vitano ni kuwepo na fomu maalumu inayoonesha malipo yote ya mapato yanayofanyika; uwepo wa sheria

inayoelekeza kampuni za madini, mafuta na gesi kutoa taarifa za malipo ya mapato yaliyofanyika Serikalini; uthibitisho wa takwimu za mapato zilizotolewa na Taasisi za Serikali kuwa zimekaguliwa kwa viwango vya kimataifa; uthibitisho kwamba malipo yote ya kampuni za madini, mafuta na gesi asili yamewasilishwa kwa *reconciler;* na uthibitisho kwamba malipo yote yaliyopokelewa na Serikali yamewasilishwa kwa *reconciler*. Bodi kwa kutambua jitihada iliyofanyika iliiongezea nchi yetu muda wa awali wa uanachama kwa miezi mingine 18 hadi tarehe 15 Februari, 2013. Katika kipindi hicho Tanzania itatakiwa iwe imekamilisha vigezo vyote vya kuiwezesha kupata uanachama kamili.

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2012 Kamati ilikamilisha taarifa ya uchambuzi na uandaaji wa mapendekezo ya sheria ya usimamizi wa shughuli za *TEITI.* Taarifa hiyo kabla ya kukamilishwa, ilijadiliwa na wadau mwezi Septemba, 2011 na Machi, 2012. Kamati Tekelezi inakamilisha maandalizi ya kutoa elimu kuhusu shughuli za *TEITI* ili kuwafikia wananchi wengi zaidi nchini, hasa katika wilaya zilizo na shughuli za uchimbaji wa madini na gesi asili ili kupata maoni yatakayozingatiwa wakati wa uandaaji wa Sheria ya *TEITI.*

Mheshimiwa Spika, taarifa ya pili ya *TEITI* ya ulinganisho wa malipo na mapato yanayotokana na shughuli za uchimbaji madini na gesi asili kwa hesabu za Mwaka 2009/10 ilikamilika na kutolewa kwa umma tarehe 31 Mei, 2012. Matokeo yanaonesha kuwa malipo yaliyopokelewa Serikalini ni Shilingi bilioni 419

ikilinganishwa na Shilingi bilioni 424 zilizolipwa na kampuni za utafutaji na uchimbaji madini, mafuta na gesi asili. Tofauti hiyo ya Shilingi bilioni tano ni ndogo ikilinganishwa na tofauti ya Shilingi bilioni 46.5 iliyoainishwa katika taarifa ya kwanza ya *TEITI.* Hali hii inaonesha maboresho makubwa katika usahihi wa takwimu za malipo kati ya Serikali na kampuni husika.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango wa *EITI* umekuwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ucheleweshaji wa upatikanaji wa takwimu za malipo kutoka kwa baadhi ya wadau wanaotakiwa kuwasilisha taarifa hizo. Hali hii huathiri utoaji wa taarifa za ulinganisho wa malipo na mapato kwa wakati. Natoa wito kwa wadau hao kuwasilisha takwimu husika zinapohitajika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Sekta ya Madini imekuwa ikileta manufaa mbalimbali kwa Taifa, wananchi wengi bado wameendelea kuwa na mtazamo hasi juu ya sekta hiyo. Mtazamo huo unatokana na wananchi kutofahamu kwa kina manufaa yanayotokana na shughuli za uchimbaji madini nchini, ambapo wengi hufikiri faida inayopatikana ni mrabaha pekee. Ukweli ni kwamba, yapo manufaa mengi zaidi ya malipo ya mrabaha.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Mwaka 2005 hadi 2011 manufaa mbalimbali yamepatikana kutokana na uwekezaji wa migodi mikubwa ya madini, ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa mapato ya Serikali kutokana na kodi mbalimbali kutoka Shilingi bilioni 37.16 hadi kufikia Shilingi bilioni 208.68; kuongezeka kwa ajira

ya Watanzania kutoka 3,360 hadi kufikia 7,753; kuongezeka kwa ununuzi wa bidhaa na huduma za ndani unaofanywa na migodi hiyo kutoka Dola za Marekani milioni 237.97 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 379.57; na kuongezeka kwa mrabaha unaolipwa Serikalini kutoka Dola za Marekani milioni 15.8 hadi Dola za Marekani milioni 57.5.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu zilizopo, wastani wa gharama za uzalishaji kwa wakia moja ya dhahabu ni Dola za Marekani 520. Kwa sasa mgawanyo wa mapato ya migodi mikubwa ni pamoja na mrahaba na kodi mbalimbali asilimia nane ya mapato; gharama za uzalishaji ni asilimia 57 ya mapato; marejesho ya mitaji/mikopo na riba ni asilimia 19.5 ya mapato; faida na gawio kwa wanahisa ni asilimia 15 ya mapato; na gharama za miradi ya huduma za jamii ni asilimia 0.5 ya mapato.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizo zinatoa taswira nzima ya mapato yatokanayo na shughuli za migodi mikubwa ya dhahabu nchini. Napenda kusisitiza kuwa mapato ya Serikali yanatarajiwa kuendelea kuongezeka kadiri migodi inavyokamilisha kurejesha mitaji na kuanza kulipa kodi ya mapato. Serikali itaendelea kuimarisha ukaguzi na uhakiki wa hesabu za fedha za migodi ili kuhakikisha kuwa migodi hiyo inalipa kodi na mrabaha stahiki.

Mheshimiwa Spika, Duniani kote migodi mikubwa inajizatiti katika utoaji wa huduma za jamii kwa hiari kwenye jamii inayozunguka mgodi na maeneo mengine kwenye nchi husika. Migodi mikubwa iliyopo

nchini imekuwa ikitoa huduma hizo katika nyanja za afya, elimu, maji, utunzaji wa miundombinu, utunzaji wa mazingira na uwezeshaji kiuchumi. Katika kipindi cha kuanzia Mwaka 1998 hadi 2011, migodi mikubwa nchini imetumia takriban Dola za Marekani milioni 38.6 kwa ajili ya huduma za jamii, sawa na asilimia 0.5 ya mapato yote ya migodi. Uzoefu wa kimataifa unaonesha kuwa, migodi mikubwa katika mataifa mbalimbali imekuwa ikitumia kati ya asilimia 0.3 hadi 2 ya mapato yake kwenye huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuthamini mchango unaotolewa na migodi katika eneo hilo. Serikali imeendelea kuhimiza migodi kuongeza mchango wake zaidi katika eneo hilo. Aidha, Serikali inaandaa mwongozo wa Kitaifa kuhusu huduma za jamii zitolewazo na migodi ili kutoa msukumo zaidi kwa migodi kutimiza wajibu wao na kuhakikisha kuwa, miradi ya huduma za jamii inayotekelezwa na migodi inakuwa shirikishi na inayozingatia vipaumbele vya jamii husika. Mwongozo huo utakamilika katika Mwaka 2012/13.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2011/12, Wizara iliendelea kukarabati na kujenga ofisi za madini ili kuboresha mazingira ya utendaji kazi. Katika kipindi hicho ujenzi wa Ofisi ya Madini ya Kanda ya Kati (Singida) ulikamilika na ukarabati wa Ofisi ya Madini Kanda ya Kati - Magharibi (Shinyanga) ulianza.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania *(TMAA)* uliendelea kutekeleza majukumu yake na kuwezesha kupatikana kwa mafanikio

mbalimbali, ambapo katika kipindi cha Julai, 2011 hadi Juni, 2012 Mgodi wa *Golden Pride* uliopo Nzega unaomilikiwa na Kampuni ya *Resolute* umelipa kiasi cha Shilingi bilioni 37.2 kama kodi ya mapato *(corporate tax).* Hivyo, jumla ya kodi ya mapato iliyolipwa na mgodi huo tangu uanzishwe hadi sasa ni Shilingi bilioni 71.1. Katika kipindi hicho, Mgodi wa Dhahabu wa Geita unaomilikiwa na Kampuni ya AngloGold Ashanti umelipa jumla ya Shilingi bilioni 188.1 kama kodi ya mapato. Hivyo, jumla ya kodi ya mapato iliyolipwa na mgodi huo tangu uanzishwe ni Shilingi bilioni 191.3. Kiasi hicho cha kodi ya mapato kisingefikiwa endapo kazi ya ukaguzi wa gharama za uwekezaji na uendeshaji isingefanywa na *TMAA* kwa kushirikiana na *TRA.*

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kuiwezesha *STAMICO* kutekeleza majukumu yake. Mwezi Oktoba, 2011 Shirika lilisaini makubaliano na Kampuni ya *Tanzanian American International Development Corporation (2000) – TANZAM 2000 Limited* kwa ajili ya kufufua upya Mgodi wa Dhahabu wa Buckreef Mkoani Geita. *STAMICO* inamiliki hisa asilimia 45 na ina Wajumbe katika Bodi ya Wakurugenzi na katika Kamati ya Kusimamia Utekelezaji wa Mradi. Mbali ya kodi na mrabaha, Serikali kupitia *STAMICO* itanufaika kwa kupata gawiwo la faida kutokana na asilimia 45 za hisa katika mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kwanza iliyochukuliwa na kampuni ya ubia imekuwa kuendeleza upembuzi yakinifu unaojumuisha uchorongaji miamba kwa lengo la kuthibitisha

mashapo zaidi. Hadi mwishoni mwa mwezi Juni, 2012 mashapo yaliyopatikana yalikuwa wakia milioni 2.72 za dhahabu. Kiasi hiki cha dhahabu kina thamani ya Dola za Marekani bilioni 4.35, sawa na Shilingi bilioni 6,963.20 kwa wastani wa bei ya dhahabu ya Dola za Marekani 1,600 kwa wakia. Aidha, katika kipindi hicho *STAMICO* iliingia ubia wa hisa asilimia 50 kwa 50 na *Obtala Resources* kwa ajili ya kufungua migodi ya dhahabu yenye ukubwa wa kati kwa ubia na Watanzania wenye leseni na kuendesha vituo vya kununulia dhahabu.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2011 *STAMICO* ilikabidhiwa eneo la Mgodi wa Buhemba. Baada ya kukabidhiwa eneo hilo, *STAMICO* iliweka ulinzi shirikishi kwa kuwatumia wananchi wa Kata za Buhemba na Mirwa. Vigezo vya kumpata mbia viliandaliwa, ambapo *STAMICO*, kwa niaba ya Serikali, itabaki na hisa zisizopungua asilimia 40. Vilevile, *STAMICO* itapata gawio la asilimia 30 la dhahabu itakayozalishwa kutokana na marudio ya mabaki ya uchimbaji wa zamani. Jumla ya kampuni 42 zilijitokeza kuomba ubia na *STAMICO* na zote zilialikwa kwenye zabuni. Hata hivyo, ni kampuni 11 tu ndizo zilizowasilisha zabuni. Uchambuzi wa zabuni hizo unaendelea chini ya kamati ya wataalamu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2011/12 Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST),* ulipima na kuchora ramani mpya nne za jiolojia za *QDS* 194, 212 na 230 zilizoko Chunya na *QDS* 148 iliyoko Kilindi. Wakala pia ulipima na kuchora ramani mpya mbili za jiokemia za *QDS* 212 na 230. Aidha, ramani 53 za zamani za mfumo wa *QDS*

zilibadilishwa kutoka kwenye mfumo wa karatasi na kuzifanya kuwa kwenye mfumo wa *digital.*

Mheshimiwa Spika, Wakala kwa kupitia ufadhili wa *African Array Program* ulipata msaada na kufunga vituo viwili vipya vya kupimia matetemeko ya ardhi katika maeneo ya Geita na Mtwara ambavyo vyote vilifungwa pamoja na *Differential Global Positioning Systems.* Aidha, takwimu za matukio ya matetemeko ya ardhi ziliendelea kukusanywa katika vituo hivyo viwili vipya pamoja na vile vya zamani vilivyoko Dodoma, Kibaya, Kondoa, Babati, Mbeya, Singida na Manyoni. Wakala ulifanya utafiti wa kina wa upatikanaji wa nishati ya jotoardhi *(geothermal energy)* katika eneo la Ziwa Ngozi na kubainisha maeneo matatu yanayofaa kuchoronga mashimo ya kina kirefu ya kupimia kiasi cha joto katika eneo hilo. Pia, utafiti wa upatikanaji wa madini kwa kutumia *Satelite Palsar Radar Images* ulifanyika kwa ufadhili wa *Japan Oil Gas and Metals Corporation (JOGMEC).* Kutokana na matokeo ya utafiti huo, maeneo yatakayopewa kipaumbele kwa ufuatiliaji wa kina ni pamoja na Nachingwea, Kilosa, Mpwapwa na Simbanguru – Mazoka (Manyoni).

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2011/12, Chuo cha Madini – Dodoma kiliendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Cheti na Stashahada kwa jumla ya wanafunzi 240 katika fani za Jiolojia na Utafutaji Madini *(Geology and Mineral Exploration)*; Uhandisi Migodi *(Mining Engineering)* na Uhandisi Uchenjuaji Madini *(Mineral Processing Engineering).* Jumla ya wanafunzi 55 walihitimu katika fani za *Geology and Mineral Exploration* (20); *Mining Engineering* (21); na *Mineral*

*Processing Engineering* (14). Aidha, Chuo kiliandaa mitaala ya ngazi za stashahada katika fani za Uhandisi na Usimamizi wa Mazingira Migodini; na Jiolojia ya Mafuta na Gesi na kuiwasilisha *NACTE* kwa ajili ya kupata uhalali na ithibati *(accreditation).*

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya muda mfupi yameendelea kutolewa kwa wataalamu wanaofanya kazi katika migodi mbalimbali nchini, ikiwemo migodi ya dhahabu ya North Mara na Geita. Pia, Chuo kimeendelea kuainisha matatizo ya wachimbaji wadogo katika maeneo ya Nyarugusu, Lwenge na Rwamugaza. Lengo ni kuanza kutoa mafunzo ya umahiri katika Mwaka 2012/13 ili kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Chuo kinakabiliwa na changamoto mbalimbali, hususan madarasa na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Uzoefu kutoka nchi mbalimbali duniani unaonesha kuwa ili kufanya kazi kwa ufanisi, mtaalamu mmoja anapaswa kufanya kazi na mafundi watano wa kumsaidia (uwiano wa 1:5). Kwa hapa nchini hali hiyo haipo kwa kuwa kuna vyuo vikuu viwili (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma) vinavyotoa wataalamu wa fani za madini katika ngazi ya shahada ambapo wastani wa wahitimu 180 hutolewa kila mwaka. Ili kufikia uwiano huo, Chuo cha Madini kitaendelea kuboresha miundombinu ili kuwa na uwezo wa kutoa wahitimu wasiopungua 900 kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Utafiti na Uendelezaji wa Sekta ya Madini cha *Southern and Eastern African Mineral Centre (SEAMIC)*. kilichopo Kunduchi, Jijini Dar

es Salaam, kimeendelea kutoa mafunzo na huduma za kitaalamu kwa Sekta za Madini za Nchi Wanachama na sekta binafsi zinazowekeza katika madini. Nchi Wanachama wa *SEAMIC* ni Angola, Comoro, Ethiopia, Kenya, Msumbiji, Sudan, Tanzania na Uganda. Aidha, Kikao cha Mawaziri wa Madini wa nchi wanachama kilifanyika Jijini Dar es Salaam mwanzoni mwa mwezi Juni, 2012 katika utaratibu wa kila mwaka wa kukutana kutathmini utendaji wa kituo hicho. Katika mkutano huo, Tanzania iliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kikao cha Mawaziri wa *SEAMIC* na kupewa jukumu la kusimamia shughuli za kituo kwa kipindi cha Mwaka 2012/13, wakati Sudan ilichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti na kupewa jukumu la kuandaa mkutano ujao wa Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya madini utakaofanyika mwezi Mei, 2013 Jijini Khartoum, Sudan. Kutokana na Kituo hiki wadau wa Sekta ya Madini wananufaika kwa kupeleka sampuli mbalimbali kwa ajili ya kufanyiwa utambuzi wa madini yaliyomo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira na maendeleo ya watumishi, katika Mwaka 2011/12 Wizara ilidurusu muundo wa utendaji kazi ili kuongeza ufanisi wa shughuli zake. Katika muundo huo, sehemu mbili zimeongezwa ambazo ni Sehemu ya Uongezaji Thamani Madini iliyopo chini ya Idara ya Madini na Sehemu ya Matumizi ya Gesi iliyopo chini ya Idara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza tija na motisha kwa watumishi, katika Mwaka 2011/12 Wizara iliwapandisha vyeo watumishi 80, kuthibitisha kazini watumishi 63 na kuwabadilisha kazi watumishi watatu.

Aidha, Wizara iliwapeleka mafunzoni jumla ya watumishi 112 katika fani mbalimbali. Kati ya hao, 33 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na 79 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuelewa na kuthamini mchango wa watumishi wanapokuwa na afya njema, Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe, chakula na madawa maalumu kwa watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (VVU) na wenye UKIMWI kama inavyoagizwa na Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa Mwaka 2006. Wizara itaendelea kutoa huduma hizo ikiwa ni pamoja na huduma ya upimaji wa hiari wa VVU kwa watumishi. Aidha, elimu juu ya masuala ya UKIMWI itaendelea kutolewa kwa watumishi wa Wizara na wachimbaji wadogo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2012/13 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/12 – 2015/16; Malengo ya Taifa ya MKUKUTA II; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 - 2015; Mpango Mkakati wa Wizara ya Nishati na Madini 2011/12 – 2015/16; Maagizo ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa kwa Wizara ya Nishati na Madini kwa nyakati tofauti; Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2012/13; na ushauri uliotolewa na Bunge pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2012/13, unatoa mwelekeo wa

kukabiliana na changamoto zilizopo katika Sekta za Nishati na Madini. Mpango huu unalenga kutekeleza Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati ambayo itakuwa na manufaa katika kipindi cha muda mfupi na wa kati. Hii ni katika kuhakikisha kuwa Sekta za Nishati na Madini zinachangia ipasavyo katika maendeleo ya Taifa na hatimaye kuwezesha juhudi za Serikali katika kupunguza umaskini. Kufikiwa kwa lengo hilo kutarudisha imani ya Watanzania kuhusu utekelezaji wa mipango ya Serikali kwa vitendo chini ya dhana ya uwajibikaji na uwazi katika shughuli za umma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka 2012/13, Wizara inalenga kuimarisha zaidi usimamizi wa Sekta za Nishati na Madini ikiwa ni pamoja na kuboresha makusanyo yatokanayo na sekta hizo ili kuwezesha utekelezaji wa mipango ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato ya Serikali kutoka Shilingi 131,266,153,300 zilizokadiriwa kwa Mwaka 2011/12 hadi kufikia Shilingi 193,007,543,000 kwa Mwaka 2012/13, sawa na ongezeko la asilimia 47. Mapato hayo yatakusanywa kwa kutumia mikakati mbalimbali ikiwemo kuendelea kukusanya mauzo ya gesi asili; kuboresha mikataba ya uzalishaji na ugawanaji wa mapato ya mafuta na gesi asili; kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Kanuni zake pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Sheria hiyo; kuongeza kasi ya utoaji wa leseni kwa kuimarisha Mfumo wa Utoaji Leseni za Madini; kuendelea kutoa huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo ili kuongeza tija katika uzalishaji madini;

kuendelea kuimarisha Ofisi za Madini Kanda na Afisa Mkazi kwa kuzipatia rasilimali watu na fedha; na kuongezeka kwa mauzo ya madini yaliyoongezwa thamani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati hii, natumia fursa hii kuwakumbusha na kuwahimiza wamiliki wote wa leseni za madini nchini kuhakikisha kuwa wanalipa mrabaha, kodi na tozo mbalimbali kulingana na Sheria za nchi na kuyaendeleza maeneo ya utafutaji na uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2012/13, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kupanua na kuboresha miundombinu ya gesi asili na mafuta; kuongeza uwezo wa kufua umeme; ujenzi wa njia za kusafirisha na kusambaza umeme; kuongeza kasi ya kupeleka umeme makao makuu ya wilaya na vijijini; kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu katika ufuaji umeme; kuhamasisha matumizi bora ya nishati; kuendeleza shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asili, kudurusu na kuandaa sera, sheria, mipango na mikakati inayohusu Sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2012/13, Serikali itaanza ujenzi wa mitambo miwili ya kusafisha gesi asili katika maeneo ya Songo Songo Kisiwani na Mnazi Bay na ujenzi wa bomba la gesi asili lenye urefu wa kilometa 532 kutoka Mnazi Bay, Mtwara na Songo Songo Kisiwani (Kilwa) hadi Dar es Salaam kupitia Somanga Fungu. Utekelezaji wa Mradi huu utakuwa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ni ujenzi wa bomba la gesi asili lenye kipenyo cha inchi 24 na urefu

wa kilometa 25 kutoka Songo Songo Kisiwani hadi Somanga Fungu - Kilwa; na ujenzi wa bomba lenye kipenyo cha inchi 36 na urefu wa kilometa 197 kutoka Somanga Fungu - Kilwa hadi Dar es Salaam. Awamu ya pili, itahusisha ujenzi wa bomba lenye kipenyo cha inchi 36 na urefu wa kilometa 290 kutoka Mnazi Bay, Mtwara hadi Somanga Fungu. Katika Mwaka 2012/13, Serikali imetenga Shilingi bilioni 63 kama sehemu ya mchango kwa ajili ya ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi asili na bomba la kusafirisha gesi asili. Gharama ya Mradi huu ni Dola za Marekani milioni 1,225.3, sawa na Shilingi trilioni 1.96.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa mradi wa bomba la gesi asili kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam mwishoni mwa Mwaka 2013, kutawezesha mitambo ya umeme kutumia gesi asili badala ya mafuta ambayo ni ghali na hivyo kuokoa zaidi ya Dola za Marekani milioni 900 kwa mwaka. Vilevile, matumizi ya gesi asili yatapunguza utegemezi wa umeme unaofuliwa kutokana na maji na hivyo kuongeza uwezo wa upatikanaji umeme wa uhakika. Kwa upande mwingine, upatikanaji wa gesi asili ya kutosha katika Jiji la Dar es Salaam utachochea matumizi zaidi kwenye viwanda, taasisi, magari na majumbani.

Mheshimiwa Spika, ili kuanza utekelezaji wa mradi wa bomba la gesi asili, Serikali imefanya tathmini ya mali kwenye maeneo ambayo bomba litapita. Fidia itaanza kulipwa kwa wananchi husika kuanzia mwezi Agosti, 2012.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka 2012/13, Wizara itaendelea na utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asili kwenye nyumba 30,000, hoteli na taasisi 10, magari 8,000 na vituo vitatu vya kujazia gesi asili kwenye magari Jijini Dar es Salaam. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 35, sawa na takriban Shilingi bilioni 56. Kufuatia mafanikio yaliyopatikana kutokana na mradi wa majaribio katika nyumba 70, magari 45 na kituo kimoja cha kujazia gesi asili kwenye magari, wigo wa usambazaji wa gesi asili utaongezwa ili kuwafikia wateja wengi zaidi. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imetenga Shilingi bilioni 20 kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuhamasisha matumizi ya gesi asili kwenye taasisi, majumbani, viwandani na kwenye vyombo vya usafiri, Serikali imeamua kuondoa kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vitakavyotumika kwa ajili ya gesi iliyoshindiliwa *(compressed natural gas)* na vya kujengea mabomba ya kusafirisha gesi asili *(piped natural gas)* vikiwemo mita za kupimia gesi asili na majiko mahususi yanayotumia gesi asili tu.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa nchi inafaidika na rasilimali zilizopo, umiliki wa miundombinu kama mitambo ya kusafisha na kusafirisha gesi asili umeangaliwa upya. Kwa kuzingatia hilo, Serikali kupitia *TPDC* itamiliki bomba jipya la gesi asili litakalojengwa kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam pamoja na mitambo ya kusafisha gesi katika visima vilivyopo Songo Songo na Mnazi Bay. Aidha, *TPDC* itakamilisha

ufufuaji wa Kampuni ya *GASCO* ili iweze kusimamia majukumu ya usafishaji na usafirishaji wa gesi asili hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Mwaka 2012/13, Serikali itaanza kutekeleza Mradi wa Kinyerezi I MW 150 ili kuongeza uwezo wa kufua umeme. Aidha, Serikali itakamilisha mikataba ya mikopo na benki za *JBIC* na *ABSA* ifikapo mwezi Septemba, 2012 kwa ajili ya ujenzi wa mtambo wa Kinyerezi II MW 240. Utekelezaji wa mradi utaanza baada ya kusainiwa kwa mikataba hiyo. Mitambo hii ina uwezo wa kutumia gesi asili au mafuta ya ndege *(Jet–A1).* Mitambo hiyo itakapokamilika itaongeza MW 390 katika Gridi ya Taifa na itamilikiwa na Serikali kupitia *TANESCO*. Katika Mwaka 2012/13 Serikali imetenga Shilingi bilioni 18 kama mchango wake katika kutekeleza Miradi hiyo. Jumla ya gharama ya miradi hii miwili ni Dola za Marekani milioni 598, sawa na Shilingi bilioni 956.8.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2012/13 Serikali kupitia *STAMICO* itatafuta mbia kwa lengo la kuendeleza Mradi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira MW 200 kwa manufaa ya Taifa. Lengo la Mradi huu ni kuanza uzalishaji wa umeme wa MW 200 katika Mwaka 2015/16, ambapo MW 50 zitaanza kufuliwa Mwaka 2014/15 na kujenga njia ya umeme ya kV 220 kutoka Kiwira hadi kituo cha kupozea umeme cha Uyole, Mbeya. Utekelezaji wa Mradi huu utawezesha kuongezeka kwa umeme wa bei nafuu kwenye Gridi ya Taifa. Mradi huu unakadiriwa kugharimu Dola za Marekani 400, sawa na Shilingi bilioni 640.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2012/13, Kampuni ya *Kilwa Energy* itaanza ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi na kuanza utekelezaji wa Mradi wa Somanga Fungu wa MW 320. Mradi huo utazalisha MW 230 kwa kuanzia, ambapo MW 90 za ziada zitazalishwa baada ya miezi 20. Gharama za Mradi huu ni Dola za Marekani milioni 365, sawa na Shilingi bilioni 584.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Murongo/Kikagati MW 16 ni wa kujenga miundombinu ya kusambaza umeme katika Mji Mdogo wa Murongo Mkoani Kagera. Lengo ni kuwezesha Wakazi wa Murongo/Kikagati kuunganishiwa umeme wa MW 16 utakaozalishwa kutoka katika maporomoko ya maji ya Mto Kagera. Mradi utaendelezwa kwa ushirikiano kati ya Tanzania na Uganda, ambapo kila nchi itapata MW 8. Kazi zilizopangwa kufanyika chini ya Mradi ni ujenzi wa njia za kusambaza umeme za msongo wa kV 33 na kV 0.4; ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 33 yenye urefu wa kilometa 194 na kusambaza umeme katika Mji Mdogo wa Murongo pamoja na vijiji 24. Katika Mwaka 2012/13, Serikali imetenga Shilingi bilioni 12 kwa ajili ya ujenzi wa njia na usafirishaji na usambazaji umeme kwa upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2012/13, utekelezaji wa Mradi wa ORIO katika maeneo ya Biharamulo, Mpanda na Ngara utaanza. Mradi huo utahusisha ufungaji wa jenereta za kufua MW 2.5 kwa kila eneo pamoja na usambazaji wa umeme katika maeneo hayo. Mradi huo utatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Kifalme ya

Uholanzi. Mradi huo utagharimu Euro milioni 34, sawa na Shilingi bilioni 67.49 na wateja wa awali 100,000 wataunganishwa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ukarabati wa Mitambo katika Vituo vya Kufua Umeme unahusu ukarabati wa mitambo ya vituo vitano vya kufua umeme unaotokana na nguvu za maji. Mitambo hii ni Kidatu, Kihansi, Mtera, New Pangani Falls na Nyumba ya Mungu. Mradi utafadhiliwa kwa msaada wa Serikali ya Norway kwa asilimia 32, kwa Mwaka 2012/13 Serikali hiyo imetoa Shilingi bilioni 2.43. Katika kutekeleza Mradi huu, *TANESCO* itachangia asilimia 68. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwaka 2013/14. Aidha, ukarabati wa mitambo ya Kituo cha Hale utatekelezwa kwa ufadhili wa Serikali ya Sweden kwa kiasi cha Shilingi bilioni 4.5.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya umeme katika Jiji la Dar es Salaam. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kukarabati vituo vya kupozea umeme katika maeneo ya Ilala, Temeke, Kinondoni Kaskazini na Kinondoni Kusini; kukamilisha ufungaji wa transfoma zenye uwezo mkubwa katika maeneo ya Mbezi Beach, Mbagala, Kigamboni, Gongolamboto, Kurasini na Ubungo; kubadilisha nyaya ndogo na zilizochakaa; kubadilisha nguzo zilizooza za njia za msongo mdogo na mkubwa za umeme; kujenga njia kubwa za umeme za msongo wa kV 33 ili kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika Jijini. Katika Mwaka 2012/13 jumla ya Shilingi bilioni 52 zimetengwa kutumika katika Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Finland itatoa kiasi cha Euro milioni 25 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kupozea umeme cha kV 132/33/MVA 2x45 *city centre*; ujenzi wa njia ya umeme chini ya ardhi kutoka kituo cha Ilala hadi kituo kipya cha *city centre*; ujenzi wa njia ya umeme chini ya ardhi kwa ajili ya kuunga Kituo cha Kariakoo – Railway – Sokoine na kituo cha zamani cha *city centre*; kuanzisha kituo cha kuongozea mifumo ya usambazaji umeme katika msongo wa kV 33 na kV 11 *(SCADA);* kuanzisha mfumo wa kuangalia na kutoa taarifa za usambazaji umeme katika msongo mdogo wa umeme. Serikali ya Tanzania itachangia Euro milioni 1.5 kwa ajili ya kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuwezesha na kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Iringa – Shinyanga kV 400 *(backbone)*, ambapo kazi zitakazofanyika ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa njia ya msongo wa kV 400; ujenzi wa vituo vinne vya kupozea umeme katika Mikoa ya Iringa, Dodoma, Singida na Shinyanga; na ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa njia za usambazaji umeme. Vyanzo vya fedha kwa ajili ya mradi huu ni kutoka Benki ya Dunia, *JICA, AfDB, NORAD, Sida,* Taasisi ya Korea Kusini *(ECDF)* na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya *(EIB).* Fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza Mradi huo kwa Mwaka 2012/13 ni Shilingi bilioni 12.5 na fedha za nje ni Shilingi bilioni 7.5.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kufanyika katika Mwaka 2012/13 chini ya Mradi wa Makambako – Songea kV 220 ni uandaaji wa michoro ya Mradi; shughuli za ugani *(Aerial Flight Survey);* uandaaji wa

zabuni za kumpata mkandarasi; na ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa Mradi huo wa njia ya msongo wa kV 220. Katika Mwaka 2012/13, Serikali imetenga Shilingi bilioni 9.5 na fedha za nje ni Shilingi bilioni 7.5 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, lengo la Mradi wa North-West Grid kV 220 ni kujenga njia ya umeme ya msongo wa kV 220 kutoka Geita kwenda Nyakanazi – Kigoma – Mpanda – Sumbawanga hadi Mbeya. Lengo ni kuipatia mikoa hiyo umeme wa gridi. Gharama za Mradi ni Dola za Marekani milioni 792.9, sawa na Shilingi bilioni 1,268.64, ambapo Benki ya Exim ya China itagharimia asilimia 85 na Serikali itachangia asilimia 15. Katika Mwaka 2012/13 Shilingi bilioni tano zimetengwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa Mradi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, 2010 – 2015, Ibara ya 63(c), Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* itaendelea na kazi ya kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya za Nanyumbu, Mkalama, Kakonko, Uvinza, Mlele, Kalambo, Nyasa, Buhigwe, Momba, Itilima, Busega, Ikungi, Chemba na Kyerwa. Aidha, upelekaji umeme Makao Makuu ya Wilaya za Mbogwe na Bukombe utaendelea kutekelezwa chini ya Mradi wa *Electricity V* unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*). Makao Makuu ya Wilaya Mpya ya Nyang'hwale utatekelezwa chini ya Mradi wa *Millenium Challenge Corporation (MCC)* ya Serikali ya Marekani.

Mheshimiwa Spika, upelekaji umeme katika Wilaya hizo utahusisha ufungaji wa transfoma na usambazaji umeme kwenye njia zenye msongo wa kV 11 na 33 na ujenzi wa njia ya usambazaji zenye msongo wa kV 0.4. Kutekelezwa kwa kazi hizo kutawezesha kuunganisha wateja wa awali wapatao 80,000. Aidha, Wakala kwa kushirikiana na *TANESCO* utaendelea na kuwezesha utekelezaji wa mradi kabambe katika mikoa 16. Katika Mwaka 2012/13, mbali na vyanzo vingine vya fedha, Wakala umetengewa jumla ya Shilingi bilioni 150, zikiwemo Shilingi bilioni 16.6 fedha za nje ili kutekeleza awamu ya pili ya Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini ikiwa ni pamoja na kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya Mpya.

Mheshimiwa Spika, kwa takriban miaka mitano Mikoa ya Lindi na Mtwara imekuwa ikipata huduma ya umeme kutoka kwa Kampuni ya Artumas iliyokuwa inamiliki mitambo ya MW 18 iliyopo Mtwara. Kutokana na mdororo wa uchumi, Kampuni ya Artumas ilishindwa kutoa huduma hiyo na kuamua kuuza mitambo hiyo kwa Kampuni ya Wentworth, ambayo baadaye nayo iliiuzia Serikali kupitia *TANESCO* mwezi Machi, 2012. Katika Mwaka 2012/13 *TANESCO* itaendelea kutoa huduma za usambazaji umeme na uboreshaji miundombinu ya umeme katika Mikoa ya Mtwara na Lindi, ambapo Shilingi bilioni tano zimetengwa kupitia Wakala wa Nishati Vijijini. Katika zoezi hilo jumla ya vipozea umeme 48 vitafungwa na kuwezesha kuunganisha wateja wa awali 2,400.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya vikwazo vinavyokwamisha jitihada za Serikali za kuhakikisha

kuwa huduma ya umeme inawafikia wananchi wengi zaidi na kwa kasi kubwa ni gharama kubwa za kuunganisha umeme na kipato cha wananchi wengi wanaohitaji kupata huduma ya umeme. Gharama hizo zimekuwa ni kikwazo katika azma ya Serikali ya kutimiza lengo la asilimia 30 ya wananchi watakaounganishiwa umeme ifikapo Mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia changamoto hizo, Serikali kupitia *TANESCO* imedhamiria kupunguza gharama za kuunganisha umeme wa njia moja *(single phase)* kwa wateja wadogo mijini na vijijini kwa wastani wa kati wa asilimia 30 na 77. Kwa kufanya hivyo, wateja wengi watamudu gharama na hatimaye kuongeza kasi ya kuunganisha umeme.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uamuzi huo wa Serikali, gharama za uunganishaji umeme zitakuwa kama ifuatavyo: Kwa wateja watakaojengewa njia moja *(single phase)* kwenye umbali usiozidi mita 30 bila kuhitaji nguzo, katika maeneo ya vijijini watalipa Shilingi 177,000 na wa mijini watalipa Shilingi 320,960 badala ya Shilingi 455,108 zinazolipwa na wateja hao kwa sasa. Punguzo hili ni sawa na asilimia 61.11 kwa wateja waishio vijijini na asilimia 29.48 kwa wateja waishio mijini.

Mheshimiwa Spika, kwa wateja watakaojengewa njia moja *(single phase)* na kuwekewa nguzo moja, katika maeneo ya vijijini watalipa Shilingi 337,740 na wa mijini watalipa Shilingi 515,618 badala ya Shilingi 1,351,884 zinazolipwa na wateja hao kwa sasa. Punguzo hili ni sawa na asilimia 75.02 kwa wateja

waishio vijijini na asilimia 61.86 kwa wateja waishio mijini. Aidha, kwa wateja watakaojengewa njia moja na kuwekewa nguzo mbili katika maeneo ya vijijini watalipa Shilingi 454,654 na wa mijini watalipa Shilingi 696,670 badala ya Shilingi 2,001,422 zinazolipwa na wateja hao kwa sasa. Punguzo hili ni sawa na asilimia 77.28 kwa wateja waishio vijijini na asilimia 65.19 kwa wateja waishio mijini. Viwango hivyo vya gharama vitaanza kutumika mwezi Januari, 2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeanzisha utaratibu wa kugharimia miundombinu ya kuwafikishia umeme wateja kwa Miradi inayopata ruzuku kutoka Mfuko wa Nishati Vijijini *(REF)*. Utaratibu huu utatumika kwa wateja watakaokuwa wamefunga nyaya za umeme kwenye nyumba zao katika maeneo ya Miradi husika. Mpango huo utapunguza gharama za kuunganishiwa umeme kwa wastani wa asilimia 80 kulingana na idadi ya nguzo na mfumo utakaotumika, yaani *single* au *three phase*. Idadi ya wateja wa awali watakaounganishiwa umeme kupitia mpango huo ni 100,000.

Mheshimiwa Spika, lengo la Mradi wa Uendelezaji wa Umeme Utokanao na Maporomoko Madogo ya Maji ni kufanya utafiti na kuendeleza miradi midogo ya maporomoko ya maji *(mini hydro)* kwa ajili ya kuzalisha umeme kwa maeneo yaliyo nje ya Gridi ya Taifa. Kazi zilizopangwa kufanyika Mwaka 2012/13 ni kumpata Mshauri kwa ajili ya kufanya tafiti kwenye vyanzo vilivyobainishwa; na kuwezesha ununuzi wa mitambo ya uzalishaji na kujenga kwenye vyanzo

vitakavyoonekana vinafaa kuendelezwa. Kiasi cha Shilingi bilioni 4.5 zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuendeleza Shughuli za Utafutaji wa Gesi Asili na Mafuta; Serikali kupitia *TPDC* itatangaza maeneo mapya ambayo hayajapata wawekezaji kwa ajili ya utafutaji mafuta na gesi asili. Zabuni ya awamu ya nne *(4th Off-shore Licensing Round)* kwa ajili ya kunadi maeneo mapya ya uwekezaji inatarajiwa kutangazwa mwezi Septemba, 2012 Jijini Houston, Marekani.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia kwa karibu shughuli za utafutaji mafuta na gesi asili na kuhakikisha kuwa shughuli hizo zinafanyika kulingana na mpango kazi ulioainishwa kwenye mkataba. Natoa rai kuwa, Serikali haitasita kufuta mikataba kwa kampuni zitakazoshindwa kutekeleza mpango kazi kwa muda uliopangwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia *TPDC* itaendelea kujenga uwezo wa kufanya ukaguzi ili kuhakikisha kuwa kampuni zote zinazofanya utafiti na uzalishaji wa gesi asili na mafuta zinatekeleza kazi zake kwa mujibu wa mikataba iliyopo. Aidha, Serikali itadurusu mikataba iliyopo na kufanya uchambuzi wa kina kabla ya kuingia mikataba mipya ya uzalishaji na ugawanaji mapato ya mafuta na gesi asili ili kuhakikisha kuwa maslahi ya Taifa yanazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2012/13, Kanuni za Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja zitapitiwa na kuboreshwa ili kuondoa upungufu uliojitokeza. Aidha,

muundo na upatikanaji wa Wajumbe wa Bodi ya Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja *(PIC),* utapitiwa upya ili kuboresha ufanisi wa mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia azma ya Serikali ya kuihuisha Kampuni ya Mafuta ya Taifa *(COPEC)* ambayo ni kampuni tanzu ya *TPDC,* mwezi Agosti, 2011 *EWURA* ilitoa leseni kwa Kampuni hiyo kuanza biashara ya uagizaji na usambazaji wa mafuta nchini. Katika Mwaka 2012/13 Serikali itatafuta njia bora ya kuiwezesha *COPEC* kuanza utekelezaji wa jukumu hilo, ikiwa ni pamoja na kuidhamini *COPEC* kuweza kukopa kutoka katika benki za ndani na kuiwezesha kupata mafuta ya mkopo yenye masharti nafuu kutoka nchi zinazozalisha mafuta duniani. Lengo ni kuwa na uhakika wa upatikanaji *(security of supply)* wa mafuta nchini.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Nishati imeendelea kukua kwa kasi kubwa, hali inayohitaji kuwepo kwa sera madhubuti, inayozingatia ukuaji huo pamoja na changamoto zilizopo. Hivyo, pamoja na jitihada za kudurusu Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2003, Serikali imelazimika pia kuandaa Sera nyingine katika sekta hiyo zikiwemo Sera za Gesi Asili, Nishati Vijijini, Biofuel na Nishati Jadidifu. Katika Mwaka 2012/13, Wizara itakamilisha durusu ya Sera ya Nishati ya Mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, wadau wengi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa na shauku kubwa ya kuona kuwa Sera, Sheria na Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asili vinakamilishwa haraka ili

utekelezaji wake uweze kuanza. Hata hivyo, utayarishaji wa Sera, Sheria na Mpango Kabambe unahitaji uchambuzi wa kina na ushirikishwaji mpana wa wadau. Lengo ni kuhakikisha kuwa kunakuwa na usimamizi bora wa matumizi ya rasilimali hii kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2012/13, Wizara itakamilisha Sera, Sheria na Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asili. Sera na Sheria ya Gesi Asili zitakazoandaliwa zitazingatia uhamasishaji wa ushiriki wa Watanzania wakiwemo wenyeji wa mikoa ambayo shughuli za gesi na mafuta zinafanyika; kuongeza kiwango cha mrabaha; kuwezesha *TPDC* kushiriki zaidi katika uwekezaji; mgawanyo wa majukumu ya wadau wa sekta ndogo ya gesi na mafuta; na mwekezaji kulipa kiasi cha fedha kisichorudishwa *(signature bonus)* wakati wa kusaini mkataba.

Mheshimiwa Spika, lengo la Wizara ni kuweka mazingira wezeshi katika uendelezaji wa nishati ya jotoardhi *(geothermal)* nchini. Shilingi bilioni 1.0 zimetengwa katika Mwaka 2012/13 kwa ajili ya kuwezesha tathmini na kuchoronga visima vya majaribio kwenye eneo la Ziwa Ngozi (Mbeya). Maeneo mengine yenye viashiria vya kuwepo jotoardhi ni pamoja na Songwe (Mbeya); Ziwa Eyasi, Manyara na Natroni (Manyara); Mto Luhui - Rufiji (Pwani); na Kisaki (Morogoro). Mafanikio ya uchorongaji huo yatawezesha kubainisha uwepo wa joto la kutosha kwa ajili ya ufuaji umeme, hivyo kuongeza wigo wa vyanzo vya kufua umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, katika uendelezaji wa nishati kwa kutumia tungamotaka, Wizara inalenga kuhamasisha matumizi ya majiko banifu, mabaki ya mazao ya mashambani na taka salama za viwandani katika kuzalisha umeme na *biogas* kwa kupikia. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kuwezesha ujenzi wa mitambo ya *biogas* katika Kanda ya Ziwa kwenye shule na zahanati; kuhamasisha matumizi ya majiko banifu kwenye taasisi mbalimbali kama magereza na shule. Kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kazi hizo katika Mwaka 2012/13 ni Shilingi milioni 261.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2012/13 jitihada zitaelekezwa katika kuweka mazingira wezeshi ya kisera, kisheria na kitaasisi ili kuendeleza *biofuel* nchini. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kukamilisha Sera ya *Biofuel;* kuandaa mkakati wa kutekeleza sera; kujenga uwezo wa taasisi za Serikali katika kusimamia masuala ya *biofuel;* na kuandaa Sheria ya *Biofuel*. Jumla ya Shilingi bilioni 2.19 zikiwemo Shilingi milioni 50, fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhamasisha matumizi bora ya nishati kupitia Mradi wa *Low Carbon Energy Efficient and Climate Change Mitigation.* Mradi huo ni wa miaka minne na unalenga kusaidia upatikanaji na kuhamasisha matumizi endelevu ya nishati kwa wananchi wengi, hususan, maeneo ya vijijini. Mradi huo pia utahamasisha Halmashauri za Wilaya kuweka kipaumbele katika kuendeleza Miradi ya Nishati Jadidifu *(renewable energies)* na matumizi bora ya nishati *(energy*

*efficiency)* kwa kutenga fedha za Miradi hiyo katika mipango yao. Mradi unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)* na Serikali. Ili kutekeleza Mradi huu, kwa Mwaka 2012/13 *UNDP* imetoa Shilingi bilioni 1.33.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini: Katika Mwaka 2012/13, Wizara itaendelea kuboresha Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini, hususan kuongeza kasi ya mawasiliano ya mfumo huo kwa kutumia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; kuongeza idadi ya watumishi wenye ujuzi wa kutumia mfumo huo; kuboresha kanzidata *(database);* na kuendelea kuongeza vitendea kazi kwenye ofisi zote zinazotumia mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kukamilisha taratibu za kisheria za kutenga na kugawa maeneo kwa ajili ya uchimbaji mdogo. Maeneo hayo ni pamoja na Nyakunguru, Goronga, Gibaso na Mogabiri (Tarime); Kapalamsenga (Mpanda); Ilagala (Kigoma Vijijini); Ibaga na Mpambaa (Mkalama); Isenyela (Chunya); na Makanya (Same). Maeneo yote haya yana jumla ya hekta 105,163 zinazoweza kutolewa leseni takriban 10,516 za uchimbaji mdogo zenye ukubwa wa hekta 10 kila moja.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 8.9 kwa ajili ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo ikiwa ni pamoja na kuwapa mikopo kwa Mwaka 2012/13. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 2.5 ni fedha za ndani na Dola za Marekani milioni nne, sawa na Shilingi bilioni 6.4, ni fedha za nje kupitia Mradi wa

Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini *(SMMRP)* unaofadhiliwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia. Kutolewa kwa fedha hizo kutawezesha wachimbaji wadogo kufanya kazi zao kwa kutumia nyenzo za kisasa hivyo kuongeza tija na ufanisi na hatimaye kusaidia katika juhudi za kupunguza umaskini wa kipato kama ilivyoelekezwa katika Malengo ya MKUKUTA II.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusu biashara na masoko ya madini, masuala ya afya, usalama na utunzaji mazingira katika shughuli za uchimbaji madini ili waweze kuzingatia Sheria na Kanuni za Madini.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha usimamizi na uratibu wa shughuli za uongezaji thamani madini nchini, Wizara imeanzisha Sehemu ya Uongezaji Thamani Madini. Katika Mwaka 2012/13, Sheria ya Uongezaji Thamani Madini itaandaliwa. Vilevile, Wizara itashirikiana na wadau mbalimbali katika kuboresha mbinu bora za uchenjuaji madini kwa ajili ya kunufaisha wachimbaji wadogo wengi zaidi. Kwa kufanya hivyo, ni matarajio ya Serikali kuwa kiasi cha madini yanayoongezwa thamani kitaongezeka kutoka asilimia sifuri hadi asilimia 70 ya tani 30,000 ya shaba ghafi zinazozalishwa na wachimbaji wadogo na wa kati kwa mwaka kwa sasa; na kutoka asilimia 35 hadi asilimia 50 ya kilo milioni 1.3 za vito zinazozalishwa kwa mwaka kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika Maonesho ya Kwanza ya

Kimataifa ya Vito na Usonara, Wizara itaandaa maonesho ya pili yanayotarajiwa kufanyika tarehe 18 hadi 22 Aprili, 2013 Mjini Arusha kwa kuhakikisha kuwa yanafanikiwa zaidi na kuboresha mfumo wa soko la madini, uhamasishaji uongezaji thamani; na uendelezaji tasnia ya uchimbaji wa madini ya vito nchini. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia tasnia ya almasi na vito hapa nchini kwa kutambua, kuchambua na kuthamini madini hayo kupitia Kitengo cha *TANSORT.*

Mheshimiwa Spika, Wizara Itaendelea kusimamia Sheria zote zinazohusu Afya, Usalama na Utunzaji wa Mazingira migodini kwa kuimarisha kaguzi katika migodi mikubwa, ya kati na midogo. Aidha, katika kuhakikisha kuwa migodi ya wachimbaji wadogo wa madini wa Kitalu B kilichopo Mererani Wilayani Simanjiro, haiathiriki na mafuriko kutokana na mvua, Serikali imeanza ujenzi wa mtaro katika eneo la D'souza. Kazi hii inatarajiwa kukamilika katika Mwaka 2012/13 na imetengewa Shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Spika, mipango ya ufungaji migodi *(mine closure plans)* ya Geita, Tulawaka, Bulyanhulu, Buzwagi, Williamson Diamond na TanzaniteOne itaboreshwa na kukamilishwa katika Mwaka 2012/13. Baada ya mipango hiyo kupitishwa, migodi husika itaanzisha mifuko ya ukarabati wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka 2012/13, Wizara itadurusu Sheria ya Baruti ya Mwaka 1963 ili iendane na mazingira na teknolojia ya sasa. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo

kuhusu utunzaji, usafirishaji na utumiaji wa baruti; na kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa baruti ili waweze kwenda na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Shughuli za *TEITI:* Katika kipindi cha Mwaka 2012/13, Kamati Tekelezi itaendelea kuandaa Sheria ya *TEITI* pamoja na kujenga uwezo juu ya uendeshaji wa *TEITI* kwa Wajumbe wa Kamati na Sekretarieti. Kamati pia imepanga kuelimisha na kuhamasisha wachimbaji wadogo kushiriki katika utoaji wa takwimu za malipo katika uandaaji wa ripoti ya tatu ya *TEITI* itakayohusisha hesabu za kipindi cha Mwaka 2010/11. Lengo ni kubaini mchango wa sekta ndogo ya uchimbaji madini kama ilivyo kwa kampuni kubwa ili kuwezesha Serikali kupima maendeleo ya ukuaji wa sekta hii mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya njia ya kuongeza Fungamanisho la Sekta ya Madini na Sekta nyingine za Uchumi ni kuhakikisha kuwa kampuni zinazojihusisha na shughuli za madini nchini zinatumia kwa wingi huduma na bidhaa za ndani kadiri zinavyopatikana. Hii ni katika kutekeleza Sera ya Madini ya Mwaka 2009 ambayo inasisitiza kampuni za madini kutumia huduma na bidhaa zinazopatikana hapa nchini kama vifaa vya ofisi, chakula na vinywaji, ushauri wa kisheria, ulinzi, utunzaji wa mazingira na chokaa. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itaendelea kuweka mkazo kwa kampuni za madini kutumia bidhaa na huduma za hapa nchini ili kuhakikisha kuwa Watanzania wananufaika na shughuli za uchimbaji madini.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa, migodi mikubwa ya dhahabu nchini imenunua bidhaa na huduma za ndani zenye thamani ya takriban Dola za Marekani bilioni 3.5, na nje Dola za Marekani bilioni 4.3 katika kipindi cha kuanzia Mwaka 2001 hadi 2011. Kwa takwimu hizo, ununuzi wa ndani ni asilimia 44.8 na wa nje ni asilimia 55.2. Serikali bado hairidhishwi na kiwango hicho cha ununuzi wa ndani. Hivyo, wamiliki wa migodi wanatakiwa kutoa kipaumbele kwa kununua bidhaa za ndani ambazo zinakidhi viwango.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2012/13, Wizara itaanzisha utaratibu wa kubainisha mahitaji muhimu ya huduma na bidhaa zinazohitajika kwenye kampuni za madini. Utaratibu huu utakuwa ni msingi wa kuwahamasisha na kuwawezesha Watanzania kukidhi viwango vya huduma na bidhaa zinazohitajika migodini. Lengo ni kuongeza kiwango cha ununuzi wa bidhaa na huduma za ndani ili kuleta manufaa zaidi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka 2012/13 Wizara itaanza ujenzi wa Ofisi ya Madini ya Kanda ya Magharibi (Mpanda), Kanda ya Kusini (Mtwara) na Ofisi ya Afisa Madini Mkazi (Dodoma). Aidha, ukarabati wa Ofisi ya Madini Kanda ya Kati - Magharibi (Shinyanga) na Ofisi ya Madini ya Kanda ya Kaskazini (Arusha) utakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na usalama zaidi katika kazi zinazofanywa na Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania *(TMAA)* na Kitengo cha *TANSORT,* Wizara imeona ni vyema taasisi hizo ziwe na jengo la kudumu

na kuepusha gharama kubwa za ukodishaji wa majengo ya ofisi. Katika Mwaka 2012/13 Wizara itaanza maandalizi ya ujenzi wa jengo hilo. Mbali na matumizi ya ofisi, jengo hilo litakuwa ni Kituo cha Kimataifa cha Biashara ya Madini nchini.

Mheshimiwa Spika, Kituo hicho kitatoa huduma mbalimbali zikiwemo ukaguzi na uhakiki wa madini hususan dhahabu, almasi na vito; utambuzi na uthamini wa madini ya almasi na vito; vyumba maalumu vya kuuzia na kununulia madini ya dhahabu, almasi na vito; vyumba vya kuhifadhi madini; na utoaji wa vibali kwa ajili ya kusafirisha madini nje ya nchi. Pia, Kituo kitakuwa na sehemu salama ya kufanyia biashara ya madini, kuongeza makusanyo yatokanayo na biashara ya madini na kuwapatia soko wafanyabiashara wa madini nchini.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ukaguzi Madini Tanzania – TMAA: Katika Mwaka 2012/13, Serikali itaongeza kasi ya ukaguzi na udhibiti wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini nchini kupitia *TMAA* ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Madini inaleta manufaa zaidi kwa Taifa. Ukaguzi utakaofanyika utahusisha migodi mikubwa, ya kati na midogo kwa madini yote. Pia, Wakala utaendelea kujenga uwezo kwa watumishi wake katika kubainisha maoteo ya mapato ya Serikali kutoka kwenye Sekta ya Madini kwa kutumia mfumo wa kisasa *(revenue forecasting model)* ili kuwa na takwimu za uhakika za mapato ya Serikali kutoka sekta hiyo na kuzitumia katika kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali. Wakala pia utaendelea kuboresha maabara yake ili iweze kupata usajili katika Shirika la Viwango

vya Kimataifa *(ISO 17025)* na hivyo kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Spika, ili nchi yetu iweze kunufaika zaidi na shughuli za uchimbaji mkubwa wa madini nchini, mikakati iliyopo ni pamoja na kuhakikisha kuwa migodi inaendelea na mingine inaanza kulipa kodi ya mapato na gawio kwa migodi ambayo Serikali ina hisa. Kabla mgodi haujaruhusiwa na Serikali kujengwa, wamiliki wake wanawajibika kuwasilisha taarifa za upembuzi yakinifu zinazoonesha gharama za uwekezaji, muda wa mgodi kurudisha gharama na muda wa kuanza kulipa kodi ya mapato. Kimsingi, taarifa hizo ndizo zinazotumiwa na Serikali kufikia uamuzi wa kuingia mkataba wa uendelezaji mgodi na kampuni husika.

Mheshimiwa Spika, bei ya dhahabu katika soko la dunia imeendelea kupanda kwa kiwango kikubwa, ukilinganisha na kiwango cha nyuma wakati migodi hiyo inaanzishwa. Hali hiyo inawezesha muda wa urejeshaji gharama za uwekezaji kupungua na hivyo kuanza kulipa kodi ya mapato mapema. Hata hivyo, licha ya kupanda kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia, baadhi ya migodi haijaanza kulipa kodi ya mapato kwa madai kwamba haijarudisha gharama za uwekezaji. Hivyo, Serikali kupitia Wakala wa Ukaguzi wa Madini kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato *(TRA)*, itaendelea kukagua na kuhakiki gharama za uwekezaji na uendeshaji kwenye migodi mikubwa na ya kati ili kuhakikisha kodi hizo zinalipwa mapema.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa rai kuwa migodi yote ianze kulipa kodi ya mapato bila kuleta visingizio kuwa hawajarudisha gharama au wanapata hasara pamoja na muda walioonesha kwenye taarifa za upembuzi yakinifu kufika. Bei zilizoainishwa kwenye taarifa za upembuzi yakinifu kwa wakati huo ni ndogo mara tano ya bei ya sasa, hali inayoashiria kuwa migodi imerudisha gharama za uwekezaji mapema kuliko inavyokadiriwa kwani gharama za uendeshaji haziwezi kupanda sawa na bei ya dhahabu inavyopanda. Ni matumaini yangu kuwa kama mwekezaji ameendelea kuchimba kwa muda wa miaka mitano hadi saba ameshapata faida na kurejesha gharama zake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali hiyo, kupitia Bunge lako Tukufu, naagiza kampuni zote zilizochimba madini kwa miaka mitano na kuendelea, zianze kulipa kodi ya mapato bila kuleta visingizio. Na kama Kampuni bado inapata hasara na haiwezi kuchangia katika uchumi wa Taifa kwa kulipa kodi ya mapato, ifunge mgodi wake na kuondoka kwa kuwa madini hayaozi. Haiwezekani kukaa miaka saba unaendelea kupata hasara lakini upo. Serikali itaendelea kushirikiana na Kampuni zilizo tayari kuanza kulipa kodi ya mapato kwa wakati bila masharti.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa na Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)*, katika Mwaka 2012/13 ni kuendelea kusimamia kwa karibu upembuzi yakinifu unaofanyika kwenye Mradi wa Dhahabu wa Buckreef; kufanya majadiliano na kuingia mkataba wa ubia na kampuni itakayoibuka mshindi kwa ajili ya

kuliendeleza upya eneo la Mgodi wa Buhemba; na kuanzisha uzalishaji wa dhahabu kutokana na mabaki ya uchimbaji wa zamani katika eneo hilo. Uzalishaji huo pamoja na huduma mbalimbali utatoa ajira ya Watanzania wasiopungua 120.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO),* itaendelea kuwatambua wachimbaji wadogo kwa kuanzisha kanzidata *(database)* itakayokuwa na taarifa na takwimu zote muhimu zinazowahusu; kufanikisha upatikanaji wa mikopo, mitambo, vifaa na zana za uchimbaji; kutoa elimu na huduma za ushauri katika utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji na uingiaji wa mikataba. Kazi zote hizi zitafanyika kwa kushirikisha idara na taasisi zote ambazo zimekuwa zinatoa huduma kwa wachimbaji wadogo. Taasisi hizo ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(UDSM);* Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam *(DIT);* Shirika la Uendelezaji Viwanda Vidogo *(SIDO);* Chuo cha Ufundi Stadi *(VETA);* kampuni na taasisi binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2012/13, Wakala Wa Jiolojia Tanzania – *GST,* utafanya upimaji na uchoraji wa ramani tano za jiolojia na jiokemia (QDSs 280, 281, 282, 283 na 284) katika Wilaya za Kilwa, Lindi, Liwale na Ruangwa. Wakala pia, utafanya kazi ya ukusanyaji wa takwimu za jiofizikia kwa kutumia ndege *(High Resolution Airborne Geophysical Survey – Gravity, Magnetic, Radiometric and Elecromagnetic)* katika QDSs 34 katika Mikoa ya Dodoma, Manyara, Mbeya, Morogoro, Pwani, Singida na Tanga. Zoezi hili litagharimiwa kwa pamoja kati ya Serikali na Benki ya

Dunia, ambapo Serikali itachangia Shilingi milioni 750 na Benki ya Dunia itatoa mkopo wa Dola za Marekani milioni 11.55. Aidha, ramani 60 za zamani zitabadilishwa kutoka kwenye mfumo wa karatasi na kuziweka kwenye mfumo wa *digital.*

Mheshimiwa Spika, Wakala pia umepanga kufanya ukarabati mkubwa kwenye kituo cha kupimia matetemeko ya ardhi kilichopo Dodoma ili kiweze kunakili moja kwa moja kwenye mfumo wa kompyuta *(server)*, taarifa za matetemeko mara yanapotokea *(real time seismic station).* Aidha, ukusanyaji wa takwimu za matukio ya matetemeko ya ardhi kutoka kwenye vituo kumi vya kupimia matetemeko ya ardhi vilivyoko nchini (Babati, Dodoma, Geita, Kibaya, Kondoa, Mahale, Manyoni, Mbeya, Mtwara na Singida) utaendelea ikiwa ni pamoja na kuchakata takwimu hizo na kuandaa taarifa za matukio hayo. Wakala utaendelea kuboresha miundombinu, vitendea kazi na rasilimali watu ili kuongeza ufanisi na tija.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2012/13, Chuo cha Madini Dodoma – *MRI*, kitaendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Cheti na Stashahada katika fani za Jiolojia na Utafutaji Madini, Uhandisi Uchimbaji Madini na Uhandisi Uchenjuaji Madini. Pia, kwa kutambua umuhimu wa kuwa na wataalamu wa kutosha katika sekta ndogo ya mafuta na gesi asili nchini, Chuo kitaanzisha kozi mpya za Jiolojia ya Mafuta na Gesi; na Uhandisi na Usimamizi wa Mazingira Migodini katika ngazi ya Cheti na Stashahada. Aidha, Watumishi wa Chuo

wataendelezwa kitaaluma na kitaalamu ili waweze kutoa mafunzo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zitakazofanyika ni uendelezaji wa miundombinu kwa kuanza ujenzi wa jengo la taaluma lenye vyumba vya mihadhara vyenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 100 kila kimoja na ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua watumiaji 500 kwa wakati mmoja. Lengo ni kupanua wigo wa mafunzo na kudahili wanafunzi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2012/13 Wizara itaajiri jumla ya watumishi 267 wa kada mbalimbali. Kati ya hao watumishi 65 ni kwa ajili ya Wizara, *TPDC* 51, *REA* 16, *MRI* 33, *STAMICO* 30, *TMAA* 15 na *GST* 57. *TANESCO* itaendelea kuajiri watumishi kulingana na taratibu zilizounda Shirika hilo. Aidha, ili kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa Sekta za Nishati na Madini, Wizara imepanga kuwajengea uwezo jumla ya watumishi 206 kwa kutoa mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Mbali na fani za mafuta na gesi asili, kipaumbele kitatolewa katika maeneo maalumu yakiwemo *energy economics; geothermal; uranium; mineral economics; diamond valuation and sorting*; na *contracts negotiations and management in energy and mineral sectors.*

Mheshimiwa Spika, kufuatia ugunduzi mkubwa wa gesi asili nchini, Wizara imeanzisha Mpango wa Uendelezaji Rasilimali Watu *(Marshall Plan on Capacity Building and Development in Oil and Gas Industry 2012 – 2016).* Mpango huu utawezesha Watanzania kati ya 30 hadi 50 kupata elimu katika ngazi ya shahada na

shahada za uzamili kwenye fani za mafuta na gesi asili. Maeneo yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na *petroleum geosciences, petroleum geophysics, petroleum geochemistry, petroleum engineering, energy modelling, oil and gas economics, oil and gas accounting and auditing, oil and gas legal regimes* na *contract negotiations.* Mpango huu utatekelezwa na Wizara kwa kushirikiana na *TPDC* kupitia fedha za uendelezaji rasilimali watu zinazotokana na mikataba ya uzalishaji na ugawanaji wa mafuta na gesi asili pamoja na Washirika wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia lengo hilo, katika Mwaka 2012/13 Wizara imeamua kusomesha wanafunzi 10 waliofanya vizuri kidato cha sita katika masomo ya physics, chemistry na mathematics na wenye nia ya kuchukua shahada ya kwanza katika fani ya mafuta na gesi asili katika Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM).* Vilevile, Wizara itachangia gharama za masomo kwa wanafunzi 15 watakaochaguliwa kujiunga katika ngazi ya Cheti na Stashahada katika Chuo cha Madini, Dodoma *(MRI).*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeanza kutayarisha mitaala ya shahada ya uzamili katika fani ya gesi na mafuta na wanafunzi watakaogharimiwa na Wizara yangu wataanza masomo katika Mwaka 2013/14. Pia, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam *(DIT)* inatayarisha mitaala ya stashahada/shahada kwenye fani hii.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa Serikali wa kupunguza matumizi ya fedha za umma,

hasa katika ununuzi wa magari yenye gharama kubwa, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yangu itatekeleza kwa dhati agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu la kudhibiti matumizi ya magari ya aina hiyo kuanzia Mwaka 2012/13. Katika utekelezaji huo, Viongozi Waandamizi wa Wizara wakiwemo Makamishna na Wakurugenzi waliokuwa wanahudumiwa na magari ya gharama kubwa wataanza kutumia magari ya kawaida, ambayo ujazo wa injini hautazidi sentimita za ujazo *(CC)* 3,000 kwa utaratibu wa kukopeshwa.

Mpango huo utawezesha Wizara kuokoa zaidi ya Shilingi bilioni 1.4 kwa mwaka. Fedha hizo zitatumika katika shughuli nyingine za maendeleo. Aidha, mpango huo utapunguza matumizi ya magari ya Serikali baada ya saa za kazi na siku ambazo siyo za kazi.

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa Kimataifa: Wizara ilinufaika na itaendelea kupata misaada na ushirikiano kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo kwa kipindi cha Mwaka 2012/13. Kwa niaba ya Serikali, napenda kutoa shukurani kwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, hususan katika kuwezesha kupatikana kwa mkopo wa masharti nafuu wa Mradi mkubwa wa ujenzi wa bomba la gesi asili kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. Aidha, natoa shukrani kwa Serikali za nchi za Brazil, Canada, Finland, Marekani, Norway, Sweden, Trinidad na Tobago na Urusi. Vilevile, natoa shukurani kwa Benki ya Exim ya China, Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini *(DBSA),* Benki ya *HSBC,* Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya

Afrika *(AfDB),* Benki ya *BADEA,* Benki ya Uwekezaji ya Ulaya *(EIB),* Umoja wa Ulaya *(EU),* pamoja na taasisi na mashirika ya *AFD* (Ufaransa), *CIDA* (Canada), *DANIDA* (Denmark), *ECDF* (Korea Kusini), *FINIDA* (Finland), *JICA* (Japan), *MCC* (Marekani), *NORAD* (Norway), *OFID* (Saudi Arabia), *ORIO* (Uholanzi) na Sida (Sweden), *GEF, GVEP, IDA, IFC, UNDP, UNEP, UNIDO, UNICEF* na Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru Naibu Mawaziri wa Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, anayesimamia masuala ya nishati; na Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, anayesimamia masuala ya madini, kwa kunisaidia kwa kiasi kikubwa na kwa dhati kabisa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nawashukuru Mawaziri wote walionitangulia katika kuongoza Wizara ya Nishati na Madini. Napenda kumshukuru Katibu Mkuu, Bw. Eliakim C. Maswi, kwa uchapakazi wake mahiri na ushirikiano alionipa katika kipindi hiki kifupi tangu niteuliwe kuwa Waziri wa Nishati na Madini. *(Makofi)*

Vilevile, nawashukuru Makamishna wote, Wakuu wa Idara na Vitengo, Viongozi wa Taasisi na Bodi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao katika kufanikisha maandalizi ya bajeti hii. Mwisho lakini si kwa umuhimu, nawashukuru watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake kwa michango yao iliyowezesha kuandaliwa kwa mpango na bajeti hii. Natumia fursa hii kuwakumbusha watumishi wote wa Wizara kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia viapo

tulivyojiwekea siku ya tarehe 21 Mei, 2012 tulipokutana kwa mara ya kwanza. Kipekee, naomba nimshukuru sana mke wangu Bertha Muhongo, wanangu Godfrey Chirangi, Musuto Chirangi, Dkt. Bwire Chirangi na Rukonge Muhongo pamoja na familia yangu kwa ujumla kwa msaada mkubwa wanaonipa. Vilevile namshukuru Mpiga Chapa wa Serikali kwa kukamilisha Taarifa hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mwaka 2012/13 inalenga kutatua matatizo ya kutopatikana kwa umeme wa kutosha na wa uhakika nchini; na kuimarisha usimamizi wa Sekta za Nishati na Madini ili kuongeza mchango wake katika kukuza uchumi wa Taifa, kuongeza ajira hasa kwa vijana na kupunguza umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe bajeti ya jumla ya Shilingi 641,269,729,000 kama ifuatavyo:-

(i) Bajeti ya Maendeleo ni Shilingi 531,190,861,000, sawa na asilimia 82.83 ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo, Shilingi 431,190,861,000 ni fedha za ndani, sawa na asilimia 81.17 ya fedha za maendeleo na Shilingi 100,000,000,000 ni fedha za nje, sawa na asilimia 18.83; na

(ii) Matumizi ya Kawaida ni Shilingi 110,078,868,000, sawa na asilimia 17.17 ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo Shilingi 17,292,347,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Wizara, Mashirika na Taasisi zake (sawa na asilimia 2.70 ya

bajeti yote ya Wizara) na Shilingi 92,786,521,000, sawa na asilimia 14.47 ya bajeti yote ya Wizara, ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC).*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ambaye alishughulikia Wizara ya Nishati na Madini; Mheshimiwa Zedi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI – MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii, kumshukuru Mungu, aliyeniwezesha kuwa na nguvu ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2011 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii yote iingie kwenye *Hansard.*

Awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii, kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa imani na heshima

waliyonipa ya kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii inayosimamia Sekta muhimu kwa Uchumi wa Taifa letu, kufuatia aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa January Y. Makamba, kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; tunampongeza sana na kumwombea heri. Aidha, naomba kuwahakikishia Wajumbe wa Kamati, Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kuwa, sitawaangusha na nawaomba ushirikiano katika kutekeleza majukumu yetu ya Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, niweze kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwa muda wa siku tatu kuanzia tarehe 6 hadi 8 Juni, 2012, katika Ukumbi wa *NSSF – Water Front* (Dar es Salaam), Kamati ilifanya vikao na Wizara ya Nishati na Madini kwa lengo la kupokea utekelezaji wa Maoni ya Kamati uliotolewa wakati wa bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 na kujadili na kuchambua mwelekeo wa bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, katika kikao kilichofanyika tarehe 6 Juni, 2012 katika Ukumbi wa *NSSF Water Front Dar es Salaam*, Kamati ilipokea taarifa ya Wizara juu ya utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 na kubaini baadhi ya maeneo ambayo Serikali bado haijachukua hatua za kuridhisha. Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na:-

(i) Ukamilishwaji wa Sera na Sheria ya Gesi. Pamoja na taarifa ya Wizara kuwa Sera ya Gesi itakamilika mwezi Septemba na Sheria yake Mwezi Disemba 2012, Kamati haioni jitihada za makusudi za utekelezaji wake.

(ii) Kuongeza bajeti ya *REA* kutokana na mapato ya ongezeko la kodi ya mafuta ya taa na tozo ya shilingi tano kwa kila dakika ya maongezi ya simu. Kamati hadi sasa haioni jitihada za Serikali katika utekelezaji wa suala hili.

(iii) Mkakati wa kuwawezesha Watanzania kutoa huduma na bidhaa migodini. Kamati bado haioni jitihada za Serikali katika kutekeleza suala hili.

(iv) Kamati mara kadhaa imeshauri kuhusu upanuzi wa miundombinu ya mafuta kabla ya kuanza kwa mfumo wa *bulk procurement.* Kamati imebaini mfumo umeanza ilhali miundombinu haijapanuliwa, hali inayozoretesha mfumo huu.

(v) Mkakati wa kuandaa Wataalamu wa Kitanzania katika kusimamia Sekta ya Gesi nchini. Kamati haioni jitihada za utekelezaji wa suala hili.

(vi) Kamati kwa mara kadhaa imeshauri Mradi wa ujenzi wa mtambo unaotumia mafuta mazito *(Heavy Fuel Oil - HFO)* kuzalisha MW 60 ulioko Nyakato Mwanza ubadilishwe kutokana na ugumu wa kusafirisha mafuta, lakini Serikali bado inaendelea na ujenzi wake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii, Kamati inaendelea na msimamo wake kuwa ushauri na maelekezo yake yaliyotolewa awali yatekelezwe na kwa msisitizo, maeneo ambayo Serikali haijazingatia ushauri wa Kamati, tutayarejea tena katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Wizara ilitengewa jumla ya shilingi 538,514,071,000. Fedha hizo zililenga katika kuongeza uzalishaji umeme kwa kutekeleza mkakati wa kuimarisha Sekta ya Umeme ili kupunguza mgawo wa umeme; kupanua na kuimarisha Gridi ya Taifa; kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya na Vijijini; kuimarisa usimamizi wa Sekta ya Madini; na kuimarisha taasisi zilizo chini ya usimamizi wa Wizara. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012, fedha iliyotolewa kwa Wizara ilikuwa shilingi 453,223,402,600 tu, sawa na asilimia 84 ya fedha zote zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati hairidhishwi kabisa na utoaji huu wa fedha hasa ikizingatiwa kuwa Wizara hii ni muhimu sana kwa ustawi wa uchumi wa nchi. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kwa mwaka huu wa fedha,

kuhakikisha inatoa fedha zote zitakazoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka huu wa Fedha wa 2012/2013, Wizara ya Nishati na Madini inaomba jumla ya shilingi 641,269,729,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 110,078,868,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambazo pia zimegawanywa katika sehemu mbili; Shilingi 17,292,347,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Wizara na Mashirika yaliyo chini yake na shilingi 92,786,521,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(Other Charges - OC).* Aidha, Miradi ya Maendeleo inaombewa jumla ya Shilingi 531,190,861,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 431,190,861,000 ni fedha za ndani na shilingi 100,000,000,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Wizara hii kwani kiwango kinachoombwa ni nyongeza ya asilimia 19 ya kiasi cha shilingi 538,514,071,000 kilichoidhinishwa na Bunge katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, licha ya Serikali kuongeza bajeti ya Wizara hii, Kamati bado inaona ongezeko hili haliendani na hali halisi ya mahitaji ya Wizara hii hasa ikizingatiwa kuwa Sekta zilizo chini ya Wizara hii ni muhimu sana katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Wizara hii ipewe kipaumbele cha kwanza na kutengewa fedha za kutosha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya mapitio ya taarifa mbalimbali za utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 na Mipango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya kuzingatiwa ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara ya Nishati na Madini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, licha ya taarifa nyingi zilizowasilishwa na Kamati zenye lengo la kuishauri Serikali njia bora za kupunguza tatizo la umeme, bado hali ya upatikanaji wa umeme siyo ya kuridhisha na hii inatokana na sababu mbalimbali ambazo tumekuwa tukizisema mara kwa mara, ikiwemo ya mabadiliko ya tabia nchi yanayopelekea ukosefu wa mvua za kutosha na hivyo kuathiri mitambo ambayo inatumia maji. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, uzalishaji wa mitambo ya maji ulikuwa asilimia 45 ya umeme wote uliozalishwa nchini ikilinganishwa na uwezo wake wa asilimia 51.

Mheshimiwa Spika, hofu ya Kamati hapa ni kuwa, ifikapo miezi ya kiangazi ya Agosti mpaka Oktoba, hatutaweza kuzalisha sehemu kubwa ya umeme utakanao na maji na hivyo kutegemea umeme unaozalishwa kwa gesi na mafuta tu.

Mheshimiwa Spika, hofu nyingine inatokana na ukweli kwamba, wazabuni wanaoiuzia *TANESCO* mafuta na gesi wanadai kiasi kikubwa cha fedha na endapo watasimamisha kutoa huduma ya gesi na mafuta katika kipindi ambacho hakuna maji ya kuzalisha umeme wa kutosha nchi nzima itaingia gizani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukosefu wa maji na hofu ya madeni, kuna suala moja limesahaulika kwa muda mrefu na kujikuta nchi inajikita katika kuhamasisha uzalishaji wa umeme na kusahau miundombinu ya kufua na kusafirisha umeme ambayo imekuwa chakavu sana na hivyo kufanya asilimia 22.5 ya umeme wote unaozalishwa kupotea njiani na mwingine kushindwa kusafirishwa kwenda kwa watumiaji. Ni ukweli uliowazi kuwa, Serikali imetumia juhudi na gharama kubwa sana katika Sekta Ndogo ya Uzalishaji Umeme. Kamati inashauri ili umma uweze kufaidika na juhudi hizo, tuendelee kujifunga mkanda kwa kuboresha mfumo wa usafirishaji mpaka kwa mtumiaji wa mwisho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha, kiasi cha shilingi bilioni 56.5 kimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya vituo sita vya kufua umeme unaotokana na maji na shilingi bilioni 25.1 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya kusafirisha umeme katika Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Kilimanjaro tu.

Kamati inaona bado fedha za ukarabati wa miundombinu ni kidogo sana hasa ikizingatiwa kuwa ni mikoa miwili tu ndiyo imetengewa fedha ikiacha mikoa 28 bila hatua yoyote.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imebarikiwa kuwa na vyanzo vingi vya kuzalisha umeme ikiwemo gesi asili, makaa ya mawe, urani, joto ardhi na upepo. Kamati inaamini kuwa vyanzo hivi vyote vikitumiwa ipasavyo, hakika suala la upungufu wa umeme kwetu litakuwa

historia kwani umeme utakaozalishwa utaweza kuwafikia wananchi wengi zaidi ikilinganishwa na idadi iliyopo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ni asilimia 17 tu ya Watanzania ndiyo wanapata umeme na kati ya hao asilimia 14 ni wale wanaoishi mijini. Ikizingatiwa kuwa asilimia 85 ya Watanzania wanaishi vijijini na kati yao asilimia tatu tu ndiyo wanapata umeme, hiyo inadhihirisha kuwa usambazaji umeme hauna uwiano mzuri hali inayopashwa kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetafakari kwa kina changamoto zilizopo kwenye sekta ya umeme na inapenda kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iamue kwa dhati kabisa kuhakikisha tatizo la upatikanaji wa umeme nchini linakwisha kwa kutenga fedha za kutosha kwenye miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji kwani maeneo yote haya matatu yanategemeana. Imejitokeza kwa maeneo mengi nchini kukosa umeme licha ya umeme kuzalishwa wa kutosha kutokana na miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme kuwa chakavu na hivyo kushindwa kuhimili mzigo.

(ii) Kamati bado ina mashaka juu ya mradi wa ujenzi wa mtambo unaotumia mafuta mazito *(Heavy Fuel Oil - HFO)* kuzalisha megawati 60 ulioko Nyakato Mwanza. Mtambo huu unatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2013 licha ya taarifa za awali kuonesha ungekamilika mwezi Juni 2012. Pamoja na ucheleweshaji mashaka ya Kamati ni juu ya ugumu wa

kusafirisha mafuta mazito kwenda Mwanza ukizingatia umbali kutoka bandari ya Dar es Salaam na uzoefu tulionao katika kusafirisha mafuta kwenda kwenye mitambo ya *IPTL*.

Kikwazo cha usafirishaji kinaongezewa uzito na tatizo la utunzaji kwani si rahisi kupata Kampuni ya kukusaidia kukutunzia au kukuazima mafuta *(hospitality arrangement*) Mwanza endapo mtambo huo wa Nyakato utaishiwa mafuta. Kamati bado inarudia ushauri wake ambao imeutoa zaidi ya mara moja kuwa Serikali iangalie uwezekano wa Mtambo huo wa kutumia mafuta mazito uende sehemu ambayo upatikanaji wa mafuta hayo ni wa uhakika na mtambo huo wa Mwanza utumie dizeli.

(iii) Pamoja na ahadi iliyotolewa na Waziri Mkuu mnamo mwezi Agosti, 2011 kuwa Serikali itaipa dhamana *TANESCO* ili iweze kukopa jumla ya shilingi bilioni 408, ahadi hii bado haijatekelezwa mpaka sasa. Kamati inaitaka Serikali ieleze bayana kama dhamana inatakiwa au la na kama haihitajiki ni nini mbadala au suluhisho la kilio chetu cha awali. Ikumbukwe maamuzi ya kuitaka Serikali kuidhamini *TANESCO* kupata mkopo huu yalitokana na Azimio la Bunge.

(iv) Kwa muda mrefu sasa nchi yetu imejikuta ikiingia gharama kubwa kulipia mitambo ya kukodi na hasa suala la *capacity charge*. Kamati mara kwa mara imeshauri Serikali kununua mitambo yake badala ya ile ya kukodi. Kwa mfano, kwa mwaka 2011/2012 mitambo yote ya kukodi imetugharimu shilingi 144,907,258,894/= kama *capacity charge*. Huu ni

mzigo mkubwa sana kwa Taifa letu. Kamati inaitaka Serikali kutoa taarifa katika kutekeleza ushauri huu wa Kamati juu ya suala hili.

(v) Kwa mara kadhaa Kamati imeshauri juu ya kuanzishwa kwa Mfuko wa kuendeleza nishati ya umeme nchini kwa lengo la kutumia Mfuko huo kama mtaji (*Equity*) ili fedha zake zitumike katika kuboresha huduma ya upatikanaji wa umeme nchini na pia kukopa kutoka vyombo vingine vya fedha. Lakini bado suala hili limekuwa gumu kutekelezwa licha ya umuhimu wake. Kamati inasisitiza ushauri wake wa awali kuwa Serikali ianzishe Mfuko huu na utunishwe kwa vyanzo vifuatavyo:-

(a) Kuanzisha ushuru wa huduma ya nishati ya umeme (*surcharge*) kwa makampuni yanayotumia umeme mwingi.

(b) Msamaha wa kodi ya kuagiza vipuri vya mitambo ya kuzalisha na kufua umeme iwe inalipwa moja kwa moja kwenye Mfuko huo badala ya kwenda Hazina.

(c) Msamaha wa kodi ya kuagiza mafuta ya kuendesha mitambo ya kufua umeme *(import excise duties*) iwe inalipwa moja kwa moja kwenye Mfuko huo badala ya kwenda Hazina.

(d) Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* itokanayo na mauzo ya umeme iwe inalipwa moja kwa moja kwenye Mfuko badala ya kwenda Hazina.

(e) Mifuko ya Hifadhi ya Jamii isaidie kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha Mfuko wa uendelezaji wa nishati

(vi) Zimekuwepo taarifa za mipango mbalimbali ya kuzalisha umeme ikiwemo *Stiglers Gorge* na ile ya Kiwira inayosimamiwa na mamlaka mbalimbali. Kamati inashauri, kwa kuwa Wizara ya Nishati na Madini ndiye mmiliki na msimamizi mkuu wa *Power System Master Plan* ya Taifa, taasisi zote zitakazojihusisha na uzalishaji wa umeme, toka hatua ya awali zifanye kazi kwa karibu na Wizara. Ili kufanikisha azma ya ushauri na usimamizi ni busara pia Bunge likapewa taarifa kupitia Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme vijijini; ninapozungumzia umeme naomba nirejee takwimu za usambazaji wa umeme nilizoeleza awali. Tumeweza kusambaza umeme kufikia asilimia 17 ya kaya zote nchini, kati ya hizo asilimia tatu ni wakazi wa vijijini, asilimia 14 wakiwa mijini. Pamoja na kuwa kiwango cha asilimia 17 kwa nchi ni kidogo lakini asilimia tatu kwa Watanzania asilimia 85 wanaoishi vijijini bado ni kidogo mno.

Mheshimiwa Spika, hali hii inapingana na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa muda mfupi ambao unataka ifikapo mwaka 2016 wananchi wa vijijini wafikiwe na umeme kwa asilimia 16. Aidha, Kamati haioni kama ni sawa na haki wananchi wa vijijini kukosa umeme. Pamoja na utetezi uliopo kuwa shughuli nyingi za kiuchumi zipo mjini, Kamati bado inaamini kuwa kwa kupeleka umeme zaidi vijijini

tutaweza kuchangamsha uchumi vijijini na kupata manufaa ya kiuchumi na kijamii vijijini na mijini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri ufuatao ili kuboresha upatikanaji wa umeme vijijini:-

(i) Serikali iongeze bajeti ya Wakala wa Umeme Vijijini ili wananchi wengi zaidi waweze kunufaika na huduma hii muhimu kwani uwepo wa umeme utasaidia pia kuongeza thamani ya mazao yao kwa kuwa na viwanda vya usindikaji *(processing industries)* kuliko ilivyo sasa mazao mengi yamekuwa yakiharibika kabla ya kufika sokoni.

(ii) Sehemu ambazo *REA* imepitisha/itapitisha umeme karibu na wananchi basi mamlaka zilizoko sehemu hizo zishirikiane na wananchi kuhakikisha nyumba za wananchi, majengo ya Serikali na asasi nyingine zinafunga umeme mara moja ili kuonesha mafanikio ya mradi.

(iii) Kwa kuwa maeneo mengi ya vijijini hayafikiwi na umeme wa gridi ya Taifa, Kamati inashauri jitihada ziongezwe kwenye kusambaza umeme unaotokana na nguvu ya jua (*solar*) wakati tukisubiri gridi kufika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sSekta Ndogo ya Gesi; Kamati imefarijika na juhudi zinazoendelea za utafutaji wa mafuta na gesi nchini kwani kasi iliyopo ni kubwa na inaonesha mafanikio ya hali ya juu. Makampuni mbalimbali makubwa yamekuwa mstari wa mbele

katika utafutaji huo katika maeneo ya nchi kavu, mwambao na bahari ya kina kirefu. Ugunduzi wa gesi kwenye visima vitatu vilivyochimbwa na Kampuni ya *Ophir* na *British Gas* mwaka 2010/2011, ulidhihirisha uwezekano mkubwa wa miamba tabaka iliyopo kwenye kina kirefu cha maji baharini kuwa na uwezo wa kuhifadhi mafuta au gesi kwani kunakisiwa kuwepo kwa gesi kiasi cha futi za ujazo trilioni 7.5 hadi 12.5.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ugunduzi huo na umuhimu wake kwa Taifa, Kamati inaamini kuwa gesi ni mkombozi wa Mtanzania. Serikali iamue sasa Gesi Kwanza na hii inatokana na ukweli kwamba matumizi na faida za gesi kiuchumi na kijamii ni kubwa sana. Takwimu zinaonesha kuwa kwa kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, kiasi cha futi za ujazo bilioni 4.28 cha gesi kilitumika katika viwanda na taasisi badala ya mafuta na *Liquified Petroleum Gas (LPG*) na hivyo kuokoa fedha za kigeni kiasi cha dola za Marekani milioni 71.77.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kipindi hicho hicho kiasi cha gesi chenye futi za ujazo bilioni 22.69 kilitumika katika kuzalisha umeme badala ya mafuta mazito na mafuta ya ndege *(Heavy Fuel Oil na Jet A1*) na hivyo kuokoa fedha za kigeni kiasi cha dola za Kimarekani milioni 748.32 ambazo zingetumika kununulia mafuta hayo.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo haya mawili jumla ya futi za ujazo bilioni 26.97 zilitumika na kuokoa takribani shillingi za Kitanzania trilioni 1.2 katika kipindi cha miezi tisa pekee katika fedha za kigeni. Huu ndio

umuhimu wa gesi asili na neema tuliyopewa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, utaona dhahiri kuwa kutumia gesi kuna faida kubwa sana kiuchumi. Upatikanaji wa gesi asili kwa wingi kutapunguza kasi ya uagizaji wa mafuta jamii ya petroli *(import substitution),* hivyo kuokoa fedha haba za kigeni. Aidha, kwa matumizi ya majumbani hususan mkaa, tafiti zinaonesha kuwa katika Jiji la Dar es Salaam magunia ya mkaa yapatayo 40,000 hutumika kwa siku yenye gharama ya shilingi bilioni 584 kwa mwaka, endapo tutaweza kujenga na kutumia mtandao wa gesi asili kwa Jiji la Dar es Salaam tu tutatumia nishati ya shilingi bilioni 408 na hivyo kuokoa shilingi bilioni 176 ikiwemo faida kubwa ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu huo wa gesi, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuamua kujenga Bomba kubwa la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es salaam kwa mkopo wa dola za marekani bilioni 1.225. Aidha, ikumbukwe kuwa mradi huu ulitakiwa kuanza tangu mwaka 2011 lakini ilishindikana kutokana na sababu mbalimbali. Hivyo basi, Kamati inaitaka Serikali kuchukua jitihada za makusudi za kuhakikisha bomba hili linakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa mnamo mwaka 2013 kwani kinyume na hapo miradi mingi ambayo inategemea gesi hii ili kuanza utekelezaji haitawezekana na hivyo nchi kujikuta inaingia gizani hali ambayo haitaweza kuvumilika.

(ii) Kama ilivyokubalika katika vikao vya Wizara na Kamati tunasisitiza kuwa, Sera na Sheria za Sekta Ndogo ya Gesi Asili vipitiwe haraka na kwa umakini wa hali ya juu na viwasilishwe kwa maamuzi kwenye Bunge la Mkutano wa Tisa.

(iii) Jambo kubwa ambalo Kamati inasisitiza ni kuwa, lazima liwemo ndani ya Sera ya gesi na ndani ya Sheria ya Gesi, ni namna bora ya kusimamia mapato yatakayotokana na gesi (*Natural Gas Revenue Management),* Kamati inashauri kuwa, mapato yote yatokanayo na gesi, yasichanganywe na mapato mengine kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina na badala yake, yawekwe kwenye Mfuko wake Maalum na yaelekezwe kwenye matumizi maalum yatakayoidhinishwa na Bunge.

(iv) Kamati inasikitishwa na uamuzi wa Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*) kuendelea na mchakato wa ugawaji wa vitalu vipya nane vya utafutaji na uchimbaji wa gesi. Msimamo wa Kamati ni kuwa, wakati bado kuna kizungumkuti cha mikataba isiyo na tija kwa Taifa hili iliyotokana na ukosefu wa usimamizi thabiti wa kisheria, *TPDC* isitishe ugawaji wa vitalu vipya vya uchimbaji mpaka hapo Sheria ya Gesi itakapokuwa tayari na kuanza kutumika rasmi.

(v) Pamoja na kutambua jitihada zinazofanywa na timu ya majadiliano ya Serikali *(Government Negotiating Team)* kuhusu fedha dola za Kimarekani 64,000,000 zinazohusisha Kampuni ya *Pan African*

*Energy Tanzania Limited (PAT),* msimamo wa Kamati ni kuwa dola za Kimarekani milioni 20.1 zilizothibitishwa na pande zote mbili hazina mjadala wa kulipwa. Kwa mara nyingine tena, Kamati inaendelea na msimamo wake wa kuitaka Serikali imtake mbia wake *(PAT)* alipe fedha hizo mara moja.

(vi) Kamati inashauri, Serikali iwekeze katika mawasiliano kwa kuwa wa kwanza kuwajulisha wananchi nini kinachoendelea katika sekta. Pamoja na kupewa taarifa, umma uelimishwe juu ya manufaa ya sekta hii na ni kwa vipi hatuwezi kukumbana na matatizo yaliyotupata katika mikataba ya nyuma *(PAT)* na ile ya madini.

Mheshimiwa Spika, Mafuta jamii ya petroli kama nishati ni nyenzo muhimu kwa maendeleo na ustawi wa nchi. Ustawi wa sekta za usafiri na usafirishaji, viwanda, mawasiliano, kilimo, biashara na shughuli za kijamii hutegemea kwa kiasi kikubwa nishati hii. Kamati yetu kwa kipindi cha uhai wake tumejitahidi kushauri na kusimamia sekta ya mafuta kwa kuangalia mfumo wa upatikanaji wake, ubora na bei. Kamati yetu imeishauri Serikali kupitia vikao mbalimbali na tumeandika taarifa mahsusi kuhusu shughuli za mafuta jamii ya petroli (*down stream activities).*

Mheshimiwa Spika, Ubora wa mafuta; itakumbukwa kuwa kabla ya Bajeti ya Mwaka 2011/12, Taifa lilikuwa na tatizo la uchanganyaji wa mafuta ulioathiri ubora kwa kiwango cha hali ya juu. Jitihada kubwa zilifanyika ikiwemo matumizi ya vinasaba, lakini hatukupata mafanikio chanya katika kudhibiti uhalifu

huu. Wakati wa Bajeti ya Mwaka 2011/2012, Kamati hii ilitoa ushauri wa kuongeza kodi ya ushuru kwenye mafuta ya taa ili iwiane na ile ya petroli audizeli kwa lengo la kupunguza kichocheo cha uchakachuaji. Serikali ilipokea ushauri wa Kamati na kuongeza kodi hiyo. Mpaka tunapoandika taarifa hii uchakachuaji umeshuka kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na manufaa ya kuwa na mafuta yenye ubora ni muhimu wadau wote tukatambua kuwa uamuzi huu muhimu uliliwezesha Taifa kuokoa kiasi kikubwa cha fedha kwa njia ya kodi. Itakumbukwa uchakachuaji wa mafuta ulikuwa unawapatia wahusika kati ya shillingi bilioni 30 mpaka 50 kwa mwezi. Kipimo rahisi cha ukweli huu ni kuwa baada ya uamuzi huu kiasi cha mafuta ya taa kinachoagizwa kimepungua kwa wastani wa asilimia 62.1, hii ni kwa kulinganisha kiasi kilichoagizwa katika vipindi vinavyofanana yaani, Januari – Juni 2011 na mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika kudhibiti uchakachuaji, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Mamlaka husika hasa *EWURA* na *TRA* waelekeze nguvu katika kudhibiti uchakachuaji na ushushaji mizigo inayokwenda nchi jirani kwa kutumia *road patrol, GPS* na uhakiki wa kushtukiza mipakani hata njiani. Pia usambazaji wa mafuta ya ndege na yale ya kuendesha mitambo ya umeme ambayo kimsingi kampuni husika ni chache usimamiwe kwa karibu kuzuia kuingia sokoni.

(ii) *EWURA* iwekeze katika uchunguzi na upelelezi juu ya njia nyingine zinazoweza kutumika kuathiri ubora wa mafuta na kukosesha Serikali mapato. Taarifa juu ya uchanganyaji wa *condensate* zifanyiwe kazi na hatua kali zichukuliwe haraka. Aidha, ushauri wa Kamati juu ya kuongeza adhabu kwa wanaochezea ubora wa mafuta bado huko pale pale.

(iii) Kutokana na hali halisi ya kupungua kwa tatizo la uchakachuaji mradi wa vinasaba uliobuniwa kudhibiti uchanganyaji wa mafuta usitishwe. Pia kwa kuwa tozo hii ilishazoeleka kwa wadau tunashauri pato kutokana na njia hii ambayo ni takribani shillingi bilioni 10 kwa mwaka ipelekwe kwenye miradi ya umeme ya *REA*.

(iv) Kutokana na kuongezeka kwa fursa katika sekta ya mafuta na gesi asili, moja ya sekta ambayo Watanzania wote wameweka matumaini yao, sekta ambayo inajenga uhitaji wa rasilimali nyingi ikiwemo dhamana za Serikali, Kamati inashauri sekta hii muhimu iundiwe Mamlaka ya Udhibiti itakayoisimamia kwa karibu, yaani *Energy Regulatory Authority (ERA)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali kudhibiti bei ya mafuta kupitia *EWURA* na uamuzi wa uagizaji mafuta kwa wingi bado mwananchi wa kawaida hajaona matunda ya jitihada hizo. Kamati inatambua kuwa jitihada zenye nia nzuri zimekumbana na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia, lakini pia kudhoofu kwa fedha yetu hapa nyumbani. Kamati inashauri Serikali kwa kutumia mamlaka zake

zote iendelee kutafakari njia bora zaidi za kudhibiti bei kubwa ya mafuta. Kamati yetu inaahidi kutoa ushirikiano na Serikali katika kutimiza azma hii.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Wingi *(Bulk Procurement System)* kwa pamoja ulianzishwa kwa lengo la kuleta unafuu wa bei za mafuta nchini, kuboresha upatikanaji wa takwimu sahihi za mafuta yanayoingizwa nchini na pia kuboresha makusanyo ya kodi itokanayo na biashara ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza haya, Serikali iliunda Kamati ya usimamizi wa mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja ili ikuhakikisha mfumo unafanya kazi na pia kumshauri Waziri kuhusu masuala ya usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini. Aidha, Makampuni ya mafuta yalikamilisha usajili wa Kampuni inayoratibu uagizaji wa mafuta kwa pamoja *(Petroleum Importation Coordinator – PIC*) na pia kanuni ziliundwa kwa lengo la kusaidia usimamizi wa mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na malengo mazuri ya mfumo huu, utekelezaji wake umeonesha upungufu mkubwa hali inayoashiria hasara kubwa kwa sekta hii siku za usoni:-

(i) Viwango vinavyotumika kuamua bei ya manunuzi (*premium*) vimeendelea kuwa vya juu kuliko kabla ya mfumo huu.

(ii) Kiasi kikubwa cha mafuta kinapotea kwa kulinganisha takwimu za bandari ya kupakia na ile ya kupakulia (*KOJ*) na hii gharama kusukumwa kwa mlaji au kudhoofisha pato la makampuni shiriki.

(iii) Uendeshaji wa kampuni ya uagizaji mafuta (*PIC*) unatia mashaka hali inayoweza kuliingiza Taifa katika hasara kubwa kutokana na kujengeka kwa gharama zisizo wazi kwa walaji.

(iv) Kumekuwepo hali ya kutokuwa huru, kutokuaminiana na ushirikiano duni miongoni mwa wadau.

(v) Mafuta yanayoagizwa yamekuwa na viwango duni ikilinganishwa na kipindi kabla ya mfumo. Dizeli nyingi inayoingizwa imekuwa ni ile ya kiwango cha chini kinachotakiwa (*minimum cut point)* ikilinganishwa na kipindi kilichopita ambapo kuna makampuni yaliteka soko kwa kuleta dizeli ya kiwango cha juu.

(vi) Umejitokeza upungufu mkubwa katika udhibiti wa ubora wa mafuta ambapo petroli yenye *ethanol* kupita kiasi imeingizwa nchini bila kugundulika mpaka pale ilipoleta madhara kwa walaji.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maoni na ushauri juu ya mfumo wa uagizaji mafuta kwa wingi naomba nirejeee msimamo wa Kamati kuhusu uamuzi wa Bunge. Kamati yetu bado inaunga mkono Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Wingi kwa nia na malengo yaliyoainishwa Bungeni wakati wa kupitisha uamuzi wa

kutumia mfumo huu. Kwa msimamo wetu huo Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Kama tulivyoshauri wakati wa kuanzisha mfumo huu, Serikali ihakikishe miundombinu itakayoleta ufanisi wa uagizaji wa pamoja imejengwa na ijengwe haraka. Kwa kuwa na miundombinu itakayowezesha meli kubwa *(LR 1 to LR 2)* kufunga kwenye boya viwango vya *premium* vitashuka.

(ii) Ni masikitiko ya Kamati kuwa ushauri wa njia rahisi ya kuzuia hasara itokanayo na tofauti ya takwimu katika bandari mbili ulipuuzwa na Serikali. Tunashauri tena utaratibu wa kubadili miliki ufanyike katika bandari ya kupakulia *(KOJ)* badala ya kutumia takwimu za bandari ya kupakia. Pamoja na kupuuzwa kwa ushauri wa Kamati, tunapenda kuhoji kama uamuzi wa kupuuza ushauri ulitokana na uelewa duni wa watendaji au ni katika kutimiza maslahi binafsi.

(iii) Serikali iingilie kati utendaji wa *PIC* kwani upungufu unaoonekana sasa ni vigezo tosha vya ukiukwaji wa mfumo bora wa uagizaji wa mafuta kwa wingi. Kuongezeka kwa gharama za ucheleweshaji na mlundikano wa meli, baadhi ya makampuni kushindwa kulipia mizigo kwa wakati, utangazaji wa tenda kwa kiasi ambacho ni zaidi ya uwezo wa miundombinu kupakua na kushindwa kudhibiti makampuni waviziaji (*speculators*).

(iv) Serikali ilenge kuboresha sekta ndogo ya mafuta kwa kuhakikisha wadau wanajenga maelewano miongoni mwao. Ustawi wa sekta kwa

maslahi ya Taifa, ufanisi na tija kwa walaji vitapatikana iwapo washiriki wanaendesha shughuli zao kwa uhuru.

(v) Kamati imesikitishwa na upungufu katika kanuni zinazotawala uagizaji wa pamoja, mamlaka ya *EWURA* na *TBS* kushindwa kuzuia mafuta yasiyo na viwango kuingia sokoni. Aidha, muda uliotumiwa na maabara ya Mkemia wa Serikali katika kutoa majibu ulikuwa mrefu sana kiasi cha kutia mashaka na hofu unapofikiria hatima ya mlaji. Kamati inashauri Serikali ilipitie kwa njia ya upekee tukio hili na kurekebisha upungufu uliojitokeza.

(vi) Pamoja na kuchelewa kutoa majibu taarifa za Mkemia wa Serikali zinaonesha petroli iliyouzwa nchini kwa kipindi cha Januari na Machi 2012 ilikuwa na *ethanol* zaidi ya kiwango kinachotakiwa. Kamati inashauri, kwa kuwa upangaji wa bei ya mafuta ulizingatia viwango vya petroli vya *mediteranian* na kwa kuwa mkandarasi aliahidi kuleta petroli yenye viwango, hivyo basi, kwa kuchanganya mafuta ambayo bei yake ya soko haizidi dola za Kimarekani 300 kwa tani badala ya ile ya wastani wa dola za Kimarekani 950 kwa tani. Kutokana na jambo hili, Serikali iwaombe radhi Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu.

(vii) Kwa kuwa Bunge liliamua kwamba mafuta yote yanayotumika kwenye soko la ndani yatanunuliwa kwa mfumo wa uagizaji kwa pamoja *(Bulk Procurement)* na kwa kuwa kumekuwepo na taarifa kuwa kuna mafuta ya matumizi ya ndani ambayo hayapitii mfumo huo. Kamati inakusudia

kuunda Kamati ndogo ili kubaini ukweli juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kudokezea jinsi miundombinu ya mafuta ilivyochangia kudhorotesha mafanikio ya mfumo wa uagizaji kwa wingi, napenda nirejee na kuelezea kwa sehemu hii kwa kina. Tunapoongelea miundombinu ya mafuta tunamaanisha miundombinu ya kupakua na matenki ya kuhifadhi. Kwa ufupi ni kwamba hali ya miundombinu ya kushusha mafuta bado haikidhi mahitaji ya sasa. Katika vikao vyake na Mamlaka ya Bandari Tanzania (*TPA*) Kamati ilijulishwa mradi wa ujenzi wa boya kubwa la kupakua mafuta *(Single Point Mooring – SPM)* ungekamilika mwezi Machi, 2012 na baadaye mwezi Juni, 2012. Mpaka Kamati inaandika taarifa hii, bado ujenzi huo haujakamilika. Kamati inashauri Serikali isimamie ukamilishwaji wa ujenzi huu muhimu.

Mheshimiwa Spika, suala la hifadhi ya mafuta nalo ni tatizo. Kamati ilielezwa hapo awali kuwa *TPA* wanatafuta eneo kwa ajili ya ujenzi wa matenki ya kuhifadhi mafuta. Kupitia Kamati tulishauri hifadhi hiyo isijengwe Kurasini karibu na *dockyard* kwani gharama za kusawazisha kiwanja zitazolipwa kwa hela za wananchi ni kubwa sana. Kamati ilishauri na inaendelea kushauri kuwa, ili kuokoa fedha za Watanzania, *TPA* watumie eneo la kutosha lililopo nje ya uzio wa *TIPER*.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati inaishauri *TPA* kuwa, badala ya kutumia mabilioni ya fedha za Watanzania

kujenga matenki mapya, *TPA* iingie makubaliano maalum ya kutumia matenki makubwa ya hifadhi ya *TIPER*, yenye uwezo mkubwa wa kuhifadhi ambao kwa sasa hautumiki wa futi za ujazo 147,000. Ikumbukwe kuwa hifadhi kubwa ya mafuta ya *TIPER* inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 50, Kamati inaishauri Serikali kutotumia mabilioni ya fedha kujenga matenki mapya ya kuhifadhia mafuta, wakati Serikali hiyo hiyo inamiliki matanki ya kuhifadhi zaidi ya futi za ujazo 147,000, matenki ambayo kwa sasa ujazo wake wa uhifadhi wa mafuta unatumika kwa asilimia ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kampuni ya Taifa ya Mafuta; Mapitio ya taarifa ya Wizara na asasi zilizo chini yake yamedhihirisha upungufu ambao Serikali kwa haraka inabidi iufanyie maamuzi. Mipango na mikakati ya Serikali haioneshi ni kwa vipi itaendesha na kudhibiti Sekta ndogo ya mafuta *(down stream activities)* kwa marefu na mapana yake. Hali hii inaliweka Taifa katika hatarisho pale ambapo makampuni ya mafuta yaliyopo yatakapositisha shughuli kwa sababu moja au nyingine. Mbali na tishio la kusitisha shughuli ni uwekezaji usiozingatia mahitaji ya Taifa kwa makampuni kulenga maeneo yenye faida kubwa tu. Kamati inahoji utekelezaji wa maagizo ya Bunge juu ya ufufuaji na uendeshaji wa *COPEC* umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kukalia kiti cha rubani katika kuendesha sekta hii. Tungependa kuona Wizara inaandaa na kuwa na wataalam wanaomudu shughuli za usafirishaji, hifadhi, ubora, masoko na uchukuzi wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua mchango wa Sekta ya Madini katika maendeleo ya Taifa endapo kunakuwepo usimamizi wa kutosha. Hata hivyo, mchango wa sekta hiyo umekuwa sio wa kuridhisha kutokana na upungufu mbalimbali. Takwimu zinaonesha kuwa katika mwaka wa fedha 2011/2012, kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji wa mawe kilishuka na kuwa asilimia 2.2 ikilinganishwa na asilimia 2.7 mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kushuka kwa kiwango cha shughuli za kiuchumi za madini, lakini thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi yaliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 1536.93 mwaka 2010/2011 hadi kufikia dola za Marekani milioni 1965.23 sawa na ongezeko la asilimia 27.6 na hii ilitokana na kupanda kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa bei ya madini inaongezeka thamani katika soko la Kimataifa, mchango wake katika uchumi wa nchi ni mdogo sana. Kamati imepokea taarifa ya baadhi ya makampuni ya madini kulipa mrahaba wa asilimia nne. Aidha, Kamati haijaridhishwa na kasi utekelezaji wa sheria hii. Kamati inashauri Serikali iongeze kasi katika kuhakikisha makampuni yote yanalipa mrahaba wa asilimia nne kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na malipo ya mrabaha, kama Taifa tunategemea mapato yatokanayo na kodi ya makampuni *(corporate tax).*

Kama nilivyoeleza awali bei ya dhahabu na madini mengine imepanda kwa kiasi kikubwa katika Soko la Kimataifa, hivyo busara ya kawaida inatutuma kuamini kuwa makampuni yote yenye muda mrefu katika shughuli yanapaswa kuwa yanalipa kodi hiyo kwa sasa. Kamati inaishauri Serikali ifafanue suala hili ili kuwajengea imani wananchi.

Mheshimiwa Spika, kipo kitendawili cha Watanzania kushiriki na kushirikishwa katika sekta ya uchimbaji madini hasa unaohusisha wachimbaji wakubwa. Ni ukweli ulio dhahiri na wananchi wameaminishwa kuwa faida ya uchimbaji wa madini iko katika ugavi kwani asilimia kubwa ya gharama za utafutaji na uchimbaji wa madini ni gharama za ugavi. Hoja ya Kamati hapa ni kwa vipi Serikali inawaandaa na kuwawezesha wananchi ili wawe wagavi *(suppliers)* shindani kwa manufaa ya Taifa letu. Habari za uagizaji wa mchicha, kuku, mayai na hata nyama kutoka nje ya nchi kwa ajili ya watendaji katika shughuli za madini hazijengi taswira nzuri kwa sekta na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetafakari kwa kina changamoto zilizopo kwenye Sekta hii muhimu kwa uchumi wa Taifa hili na inatoa mapendekezo yafuatayo:-

(i) Bado mchango wa sekta hii ni mdogo sana. Hakuna muingiliano wa sekta ya madini na sekta nyingine nchini. Watanzania hawashiriki katika kutoa huduma za ugavi ambazo zinachukua takribani 80% ya gharama zote za uendeshaji wa migodi. Serikali na pale inapohusika Halmashauri za Wilaya ziwaandae

wananchi na kuwawezesha Watanzania wengi zaidi kushiriki katika kutoa huduma za ugavi.

(ii) *Local Authority Finance Act* inaitaka migodi izilipe Halmashauri 0.3% ya *Turnover* wakati *MDA's* zina kifungu kinachosema wenye migodi watalipa fedha isiyopungua dola za Kimarekani 200,000. Huu ni mkanganyiko wa hali ya juu na inazinyima Halmashauri haki yake. Serikali iamue kwa dhati kurekebisha mkanganyiko huu.

(iii) Kutokana na suala la ajira ya watoto kutofanyiwa kazi kwa ushauri uliotolewa na Kamati, tunarudia kushauri sheria ya kupinga ajira ya watoto isimamiwe ipasavyo na ikibidi kuwepo na mkakati maalum wa kutekeleza suala hili. Aidha, kwa wale watakaokiuka basi mikataba yao ifutwe au ifungwe na pia washtakiwe kwa mujibu wa sheria.

(iv) Sheria za ardhi ziangaliwe upya, ili wananchi ambao wanapisha maeneo yao kwa ajili ya uwekezaji licha ya kupata fidia ya kupisha maeneo yao, wapewe hisa kwenye migodi kama wanavyofanya katika miji mikubwa mfano Dar es Salaam (Kariakoo) kwani wanauza maeneo yao kwa ajili ya ujenzi, wanapewa hisa na baada ya miaka kadhaa wanamiliki majengo hayo.

(v) Serikali ihakikishe kuwa migodi yote mikubwa, kabla ya kuanza uchimbaji au ikiwa inaendelea na uchimbaji, inaweka dhamana ya uharibifu wa mazingira *(Rehabilitation bond)* ili mgodi unapomaliza uchimbaji wake au ukiamua kuutelekeza mgodi, basi

kuwe na fedha ambazo zitatumika kurudishia mazingira kama yalivyokuwa kabla ya mgodi kuanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wachimbaji wadogo; kwa muda mrefu Kamati imekuwa ikiongelea changamoto wanazokumbana nazo wachimbaji wadogo nchini. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kukutana na wachimbaji wadogo ili kupokea changamoto zao na kuandaa mpango mkakati wa kurekebisha hali hii kwani Kamati ilipata fursa ya kuhudhuria kikao hicho ambacho kilijumuisha wawakilishi wawili wa wachimbaji kutoka kila Mkoa. Katika kikao hicho mambo kadhaa yalizungumzwa na wadau:-

(i) Bajeti ya Mfuko wa kuwasaidia wachimbaji wadogo ni kiasi kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi;

(ii) Elimu haitolewi ya kutosha kwa wachimbaji na hivyo kufanya kazi zao kuwa ngumu;

(iii) Uhaba wa maeneo ya uchimbaji kwani maeneo mengi yamechukuliwa na wawekezaji wakubwa na wengi wanahodhi maeneo bila kuyafanyia kazi hali inayowanyima fursa wawekezaji wadogo;

(iv) Haja ya Serikali kushirikisha mamlaka zote katika kudhibiti uvamiaji wa maeneo katika kutafuta madini *(mineral rush);*

(v) Ukosefu wa masoko ya kuuza bidhaa zao; na

(vi) Kodi kubwa katika vifaa na mitambo ya kufanyia kazi ilihali makampuni makubwa yanapata msamaha wa kodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kuandaa mkutano huo wa wachimbaji wadogo ambao ulimalizika kwa kuandaa mpango mkakati wa kutatua matatizo yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

(i) Kamati imesikitishwa kuona bajeti ya wachimbaji wadogo ni ndogo na haikidhi mahitaji yao. Katika mwaka huu wa fedha shilingi bilioni 8.9, zimetengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 2.5 ni fedha za ndani na zilizobaki shilingi bilioni 6.4 ni fedha za nje. Kamati inashauri kuwa, ili kuleta ufanisi na kuifanya sekta hii iwe endelevu, tulenge kutumia fedha zinazotokana na vyanzo vya ndani na kwa kiasi kikubwa tuepuke kutegemea wahisani. Aidha, Serikali iweke utaratibu utakaohakikisha bajeti hiyo inawafikia wachimbaji wenyewe si watu wa kati.

(ii) Kutokana na wachimbaji wadogo kukosa elimu ya kutosha kuhusu masuala ya utafutaji, uchimbaji, uongezaji thamani na masoko, Kamati inashauri Serikali iweke utaratibu utakaowawezesha wachimbaji wadogo kupata mafunzo hayo muhimu. Aidha, elimu itolewe kwa mamlaka na watendaji mbalimbali ili waache kuwa kikwazo na wageuke kuwa

wawezeshi katika kujenga na kuendeleza sekta hii muhimu.

(iii) Maeneo ya uchimbaji na leseni; Kutokana na Wachimbaji wadogo kukosa maeneo ya kuchimba, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inatenga kwa kila kanda maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo kwani wachimbaji hawa ni raia wa nchi hii na wengi wao wamepisha maeneo yao kwa ajili ya wachimbaji wakubwa.

Leseni kubwa za utafiti na uchimbaji wamepewa watu ambao wengi hawazifanyii kazi na hivyo kuhodhi maeneo hayo hali inayopelekea wachimbaji wadogo kushindwa kupewa leseni ndogo za uchimbaji. Kamati inashauri Serikali iwafutie leseni wachimbaji wakubwa ambao wanahodhi maeneo bila kuyafanyia kazi na kugawa maeneo hayo kwa wachimbaji ambao wako tayari kuyaendeleza. Kamati inashauri kuwa Serikali isitoe leseni ya uchimbaji kwa mtu yeyote ambaye alipewa leseni ya utafiti na muda ukapita bila kufanya utafiti.

Kutokana na tatizo la leseni za wachimbaji wadogo kupewa kwa zaidi ya mtu mmoja, Kamati inashauri Serikali iwe makini na kuhakikisha kuwa kila leseni moja inatolewa kwa mtu mmoja na kwa wakati.

Vyama vya wachimbaji viwe vinapewa taarifa juu ya maeneo ambayo yako wazi tofauti na sasa maeneo yaliyo wazi hayajulikani na yanatumiwa vibaya na watendaji wa sekta ya madini kwa maslahi yao binafsi.

Wachimbaji wadogo waachane na tabia ya kuuza leseni zao kwa wachimbaji wakubwa kwani haitasaidia kuwainua na badala yake itaendelea kuwadididimiza kwani pesa wanayopewa mara nyingi ni ndogo na baada ya kwisha ndiyo wanaanza kulalamika hawana maeneo ili hali waliuza kwa ridhaa zao wenyewe.

Serikali itekeleze mkakati wake wa kuainisha maeneo ya wachimbaji wakubwa na wadogo kulingana na wingi wa madini ili wasiingiliane.

Serikali iweke mfumo utakaosaidia kujua mchango wa uchimbaji mdogo kwenye pato la Taifa. Hii itasaidia kuweka mikakati ya kuongeza juhudi.

Kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 ambayo iliweka bayana kuwa madini ya vito yatachimbwa na wazawa kwa asilimia 100 na kwa kuwa leseni kubwa ya Kampuni ya Kigeni ya *Tanzanite one* inaisha wakati wowote mwaka huu, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe eneo hili linagawanywa kwa wachimbaji wadogo ili kukidhi matakwa ya sheria hiyo.

(iv) Kuongeza thamani madini; Serikali isaidie ili wachimbaji waweze kupata mikopo itakayowezesha kufungua viwanda vidogo na kuweza kuongeza thamani madini yao kuliko ilivyo sasa, wanauza madini ghafi na hivyo kupata fedha kidogo. Aidha, Serikali ifute kodi katika vifaa vya kuongeza thamani ya madini.

Serikali ianzishe vyuo vya kutoa elimu ya namna ya ukataji wa madini (*processing*) kuliko utaratibu wa sasa wa kuuza madini ghafi.

Serikali idhamini wachimbaji wadogo ili waweze kukopa na hivyo kuweza kuingia ubia kwenye makampuni makubwa ya uchimbaji.

(v) Kuhusu soko na bei ya madini; Serikali iweke utaratibu wa kuwa na soko la pamoja kwa ajili ya madini yote hapa nchini yakiwemo madini ya vito na madini ya viwandani *(industrial minerals).* Aidha, kuwepo na uwazi wa bei ya madini yote.

Minada ya ndani ya madini irejeshwe na wanunuzi wahamasishwe kwenda kwenye minada ya ndani. Pia Serikali iweke utaratibu wa kuwa na maonyesho ya madini mbalimbali (*exhibition*) hii itasaidia kuinua soko la madini nchini.

(vi) Maeneo mengi ya wachimbaji wadogo hayana umeme hali inayopelekea kuingia gharama kubwa kununua dizeli kwa ajili ya kuendesha mitambo yao. Kamati inashauri Serikali iweke utaratibu utakaowezesha maeneo ya wachimbaji kupatiwa umeme ili kuwapunguzia gharama.

(vii) Kumekuwepo na biashara haramu ya madini nchini hali inayochafua taswira ya sekta. Tunashauri pamoja na jitihada za kuhamasisha maendeleo ya sekta Serikali iingilie kati na kuhakikisha inakomesha tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira; Mwaka 2005, Serikali iliingia mkataba wa ubia na Kampuni ya *Tan Power Resources (TPR)* kwa ajili ya kuendeleza mgodi wa Makaa ya mawe Kiwira kwa hisa za asilimia 30 (Serikali) kwa asilimia 70 *(TPR)*. Serikali ilikabidhi mgodi kwa Kampuni ya *Kiwira Coal and Power Limited (KCPL)* ili kuendesha mradi huo. *KPCL* ilichukua mkopo wa jumla la shilingi bilioni 16.9 kutoka *CRDB, PSPF* na *NSSF.*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, *KPCL* ilishindwa kuendeleza mgodi huo na Serikali iliamua kuuchukua mgodi huo ili kuumiliki kwa hisa za asilimia 100. Kwa kuwa *KPCL* ilikuwa inadaiwa madeni ambayo pamoja na riba yamefikia jumla ya shilingi bilioni 32.19 na kwa kuwa Serikali imeamua kuuchukua mgodi huo, inapaswa kisheria kuchukua mali na madeni yake yote.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli kwamba wadeni wa *KPCL* wameanza taratibu za kuishtaki Serikali kwa kushindwa kulipa madeni yao, ni dhahiri madeni haya hayakwepeki. Kamati inashauri fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 32.19 zilipwe na wahusika washtakiwe kwa kushindwa kutimiza wajibu wao. Aidha, Kamati inahoji ilikuwaje Serikali kuukabidhi mgodi kwa Kampuni ambayo haina uwezo, Je, *due diligence* haikufanyika?

Mheshimiwa Spika, Kamati haikubaliani na malipo mengine yanayofikia kiasi cha shilingi bilioni nane ambazo zimetengwa kwa ajili ya kulipia tozo ya usimamizi *(Management fees)* kwa Kampuni ya *TPR* kwa kuwa Kampuni hiyo ilishindwa kuuendeleza mgodi

huo. Aidha, Kamati inapendekeza fedha hizo shilingi bilioni nane zipelekwe *REA* ili kuboresha huduma ya usambazaji wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa Taasisi za Wizara; kwanza ni Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO)*; Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* ndiyo mtendaji mkuu wa kufua, kununua, kusafirisha, kusambaza na kuuza umeme Tanzania Bara na pia kuuza umeme wa jumla *(bulk supply)* kwa visiwa vya Pemba na Unguja. Hivyo basi, ni dhahiri kuwa uhakika wa upatikanaji wa nishati ya kutosha nchini Tanzania inategemea kwa asilimia 100 utendaji kazi mzuri wa Shirika hili.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* ina hali mbaya kifedha. Kamati kwa kutambua umuhimu wa Shirika hili, inatoa ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

(i) Kamati kwa mara nyingine tena inaishauri Serikali kuwa, ankara za *TANESCO* zihusishe gharama halisi za kufikisha umeme kwa mlaji *(cost reflective).* Aidha, kwa tabaka la walaji ambao Serikali ingependa wanunue umeme kwa bei nafuu zaidi, tunashauri Serikali itoe ruzuku kwa kiasi halisi cha umeme uliokwenda kwa wahusika.

(ii) Ili *TANESCO* iweze kujiendesha ni lazima taasisi zote zinazopata huduma ya umeme zilipe ankara zao kwa wakati. Takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Julai 2012, *TANESCO* ilikuwa inadai wateja wake jumla ya shilingi bilioni 266. Kati ya hizo shilingi bilioni 240 ni za watu binafsi na shilingi bilioni 26 ni ta taasisi za umma. Kamati inashauri kuanzia sasa sheria ianze

kuchukua mkondo wake na *TANESCO* iwakatie umeme na pia kuwashtaki wale wote watakaoshindwa kulipa ankara zao kwa wakati.

(iii) Kutokana na gharama za uzalishaji wa umeme kuwa juu ikilinganishwa na bei ya kuuza umeme, ili kuwapunguzia *TANESCO* mzigo huo, Kamati inashauri Serikali itoe msamaha wa kodi ya kuagiza mafuta ya kuendesha mitambo *(Import and excise Duty)* na Vipuri vya mitambo ya kuzalisha umeme.

(iv) Kamati inaitaka Serikali iiwezeshe *TANESCO* ili iweze kumiliki mitambo yake yenyewe badala ya utaratibu wa sasa wa kukodi mitambo ambayo inaliingiza Taifa kwenye hasara kubwa. Aidha, kwa mitambo ambayo tayari ipo nchini na *TANESCO* inalipa *capacity charges*, Kamati inaitaka Serikali yenyewe ndiyo ilipie gharama hizo ili kuipunguzia *TANESCO* mzigo mkubwa ilionao.

(v) Kamati inaishauri *TANESC*O kutoa kipaumbele katika kuboresha miundombinu ya kusafirisha umeme ili kupunguza au kuondoa kabisa kiwango kikubwa cha umeme kinachopotea njiani ambacho kinafikia asilimia 22.5.

(vi) Serikali ifanye tathmini ya faida *(cost benefit analysis)* ili kuona umuhimu wa kuligawa Shirika hili ili kuongeza ufanisi wa maeneo yote (uzalishaji, usambazaji na usafirishaji).

(vii) *TANESCO* iwekeze kwa kasi kwenye miradi ya gesi kwani ni nafuu kwa maana ya gharama na miradi yake haichukui muda mrefu kuijenga.

(viii) Ili kuwapunguzia wananchi mzigo wa kulipa gharama za kuunganisha umeme kwa mkupuo, *TANESCO* iweke utaratibu wa kuingiza gharama hizo kwenye ankara zao za mwezi.

Mheshimiwa Spika, pili ni Wakala wa Nishati Vijijini (*REA),* ulioanzishwa kwa lengo la kuboresha, kuhamasisha na kuwezesha upatikanaji wa matumizi ya nishati bora vijijini. Pamoja na malengo haya, Wakala huu unashindwa kutekeleza malengo hayo ipasavyo na hii inatokana na kutotengewa fedha za kutosha na wakati mwingine hata zile zilizoidhinishwa na Bunge kutototolewa zote. Takwimu zinaonesha kuanzia Mwaka wa Fedha 2007/2008 hadi 2011/2012, *REA* ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 201.066, lakini fedha iliyotolewa ni shilingi bilioni 116.618 sawa na asilimia 58 tu.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa kwa utoaji huu wa fedha dhamira ya *REA* haiwezi kutekelezwa na hivyo wananchi wengi wa Tanzania ambao wanaishi vijijini hawawezi kufikiwa na huduma hii muhimu. Kamati imetafakari kwa kina changamoto za *REA* na inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Kutokana na umuhimu wa *REA* katika kusambaza umeme vijijini, bajeti ya Wakala huu iongezwe ili wananchi wengi wa vijijini waweze kufikiwa na huduma hii muhimu kama ilivyoainishwa kwenye

Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa muda mfupi ambao unataka ifikapo mwaka 2016 asilimia 16 za kaya ziwe zimefikiwa na umeme. Aidha, fedha yote itolewe kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

(ii) Serikali itumie mapato yatokanayo na madini katika kuendeleza miradi ya umeme iliyo chini ya *REA.*

(iii) Serikali itekeleze ushauri wa Kamati wa kutumia fedha zilizookolewa kutokana na mapendekezo ya Kamati ya kulinganisha kodi na ushuru wa mafuta ya taa na dizeli. Msimamo wa Kamati ni kuwa, kutokana na zoezi hilo kuokoa takribani shilingi bilioni 600 kwa mwaka, basi *REA* watengewe shilingi bilioni 300 mahususi kwa ajili ya kuongeza kasi ya kusambaza umeme vijijini.

(iv) *REA* ihakikishe inafikisha miradi kwenye vijiji ambavyo bado havijaguswa ili kuleta uwiano wa mgawanyo wa huduma hii muhimu.

(v) Katika kuhakikisha umeme unawafikia wananchi wengi zaidi wa vijijini, *REA* iwekeze pia kwenye miradi ya umeme wa jua *(solar)* badala ya kusubiri umeme wa gridi ya Taifa.

(vi) Katika kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa wakati, *REA* iamue miradi michache ya vipaumbele ambayo itakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, tatu ni Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC);* Shirika hili linajihusisha na kazi za msingi za utafiti, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asili

nchini. Pia Shirika hili linalo jukumu la kusimamia shughuli za utafutaji na uchimbaji unaofanywa na makampuni ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza *TPDC* kwa kuendelea kubuni miradi mbalimbali ya matumizi ya gesi asili ambayo kwa kweli faida zake kiuchumi ni kubwa. Ukiangalia mradi wa mtandao wa gesi asili katika Jiji la Dar es Salaam ambao gharama yake itakuwa ni dola za Marekani milioni 55.1. Mradi huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi kwenye taasisi mbalimbali, majumbani na vituo vya kujazia gesi asili kwenye magari. Faida zake kwa mwaka zinakadiriwa kuwa ni shilingi bilioni 201.7.

Mheshimiwa Spika, *TPDC* ndiyo taasisi ambayo ina jukumu la kusimamia sekta hii ya gesi ilihali haina watumishi wa kutosha. Itakumbukwa kuwa matatizo yaliyopelekea Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kuiibia Serikali yetu yalitokana na ukosefu wa watumishi wa kutosha kuweza kukagua hesabu za kampuni hii. Pamoja na Serikali kutoa kibali ili *TPDC* iweze kuajiri watumishi 51, lakini watumishi hao hawatoshi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa *TPDC* kwa mukstakabali wa sekta ndogo ya mafuta na gesi nchini, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali iweke utaratibu utakaowezesha *TPDC* kuajiri watumishi ambao ni muhimu pale mahitaji yanapojitokeza bila ya kufuata mlolongo mrefu. Uwepo na ushiriki wa wafanyakazi Watanzania na

wajiriwa wa Serikali, mbali ya faida ya kupata ujuzi, itawaondoela wananchi dhana ya tunaibiwa kwani watajua na kushiriki kanuni za kuendesha sekta.

(ii) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa taasisi hii na kuipatia fedha zake zote kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Kamati bado inashauri Serikali iendelee kuitengea fedha za kutosha *TPDC* ili iweze kukamilisha mradi wake wa mtandao wa gesi asili katika Jiji la Dar es Salaam ambao una faida kiuchumi na uwezo wa kuokoa takribani shilingi bilioni 210.7 kwa mwaka. Aidha, kwa maeneo ambayo Serikali itashindwa kutoa fedha kwa *TPDC*, basi ni vyema itoe dhamana ili *TPDC* waweze kukopa kwenye mabenki ili kuendeleza mradi huu.

(iii) Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii iipatie kibali *TPDC* ili leseni itolewe kwa eneo la Wembere, Ziwa Natron, Eyasi na Manyara ambalo kwa kiasi kikubwa lipo kwenye Hifadhi ya Taifa kwa kwa ajili ya kufanya utafiti wa mafuta au gesi.

(iv) Kamati bado inasisitiza kuwa umefikia wakati Serikali iamue kwa dhati kabisa kuboresha jeshi lake la maji *(navy)* ili waweze kulinda maeneo ya utafiti ambayo yanatumia kampuni binafsi kuweka ulinzi dhidi ya maharamia kwani kuweka kampuni binafsi pia siyo salama kwa nchi.

(v) Kamati inashauri Serikali ikae na kukubaliana na Malawi kuhusu mpaka katika Ziwa Nyasa kwani tayari utafiti unaanza wakati bado kuna mgogoro kwa nchi zetu.

(vi) Msumbiji imegundua gesi nyingi katika maeneo ya mpakani, Serikali ikubaliane na Msumbiji ili ikibidi kuingia mkataba wa pamoja *(unitization agreement)* katika utafiti au uchimbaji wa mafuta katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji.

(vii) Kamati inashauri Serikali sasa, iamue na kuanzisha kampuni ya gesi asili – *GASCO* ambayo pamoja na majukumu mengine itahusika na usafirishaji, usambazaji, matumizi na masoko ya gesi asili.

(viii) Kamati kwa kuzingatia kasi ya utafutaji mafuta na gesi asili duniani, inashauri Serikali kupitia mamlaka za juu iamue shughuli za utafutaji rasilimali hii katika visiwa vya Pemba na Zanzibar ziendelee.

Mheshimiwa Spika, nne ni Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* ambalo lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge mwaka 1972, (*The State Mining Corporation (Establishment) Order 1972)* chini ya Sheria ya *The Public Corporation Act, 1969* kwa madhumuni ya kujihusisha na shughuli za utafutaji, uchimbaji, uuzaji na biashara ya madini.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 1996 Serikali iliamua kufunga mashirika mama ikiwemo *STAMICO* na hivyo kuwekwa chini ya Tume ya Rais ya kurekebisha Mashirika ya umma. Hivyo basi, kwa zaidi ya miaka kumi Shirika likaendelea kuwepo kwa kujiendesha lenyewe likisubiri utekelezaji wa uamuzi wa Serikali. Hata hivyo, Mwaka 2007 Serikali ilipitia ushauri uliotolewa na Kamati ya Mheshimiwa Jaji Bomani na

kutengua uamuzi wake wa awali na hivyo kuiondoa *STAMICO* rasmi katika orodha ya mashirika ambayo yangebinafsishwa kupitia Tangazo rasmi lililochapishwa kwenye Gazeti la Serikali tarehe 03/04/2009 kupitia *Government Notice No. 88.*

Mheshimiwa Spika, kufuatia hatua hiyo ya kuirudisha *STAMICO,* Shirika limefanikiwa kuingia ubia na Kampuni ya *Tanzania Royalty Exploration Corporation Limited* ya Canada katika uendelezaji wa Mgodi wa *Buckreef* kwa hisa za 55 kwa 45. *STAMICO* imechukua hisa ya asilimia 70 ya mgodi wa KIWIRA zilizokuwa zinamilikiwa na Kampuni ya *Tan Power Resources Limited* na hivyo kufanya Serikali kuwa na hisa zote kwa asilimia 100 na kwa sasa imeanza kuuimarisha mgodi. Aidha, *STAMICO* imepewa leseni ya utafutaji wa madini katika mgodi wa Buhemba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo, lakini bado *STAMICO* inakabiliwa na changamoto kuu ya ukosefu wa fedha hasa ikizingatiwa kuwa Shirika lilisimama kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hiyo nzuri, Kamati inaishauri Serikali itekeleze yafuatayo ili kuliwezesha Shirika hili kuendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo:-

(i) Kwa kuzingatia matakwa yaliyopo kwenye Sheria ya Madini ya 2010 ya kutaka Serikali kuwa na kiwango cha hisa katika migodi *(free - carried interest),* Kamati inashauri Serikali kusimamia suala hili.

(ii) Kamati iendelee kuongeza Bajeti ya *STAMICO* ili iweze kushiriki vyema katika kusimamia sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, tano ni Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA); Kamati inafarijika na kazi zinazofanywa na Wakala wa Ukaguzi wa Madini kwani umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la utoroshaji wa madini na hivyo kuongeza pato la uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi wanayofanya, Wakala unakumbana na changamoto mbalimbali kama ufinyu wa bajeti, elimu ndogo kwa wachimbaji wadogo hasa katika masuala ya usimamizi wa mazingira na kushamiri kwa biashara haramu ya madini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Bajeti ya Wakala huu iongezwe ili kukidhi mahitaji yao.

(ii) Serikali ianze mara moja mchakato wa kuufanya Wakala uwe mamlaka kamili na uweze kukagua pia wakandarasi wote wanaotoa huduma na kuuza bidhaa migodini ili kuhakiki gharama za uzalishaji za Migodi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji kodi katika sekta ya Madini.

(iii) *TMAA* iongeze juhudi katika kutoa elimu kwa jamii kuhusu usimamizi bora wa mazingira.

(iv) Wizara, *TMAA* na taasisi nyingine zinazohusika na sekta ya madini wawekeze zaidi katika kujenga taswira chanya kwenye mtazamo wa wananchi kwa kuwaonesha manufaa ya uendelezaji wa sekta hii na kuondoa mawazo hasi kuwa sekta ya madini haina mchango katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sita ni Wakala wa Jiolojia (*GST)*; Wakala wa Jiolojia Tanzania una jukumu la kukusanya, kuchambua, kutafsiri, kutunza takwimu na taarifa mbalimbali za kijiosayansi (jiolojia, jiokemia na jiofizikia), kutengeneza na kusambaza ramani mbalimbali, takwimu na taarifa mbalimbali zinazoainisha kuwepo kwa aina ya miamba. Pamoja na hayo, Wakala unafanya uchunguzi wa kimaabara kwa sampuli mbalimbali za miamba, madini, maji, mimea na udongo kwa ajili ya tafiti mbalimbali nchini na kuratibu utokeaji wa majanga kama vile matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano, maporomoko ya ardhi, mionzi asili na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kama majukumu ya wakala huu yanavyojieleza kuwa ni majukumu muhimu sana kwa mustakabali wa sekta ya madini. Lakini utaona kuwa bajeti anayotengewa wakala huu hususan ya maendeleo haiendani kabisa na majukumu yake na pia haitolewi yote. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wakala uliidhinishiwa fedha za maendeleo jumla ya shilingi bilioni 1.2, lakini hadi kufikia mwezi Juni, 2012 Wakala ulikuwa umepokea shilingi milioni 314.6 sawa

na asilimia 33.3 tu. Kamati haikubaliani na hali hii kabisa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto mbalimbali zinazoukabili Wakala huu, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Kutokana na ukweli kuwa Wakala huu ndiyo mwongozo wa kujua maeneo yenye madini na kiasi kilichopo, Serikali iwawezeshe kwa kuwapatia rasilimali za kutosha ikiwemo rasilimali watu. Aidha, Kutokana na uhaba wa wataalam, Kamati inashauri Serikali ione umuhimu huu na kutoa kibali cha ajira ya kutosha ili wakala usipwaye.

(ii) Kwa kuwa pamoja na kazi nyingine, *GST* ina jukumu la kudhibiti ubora wa majengo, Serikali iweke utaratibu utakaoiwezesha GST kutoa vyeti *(certificate)* kwa ujenzi wa majengo yanayozidi ghorofa moja na vyeti hivyo viwe vinalipiwa.

(iii) Serikali iiwezeshe *GST* ili ikamilishe ujenzi wa *Geomuseum* kwani itasaidia kuongeza mapato. Nchi kama Norway inapata fedha nyingi kutokana na *museum* yao ya mafuta na gesi.

(iv) Pamoja na nia nzuri ya ku-*centralize* sekta zote bado kuna tatizo, hivyo Serikali iziache Wakala au Taasisi kufanya kazi zake kwa mujibu wa *establishment order* zao na kuwapa nafasi ya kuajiri pale inapotokea umuhimu wa kufanya hivyo badala ya utaratibu wa sasa wa vibali vyote kutoka utumishi.

(v) Kamati imebaini kuwa katika mfumo wa utumishi kuna baadhi ya kada hazipo licha ya kuwa zina umuhimu sana katika utendaji kazi wa taasisi mbalimbali na Taifa kwa ujumla. Ukiangalia kada za mafundi mchundo (*Artisanal*), kada hizi hazipo. Kamati inashauri Serikali iboreshe muundo wa utumishi ili kuwepo na aina hii ya watumishi kwani wanahitajika katika taasisi mbalimbali ikiwemo *GST* lakini kwenye muundo wa utumishi hawapo.

Mheshimiwa Spika, saba ni Chuo cha Madini, Dodoma ambacho kilianzishwa rasmi mwaka 1982. Chuo hiki kinatoa mafunzo ya ufundi sanifu katika sekta ya madini katika fani za jiolojia na utafutaji madini, uhandisi na uhandisi uchenjuaji madini. Aidha, chuo kinafanya tafiti katika shughuli za madini kwa lengo la kuboresha utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji na uuzaji wa madini wenye faida na kutoa ushauri katika sekta ya madini kwa wadau wa madini.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatambua umuhimu wa Chuo hiki katika kuendeleza taaluma mbalimbali hususan katika masuala ya madini. Lakini chuo hiki bado kina changamoto mbalimbali zikiwemo za idadi ndogo ya wanafunzi wanaodahiliwa kwa mwaka ikilinganishwa na mahitaji halisi ya soko na idadi ya wanaoomba kujiunga na chuo. Hii inatokana na ukweli kwamba chuo hakina miundombinu ya kutosha madarasa, maabara na kadhalika

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa chuo hiki katika sekta ya madini nchini, Kamati

inashauri Bajeti ya Chuo hiki iongezwe ili isaidie katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuboresha miundombinu ya chuo kwa maana ya kumbi za kufundishia na kumbi za mikutano kwani wanafunzi wanaoomba na kufaulu usaili ni wengi ikilinganishwa na wanafunzi wanaodahiliwa kutokana na miundombinu haba ya chuo.

(ii) Kuongeza vifaa vya kufundishia vya maabara na vya kufanyia mafunzo kwa vitendo.

(iii) Kununua vyombo vya usafiri vya uhakika na vyenye uwezo wa kuwahudumia wanafunzi wengi zaidi mara wanapotakiwa kutoka nje ya chuo kwa ajili ya kufanya mafunzo kwa vitendo.

(iv) Kutokana na changamoto ya uhaba wa wakufunzi, Serikali iamue kwa dhati kuongeza idadi ya wakufunzi na kuwaongezea elimu wale waliopo kwani bila wakufunzi ni dhahiri elimu itakayotolewa haitakuwa ya kiwango kizuri na pia kupunguza morali ya wakufunzi wachache waliopo kutokana na kuzidiwa na kazi.

(v) Makampuni ya madini yahakikishe yanaongeza nafasi za wafanyakazi kwenye makampuni yao wanaohitimu katika chuo hiki. Aidha, watoe nafasi za mafunzo maalum ya vitendo kwa wanafunzi kwenye migodi yao ili kuwapa utaalam unaoendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika sekta ya madini.

(vi) Serikali isaidie chuo hiki ili ile azma yake ya kuanzisha mtaala wa mafuta na gesi iweze kutekelezwa hasa katika kipindi hiki ambacho ugunduzi wa gesi nchini umeonesha matumaini ya hali ya juu.

(vii) Kutokana na umuhimu wa chuo hiki katika sekta ya madini nchini, Kamati inashauri sehemu ya *Skill development levy* inayotolewa na Makampuni ya Madini iende kwenye Chuo cha Madini ili kukiboresha.

(viii) Umefika wakati sasa chuo hiki kitungiwe sheria kwani kiliundwa kwa mujibu wa tamko tu.

Mheshimiwa Spika, nane ni Kitengo cha Ukaguzi wa Almasi (*TANSORT);* Kitengo hiki kilianzishwa mwaka 1996. Kitengo kilianzishwa kwa ajili ya kuchambua na kuthaminisha aina zote za madini ya almasi na vito na kutoa ushauri wa masoko bora ya kuuza madini. Tangu kuanzishwa kwake, *TANSORT* imesaidia wachimbaji wengi kuelewa thamani ya madini yao na pia kuwatafutia masoko nje ya nchi ukizingatia ukweli kuwa soko la ndani bado ni changa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuamua kujenga jengo la kuuzia madini na vito *(one stop center)*. Aidha, Kamati inashauri ujenzi wa jengo hilo ukamilike mapema kama ilivyopangwa ili kupunguza utapeli unaoendelea nchini. Pia ni imani ya Kamati kuwa hatua hiyo itavutia wananchi walio wengi kuwekeza katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, tisa ni Tasnia ya Uziduaji *(TEITI)* ambayo ilisajiliwa tarehe 14 Februari 2009 kwa dhumuni

la kuweka mfumo wa uwazi katika usimamizi wa uvunaji wa maliasili za madini, mafuta na gesi ili kuchochea ukuaji wa maendeleo na kuondoa umaskini. Katika taarifa yake ya kwanza iliyotolewa mwezi Februari, 2011 *TEITI* ilionesha kuwepo kwa tofauti kati ya fedha zilizolipwa na makampuni ya uchimbaji wa madini na gesi asili na zile zilizopokelewa na Serikali. Hata hivyo, suala hili lilirekebishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza juhudi zilizofanywa za kuanzishwa kwa chombo hiki ambacho kinahusisha wadau kutoka makundi ya Vyama vya Kijamii, Serikali na Kampuni za Madini. Aidha, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Kamati inaendelea na ushauri wake wa awali kuwa Serikali ilete Muswada wa Sheria Bungeni ili chombo hiki kiwepo rasmi kisheria na hivyo kuwa na nguvu zaidi.

(ii) Bajeti ya chombo hiki muhimu iongezwe

Mheshimiwa Spika, naomba nirejee kuishauri Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini juu ya shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asili. Wananchi walio wengi hawana uelewa wa nini kinachoendelea katika sekta hii. Watanzania wanajenga matumaini makubwa na wakati huo huo wakikata tamaa. Wapo wanaodai nchi yetu inaporwa au kuibiwa jumla jumla.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati ni kuwa zoezi zima la uendeshaji na udhibiti wa sekta hii liwe na

uwazi wa hali ya juu. Pamoja na utaratibu wa kuendesha shughuli kwa uwazi juhudi ziongezwe katika kuwafahamisha wananchi kila linalotokea katika sekta.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati ya moyo wangu napenda kuwashukuru tena wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa imani waliyonipa ya kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii. Nawaahidi ushirikiano wa hali ya juu. Aidha, napenda kutambua mchango wao mkubwa katika kuhakikisha Taarifa hii inakuwa hivi ilivyo, ni dhahiri mtaona wajumbe walivyofanya kazi kubwa. Napenda kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mjumbe; Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi Mjumbe; Mheshimiwa Catherine Valentine Magige Mjumbe; Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari Mjumbe; Mheshimiwa Charles Poul Mwijage, Mjumbe; Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mjumbe; Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mjumbe; Mheshimiwa Daktari Festus Bulugu Limbu, Mjumbe; Mheshimiwa Shafin Amedal Sumar, Mjumbe; Mheshimiwa *Engineer* Athuman Rashid Mfutakamba, Mjumbe na Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagulla, Mjumbe; Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mjumbe; Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mjumbe; Mheshimiwa Suleiman Nchambis Suleiman, Mjumbe; Mheshimiwa Kisyeri

Werema Chambiri, Mjumbe; Mheshimiwa Ali Mbarouk Salim, Mjumbe; Mheshimiwa Sarah Ali Msafiri, Mjumbe; Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe, Mjumbe; Mheshimiwa Vicky Kamata, Mjumbe; Mheshimiwa John Mnyika, Mjumbe na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza kwa uongozi thabiti wewe binafsi, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge. Hakika mnaliendesha vyema Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, Waziri wa Nishati na Madini; Mheshimiwa Stephen Maselle, Naibu Waziri anayeshughulikia Madini na Mheshimiwa George Simbachawene, Naibu Waziri anayeshughulikia Nishati kwa kuteuliwa kuiongoza Wizara hii yenye sekta muhimu kwa Taifa letu. Aidha, nawashukuru kwa kushiriki vyema katika kuwasilisha bajeti na kutoa ufafanuzi pale ulipohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Eliakim Maswi kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati katika kufanikisha majukumu yake ya Kikatiba ya kuisimamia Wizara ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Daktari Thomas D. Kashilillah kwa ushirikiano anaoipa Kamati katika majukumu yake ya kila siku. Aidha, nawashukuru Wafanyakazi wote wa Ofisi ya

Bunge kwa kuisaidia Kamati katika utendaji kazi wake. Nampongeza sana Katibu wa Kamati hii Pamela Pallangyo kwa kuratibu vyema shughuli zote za Kamati bila kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini, Fungu 58 kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, jumla ya shilingi 641, 269, 729,000/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA-MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote niungane na wote wenye mapenzi mema katika kuomba ulinzi wa Mwenyezi Mungu wakati tukitimiza wajibu wa Kibunge kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Kanuni Kudumu za Bunge (Toleo la mwaka 2007), kifungu cha 99(7) wa kuishauri na kuisimamia Serikali; kwa kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012 na makadirio ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, nitumie pia nafasi hii kuwashukuru Watanzania wenzangu wa kada, hadhi na ngazi mbalimbali katika taasisi na maeneo mengi

ndani na nje ya nchi waliouniunga mkono kwa hali na mali katika kipindi chote cha misukosuko ya kusimamia ukweli na uwajibikaji: katika kuifuatilia Serikali na kuunganisha wadau wengine kuwezesha maendeleo katika Jimbo la Ubungo; wakati wa kesi ya kupinga matokeo ya ushindi wetu; wakati wa operesheni za kuhamasisha mabadiliko katika maeneo mengine nchini na katika uwakilishi wa wananchi Bungeni. Utaratibu wa kupokea maoni na kutoa taarifa za mara kwa mara za maendeleo kupitia mikutano na wananchi pamoja na katika mtandao wa *http://mnyika.blogspot.com* tutaendelea nao. Kaulimbiu yetu ni ile ile: AMUA; Maslahi ya Umma Kwanza.

Mheshimiwa Spika, Sekta za Nishati na Madini zina umuhimu maalum katika uchumi wa nchi na maisha ya wananchi katika kipindi cha sasa na muda mrefu ujao. Wakati nishati ikiwa nyenzo ya kuendesha maisha ya kiuchumi, kisiasa na kijamii ya wananchi na nchi kwa ujumla; madini ni mtaji na ni kati ya mitaji mikubwa ya kuwezesha maendeleo ya haraka ya Taifa. Hata hivyo, pamoja na Tanzania kujaliwa rasilimali hizi nyingi ikiwemo watu, ardhi yenye rutuba, maji (bahari, mito na maziwa), kuwa katika eneo la kimkakati la kijiografia kwa biashara na maliasili, bado takwimu za hali ya uchumi kwa mwaka 2011 zinaonesha sehemu kubwa ya Watanzania wako kwenye lindi la umaskini.

Mheshimiwa Spika, tunajadili sekta za nishati na madini wakati Taifa likiwa kwa mara nyingine tena kwenye tishio la mgawo wa umeme pamoja na Serikali

kukanusha kwamba hakutakuwa na mgawo wa umeme.

Mheshimiwa Spika, tunajadili mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012, wakati kwa mara nyingine tena kukiwa na mvutano baina ya Watendaji Waandamizi wa Wizara ya Nishati na Madini na Taasisi zake wakiwa katika mvutano ambao umeambatana na kutuhumiana hadharani kupitia vyombo vya habari juu ya tuhuma za ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka.

Mheshimiwa Spika, tunajadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2012/2013 wakati kukiwa na tuhuma za vigogo wa Serikali kuingiziwa fedha kifisadi katika akaunti zao za nchini Uswisi na makampuni ya nje ya utafutaji na uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asili huku viongozi wa dini wakiwa wamezindua ripoti juu ya ukwepaji kodi na upotevu wa mapato kwa Serikali unaogusa pia makampuni kwenye sekta za nishati na madini *(The One Billion Dollar Question).* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba kila mmoja wetu atafakari kwa ukweli wa nafsi na nafasi yake tumefikaje hapa kama Taifa na kwa pamoja tukubaliane kuwa Wabunge tuwajibike kuisimamia Serikali kuhakikisha maazimio yote ya Bunge kuhusu sekta za nishati na madini ya miaka mbalimbali yanatekelezwa kwa haraka na kwa ukamilifu. Naamini iwapo maazimio ya Bunge juu ya Mkataba baina ya *TANESCO* na Kampuni ya *Richmond Development Company LLC* yangetekelezwa yote na kwa wakati toka mwaka

2008, maazimio ya Bunge juu ya uendeshaji wa sekta ndogo ya gesi asili ya mwaka 2011 yangezingatiwa yote na kwa haraka, maazimio kuhusu uhalali wa utaratibu wa Wizara ya Nishati na Madini kuchangisha fedha kwa ajili ya kupitisha bajeti Bungeni ya mwaka 2011 yangechukuliwa kwa uzito unaostahili; Taifa lingeepushwa kurudia mijadala ile ile kuhusu Wizara hii hii mara kwa mara. Aidha, kambi Rasmi ya Upinzani inatoa mwito kwa Bunge kupitisha maazimio ya kutaka uwajibikaji wa Serikali kwa kushindwa kutekeleza maazimio ya Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Nchi, Ibara ya 52(1) Waziri Mkuu, ndiye mwenye madaraka juu ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na Shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Ni muhimu basi, badala ya kupokea majibu ya Wizara ya Nishati na Madini pekee ambayo imeendelea kugubikwa na lundo la tuhuma mbalimbali, Waziri Mkuu atoe kauli Bungeni kuhusu kujirudia rudia kwa madai ya ufisadi na uzembe katika sekta za nishati na madini. (*Makofi*)

Aidha, pamoja na mabadiliko ya Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wa Wizara ya Nishati na Madini na taasisi zake ya mara kwa mara, Rais ashauriwe kutumia nguvu zake za kikatiba za ibara ya 33, 34, 35 na 36 kuwezesha hatua za kisheria kuchukuliwa kwa wote waliotuhumiwa kwa ufisadi, uhujumu uchumi na matumizi mabaya ya madaraka kwa mujibu wa maazimio ya Bunge na

taarifa mbalimbali za Serikali ili kurejesha misingi ya uadilifu na uwajibikaji katika sekta za nishati na madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivyo kwa ujumla mjadala wa mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na makadirio ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2012/2013, ulenge katika kuliepusha Taifa letu kuendelea kutumbukia katika 'laana ya rasilimali' kama ilivyojitokeza katika Mataifa mengine. Tuhakikishe tunalinda uhuru wa Taifa letu dhidi ya uporaji wa ardhi na rasilimali zake yakiwemo madini, mafuta na gesi asili ulio katika tishio la ubeberu mamboleo, ufisadi na udhaifu wa kimifumo. Aidha, kupitia mchakato wa Katiba mpya wananchi watoe maoni ya kuhakikisha kuwa rasilimali za muhimu ikiwa ni pamoja na madini, mafuta na gesi zinawekewa mfumo wa kunufaisha Watanzania wote na pia mikataba kuhusu rasilimali hizo inaridhiwa na Bunge. (*Makofi*)

Tuchangie mjadala wa sekta hizi nyeti tukikumbuka maneno ya hayati Mwalimu Nyerere katika kitabu chake cha TUJISAHIHISHE cha mwaka 1962, nanukuu: "Lakini woga unaweza kutokana na tamaa ya kila binadamu kupendwa na binadamu wenzake. Sisi wote tunayo tamaa hii, au sivyo tusingekuwa binadamu. Woga huu huweza ukamfanya mtu kuvumilia maovu, hasa kama maovu yale yanatendwa na walio wengi kwa walio wachache, au yanatendwa na wakubwa kwa wadogo. Kwa kuogopa kuwaudhi wengi tunawaacha

watende makosa bila kuwasahihisha, wasije wakatuchukia. Huu ni ubinafsi mbaya sana.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2011/2012, tarehe 15 Julai, 2011 niliwasilisha Bungeni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2010/2011 na makadirio ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Kufuatia maoni hayo, yapo masuala machache ambayo Serikali imeyazingatia kwenye utekelezaji na mengine mengi Serikali haikuyazingatia pamoja na umuhimu wake kwa maslahi ya nchi na maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika hatua hii ningependa kutambua maoni ambayo yamezingatiwa kuhusu gesi asili, ikiwemo ujenzi wa bomba pamoja na utandazaji wa mtandao. Hivyo, kupitia mapitio haya ya utekelezaji, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze hatua ilizochukua juu ya maoni hayo ambayo baadhi yalijitokeza pia kwenye maoni ya Kamati za Kudumu za Bunge na michango ya Wabunge kwa nyakati mbalimbali. Hakuna sababu ya kutumia muda mrefu kutoa na kujadili maoni mapya ikiwa hakuna mfumo thabiti wa kuhakikisha maoni na maazimio yanatekelezwa kwa wakati na kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na urefu wa hotuba hii na ufinyu wa muda wa kuiwasilisha nitaeleza masuala machache. Hata hivyo, naomba maoni na mapendekezo yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kwa mujibu wa hotuba kamili niliyoiwasilisha mezani.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilipitia kitabu cha pili cha matumizi ya kawaida ya Wizara ya Nishati na Madini *(Volume II Supply Votes),* Fungu la 58 kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na kubaini kwamba ilikuwa ni bajeti ya mgawo mkubwa wa posho na ufujaji ya zaidi ya shilingi bilioni 7.9 ya posho na matumizi mengine yasiyo ya lazima. Kambi Rasmi ya Upinzani iliitaka Serikali ifanye marekebisho kwenye bajeti ili fedha hizo zipunguzwe na kuelekezwa kwenye kuongeza ujenzi wa miundombinu wa Chuo cha Madini, Dodoma na kuongeza kiwango cha fedha katika Mfuko wa wachimbaji wadogo wa madini.

Mheshimiwa Spika, aidha, yako matumizi mengine ya ujenzi wa maofisi na gharama kubwa za kisheria yaliyopaswa kuhamishiwa katika miradi muhimu ya maendeleo ikiwemo ya umeme vijijini. Kwa kuwa Wizara iliahidi kuufanyia kazi ushauri wa kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza kiwango cha fedha kilichookolewa kutokana na kutekeleza ushauri huo na kutoa pia maelezo ni kwa nini katika makadirio ya mwaka 2012/2013, pamejitokeza kwa mara nyingine tena matumizi yasiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilitaka kiwango cha bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kuongezwa ili vipaumbele vifuatavyo viweze kuzingatiwa kwa uzito unaostahili: Kuwekeza fedha za kutosha kwenye sekta ya umeme na Gesi ili kumaliza kabisa tatizo la nishati ya Umeme na kupunguza gharama za maisha.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo ziambatane na kuwekeza katika Bomba la Gesi, pamoja na ujenzi wa mtambo wa kutengeneza Gesi *(LPG extraction Plant)* ili kuwezesha gesi kutumika kwenye magari, viwandani na majumbani; kuhakikisha tunazalisha *360MW* za umeme kila mwaka ili kufikia malengo ya Mpango wa Maendeleo wa miaka Mitano na kumaliza tatizo la mgawo wa umeme na mwisho kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya usafirishaji na usambazaji wa umeme vijijini ili kuchangia katika ukuaji wa uchumi vijijini.

Mheshimiwa Spika, kusuasua kwa utekelezaji wa mpango wa dharura wa umeme, ili kushinikiza nyongeza hiyo ya bajeti na utekelezaji wa vipaumbele hivyo, Kambi Rasmi Bungeni ilipendekeza Bunge kupitisha azimio la kutangaza kwamba ukosefu wa nishati ni janga la Taifa na kupitisha mpango wa dharura na maamuzi ya hatua za haraka ambazo Serikali inapaswa kuzichukua kwa uwajibikaji wa pamoja.

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 Julai, 2011 Waziri Mkuu Mizengo Pinda alikubaliana na mapendekezo yetu na hivyo wakati anatoa hoja ya kuahirisha majumuisho ya mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini akaahidi kwenda kukata fedha kwenye posho na matumizi mengine yasiyokuwa ya lazima katika bajeti ya Serikali ili kuelekeza fedha kwenye mradi wa dharura wa umeme.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo inaelekea ahadi hiyo ilikuwa hewa kwani tarehe 13 Agosti, 2011 Serikali ikageuka na kuleta mpango wa dharura tofauti ambao ulijikita katika Serikali kuidhamini *TANESCO* kwenda kukopa kwenye mabenki ya kibiashara zaidi ya bilioni 400. Pamoja na kuikumbusha Serikali Bungeni kutekeleza ahadi hiyo ya Waziri Mkuu, Serikali ilipuuzia ushauri uliotolewa. Matokeo yake mpaka sasa Shirika la Umeme *(TANESCO)* halikuwezeshwa kupata kiwango cha fedha kilichopangwa na utekelezaji wa mipango husika kusuasua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba Mpango wa Dharura ulipowasilishwa Bungeni tarehe 13 Agosti, 2011 Serikali ilieleza kuwa imepanga kuongeza *MW* 572 ifikapo mwezi Disemba 2011. Kati ya hizo, *MW* 150 ilikuwa zizalishwe kupitia makubaliano baina ya Shirika la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* na *TANESCO*; ilitarajiwa kuzalishwe *MW* 50 Septemba, *MW* 50 Oktoba na *MW* 50 Novemba 2011. Kimsingi, kauli iliyotolewa Bungeni kuwa mitambo ilikuwa imepatikana haikuwa ya kweli. Hivyo, ahadi ya kupata umeme huo ilikuwa hewa. Mpaka sasa hakuna hata *MW* moja ambayo imezalishwa kwa ushirikiano kati ya *NSSF* na *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, Ujumbe ulipotumwa Marekani kwenda kuona mitambo iliyokuwa inaelezwa kwamba ipo haikukuta mitambo yoyote, walikuta kampuni ambayo haikuwa na uwezo kama ilivyokuwa kwa *Richmond Development LLC;* timu hiyo ya wataalam ilibidi kwenda Ufaransa nako ikakosa mitambo ya dharura. Hivyo, fedha nyingi za umma zimetumika kufuatilia ahadi hewa na umeme mpaka sasa

haujapatikana na Taifa limerejea kwenye utegemezi wa mitambo ya kukodi ya gharama kubwa ya umeme kwa sababu ya udhaifu na uzembe wa kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, hivyo, si kweli kwamba mpango wa dharura wa umeme umetekelezwa kwa mafanikio ya asilimia 64.5 kama inavyodaiwa na Serikali kwa kupunguza lengo lililopitishwa Bungeni, bali mpaka sasa umetekelezwa kwa asilimia 47.6 tu; katika muktadha huo, Serikali inabidi ieleze kwa ukweli ni kwa vipi mgawo wa umeme utaepukwa kwa kuzingatia pia barua ya Mwenyekiti wa Bodi ya *TANESCO* kwa Rais yenye kueleza uwepo wa tishio la mgawo wa umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine upungufu wa umeme unaojirudia rudia, matokeo ya Serikali kushindwa kutekeleza kwa wakati mpango wa kuweka mitambo ya *MW* 100 Ubungo (Dar es Salaam) na *MW* 60 Nyakato (Mwanza) ambayo iliwekwa kwenye mpango wa umeme wa mwaka 2009 ambao ulicheleweshwa na hatimaye wakati wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2010/2011, Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na Madini wote waliahidi kukamilisha uwekaji wa mitambo hiyo mapema mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo pamoja na miradi hiyo kuingizwa kwenye mpango wa dharura tarehe 13 Agosti 2011 hakukuwa na usimamizi thabiti wa kufanya ikamilike kwa wakati. Kuzinduliwa kwa mtambo wa *MW* 100 Ubungo katika mwaka wa fedha 2012/2013 ni hatua ndogo kwa kuzingatia kwamba, ilipaswa mwaka wa fedha 2011/2012, pekee Taifa liongeze jumla ya *MW* 360 toka kwenye mitambo ya kununua na si ya

kukodi ili kuendana na malengo ya mpango wa Taifa wa miaka mitano. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze sababu za kuchelewa kutekelezwa kwa miradi hiyo na hatua za uwajibikaji zilizochukuliwa kutokana na udhaifu huo.

Mheshimiwa Spika, kashfa ya ununuzi wa mafuta ya kufua umeme, Kambi Rasmi ya Upinzani tulitahadharisha kwamba mpango wa dharura wa umeme na ununuzi wa mafuta kwa ajili ya kufua umeme isitumike kama mwanya wa ufisadi na kuzalisha "*Richmond* nyingine". Inaelekea kansa hii ndani ya Serikali inayoongozwa na CCM ya kuachia dharura ziendelee kwa manufaa ya wachache imesambaa kwa kiwango cha kuwa vigumu kutibika isipokuwa kwa mabadiliko ya mfumo mzima wa utawala.

Mheshimiwa Spika, katika siku za karibuni kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wazabuni ambao wamekosa zabuni ya kuiuzia *TANESCO* mafuta ya kuendeshea mitambo ya kufua umeme ya *IPTL* kutokana na uamuzi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Eliakim Maswi wa kuipatia zabuni kampuni ya *PUMA Energy (Tz) Limited* (zamani ikiitwa BP (Tz) *Limited*) ambayo inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, licha ya malalamiko ya wazabuni hao, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu kwamba kuna kampeni kubwa imefanywa na inaendelea kufanywa ndani na nje ya Bunge hili Tukufu ili uamuzi huu wa Katibu Mkuu Maswi ubatilishwe

kwa maslahi ya makampuni hayo na wapambe wake wa ndani na nje ya Bunge lako Tukufu. Aidha, wanaoendesha kampeni hiyo wanashinikiza Katibu Mkuu Maswi ajiuzulu kwa kile kinachoitwa kitendo chake cha kukiuka Sheria ya Manunuzi ya Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa nyaraka ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo, tarehe 10 Juni, 2011 aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO* William Mhando alimwandikia Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufilisi, Vizazi na Vifo *(RITA)* iliyokuwa inasimamia ufilisi wa *IPTL* kumtaka aendeshe mitambo ya *IPTL* ili kufua *MW* 100 za umeme ili kuweza kuondoa mgawo wa umeme uliokuwa unaendelea sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, nyaraka hizo zinaonesha kwamba mara baada ya kupata barua hiyo, tarehe 24 Juni, 2011, Mtendaji Mkuu wa *RITA* alimwandikia barua Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma *(PPRA)* akimwomba mwongozo na ushauri juu ya utaratibu wa manunuzi ya mafuta ya kuendeshea mitambo ya *IPTL* kwa dharura.

Mkurugenzi Mkuu wa *PPRA* alitoa mwongozo kwa *RITA* kwa barua yake ya tarehe 28 Juni, 2011 ambapo aliielekeza *RITA* itumie mamlaka yake chini ya kanuni ya 42 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma zinazohusu Bidhaa, Kazi na Huduma zisizokuwa na Ushauri Elekezi na Mauzo ya Mali za Umma kwa Tenda, Gazeti la Serikali Na. 97 la mwaka 2005 (*Public Procurement (Goods, Works, Non-Consultant Services and Disposal*

*of Public Assets by Tender) Regulations, Government Notice No. 97 of 2005).*

Mheshimiwa Spika, Kanuni hiyo inamruhusu Afisa Masuhuli kuamua namna ya kufanya manunuzi kwa dharura bila kujali mipaka ya mamlaka yake endapo kwa kufanya hivyo kutahakikisha uchumi na ufanisi wa manunuzi hayo na endapo ataona ni kwa manufaa ya umma kwamba bidhaa au kazi zenye thamani inayozidi mamlaka yake zinunuliwe kama suala la dharura.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata mwongozo huo wa *PPRA*, Mtendaji Mkuu wa *RITA* alimwandikia Katibu Mkuu Maswi barua ya tarehe 18 Julai, 2011 kumweleza kwamba katika makampuni matano yaliyoonesha nia ya kuiuzia *IPTL* tani 500 za mafuta kwa siku zilizokuwa zinahitajika kuendeshea mitambo yake kwa mwezi Julai, 2011, kampuni za *Oilcom* na *Shell* hazikuwa na akiba ya mafuta wakati ambapo kampuni ya Mogas ilikuwa na lita laki tatu tu. Kwa upande mwingine, kampuni ya *Oryx* ilikuwa na tani 6,000, lakini ilikuwa inauza mafuta hayo kwa dola za Marekani 1,069.30 au shilingi 1,668,456.02 kwa tani.

Mheshimiwa Spika, aidha, kampuni ya *BP* (sasa *Puma Energy*) ilikuwa na tani 9,000 na ilikuwa tayari kuuza mafuta hayo kwa dola za Marekani 901.02 au shilingi 1,405,864.77 kwa tani. Kwa kuzingatia maelezo hayo, Katibu Mkuu Maswi alitoa ridhaa kwa *RITA* kununua mafuta ya kuendeshea mitambo ya *IPTL* kutoka kwa kampuni ya *BP* kwa bei iliyotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, licha ya ukweli kwamba mafuta ya *BP* yalikuwa na bei ndogo ikilinganishwa na bei ya *Oryx*, tarehe 27 Septemba, 2011 Mkurugenzi Mtendaji wa *TANESCO* alisaini mkataba wa kununua mafuta kutoka *Oryx* kwa bei ya dola za Marekani 926.98 au shilingi 1,501,707.60 kwa tani. Aidha, wiki moja kabla ya hapo, yaani tarehe 21 Septemba, Mkurugenzi Mtendaji huyo alikwishasaini mkataba mwingine na kampuni ya *Camel Oil* kwa bei ya dola za Marekani 905.24 au shilingi 1,466,488.80 kwa tani. Kama inavyoonekana, mikataba yote miwili ilikuwa na gharama kubwa zaidi kwa tani kuliko bei ya *BP*. Hata hivyo, mkataba wa *BP* ulikatishwa na *TANESCO* ikaanza kununua mafuta ya kuendeshea mitambo ya *IPTL* kutoka kwa makampuni ya *Oryx* na *Camel Oil*.

Mheshimiwa Spika, kitu cha ajabu ni kwamba licha ya mikataba ya makampuni ya *Oryx* na *Camel Oil* kuonesha bei za shilingi 1,501.70 na shilingi 1,466.49 kwa lita, *TANESCO* ilianza kununua mafuta ya makampuni hayo kwa shilingi 1,850 kwa lita! Kwa maana hiyo, kwa mikataba ya kununua jumla ya lita 16,110,000 kwa mwezi kutoka kwenye makampuni hayo, *TANESCO* ilikuwa inayalipa makampuni hayo jumla ya shilingi 29,803,500,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, kwa ulinganisho, mafuta yaliyouzwa na *BP* kwa mkataba na *RITA* yaligharimu Serikali shilingi 13,140,000,000 kwa bei ya shilingi 1,460 kwa lita. Hii ndio kusema kwamba kama *TANESCO* ingeendeleza mkataba na *BP* badala ya kuuvunja, gharama ya mafuta ya kuendeshea mitambo ya *IPTL*

ingekuwa shilingi 23,520,600,000 na hivyo *TANESCO* ingeliokolea Taifa shilingi 6,282,900,000 kila mwezi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine kumekuwa na taarifa nyingi kwenye vyombo vya habari kwamba Mkurugenzi Mtendaji Mhando hakutendewa haki aliposimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi juu ya utendaji kazi wake. Nyingi ya taarifa hizo zimetolewa bila kuwa na faida ya kuangalia nyaraka zinazohoji uadilifu na uaminifu wa Mkurugenzi Mtendaji, Mhando. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi Mkuu Mhando ni Mkurugenzi na mwanahisa wa kampuni binafsi inayoitwa *Santa Clara Supplies Company Limited* ya Dar es Salaam. Wakurugenzi wengine ni mke wake Eva Steven William, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji na watoto wao. Kwa mujibu wa taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo, mnamo tarehe 20 Desemba, 2011, *Santa Clara Supplies* iliingia mkataba na *TANESCO* ambapo *Santa Clara Supplies* ilikubaliwa kuwa mgavi wa vifaa vya ofisini vya *TANESCO* kwa gharama ya shilingi 884,550,000.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu ulisainiwa na Mkurugenzi Mtendaji, Mhando kwa niaba ya *TANESCO* na mkewe Eva Steven William kwa niaba ya *Santa Clara Supplies*. Aidha, barua ya *TANESCO* iliyoitaarifu *Santa Clara Supplies* kwamba imepatiwa zabuni hiyo iliyoandikwa tarehe 24 Novemba, 2011 ilisainiwa na Mkurugenzi Mtendaji, Mhando. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaelekeza kwamba: "Kiongozi wa umma hatajiweka katika hali ambayo maslahi yake binafsi yatagongana na wajibu wake kama kiongozi wa umma. Aidha, kuhusiana na uwazi kwa wananchi, viongozi wa umma watawajibika kutekeleza wajibu wao kwa umma na kuendesha shughuli zao binafsi kwa namna ambayo itaonekana na kuthibitika kuwa ni wazi na umma na haitatosheleza kwao kutekeleza wajibu wao kwa kufuata sheria tu."

Mheshimiwa Spika, vile vile, kuhusiana na utoaji wa maamuzi, viongozi wa umma watatekeleza wajibu wao kufuatana na sheria na kwa maslahi ya umma. Zaidi ya hayo, kuhusiana na maslahi binafsi, viongozi wa umma hawatakuwa na maslahi binafsi ambayo yanaweza kuathiriwa na maamuzi ya Serikali wanayoshiriki katika kuyafanya. Mwisho, kuhusiana na maslahi ya umma, pale wanapochaguliwa au kuteuliwa, viongozi wa umma watapanga masuala yao kwa namna itakayozuia migongano ya maslahi ya wazi, iliyojificha au inayoonekana kuwepo na pale ambapo migongano hiyo inatokea kati ya maslahi binafsi na maslahi ya umma basi itatatuliwa kwa kuangalia zaidi maslahi ya umma."

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ushahidi huu wa maandishi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Mbunge yeyote, wa Chama chochote cha siasa chenye uwakilishi ndani ya Bunge Tukufu, anayefuata imani yoyote ya dini aseme kama, kwa mujibu wa vifungu hivi vya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Mkurugenzi Mtendaji, Mhando ana

sifa za kuitwa kiongozi mwadilifu wa umma. Hivyo, pamoja na uchunguzi wa kawaida unaoendelea, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Mkurugenzi wa Mashtaka aamuru hatua za uchunguzi wa kijinai zichukuliwe dhidi ya Mkurugenzi Mtendaji Mhando kuhusu tuhuma za ufisadi na matumizi mabaya ya madaraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo hatua hizo dhidi ya Mkurugenzi wa *TANESCO* na watendaji waliohusika zisigeuzwe kuwa kafara ya kuficha uzembe na udhaifu wa Serikali kwa ujumla wake kwa kuwa taarifa za utendaji wa *TANESCO* kuhusu mpango wa dharura wa umeme pamoja na ununuzi wa mafuta uliokuwa ukifanyika zilikuwa zikiwasilishwa kwenye vikao vya Wizara ya Nishati na Madini na hata vikao vya Baraza la Mawaziri. Hivyo, ili ukweli wa kina uweze kujulikana Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa Bunge liazimie kuunda Kamati Teule ya Bunge kuchunguza masuala yote ya ukiukwaji wa sheria, matumizi mabaya ya madaraka na tuhuma za ufisadi katika utekelezaji wa mpango wa dharura wa umeme na ununuzi wa mafuta wa ajili ya mitambo ya umeme.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi huo uhusishe pia Mkaguzi Mkuu kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi *(Forensic Audit)* kwa malipo yaliyofanywa na makampuni ya *BP* (Sasa *Puma Energy*), *Oryx* na *Camel Oil* ili kubaini iwapo kuna vigogo zaidi wa Serikali waliojinufaisha kwa kisingizio cha dharura ya umeme. Izingatiwe kwamba masharti ya Ibara ya 27(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamtaka kila mtu: “Kutunza vizuri mali ya Mamlaka ya

Nchi na ya pamoja na kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu”. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani tuliitaka Serikali katika mwaka wa fedha 2011/2012, itoe taarifa kuhusu utekelezaji wa mpango wa uboreshaji wa utendaji wa Shirika la Umeme *(TANESCO)* sanjari na kutoa ripoti ya tathmini ya utekelezaji wa mpango maalum wa kurekebisha hali ya kifedha ya shirika (2006-2010). Hata hivyo, katika mwaka husika wa fedha utendaji wa *TANESCO* na hali yake ya kifedha imeendelea kusuasua huku ukigubikwa na tuhuma za ubadhirifu na udhaifu wa kiutendaji hali ambayo imepelekea pia Mkurugenzi Mtendaji na maafisa wengine waandamizi kusimamishwa na kuchunguzwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba hali hii ni matokeo ya udhaifu katika uteuzi na usimamizi wa Serikali kwa Mashirika ya Umma na inataka uwajibikaji kutokana na hali hiyo kudumu kwa muda mrefu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania ni mikataba mingapi mibovu yenye kuipa mzigo mkubwa wa kifedha *TANESCO* na kuongeza gharama kwa wananchi imefanyiwa mapitio katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, udhaifu wa kutokutekeleza mipango ya uzalishaji wa gesi na makaa ya mawe kwa wakati umesababisha utegemezi mkubwa kwenye matumizi ya mafuta katika mitambo ya kuzalisha umeme wa dharura. Takriban nusu ya umeme unaozalishwa nchini hivi sasa

unazalishwa kwa kutumia dizeli, mafuta ya ndege na mafuta mazito hali ambayo imeongeza mahitaji makubwa ya uagizaji wa mafuta toka nje ya nchi. Hii imesababisha mahitaji makubwa ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza mafuta na hivyo kuchangia katika kuporomoka kwa thamani ya shilingi.

Aidha, ongezeko kubwa la uagizaji toka nje limeathiri urari wa biashara na hivyo kuchangia katika mfumuko wa bei. Hivyo, Watanzania hivi sasa wanabeba mzigo wa kupanda kwa bei za bidhaa na gharama za maisha kwa ujumla kutokana na ufisadi kwenye mikataba, ubadhirifu katika matumizi, uzembe katika uongozi na upungufu katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya Serikali kwenye sekta ya nishati.

Mheshimiwa Spika, mzigo huu usingekuwa mkubwa iwapo Serikali ingetekeleza katika mwaka wa fedha 2011/2012, maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya kuhakikisha nyongeza ya fedha kwenye bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa upande wa Sekta Ndogo ya Gesi kwa ajili ya mitambo ya umeme na kuharakisha kuwekeza katika Bomba la Gesi pamoja na ujenzi wa mtambo wa kutengeneza Gesi *(LPG extraction Plant).*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatimaye Serikali kuzindua ujenzi wa bomba la gesi katika mwaka wa fedha 2012/2013 na ahadi ya Wizara ya Nishati na Madini kuwa ujenzi huo utakamilika katika kipindi cha miezi kumi na nane ijayo, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kutoa kauli ya uhakika kwa Taifa. Je,

katika kipindi hiki cha mpito imeweka mikakati gani ya kuhakikisha mitambo ya kufua umeme iliyopo inayotumia gesi itapata gesi inayohitajika ili kuliondoa Taifa katika upungufu wa umeme.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, tuliitaka Serikali iache kutoa kisingizio cha ufinyu wa bajeti katika kutekeleza maoni na mapendekezo ya kuongeza fedha za Miradi ya maendeleo ya sekta za nishati na madini na tulipendekeza vyanzo vya nyongeza vya mapato kwa ajili ya sekta tajwa ikiwemo, kupunguza misamaha ya kodi ikiwemo kuondoa msamaha wa ushuru wa mafuta kwa Kampuni za Madini pekee, hatua ambayo ingeongeza mapato ya shilingi bilioni 59 kutoka vyanzo vipya vya mapato tulivyovianisha. Kwa upande wa sekta ya madini kwa kurekebisha kodi katika sekta ya madini pekee yake tungeweza kukusanya shilingi bilioni 240 katika mwaka wa fedha 2011/2012. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo toka kwa Serikali ni kwa kiwango gani ushauri huo umezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu makadirio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012 ulionyesha uwezo mdogo na kasi ndogo ya kufikisha umeme vijijini kwa upande wa Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)*. Kasi ndogo ya kusambaza umeme ilielezwa pia mijini kutokana na idadi kubwa ya maombi ya wananchi wanaotaka kufungiwa umeme huku Shirika la Umeme *(TANESCO)* likiwajibu kuwa halina uwezo kwa sasa mpaka lipate miradi. Kambi Rasmi ya Upinzani ilitaka ufanyike ukaguzi wa kiufanisi kuhusu utekelezaji wa miradi ya

usambazaji wa umeme. Hivyo, Serikali inapaswa kueleza iwapo ukaguzi husika ulifanyika na hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze katika mwaka wa fedha 2011/2012, imetekeleza kwa kiwango gani mkakati wa kupunguza gharama za manunuzi na pia kupunguza kiwango cha uagizaji wa nguzo na vifaa vingine kutoka nje ili kutumia rasilimali za ndani ili kuchangia katika kukuza uzalishaji na uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, izingatiwe kwamba malalamiko yameendelea kuhusu mazingira ya kupitishwa kwa zabuni za ununuzi wa nguzo, *transforma* na nyaya za umeme kwa kiwango kikubwa toka nje ya nchi huku viwanda vya ndani mathalani *TANALEC ABB, East African Cables* (hususan kampuni tanzu ya *Tanzania Cables*) na vingine vikididimia. Hali hii imesababisha pia kukwama kwa utekelezwaji wa miradi mbalimbali ya kusambaza umeme kutokana kwa kile kinachoelezwa kuwa ni vifaa kutokupatikana kwa wakati toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imesikitishwa na kasi ndogo ya Serikali wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012, kuhusu kupunguza gharama wanazotozwa wananchi za kuunganishiwa huduma ya umeme, suala ambalo linapunguza kasi ya uunganishwaji wa umeme. Bado tumeendelea kupokea malalamiko toka kwa wananchi wanaotakiwa na *TANESCO* kulipia nguzo na

gharama nyingine za kuunganishwa umeme kwa viwango ambavyo ni vigumu kwa wananchi wa kawaida kumudu.

Hivyo, tunaitaka Serikali ieleze hatua za ziada inazokusudia kuchukua pamoja na kutekeleza maoni yetu ya kutaka *TANESCO* ibadili mfumo wa ankara ili kuruhusu kuingiza kwa mteja gharama hizo kidogo kidogo katika kipindi hiki cha mpito. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inawahimiza wananchi kutumia Kanuni za Sheria ya Umeme zilizotolewa kwenye gazeti la Serikali tarehe 4 Februari 2011 (*GN* 63) ambazo kifungu cha nne kinaeleza namna mteja atakavyofidiwa na kampuni ya usambazaji pale ambapo mteja anajigharamia mwenyewe kuvutiwa umeme ili fursa hiyo iweze kutumika ipasavyo. Hata hivyo kanuni hizo zinahitaji pia kufanyiwa marekebisho kwa kuwa zimeweka mkazo katika fidia kutolewa kutokana na malipo ya wateja wengine badala ya mapato ya Shirika kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gesi asilia, tarehe 15 Julai, 2011 Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza kuwa, nchi yetu imejaliwa utajiri wa gesi asilia katikati ya lindi la umaskini wa wananchi na kwamba Taifa letu lina fursa ya kuwa nchi kiongozi katika gesi Afrika na kushindana Kimataifa ikiwa tutaweka mstari wa mbele upeo, umakini na uadilifu katika sekta ya nishati kuepusha laana ya rasilimali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2011/2012, yanaonesha bado Serikali haichukui hatua thabiti

kushughulikia ufisadi na udhaifu wa kiuongozi katika sekta ndogo ya gesi asili hivyo hatua za haraka zisipochukuliwa katika mwaka wa fedha 2012/2013 na kuendelea rasilimali inaweza kuwa chanzo cha migogoro na kuhatarisha pia usalama wa nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa Taifa letu limekuwa likitegemea mradi mkubwa wa Songosongo kwa shughuli za uendelezaji, uzalishaji na usafirishaji ambao uko chini ya Kampuni ya *Songas*. Hata hivyo, kampuni ya *Songas* imeiajiri Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania (PAT)*, ambayo ni mshirika wa TPDC katika uzalishaji, usambazaji na ugavi wa gesi asili.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza Bungeni tarehe 15 Julai, 2011 kuhusu tuhuma za ufisadi na ukiukwaji wa mikataba katika sekta ndogo ya gesi na kutaka kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge kuchunguza suala hilo. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilifanya uchunguzi wa masuala husika na taarifa kuwasilishwa Bungeni. Hata hivyo mpaka sasa maamizio ya Bunge kufuatia taarifa hiyo hayajatekelezwa kwa ukamilifu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ni kwa nini mpaka sasa kiasi cha dola milioni 20.1 zilizopunjwa kifisadi hazijarejeshwa na Serikali iache kutumia kisingizio cha kuundwa kwa Timu ya Majadiliano *(GNT)* kuchelewesha utekelezaji wa maazimio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mradi mkubwa wa maendeleo ambao umepangwa katika mwaka wa fedha ni ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es

Salaam ambapo kwenye kasma 3162 umetengewa kiasi cha shilingi 93,000,000,000 huku kiwango kingine cha fedha za mradi huo kikitarajiwa kupatikana kutokana na mkopo kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kutokana na unyeti wa mradi huo kwa mustakabali wa nchi na maisha ya wananchi wa sasa na baadaye, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwasilisha Bungeni na kuweka wazi kwa umma mkataba wa mradi husika ili Bunge liweze kuishauri na kuisimamia Serikali kuanzia katika hatua za awali kuhakikisha kwamba maslahi ya Taifa yanalindwa katika hatua zote na pia wananchi wananufaika kutokana na fursa za uwekezaji huo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, pamoja na ujenzi wa mitambo miwili ya kusafishia gesi asili Mnazi Bay na Songo Songo kama sehemu ya mradi huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ni miradi ipi inayoambatana na mradi huo ambayo imepangwa kuwanufaisha wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara ikiwemo kuharakisha utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme wa *MW* 300 Mtwara na *MW* 230 wa Somanga Fungu (Kilwa).

Mheshimiwa Spika, pamoja na ujenzi wa Bomba la Gesi, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza mradi wa kujenga kiwanda cha kujaza gesi kwenye mitungi *(LPG)* na mradi wa usambazaji wa gesi Dar es Salaam pamoja na mradi wa matumizi ya gesi kwenye magari inayotekelezwa na Shirika la Petroli Nchini *(TPDC)* inapaswa kuongezewa rasilimali katika mwaka wa

fedha 2012/2013. Kuanza kwa utekelezaji wa mradi kwa ajili ya viwanda vichache na Kaya 57 za eneo la Mikocheni ni hatua ndogo ukilinganisha na mahitaji.

Mheshimiwa Spika, hivyo, utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2012/2013, upanuliwe wigo ili kuhusisha pia kuwezesha taasisi zingine mathalani Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuweza kuunganishwa katika mtandao wa matumizi ya gesi asili. Hatua hii itapunguza pia matumizi ya umeme katika maeneo yenye kuweza kutumia gesi na kubakiza umeme mwingine utakaoweza kutumika kwenye maeneo ikiwemo ya viwandani yenye upungufu wa nishati mbadala.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafuta, taarifa za Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2011, mfumuko wa bei ya nishati na mafuta umeongezeka kwa asilimia 41 kwa mwezi Disemba 2011, ikilinganishwa na asilimia 12.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2010. Kambi Rasmi ya Upinzani inarejea kusisitiza kwamba (ukiondoa kupanda kwa bei ya chakula kunakotokana na kushuka kwa uzalishaji na udhaifu katika usambazaji) chanzo kikuu cha hali cha mfumuko wa bei ni ongezeko la bei ya nishati hususani mafuta, umeme na gesi, hali ambayo imeshindwa kudhibitiwa kwa mikakati makini ya haraka na kuelekea kuwa tishio kwa utulivu wa Taifa kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Julai, 2011 Kambi Rasmi ya Upinzani iliitahadharisha Serikali kwamba, Muswada wa Sheria ya Fedha uliopitishwa na Bunge tarehe 22 Juni, 2011 usingeweza kupunguza ugumu wa maisha kwa wananchi kwa kuwa Serikali haikupunguza

mzigo mkubwa wa kodi badala yake iliweka kipaumbele katika kupunguza tatizo la uchakachuaji kwa kuongeza mzigo mkubwa wa kodi katika mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake ni kwamba, katika mwaka wa fedha 2011/2012, kiwango cha kodi kwenye bei ya mafuta ya *petrol* hakikupungua, kodi katika dizeli ilipungua kwa kiwango cha shilingi 99 huku mafuta ya taa yakiongezeka kodi kwa shilingi 358 kwa lita na kuongeza mzigo wa gharama za maisha kwa sababu ya udhaifu wa Serikali na vyombo vyake katika kudhibiti uchakachuaji kwa kusimamia utawala wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali ieleze ni hatua zipi ambazo Serikali imechukua dhidi ya athari za kupanda kwa bei ya mafuta ya taa kwa wananchi wa kipato cha chini na pia kwa hali ya mazingira nchini kutokana na ongezeko la matumizi ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Spika, aidha, ikiwa mkakati huu umeweza kudhibiti uchakachuaji Serikali inatoa maelezo gani kutokana na kuwepo kwa malalamiko ya kuendelea kwa aina nyingine za uchakachuaji na ni kwa nini Taifa liendelee kuingia gharama za vinasaba vinavyowekwa na *EWURA* wakati inaelezwa kwamba uchakachuaji umeweza kudhibitiwa baada ya kupandisha bei ya mafuta ya taa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, kama sehemu ya mchakato wa kupunguza gharama za mafuta kufuatia

mabadiliko ya kodi, tozo na mfumo wa uingizaji wa mafuta Serikali ieleze imefikia hatua gani katika mwaka wa fedha 2011/2012, kufanya mapitio ya mkataba baina ya *EWURA* na kampuni ya *Global Fluids International (T) Limited* kuhusu ufanisi na gharama za kuweka vinasaba na kuleta vifaa maalum vya kupima ubora *(XRF)*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiondoa kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia na ukubwa wa kodi zinazotozwa na Serikali bei ya mafuta inakuwa juu kutokana na mfumo mzima wa uagizaji, usafirishaji, uingizaji, uhifadhi na usambazaji. Mfumo uliopo unanufaisha makampuni makubwa mengi yakiwa ya kigeni na wafanyabiashara wachache wa ndani pamoja na baadhi ya viongozi wa Serikali wasiokuwa waadilifu kwa kulinyonya Taifa na kuongeza gharama za maisha kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, hali hii ndiyo iliyokwamisha kwa miaka mingi kuanza kwa mfumo wa uagizaji na uingizaji wa mafuta ya pamoja *(Bulk Procurement System)* ili kupunguza gharama. Hata hivyo, hata baada ya kuanza kwa utaratibu husika katika mwaka wa fedha 2011/2012, tija ya kutosha ya mfumo huo haijapatikana kutokana na udhaifu wa kimfumo.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza sababu za kutokurejesha hifadhi ya Taifa ya kimkakati ya mafuta *(National Strategic Oil Reserve)* pamoja na kutokukamilisha mchakato wote wa kufufua Kampuni ya Taifa ya Mafuta *(COPEC)* kinyume na ahadi ya Wizara ya Nishati na Madini ya mwaka 2011. Aidha, ni

kwa nini Serikali haikununua hisa za kampuni ya *BP* kwa kiwango cha kuwa na umiliki wa asilimia mia moja ili kuongeza miundombinu ya uhifadhi na usambazaji wa mafuta kwa uchumi na usalama wa nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Wizara ya Nishati na Madini ieleze hatua mahususi ilizochukua katika mwaka wa fedha 2011/2012 za kulinda maslahi ya nchi katika kampuni ya *TIPER* ambayo Serikali ina hisa 50% katika hatua za uingizaji na uhifadhi wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini; ili kuongeza tija na ufanisi wa *TPDC*, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo kuhusu hatua zilizochukuliwa kwenye mwaka wa fedha 2011/2012 za kulifanyia marekebisho shirika hilo ili kuwa na mamlaka itakayohusika na kutoa vibali kwenye leseni na kusimamia uchimbaji wa mafuta na gesi na kampuni itakayoshiriki katika biashara ya mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2011, thamani ya mauzo ya madini nje ilikuwa dola za Kimarekani 1,965.23 milioni ikilinganisha na dola za Kimarekani 1,536.93 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 27.9. Hii ilitokana na kupanda kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mchango kwenye pato la Taifa umekuwa ni asilimia 3.3 tu miaka karibu mitatu toka kutungwa kwa Sheria mpya ya Madini mwaka 2010. Udhaifu wa Serikali katika kusimamia

utawala wa sheria unapaswa kuondolewa kwa Bunge kupitisha maazimio ya kuisimamia Serikali kulinusuru Taifa dhidi ya hali hii ambayo utajiri wetu unaendelea kuondoka, kwa pamoja na hatua zingine, kuwezesha mwingiliano baina ya sekta ya madini na sekta nyingine za kiuchumi katika nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza hatua iliyofikia katika kuzingatia ushauri tulioutoa wa kutaka Wizara ya Nishati na Madini ishirikiane na Wizara ya Fedha kuboresha mfumo wa utoaji wa taarifa za malipo ya kodi kwa kampuni za madini ili malipo ya kila kampuni na mchanganuo wake yafahamike kwa umma badala ya mfumo wa sasa ambapo hurundikwa pamoja katika takwimu za idara ya walipa kodi wakubwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali ieleze hatua ilizochukua kwenye mwaka wa fedha 2011/2012, katika kuongeza kiwango cha mapato ikiwemo ya kodi kutokana na uchimbaji wa madini kwa kutekeleza mikakati ya kupenya kuta za umiliki na mitaji *(capital and ownership structures)* zilizojengwa kwa muda mrefu na makampuni ya Kimataifa kwa kutumia mianya ya udhaifu wa kisheria na ushawishi wa kifisadi uliosababisha mikataba mibovu katika sekta ya madini nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa kwa Serikali kuwasilisha Bungeni ripoti ya tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo ya Tume au Kamati mbalimbali ambazo ziliundwa na Serikali kwa nyakati mbalimbali kwa kutumia fedha nyingi za walipa kodi,

lakini mapendekezo yake bado hayajatekelezwa kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi Serikali inazo taarifa za makampuni makubwa ya madini kutumia sehemu kubwa ya uwekezaji wao kama mkopo *(debt financing)* na kutumia mianya hiyo ya kisheria na kimikataba kuwezesha wamiliki na wanahisa kupata faida mapema kuliko kuweka mtaji kwa kuwa riba ya mikopo huondolewa katika kukokotoa kodi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inarudia tena kuitaka Serikali iwaeleze Watanzania ni trilioni ngapi za mapato tumezikosa kati ya mwaka 1995 mpaka 2010 katika kipindi cha miaka 15 ya kuachia mianya ya upotevu wa mapato kwa kuruhusu asilimia kubwa ya mikopo kuwa mitaji. Aidha, ni hatua gani zimechukuliwa kwa waliohusika kuliingiza Taifa katika mikataba mibovu iliyoruhusu makampuni hayo kujitangazia hasara kila mwaka huku yakipata faida kubwa.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu tuna migodi mikubwa mbalimbali kati yake sita ilianzishwa kati ya mwaka 1998 -2009 kwa ajili ya kuzalisha dhahabu ambayo ni *Golden Pride Mine* (1998), *Geita Gold Mine* (2000), Bulyanhulu *Gold Mine* (2001), *North Mara Gold Mine* (2002), Buhemba *Gold Mine* (2002) na Tulawaka *Gold Mine* (2005), Buzwagi *Gold Mine* ((2009), Buhemba *Gold Mine* walifunga uzalishaji mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, migodi yote hii waliwasilisha upembuzi yakinifu Serikalini kabla ya kuanza uzalishaji na kuonesha kuwa watalipa kodi ya makampuni *(Corporate tax)*, lakini mpaka sasa ni michache tu ambayo imeanza kulipa Shilingi Bilioni 32.18 kutoka *Resolute Tanzania Limited* na Shilingi Bilioni 145.52 kutoka Geita *Gold Mine Limited* tu, pamoja na makampuni haya kunufaika na kupanda kwa bei ya dhahabu kwenye soko la dunia kwa zaidi ya mara tatu kuanzia mwaka 2002 na wakati huo huo makampuni haya yakiendelea kuweka uwekezaji mkubwa kwenye miradi yao. Kutokana na umuhimu wa sekta hii nitaeleza japo kwa kifupi kuhusiana na baadhi ya migodi hiyo mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, mgodi wa Bulyanhulu ambao mwanzoni ulitarajiwa kuwa na maisha ya miaka 15 na walitarajia kuzalisha *ounces* 400,000 za dhahabu kwa kila mwaka ila wamekuwa wakizalisha *ounces* 6.5 milioni za dhahabu kwa gharama ya kuzalisha *ounce* moja kwa dola 130. Aidha, walitegemea kuzalisha madini ya Shaba (*Copper* ) *ounces* 7.26 milioni na madini ya fedha *ounces* tano milioni na kwa sasa umri wa mgodi ni miaka 25, yaani muda umeongezeka kwa kipindi cha miaka 10 zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Bulyanhulu uliwekeza kiasi cha dola 550 milioni kwa mchanganuo wa kuwa dola 300 milioni kwa uwekezaji wa awali kabla ya kuanza uchimbaji na dola 250 milioni kwa shughuli za uendeshaji wa mgodi. Mgodi huu ulitegemea kuzalisha kiasi cha dola 900 milioni kutokana na uchimbaji na uuzaji wa madini ya shaba

(*copper*) pekee na mapato ya dhahabu yalikuwa yamewekewa ukomo wa dola 300 kwa *ounce* tu pamoja na kuwepo kwa badiliko la bei kwa zaidi ya mara tatu yaani sasa ni dola 950 kwa *ounce* moja.

Mheshimiwa Spika, ilikadiriwa kuwa mrahaba wa asilimia tatu uliotegemewa kulipwa Serikalini ni kiasi cha dola 58 milioni na fedha zilizopaswa kulipwa moja kwa moja Serikalini zilikadiriwa kuwa ni dola 64 milioni (mrahaba dola 58 milioni,mrahaba wa moja kwa moja –*direct dividend* dola milioni mbili na kodi ya zuio ya dola milioni nne).

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Bulyanhulu kwa sasa umeweza kuongeza hifadhi ya dhahabu kutoka tani 13.64 milioni na kufikia kiwango cha tani 36.05 milioni mwaka 2007 kiwango ambacho ni asilimia 90 zaidi ya kiwango kilichokadiriwa wakati wa kusaini mikataba na kuanza uchimbaji. Mpaka mwaka 2007 mgodi huu ulilipa kiasi cha dola 26.54 milioni kama mrahaba kwa Serikali na hawajalipa kodi ya makampuni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mgodi wa Geita *Gold Mine* mgodi huu ulianzishwa kwa gharama inayokadiriwa kuwa dola 152 milioni kwa ajili ya uwekezaji wote ambao ulifanywa kabla ya kuanza shughuli za uchimbaji na gharama za kuendeleza uchimbaji kwenye mgodi husika. Mgodi hu ulikuwa umeweka malengo ya kifedha kwa bei ya dola 300 kwa *ounce* na kuwa thamani halisi *(NPV)* ni dola 100 milioni, *net cash flow* dola 201 milioni, mrahaba dola 30 milioni, kodi ya makampuni dola 13 milioni, kipindi cha

kurejesha gharama miaka mitano na gharama za uzalishaji ni dola 181 kwa *ounce*.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2000 mapato halisi yalikuwa dola 14 milioni na hii ilitokana na ukweli kuwa kulikuwa na uzalishaji mdogo na pia bei iliyokuwa imetarajiwa ya dola 350 kwa *ounce* haikupatikana ila ilikuwa dola 279.321 kwa *ounce* moja. Mwaka 2004 mapato halisi yalikuwa zaidi ya mara nne ya matarajio na hii ilitokana na uzalishaji kuwa mkubwa na bei ya dhahabu kuongezeka kwani lilikuwa dola 409.271 kwa *ounce* ikilinganishwa na ukadiriaji wa dola 350 kwa *ounce* uliokuwa umewekwa awali.

Mheshimiwa Spika, ila kwa ujumla ni kuwa mapato halisi ya mgodi huu kuanzia mwaka 2001 yamekuwa yakiongezeka maradufu kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji na bei ya dhahabu kuendelea kupanda kwenye soko la dunia. Mpaka mwaka 2007 mgodi huu ulikuwa haujalipa kodi ya makampuni pamoja na uzalishaji kuongezeka na kuwa mara mbili zaidi ya matarajio na bei ya dhahabu kuwa kubwa mara tatu zaidi ya matarajio kwenye soko la dunia na hii iliufanya mgodi huu mapato yake kuongezeka zaidi ya mara tatu na mgodi uliendelea kutangaza kuwa unapata hasara na haujaweza kurejesha uwekezaji uliofanywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgodi wa Tulawaka, katika mgodi huu uwekezaji uliofanywa ulikadiriwa kuwa ni dola 34.6 milioni na gharama za uendeshaji zilitarajiwa kuwa dola 325 kwa uzalishaji wa *ounce* moja, thamani halisi *(NPV)* Dola 9.507 milioni, *net cash*

*flow* dola 29 milioni, mrahaba dola 5.367 milioni na kipindi cha kurejesha gharama miaka minne (*pay back period*) na walitarajia kulipa kodi ya makampuni mwaka 2008 ya dola 2.8 milioni.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004 hapakuwa na uzalishaji na hivyo hapakuwa na mapato yoyote ila kwa mwaka 2004 – 2007. Mapato halisi ya mgodi huu yamekuwa asilimia 72.5 ya zaidi ya makadirio ya awali yaliyowekwa. Mpaka mwaka 2007 mgodi huu haukuwahi kulipa kodi ya makampuni pamoja na ukweli kuwa uzalishaji ulikuwa asilimia saba chini ya matarajio ila mapato halisi yaliongezeka kwa asilimia 72.5 zaidi ya matarajio yaliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mgodi wa *North* Mara mpaka disemba 2007 ilikadiriwa kuwa kuna *ounce* 3.6 milioni ukilinganisha na zilizokuwa zimetangazwa awali wakati mgodi unaanza uzalishaji kuwa ni 2.94 milioni *ounce* mwaka 2002 wakati wa ufunguzi rasmi wa mgodi. Mgodi huu mpaka mwaka 2007 ulikuwa umebadilisha wamiliki kwa zaidi ya wamiliki watatu tofauti tofauti na hii inafanya kuwa ngumu sana kuweza kupata taarifa halisi za mwenendo wa mapato kutokana na kila mmiliki kuweka utaratibu wake na kuanza upya kama vile hapakuwa na kilichofanywa na mmiliki aliyemtangulia. Aidha, wamiliki wa awali waliweza kuuza migodi hii na kunufaika moja kwa moja bila Serikali kupata chochote kutokana na mauziano yaliyofanywa.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa hizi tunaweza kuelewa kuwa uzalishaji halisi wa dhahabu kwenye

migodi hiyo mitano kuanzia mwaka 1999 -2007 ulikuwa 8.388 milioni *ounces* ukilinganisha na matarajio yaliyowekwa awali kuwa ni kuzalisha 6.882 milioni *ounces* ambacho ni asilimia 21.88 zaidi ya matazamio ya awali. Umri kwa ajili ya uzalishaji wa migodi hii umeongezeka kwa wastani wa miaka minne kwa kiwango cha chini na miaka 10 kwa kiwango cha juu. Hii ilitokana na kugundulika kwa machimbo mapya ya dhahabu pamoja na kuongezeka kwa teknolojia ya kisasa zaidi kwenye tasnia hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mapato halisi yaliyoweza kupatikana kutokana na migodi hii mitano mikubwa kwa kipindi hicho cha kuanzia mwaka 1999-2007 ilikuwa dola 3.8 bilioni ambazo ni asilimia 64 juu zaidi ya matarajio yaliyowekwa wakati uwekezaji ukifanywa ambayo ni dola 2.3 bilioni. Pamoja na mapato hayo ni kuwa fedha iliyolipwa Serikalini kama mrahaba ilikuwa dola 99.6 milioni tu kwa kipindi chote hicho. Kwa migodi yote hiyo matarajio ya bei yaliyowekwa yalikuwa kati ya dola 300-350 kwa *ounce* wakati uhalisia ni kuwa bei ilipanda na kufikia kiasi cha dola 950 kwa *ounce* moja.

Mheshimiwa Spika, mapitio yaliyofanywa na Mamlaka ya Ukaguzi wa madini *(TMAA)* kuanzia mwaka 2004 - 2008 nchini yalionesha kuwa mgodi wa *Tanzanite One Tanzanite Mine (TTM)* umekuwa ukilipa mrahaba kwa kutumia viwango vya awali vya makadirio ambavyo viliwekwa wakati mgodi huu ukianzishwa nchini.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika ripoti hiyo inaonesha kuwa kampuni hii imekuwa ikitoa taarifa za zisizokuwa za kweli juu ya mauzo yaliyofanyika nchini na kwenye makampuni makubwa nje ya nchi ili kuweza kukwepa kulipa mrahaba stahiki Serikalini. Tathmini hiyo ya ukaguzi inaonesha kuwa kwa kipindi hicho kiasi cha dola 42.7 milioni kiliongezeka zaidi kulingana na kiwango kilichotangazwa nchini na kampuni hiyo. Hii maana yake ni kuwa kiasi cha dola 2.1 milioni kilichopaswa kulipwa kama mrahaba Serikalini hakikulipwa kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini kifungu cha 93 *(The Mining Act, Cap. 123)*.

Mheshimiwa Spika, suala hili ni kwa mujibu wa barua iliyotumwa kwa Meneja wa Kampuni ya *Tanzanite one* iliyoandikwa tarehe 2.10.2009 yenye Kumb. Na *DA* 23/168/01 iliyoandikwa na aliyekuwa Kamishna wa Madini Mheshimiwa Dalali Kafumu akiwataka wawekezaji hao kulipa, hata hivyo, deni hilo halikulipwa kwa wakati. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza hatua ilizochukulia kampuni hiyo. Aidha, tunaitaka Serikali kutoa maelezo ya kina kuhusu kuhamishwa kwa umiliki wa kampuni hiyo kwa kuzingatia kwamba, baada ya kutungwa kwa Sheria ya Madini ya mwaka 2010, Serikali iliahidi kwamba uchimbaji katika eneo hilo ungeachwa kwa wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuweka hadharani ripoti na taarifa zote zilizowahi kutolewa kuhusiana na uwekezaji katika uchimbaji wa madini nchini kuanzia mwaka 1995 hadi

2010 na kama Serikali imefaidika na nini kutokana na uwekezaji huo.

Pili, tunahitaji mikataba yote iwekwe hadharani kwani kutokana na taarifa hizi ni hakika kuwa mikataba yetu ni mibovu sana na tunalipotezea Taifa mapato mengi na hivyo kuendelea kudidimiza uchumi wa Taifa.

Tatu, Bunge liazimie kuwa mikataba yote mipya ya uchimbaji wa madini, mafuta na gesi lazima sasa iletwe Bungeni na kujadiliwa kwa maslahi ya Watanzania, kwani kama tukiendelea na utamaduni wa kusaini mikataba husika kisirisiri Taifa hili litaendelea kupoteza mapato kutokana na uzembe na ufisadi kwa wanaohusika na mikataba.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuendelea kuporomoka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza hatua iliyofikiwa katika kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa ya kutaka Wizara ya Nishati na Madini ishirikiane kwa karibu na Wizara ya Fedha katika kuweka mikakati na usimamizi wa kuhusisha sekta ya madini katika kuimarisha fedha yetu. Wakati umefika sasa wa kuwezesha Benki Kuu kutunza sehemu ya hifadhi yetu ya fedha za kigeni katika mfumo wa madini ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Wizara ya Nishati na Madini ishirikiane na Benki Kuu kuweka mfumo wa kununua dhahabu kwa wachimbaji wadogo wadogo na pia kutoza sehemu ya mrabaha wa dhahabu kwa ajili ya uhifadhi kama ilivyoshauriwa na Kambi Rasmi ya

Upinzani pamoja na Kamati mbalimbali za Bunge. Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kwamba, utaratibu huu uende sambamba na kusimamia mfumo wa kuhakikisha kwamba, makampuni hayo yanatunza sehemu kubwa ya fedha za nje (angalau 60%) kwenye benki za ndani ili kusaidia kudhibiti kuporomoka kwa shilingi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini ya mwaka 2010 imeipa majukumu muhimu *STAMICO* ya kuwa mwakilishi na msimamizi wa rasilimali za madini nchini kwa niaba ya Srikali. Mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2011/2012, yanadhihirisha kwamba majukumu haya muhimu ya kisheria hayajawekewa mazingira wezeshi ya kutosha ya kimfumo, kirasilimali na kikanuni takriban miaka miwili tangu kutungwa kwa sheria husika. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuharakisha marekebisho ya Sheria Ndogo (*Establishment Order*) iliyounda *STAMICO* ili kuendana na mahitaji ya sasa na kuongeza mtaji wake ikiwemo kurejesha rasilimali zilizochukuliwa ikiwemo majengo.

Mheshimiwa Spika, Serikali izingatie kwamba sera mkakati katika sekta ya madini iwe ni kuhakikisha Watanzania wana umiliki katika miradi mikubwa ya madini ama kupitia hisa za makampuni hayo kuwekwa katika Soko la Ndani *(DSE)* au kwa kampuni ya umma kushikilia sehemu kubwa ya uwekezaji hasa katika madini nyeti ikiwemo urani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wakala wa Jiolojia *(GST)* aliendelea na utekelezaji wa mradi wa kutambua maeneo ya

madini, Wizara ya Nishati na Madini ieleze iwapo utekelezaji wa mradi huo ulienda sambamba na kufanya tathmini ya kina *(mineral appraisal)* ya madini yetu ili kupendekeza mabadiliko ya kisheria na kimikataba ambayo yatawezesha utajiri wa madini yetu kutumika kama mtaji na dhamana katika hatua ya kuhakikisha Taifa letu linanufaika na rasilimali zake kama ilivyopendekezwa na Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, aidha, ni kiwango gani cha mapato kilichopatikana kwenye mwaka wa fedha 2011/2012, kutokana na kuiwezesha *GST* kutoza malipo kwa mujibu wa Sheria Ndogo *(Establishment Order)* iliyounda Wakala husika. Ili kulinda maslahi ya Taifa kuhusu matumizi ya ramani na ripoti za utafiti na uchunguzi huo. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, ukaguzi maalum *(Special Audit)* ufanyike kuhusu mfumo wa utoaji leseni za utafutaji na uchimbaji wa madini nchini ili kudhibiti uporaji *(grabbing)* unaoendelea katika rasilimali muhimu za Taifa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Julai, 2011 tulitoa tahadhari juu ya maamuzi ya Serikali ya kuendelea na hatua za mbele katika utafutaji na uchimbaji wa madini ya urani bila kukamilisha maandalizi ya kisera, kisheria, kikanuni na kitaasisi yanayohitajika, suala ambalo linaachia mianya ya upotevu wa mapato kwa Taifa kama ilivyokuwa kwenye madini mengine na pia linaweza kuhatarisha usalama. Aidha, Kambi ya Rasmi ya Upinzani ilitaka maelezo ya kina kuhusu mauzo na mabadilishano ya umiliki yaliyofanyika baina ya kampuni ya Australia *(Mantra Resources)* na Kampuni

ya Urusi ya *ARMZ Uranium Holding*, kampuni tanzu ya *Rosato*.

Mheshimiwa Spika, mauzo hayo yamehusisha kuhamishiana umiliki wa maeneo ya Tanzania, Mkuju River (Mbamba Bay) na Bahi Kaskazini (Dodoma). Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* ilifanya ufuatiliaji juu ya suala hilo, hivyo Wizara ya Nishati na Madini inapaswa kueleza kiasi gani cha fedha kimefanikiwa kupatikana na ni hatua zipi Serikali imechukua kwa Makampuni mengine ya Madini, Mafuta na Gesi asili yaliyofanya mauziano katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, licha ya ahadi ya Serikali ya toka mwaka 2010 ya kumaliza migogoro katika sekta ya madini baina ya wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo wadogo ikiwemo kudhibiti migongano kati ya wenye leseni kubwa na leseni ndogo, migogoro hiyo imeendelea katika mwaka wa fedha 2011/2012. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwasilisha Bungeni orodha ya maeneo yote yenye migogoro ya madini nchini pamoja na ratiba ya utatuzi wa migogoro husika.

Mheshimiwa Spika, pia, pamoja na kuandaa Mkakati wa Kuwaendeleza wachimbaji wadogo ili mkakati huo usiwe maneno matupu; Serikali iwasilishe pia mpango kazi na bajeti ya utekelezaji wa mkakati husika.  Aidha, Serikali ianzishe mfumo wa kisheria wa kuwezesha wananchi waliokuwa wakilimiki ardhi katika maeneo yenye madini kuweza pamoja na fidia ya

mazao na maendelezo kuwa na hisa katika umiliki wa migodi husika.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kushamiri kwa migogoro baina ya wafanyakazi na wawekezaji katika sekta ya madini, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza Wizara ya Nishati na Madini iweke mfumo wa mashauriano na Wizara nyingine ili kuharakisha utatuzi wa migogoro husika. Aidha, kumekuwepo na wimbi la malalamiko ya wafanyakazi walioachishwa katika migodi wa Bulyankulu, Kampuni ya *Caspian* katika mgodi wa Mwadui Shinyanga, masuala ambayo yanahitaji ushirikiano wa Wizara na mamlaka mbalimbali katika kuyashughulikia. Aidha, Wizara ya Nishati na Madini itoe maelezo kuhusu taarifa zilizotolewa Bungeni tarehe 13 Aprili, 2012 kuwa wafanyakazi ikiwemo wa migodini kupitia Vyama vyao walihusishwa kutoa maoni yaliyopelekea kufutwa kwa fao la kujitoa *(withdrawal benefits)*; suala ambalo Chama cha Wafanyakazi wa Migodini *(TAMICO)* kimelikanusha.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ufafanuzi uliotolewa na Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii *(SSRA)* kwa barua yenye Kumb. Na. *AE*/164/334/*Vol* II/2 umekataliwa katika migodi mbalimbali, Wizara ya Nishati na Madini imechukua hatua gani kuepusha migogoro iliyoanza kujitokeza baina ya wafanyakazi wa migodini na Serikali kufuatia kupitishwa kwa vifungu husika vya sheria vyenye kuagiza mafao kutolewa baada ya kufikisha umri wa hiyari wa kustaafu wa miaka 55 au umri wa lazima wa miaka 60.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilihoji tarehe 15 Julai 2011 kuhusu tuhuma za Kampuni ya *New* Almasi (1963) *Limited* kuchimba almasi kwa miaka 35 Mkoani Shinyanga licha ya muda wa leseni yake Na. 224 kwisha na leseni yenyewe kufutwa katika rejesta ya leseni za madini. Taarifa zilizopo zinaonesha kwamba mkataba kati ya *New* Almasi (1963) *Limited* uliingiwa kinyemela kwa lengo la kuwezesha uchimbaji wa almasi kuendelea katika eneo hilo kinyume cha sheria na ili kuendeleza wizi wa rasilimali ya nchi yetu. Mamia ya wananchi waishio maeneo jirani na eneo la *New* Almasi wamekuwa wakinyanyaswa kwa miaka mingi na vyombo vya dola kama vile Polisi, Mahakama na vyombo vya utawala kwa madai kwamba ni wavamizi wa eneo la leseni ya *New* Almasi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze hatua ilizochukua kwenye mwaka wa fedha 2011/2012, kuichunguza kampuni hiyo, uhalali wa shughuli zake za uchimbaji almasi katika eneo la Luhumbo, kiasi cha almasi iliyochimbwa kwa kipindi chote tokea tarehe 1 Juni, 1965 hadi tarehe 8 Mei, 2000 na zilizokokwenda fedha zilizotokana na mauzo ya almasi hiyo. Aidha, Serikali ifafanue utaratibu wa kisheria ambao uliiruhusu Williamson Diamond *Limited* kuendelea kuchimba almasi katika eneo la Luhumbo pamoja na utata juu ya uhalali wa leseni katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi na Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2012/2013, ni shilingi 641,269,000,000 ikilinganishwa na Shilingi 538, 514,071,000 zilizotengwa

wa Wizara mwaka 2011/2012, baada ya kufanyika kwa uhamisho wa fedha. Bajeti hiyo imeongezeka kwa Shilingi 102,755,658,000, sawa na ongezeko la asilimia 19, hata hivyo ongezeko hili ni dogo ukilinganisha na mahitaji yaliyotajwa na Mpango wa Taifa wa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mapato kwa upande wa makisio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2012/2013, ni Shilingi 193,007,543,000. Kati ya makusanyo hayo, jumla ya Shilingi 173,702,263,000 zitakusanywa na Idara ya Madini; Shilingi 19, 217,277,000 zitakusanywa na Idara ya Nishati na Petroli, na Shilingi 88,003,000 zitakusanywa na Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Wizara ya Nishati na Madini ichukue hatua zaidi za kuongeza mapato kwa kifungu cha 2001 cha Idara ya Madini Kasma 140101 ya ada za Madini na Kasma 140353 ya Mrabaha kwa pamoja. Maeneo hayo yakiongezewa usimamizi kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na kanuni zake yana uwezo wa kulipatia Taifa kiasi kisichopungua bilioni 200 katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara ya Nishati na Madini itoe maelezo iwapo matarajio ya makusanyo katika Sekta ya Nishati na Petroli kifungu cha 3001 hususani kasma 140274 yanajumuisha marejesho ya mapato ya mauzo ya gesi asili yaliyopunjwa kati ya mwaka 2004 mpaka 2010. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali izingatie kuwa mapato katika shughuli za *TPDC* za utafiti wa mafuta pamoja na mauzo ya gesi

asili yanaweza kabisa kuongeza ziada ya makadirio ya makusanyo ya bilioni 19 tu iwapo udhibiti katika gharama na ukaguzi wa mikataba utaongezeka katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, pia ili kuongeza mapato kwa Serikali na *TPDC* Kambi Rasmi ya Upinzani inataka mrabaha wa asilimia 12 kwenye gesi uanze kutozwa kwa mujibu wa sheria na isitishe mara moja utaratibu wa baadhi kuachiwa kutokulipa malipo husika kwa mujibu wa sheria. Mapitio ya kitabu cha mapato yameonesha kwamba, wakati kwenye kifungu cha 2001 cha madini kuna mrabaha hakuna kasma hiyo kwenye kifungu 3001 kinachohusika na gesi na mafuta.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Kawaida yanaombewa jumla ya Shilingi 110,078, 868,000 kati ya fedha hizo shilingi 17, 292, 347,000 ni kwa ajili ya mishahara *(P.E)* ya Wizara na Mashirika yaliyo chini yake na Shilingi 92,786, 521,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC)*. Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa rai kwa Wabunge na Bunge kuungana pamoja kabla ya kupitisha matumizi haya makubwa ya kawaida kwenye matumizi mengineyo pamoja na kuitaka Wizara ya Nishati na Madini kubana matumizi kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali itakiwe kutoa maelezo ya kina kuhusu matumizi ya kifungu cha 1005 cha Kitengo cha Sheria ambacho kina kasma ya 229900 ambayo kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kimetengewa kiasi cha Shilingi 4,000,000,000 kama gharama za utetezi wa Serikali katika kesi ya *IPTL*

ikiwemo kwa ajili ya kuilipa kampuni ya *Mkono & Company Advocates*. Izingatiwe kwamba katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali ilifanya uhamisho wa fedha wa kiasi cha Shilingi Bilioni 10 kwa ajili ya gharama za kuendesha kesi zilizopo Mahakamani zinazoihusu Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza jumla ya fedha zilizotumiwa na Wizara kati ya mwaka 1995 mpaka 2011 kwa ajili ya kulipa makampuni binafsi ya Uwakili kwenye kesi kubwa za Kitaifa na za Kimataifa pamoja na kutaja orodha ya makampuni hayo. Aidha, Serikali ieleze mkakati wa kudhibiti ongezeko la gharama za kisheria ambazo ni mzigo mkubwa kwa mashirika ya umma na wananchi walipa kodi kwa kuwa yamekuwepo mazingira ya kesi kuendelezwa kwa muda mrefu na kugeuzwa kuwa vitega uchumi vya watu wachache. Mifano ya kesi zilizodumu kwa muda mrefu ni ya *IPTL* ambayo Serikali inawakilishwa na *Mkono and Company Advocates* na ile ya *Dowans* ambayo Serikali imekuwa ikiwakilishwa kwa nyakati mbalimbali na *Rex Attorneys*.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011 Benki ya *Standard* Hong Kong ambayo ni mdeni mkuu katika sakata la *IPTL* ilifungua kesi ya madai katika Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi *(ICSID case No. ARB*/10/20) inayodai kiasi cha dola za Kimarekani milioni 225, pamoja na riba katika kuendesha kesi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika muendelezo wa Serikali kampuni ya Uwakili ya Mkono ilipewa zabuni ya

kuitetea Serikali katika shauri hilo na kwa kujiamini iliishauri Serikali kuwa kesi hiyo kama Serikali tungeshinda pamoja na Wanasheria wengine kuwa na maoni kinzani kuhusu suala hilo. Lakini kutokana na uroho na kutaka maslahi binafsi kwa Kampuni ya Mkono inaishauri Serikali isifanye usuluhishi nje ya Mahakama ya *ICSID* wakati wadai kupitia kwa Mfilisi wa Mali na Madeni za *IPTL* wanakubali kusuluhishwa nje ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaliona hili kuwa ni mchezo wa kuihujumu Serikali ambao umekuwa ukifanywa na makampuni binafsi ya Uwakili kuchelewesha kesi ili yeye aendelee kulipwa mabilioni ya fedha za walipa kodi. Huu ni uhujumu wa kodi za wavuja jasho wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, katika mwendelezo huo huo Kampuni ya *Mkono & Advocates* kwa sababu ya uzoefu wake wa kazi hiyo na ushawishi wake mkubwa kwa viongozi wa Serikali imekuwa ni kawaida kwa kampuni hiyo kuingia mikataba kuzitetea Kampuni za nje zenye kutiliwa shaka kama ilivyo Kampuni ya matangazo inayotoka bara Asia inayojiita *Asia Business Channel* inayodai kutengeneza matangazo ya biashara. Kampuni hiyo yenye mwelekeo wa kutaka kutapeli ilitambulishwa kwa Mtendaji Mkuu wa *TMAA* na Waziri wa Nishati kipindi hicho Mheshimiwa William Ngeleja kwa barua yenye Kumb. Na. *AB* 88/233/01 ya tarehe 8 Desemba, 2011. Lengo lilikuwa ni *TMAA* kuingia mkataba wa kutangaza sekta yetu ya madini nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika biashara hiyo ya kulazimisha, kampuni hiyo iliitumia Kampuni ya *Mkono & Advocates* kuandika barua ya kusudio la kuishtaki *TMAA* kama itashindwa kuilipa kampuni ya *Asia Business Channel* kiasi cha paundi za Kiingereza 35,500 kwa kazi ambayo majadiliano yalikuwa hayajafikia hatua ya mwisho. Kambi ya Upinzani inajiuliza Kampuni hii kweli ni ya wazalendo au ni ya watu ambao wanasukumwa na dhamira ya kufilisi rasilimali za Watanzania?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambayo ina mamlaka ya kuiwakilisha Serikali katika kesi zote zinazoihusu Serikali ieleze imechukua hatua gani kuhusu hali hii na ifungulie mashtaka Kampuni zote zenye kuonesha uzembe na hujuma katika kuishauri Serikali kwenye kesi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa zinazohusu nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, aidha, kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu itashindwa kutekeleza hilo ni wazi Mshauri huyo Mkuu wa Serikali katika mambo ya sheria atakuwa na yeye ameshindwa kazi na hivyo ni bora awape nafasi watu wenye uwezo wa kuangalia na kusimamia maslahi ya umma.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Maendeleo imetengewa Jumla ya Shilingi 531,190,861,000 kati yake Shilingi 431,190,861,000 ni fedha za ndani na Shilingi 100,000,000,000 ni fedha za nje. Kati ya hizo kifungu cha 2001 cha Madini kimetengewa katika Kasma 3152 Shilingi 240,000,000 tu, tena za nje kwa ajili ya Uwazi

katika Tasnia ya Uziduaji *(Tanzania Extrative Industries Transparency Initiatives –TEITI)* hivyo kutokana na umuhimu wa asasi hiyo katika kuweka mfumo wa uwazi katika usimamizi na uvunaji wa rasilimali za madini, mafuta na gesi asili ni muhimu kiwango cha fedha kikaongezwa na kuhakikisha kwamba Sheria ya TEITI inatungwa katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, aidha, taarifa zote tatu za *TEITI (Reconciliation Reports)* ziwasilishwe na kujadiliwa Bungeni. Kwa upande mwingine, Bunge lisikubali kupitisha kiasi cha Shilingi 40,000,000,000 kinachoombwa kwenye Kasma 3160 kwa ajili ya kulipia madeni ya Kiwira *(KCPL)* mpaka uhakiki ufanyike juu ya uhalali wa viwango vya madeni husika kwa kuwa mradi mzima uligubikwa na tuhuma za ufisadi na matumizi mabaya ya madaraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo ya Nishati na Petroli, kifungu cha 3001, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo kuhusu sababu za kutekelezwa taratibu kwa mradi wa *TEDAP* (Kasma 3132) ambao iwapo utaharakishwa utakuwa na mchango katika kuboresha mfumo wa gridi pamoja na kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu kama vyanzo mbadala katika uzalishaji umeme nje ya gridi. Aidha, pamoja na nyongeza ya fedha za miradi ya maendeleo kwa ajili ya Wakala pamoja na Mfuko wa Umeme Vijijini *(REA/REF)* (Kasma 3113). Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza umuhimu wa kuongeza kiwango cha fedha za ndani ili kufikia bilioni 150 ili kuharakisha kasi ya uzalishaji na usambazaji wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, pia kutokana na kasi ndogo ya usambazaji wa umeme, pamoja na kuondoa kodi katika vifaa vya umeme wa jua, Serikali ieleze hatua ilizochukua katika kuweka mazingira wezeshi kwa vifaa vya umeme wa dharura kuweza kupatikana kwa urahisi mathalani vifaa vya kuhifadhia umeme *(invertors)*. Kupitia Kasma 3147 Wizara ya Nishati na Madini inaomba 47,959,861,000 kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kwa ajili ya kununua mafuta ya kuendesha mitambo ya dharura. Hivyo, ni muhimu maelezo yakatolewa kuhusu matumizi ya fedha za mafuta ya mitambo ya dharura kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ili kujenga uhalali wa matumizi ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini inaomba shilingi 62,000,000,000 kwa ajili ya Mradi wa Kuboresha Mifumo ya Umeme Katika Jiji la Dar es Salaam (Kasma 3154). Pamoja na mradi huo kuweka mkazo katika kufunga *transfoma* kubwa zaidi na njia kubwa za umeme za msongo wa *kV* 33 kwa ajili ya wateja wakubwa wa katikati ya Jiji; mradi uweke mkazo pia katika usambazaji wa umeme pamoja na kuongeza nguvu ya umeme katika maeneo ya pembezoni ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, izingatiwe kwamba matatizo ya miundombinu ya umeme katika Jiji la Dar es Salaam kutoendana na kasi ya ongezeko la mahitaji ya umeme hayapo katikati ya Jiji pekee bali pia yapo maeneo ya pembezoni yenye ongezeko la wakazi na vitega uchumi mbalimbali. Baadhi ya maeneo hayo ni

pamoja na Malambamawili, Kwembe, Goba Matosa, Msakuzi, King'ongo na mengineyo katika Manispaa mbalimbali za Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara ieleze iwapo kiasi cha 10,000,000,000 kilichotengwa kwa ajili ya kulipa fidia wananchi wanaoishi katika maeneo hatarishi yanayozunguka mitambo ya kuzalishia umeme ya Ubungo kitatosha kukamilisha kazi hiyo kwa mwaka wa fedha 2012/2013, ili kuepusha uwezekano wa gharama kuongezeka kutokana na riba ya kuchelewa kufanya malipo kama ilivyotokea kwa miaka iliyopita.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 na kutokana na Mpango wa Dharura wa Umeme uliopitishwa Bungeni tarehe 13 Agosti, 2011 Serikali imepanga kuanza utekelezaji wa miradi ya *MW* 240 Kinyerezi ambao umetengewa shilingi 5,000,000,000 katika Kasma 3163 na *MW* 150 Kinyerezi ambao umetengewa shilingi 13,000,000,000 katika Kasma 3164. Hata hivyo, kwa miradi yote hiyo Serikali iko katika hatua ya majadiliano na kufunga mikataba ya mikopo na Kampuni za *SUMITOMO* na *Jacobsen* wakati ambapo michakato ya miradi hiyo ilianza toka mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inarejea kuitaka Serikali kutangaza matatizo ya nishati ni janga la Taifa ili kuweka mfumo wa dharura wa kushughulikia kwa haraka usimamizi wa uongozi mkuu wa nchi tofauti na sasa ambapo miradi hiyo inachukuliwa kuwa ni ya kawaida chini ya Wizara ya Nishati na Madini. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani

inataka uhakika toka Serikalini iwapo mitambo hiyo inayotarajiwa kutumia gesi itakamilika lini na iwapo itapata nishati husika kwa wakati na kwa uhakika kwa kuzingatia kuchelewa kuanza kwa ujenzi wa bomba la gesi.

Mheshimiwa Spika, pia, Serikali itaje miradi mingine ya nyongeza ambayo utekelezaji wake unakusudiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2012/2013 ili kufidia pengo la mwaka wa fedha 2011/2012 na kuhakikisha kwamba kila mwaka wastani wa *MW* 360 za mitambo isiyokuwa ya kukodi zinaingia katika Gridi ya Taifa katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Taifa wa miaka mitano (2011/2012 - 2015/2016) umelenga kuongeza uzalishaji wa umeme mpaka kufikia *MW* 2780 kwa kuongeza *MW* 1788 kwa mujibu wa miradi iliyotajwa kwenye mpango kipengele A.1.3 kuhusu nishati. Lengo hili ni dogo ukilinganisha na rasilimali ambazo zipo katika Taifa letu. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza imefikia hatua gani katika kufanya mapitio ya mpango huo na kuongeza miradi mingine mikubwa ukiwemo wa *Stiggler Gorge* ambao una uwezo wa kuzalisha *MW* 2100 kama nilivyopendekeza Bungeni tarehe 14 Juni, 2011 na kuingiza pia makadirio ya ujumla ya *MW* zinazotokana na miradi midogo midogo itakayoanzishwa katika maeneo mbalimbali kama tulivyoshauri tarehe 15 Julai, 2011.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza miradi iliyosalia kwa wakati Kambi Rasmi ya Upinzani inarudia kuitaka Wizara ya Nishati na Madini kueleza mazingira wezeshi ambayo yanakusudiwa kuandaliwa ili miradi ifuatayo iweze kupata rasilimali kwa wakati na makubaliano kukamilishwa mapema: Iringa-Mchuchuma na Ngaka (Makaa ya Mawe-300), Kiwira (*MW* 200), Singida (Upepo) na Morogoro/Iringa- Ruhudji (Maji- *MW* 358).

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa Taifa kuendelea kutegemea vyanzo ambavyo vilianzishwa na Serikali ya Awamu ya Kwanza iliyoongozwa na Hayati Mwalimu Nyerere na awamu zilizofuata sio tu zimeshindwa kuongeza kasi ya kuzalisha umeme bali pia zimeshindwa kukarabati mitambo hiyo na hivyo kuzalisha chini ya kiwango. Taarifa ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2010 ilionesha kwamba vituo vya kuzalisha umeme vilikuwa vikifua umeme kwa wastani wa 53.5 tu ya uwezo wake.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka pia Serikali kueleza imechukua hatua gani kwa mwaka 2011/2012 na inapanga kuchukua hatua gani za dharura kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kuhakikisha uwezo wa vyanzo vilivyopo, uzalishaji unaongezeka sanjari na kupunguza upotevu wa umeme kutokana na ubovu wa mifumo ya usafirishaji na usambazaji.

Mheshimiwa Spika, ili kujiandaa kitaalam kama Taifa kwa mipango kabambe ya gesi wakati nchi ikisubiri Sera ya Gesi, Sheria ya Gesi na Mpango Kabambe wa Gesi *(Gas Master Plan)* vinavyopaswa

kuwasilishwa katika Mkutano wa Tisa wa Bunge. Pia Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Wizara ya Nishati na Madini ieleze hatua iliyofikiwa katika kukamilisha mtaala wa uhandisi wa gesi na mafuta ili fani hizo ziweze kutolewa kwenye Chuo cha Madini, Dodoma. Aidha, wakati wa kuhitimisha mjadala wa Mpango wa Taifa wa miaka mitano tarehe 14 Juni 2011, Serikali ilikubali pendekezo la kuanzisha Chuo Kikuu cha Mtwara.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo hicho hakijaingizwa kwenye Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano, toleo la mwezi Juni 2012 kifungu cha A.1.5. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ni hatua zipi zitaanza kuchukuliwa kwenye mwaka wa fedha 2012/2013 na Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na mamlaka nyingine zinazohusika kuwezesha kuanzishwa kwa Chuo Kikuu hicho muhimu ambacho kitatoa mchango mkubwa kwa Taifa katika masuala ya mafuta na gesi na bidhaa zitokanazo na gesi na mafuta.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha sekta ya gesi na sekta kuwa na manufaa kwa nchi yetu, narudia tena mapendekezo kama tulivyoyatoa katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kama ilivyowasilishwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani katika hotuba yake ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nanukuu kama ifuatavyo:

“Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatoa mapendekezo yafuatayo katika kuimarisha na kuboresha sekta ya gesi na mafuta hapa nchini ili kuitayarisha nchi kwa utajiri huu mkubwa:

(i) Wananchi wanaozunguka maeneo yanayopatikana au yanayopitia gesi asili wawe sehemu ya mipango ya maendeleo ya gesi asili na hivyo kunufaika na matumizi ya gesi badala ya kuachwa, hali inayoleta manung'uniko na tishio la uendelevu wa sekta husika. Hii ni kwa sababu hasa ikizingatiwa kuwa uwekezaji unaofanywa katika sekta hii kama wananchi hawataona kuwa na wao ni wafaidika, ni rahisi sana kuweza kuhujumu miundombinu hii na kuhatarisha usalama na hata uhai wa wananchi wengine;

(ii) Ujenzi wa miundombinu ya gesi uwe unazingatia mahitaji ya muda mrefu ili kupunguza gharama na kuondokana na uhaba na uharibifu wa maliasili, mfano bomba la Songosongo liliwekwa bila kuzingatia mahitaji asili ya gesi na hivyo kujikuta kuwa wanashindwa kusafirisha gesi ya kutosha kutumiwa na wahitaji wote;

(iii) Tuwekeze kwenye kuwapa elimu na maarifa vijana wa Kitanzania na hasa kwenye Sekta ya Gesi ili waweze kupata utaalam wa jinsi ya kusimamia sekta hii kama ambavyo nchi majirani zetu wa Uganda na Msumbiji wamefanya kwa kuwapeleka vijana wao nje ya nchi ili kupata utaalam juu ya uendeshaji wa sekta hii;

(iv) Serikali iliahidi kwa Shirika la Fedha la Kimataifa kwamba Sheria ya Usimamizi Bora wa Fedha za Mafuta na Gesi *(Petroleum Revenue Management Act)* italetwa Bungeni mnamo mwezi Novemba. Kambi

ya Upinzani inasisitiza kwamba Sheria hii iletwe haraka ili kuweka wazi mapato yatokanayo na utajiri huu na namna bora ya kutumia fedha hizi ili kuzuia uchumi kuathiriwa na pia kuzuia ufisadi. Hatutaki Tanzania iwe kama nchi nyingine za Kiafrika ambazo utajiri wa Mafuta na Gesi umekuwa ni laana badala ya neema;

(v) Serikali iweke mazingira bora ya kujenga uwezo wa Watanzania kutoa huduma kwenye kila hatua ya utafutaji wa mafuta na gesi. Hivi sasa kuna zaidi ya wageni 1,200 kwenye Meli za kutafuta mafuta na gesi katika Pwani ya Mtwara, Lindi na Pwani. Kwa masikitiko makubwa sana wageni hawa wanakula hata nyanya, mchicha na vitunguu kutoka nje ya Tanzania; na

(vi) Vile vile tudhibiti makampuni ya Ulinzi kutoka nje kuwa na silaha kali kali kwa kujenga uwezo wa Jeshi letu la Majini *(Navy)* ili liwe na kikosi maalum kwa ajili ya kulinda meli za kutafuta mafuta na gesi na Makampuni haya yatozwe tozo maalum. Ni hatari sana makampuni ya kigeni kuwa na masilahi makubwa ndani ya ramani ya nchi yetu". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kusisitiza kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2012, uhakikishe misamaha ya kodi ya mafuta kwa kampuni za utafutaji wa mafuta na gesi inaondolewa. Izingatiwe kuwa uzoefu kutokana na misamaha ambayo imekuwa ikitolewa kwa

Makampuni ya Madini unadhihirisha kwamba makampuni mengi yanatumia mwanya huo kuleta mafuta yasiyo na kodi na kuyaingiza kwenye soko la ndani la reja reja.

Mheshimiwa Spika, hivyo, misamaha hii haina maslahi kwa Taifa na ni mianya mingine ya uhujumu uchumi kwa kuwa kampuni za utafutaji mafuta na gesi zinayo fursa kwa mujibu wa mikataba (*PSA)* kurejeshewa gharama zao mara baada ya mafuta kupatikana. Aidha, uamuzi huu uhusishe pia Kampuni za Madini bila kujali mikataba *(MDA)* kwa kuwa imethibitika kampuni hizi zote hutengeneza faida nono bila kulipa kodi inavyostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti hali hii ya ukwepaji kodi na kuongeza mapato ya Serikali katika mwaka wa fedha 2012/2013, Kambi Rasmi ya Upinzani inarudia kuitaka Wizara ya Nishati na Madini ieleze hatua mahususi ambazo itazichukua kutekeleza mapendekezo yafuatayo:-

- Kutunga Sheria ya kuhakikisha kwamba mikopo kwenye makampuni ya uwekezaji wa madini katika mahesabu ya kodi isizidi 60% ya mtaji;

- Kutunga Sheria kuhakikisha kwamba riba ya mikopo kwenye makampuni yanayohusiana haitaondolewa kwenye mahesabu ya kodi;

- Kufanya marekebisho ya sheria kuhakikisha kwamba kodi ya mtaji *(capital gains)* inatozwa katika mauziano ya makampuni yote ya madini ambayo mali

zake au uwekezaji wake uko nchini, hata kama mauziano hayo yamefanyika nje ya nchi kwa kuzingatia kuwa mapendekezo yaliyoingizwa kwenye Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2012 hayakuzingatia kwa ukamilifu msingi wa mapendekezo yaliyotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani mwaka 2011.

Mheshimimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuhitimisha kwa kusisitiza kwa mara nyingine kwamba, kwa sehemu kubwa matatizo katika sekta za nishati na madini yamechangiwa na sababu za kibinadamu za kutowajibika ipasavyo kisera, kimaamuzi, kiusimamizi na kiutendaji kwa viongozi wa Kiserikali wenye dhamana na watendaji wengine na hivyo kusababisha ugumu wa maisha kwa wananchi na kuathiri uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya kimfumo yanahitajika ili kuwezesha hatua za haraka za kusimamia sera sahihi, uongozi makini na taasisi thabiti katika sekta nyeti za nishati na madini sanjari na kuchukua hatua kali dhidi ya ufisadi uliofanyika katika sekta hizi, kufanya mapitio ya mikataba na kuharakisha utekelezaji wa mipango kwa ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kuwashukuru wananchi wa Ubungo kwa ushirikiano wao katika kazi nifanyazo za kuwawakilisha kwenye vyombo vya maamuzi na kuhamasisha maendeleo Jimboni. Kwa namna ya pekee nitambue mchango wa Madiwani wote tunaoshirikiana katika kipindi ninachokuwa kwenye majukumu mengine ya ujenzi wa Taifa.

Nawashukuru viongozi wa dini, washauri wangu wa kiroho na wanafamilia yetu ya Dalali kwa upendo na kuniasa kuendeleza ujasiri na uadilifu katika kusimamia ukweli, haki na ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua kwa shukrani mchango wa viongozi wenzangu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Makao Makuu, Mkoa wa Kinondoni Kanda Maalum Dar e Salaam, Jimbo la Ubungo na wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika wajibu wa kuwatumikia Watanzania na kuhamasisha mabadiliko katika Taifa letu. Hali tete na tata ya sasa inatutaka tuwe na mshikamano zaidi mpaka kieleweke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru baadhi ya viongozi katika mamlaka mliotambua kwamba "siasa siyo uadui" na kunipa ushirikiano kwenye Serikali Kuu, Wizara ya Nishati na Madini, Manispaa ya Kinondoni, katika Kamati ya Nishati na Madini na Wabunge wengine kwa ujumla katika kutekeleza majukumu ya Kibunge kwa manufaa ya Taifa letu na watu wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba Bunge lako lijadili mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012 na makadirio ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kwa kuzingatia maoni tuliyoyatoa ya kuongeza bajeti ya Wizara husika; kupokea mapendekezo ya kuzingatiwa katika Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2012 na kupitisha maazimio mahususi ya kuhakikisha sekta za nishati na

madini zinachangia kikamilifu katika kuinua uchumi wa nchi na kuboresha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, kwa hesabu nilizozipiga, idadi ya wachangiaji tunaoweza kuwapata kwa Wizara hii kama hatutatumia muda vibaya kwa namna yoyote ile watakuwa 32 tu na nyie mmeomba hapa mia moja na kitu. Kwa hiyo, nitakuwa na ambao hawajachangia hata mara ambao wako watano, waliochangia mara moja wako 18, nitakwenda na waliochangia mara mbili ambao wako 10 tu, idadi itakuwa imekwisha. Kwa hiyo, naanza kumuita Mheshimiwa Mussa Zungu kwa sababu baadaye mchana atanisaidia, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Saidi Bungala, halafu Mheshimiwa Rachel Mashishanga atafuatia. Mheshimiwa Mussa Zungu!

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi na kuwaombea kheri Waislamu wote kwenye mfungo huu. Mimi mchango wangu najikita kabisa kwenye *revenue* na hasa kwenye mapato.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana kampuni ya *Pan African Energy* ilipatikana na hatia ya kufanya kosa ya kuidhulumu na kuiibia Serikali takribani bilioni 52 na tukakubaliana kampuni hii ilipe. Kwa mujibu wa taarifa nilizoziona kwenye taarifa za *Reuters* ya tarehe 6 Juni, 2012, kampuni hii imekataa, haitalipa na cha kushangaza, wanasema inawezekana vile vile

wakaharibu miundombinu na kuharibu usambazaji wa gesi sasa hivi katika maeneo ambayo wao wanahusika nayo. Cha kushangaza kabisa *TPDC* na jina la mtu ninalo, wanasema sasa hivi haina haja ya kuzungumzia suala hili.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua, biashara kubwa ya Serikali ni kodi. Ni kwa nini pesa kama hizi zinaachwa na kwa nini *TPDC* inajikuta na wao wanaingia katika kulemaa, kuendekezwa na Mwekezaji ambaye anasema amewekeza bilioni 256 kwenye *Pan African Energy*, nani amezi-*audit* hizi? Nani amezithibitisha pesa hizi za Mwekezaji zilizoletwa katika nchi hii mpaka leo anasema na yeye ana uwekezaji wake ambao anaudai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeshukuru sana nimemsikia Waziri na nampongeza kama ndiyo itakuwa hivyo. Kama bomba hili jipya la gesi itakuwa ni mali ya Serikali hii, *that is a good job done*. Kama mikataba mliyoingia, itabidi watu wengine walimiliki bomba hili tungekuta gesi zinauzwa hovyo hovyo na Serikali na watu wa nchi hii wasingeweza kunufaika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtu anatafuta gesi, mafuta, iweje baada ya kupatikana vitu hivi anaendelea kuingia ubia na Serikali? Kwa nini asitengewe hela zake akaondoka akarudi kwa mke wake na shughuli hizi zikabaki? (*Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati hii alivyosema gesi kwanza. Gesi hii ina nafasi ya kuchangia bajeti ya nchi yetu zaidi ya 200

bila kuacha Bandari, madini, dhahabu kuacha kila kitu, 200 *percent* ya bajeti tuna uwezo wa kupata sio chini ya 18 mpaka 20 trillion kwa mwaka kutokana na udhibiti wa gesi. Sasa hivi Japani wana shida kubwa sana ya nishati, wanaachana kabisa na masuala ya *nuclear*, nimetoka Japan, nimezungumza na Serikali ya Japani, nimezungumza na Balozi wa Ujapani, wanachukua *revenue* sasa ya gesi. Mawaziri wekeni watu kwenye Ubalozi Japani watakaokuwa na uwezo wa kujua *capacity* na *deposit* ya gesi ambayo tunayo nchini mwetu. Tukiacha ubinafsi, gesi hii itawasaidia Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imepata mkono, hivi mpaka leo, ni namna gani Serikali inaweza ikapenyeza uchumi kwa wananchi wake wa kawaida? Kwa nini hakuna mpango wa bomba hili kumilikiwa na Umma wa Watanzania, hivi Watanzania milioni 15 wanashindwa kuchangia laki moja moja wakapata 1.5 *trillion* kuweza kujenga hili bomba? Serikali inatakiwa iwe na *percent* ndogo, wawekezaji wawe na *percent* ndogo, umma wanatakiwa wawe na *percent* zaidi ya 52 ndiyo njia ya kuwasaidia Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatuna sababu ya kwenda kukopa pesa tu-*enlist TPDC* katika *stock exchange* watu wahamasishwe, waelezwe umuhimu wa kumiliki hisa na bomba hili litakuwa mali ya Tanzania. Lakini nataka niseme, ubinafsi bado upo, umimi; mimi ndiyo nipate, mimi ndiyo nifaidike na kuacha wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hili suala wajaribu kulitazama upya na hizi roho mbaya mbaya

zipungue sana. Mheshimiwa Waziri yeye ni mgeni, kwa hiyo, nafikiri sasa anaweza akanyooshanyoosha mambo akahakikisha kuwa wananchi nao wanamiliki bomba hili la gesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeibiwa sana kwenye madini, tusiibiwe kwenye gesi. Mozambique ni ya nne duniani kwa gesi. *Potential* ya gesi ya Mozambique walisha-*project* na imeshatoka katika vyombo vinavyohusika katika *revenue watch*, wanategemea kupata trillion 240 *for the next ten years*. Two hundred and fourty trillion, nchi ndogo ambayo ina watu ambao hawafiki hata milioni nane, sisi tume-*project* gesi yetu itatufikisha wapi. *Trillion* 240 kwa miaka kumi ni *trillion* 24 kwa mwaka, bajeti yetu sisi hapa ni trilioni 15 tu kwa kutegemea misaada na mauzo ya baadhi ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hilo walione. Mozambique walishabadilika sasa, katika *blocks* za gesi wanapandisha viwango vya *royalty value* kutoka 25% mpaka 40%, sisi tunangoja nini, tunaogopa nini? Gesi yetu, dhahabu yetu, kwa nini kuna *guidelines* za Benki ya Dunia kutuongoza kwenye mali yetu? Tutaendelea kuwa na umaskini tukizidi kujiendekeza au kunyenyekea wawekezaji wasiokuwa na nia njema na nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *capital gain tax* katika migodi. Juzi Uganda wana kampuni iliyoanzishwa pale ya Kiingereza inaitwa *Heritage Oil*, wameuza *share* zao, wamewauzia *Tulion Oil*. Serikali ililazimishwa kulipwa *capital gain tax*, walikataa, imelipwa. Hivi karibuni

wamepokea dola za Kimarekani milioni 435 kwenye *capital gain tax*. Leo migodi inabadilishana majina tu, *nothing is earned* katika nchi sababu ya ujanja, uzembe ambao tunazubaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Uganda kwa *capital gain tax* wamepata bilioni 696 ku-*transfer shares* za *Heritage Oil* kwenda *Tulion Oil*, sisi tunangoja nini? Pesa zipo tunazitazama, matatizo hapa ya Madaktari, Wanafunzi, Walimu, Wajawazito saa zingine wanajifungua katika sehemu mbaya kwa sababu tunaziacha pesa zinakwenda nje na tunaacha baadhi ya watu kumiliki fedha katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sihitaji hiyo nchi, *North Sea*, kuna nchi kule makampuni haya haya ya kigeni mwaka 2008 yamelipa *trillion* 32 za Kitanzania kwenye kodi ya mapato ya gesi. 2011 wanalipa *trillion* 27 kwa nini? Gesi inapungua, wanakimbilia wapi? Shamba la Bibi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bila Sheria au Sera madhubuti ya kuhakikisha dhahabu hii ya upepo wa hewa tuliopewa na Mungu, tutajikuta tunarudi kule kule kwenye matatizo ya madini maeneo ambayo sasa hivi watu wanaamini.

Mheshimiwa Spika, nirudi haraka haraka kwenye dhahabu. *Revenue watch* ni chombo cha Kimataifa, tumeandika mwaka 2006 *exports* za dhahabu Tanzania wameuza mauzo ya dola milioni 773, trilioni moja na milioni mia mbili. Mwaka 1998 mpaka 2005 kwa taarifa za *revenue watch*, mauzo ya dhahabu katika soko la

dunia kutoka Makampuni ya Madini nchini mwetu ni bilioni tatu sawasawa na trilioni 4.800. Kodi iliyolipwa kwa Serikali ni bilioni 144 only, one hundred and fourty four bilion out of 4.8 *trillion*. Pesa zinaondoka, hivi hawa wamewekeza miaka yote hawajarudisha faida yao? Nani alishughulikia kujua faida za hawa watu zimerudishwa au hazijarudishwa mpaka hii leo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hizi ndizo zilizokuwa recorded, ziko zile za kinyemela zinaondoka bila watu kujua, hizo hujui ni ngapi vile vile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, nataka kusema kwenye suala la gesi hakuna msamaha wa kodi wowote. Anayetaka msamaha kwa sababu huko anakotoka hakuna msahama wa kodi, kwa nini hapa? Msamaha wa kodi uje mtu anatengeneza dawa za UKIMWI, uje anatengenza vitabu, uje anatengeneza madawati ya shule na vifaa vya hospitali, sio kwenye gesi. Kama mtaweka misamaha ya kodi kwenye gesi, hatutaelewana humu ndani, sababu gesi ni *hot cake* sasa hivi, sioni msamaha wa kodi unatolewa nchi za Kiarabu kuuza mafuta yao. (*Makofi*)

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameumba Mbingu na Ardhi, na katika ardhi, akaweka gesi, wanyama na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia, naomba nimnukuu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alisema:

“Ili tuendelee tunahitaji vitu vinne; ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora.”

Mheshimiwa Spika, ardhi tunayo. Katika ardhi kuna madini, kuna wanyama, bahari na kila kitu.

Mheshimiwa Spika, watu, tunao wengi mno. Tanzania sasa hivi tuko milioni 45 na kuna mpango sasa hivi wa uzazi wa majira, ili tupungue watu tusizaane hovyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu siasa safi na uongozi bora; tatizo la nchi hii, siasa siyo safi. Kwa kuwa, siasa siyo safi, inakuja siasa chafu; na kuwa siasa ni chafu, uongozi unakuwa nao mchafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka tumeingia katika mfumo wa Vyama Vingi, Chama Kikuu cha Upinzani Tanzania, kilikuwa Chama cha Wananchi *CUF...*

**SPIKA:** Naomba uende kwenye hoja, eeh!

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, nitakwenda. Nakwenda Mheshimiwa.

**SPIKA:** Dakika zako ni chache sana, ukianza kutoa...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, usiwe na wasiwasi kwa hilo, usiwe na wasiwasi kwa hilo! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kama siasa yetu itakuwa ni chafu, hatuwezi kupata maendeleo. Tulivyokuwa Chama Kikuu cha Upinzani (*CUF),* Chama Cha Mapinduzi kilituambia sisi ni Chama cha Waislamu, ili kwamba, Waislamu, Wakristo na Wapagani, wasituunge mkono sisi; na kilivyokuwa Chama Kikuu cha Upinzani *CHADEMA,* kikaambiwa Chama cha Kikristo na cha Kichaga, ili Waislamu, Wakristo... *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, tunaomba sana uingie kwenye hoja, ni Kanuni. Ni Kanuni, maana hiyo siyo hoja iliyoko mbele yetu. *(Kicheko)*

Sikilizeni, Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge, tunafanya kazi kwa mujibu wa Kanuni. Wakati wa mijadala mahsusi, huendi nje ya mjadala unaohusika. Sio mahali pake, tunafuata Kanuni. *(Kicheko)*

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Naomba unitii.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hatuwezi kuchangia habari za madini, bila kuona kwamba, kuna matatizo katika nchi hii. Nchi ina matatizo kisiasa. Haya tunayoyachangia, mambo ya madini haya, baadaye kutakuwa na matatizo zaidi hapo mbele. Kwa hiyo, ni lazima tuweke msingi kwanza katika siasa kwamba, siasa iwe siyo ya ubaguzi, siasa isiwe ya fitina, siasa isiwe ya kupendelea upande

mmoja, kama Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano, inavyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kuwa, umeniambia nisiendelee, lakini ninachoomba, hizi siasa chafu, Mwalimu Julius kambarage Nyerere, amezipiga vita na zisiendelee kuwepo katika nchi hii. Zikiendelea kutakuwa na mgawanyiko hasa katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, mwaka 2011 nilitoa hoja Kijiji cha Songosongo, kuna wanyama, mbuzi na ng'ombe walikufa kwa ajili ya kemikali zilizomwagwa za gesi. Mheshimiwa Waziri, akasema siyo kweli. Nilimwomba Mheshimiwa Waziri, wakati ule alikuwa Mheshimiwa Ngeleja, aje Songosongo, akutane na watu waliofiwa na wanyama hao, akakubali, lakini hakufika, na *message* yake ninayo, kwamba, nitafika Kilwa kuongea nao. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, Profesa Muhongo, lakini usiwe muongo, nakuomba kwa heshima na taadhima ufike Songosongo ukaonane na wananchi hawa ambao wamefiwa mifugo yao kwa ajili ya kemikali hizo. Nakuomba tafadhali, katika majumuisho yako, uje kueleza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pili, sisi Kilwa tunavuna gesi. Tunashukuru *Pan Africa,* sasa hivi wanatupa 0.3% na tumeshapewa awamu mbili. Awamu ya Kwanza, tumepewa Shilingi milioni 85 na awamu ya pili, tumepewa Shilingi milioni 88. Lakini kuna deni letu la nyuma Shilingi milioni 606. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati aje hapa katika majumuisho

atufahamishe, lini hela hiyo itapatikana? Kwa sababu, tuliahidiwa mwezi wa Tano, mpaka leo hatujapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Kusini (Kilwa na Mtwara) tunatajwa sana kwa ajili ya gesi. Sisi tunashangaa sana. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kifungu 145, kinasema, Madaraka ya Umma. Sisi watu wa Mikoa ya Kusini, hususan katika Wilaya ambazo zinatoa gesi, hatujashirikishwa katika mpango huu wa gesi. Tunaiambia Serikali, Mkataba uliowekwa kati ya Kampuni ya kutoa gesi Mtwara, kuileta Dar es Salaam, kabla haujaanza kazi rasmi, lazima tuijue Sera ya Gesi na Sheria ya Gesi, sisi tunapata manufaa gani watu wa Kusini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila hivyo, hatutakubali gesi itoke Kusini kuja Dar es Salaam, bila kujua Sheria inasema nini na Sera inasema nini. Tupo tayari kuipeleka Serikali Mahakamani ili tujue haki zetu watu wa Mikoa ya Kusini. Bila hivyo, haitawezekana gesi kutoka Mtwara kwenda Dar es Salaam, bila kujua Sera inatunufaisha nini watu wa Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunasema leo hadharani, isitokee kama mambo ya Nigeria. Sisi ndio walinzi wa bomba hilo la gesi. Sisi ndio waathirika wa bomba hilo la gesi, siku yoyote likilipuka sisi ni wa kwanza kuathirika. Kwa hiyo, lazima tujue sisi tunanufaika vipi na gesi hiyo? Bila hivyo, hapakaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu umeme. Mikoa mingi imetajwa hapa, lakini Mikoa ya Lindi na Mtwara, hatuna Gridi ya Taifa. Tunaomba Serikali, Mikoa ya Lindi na Mtwara, kila Tarafa ya Mkoa wa Lindi na Mtwara, lazima ipate umeme wa gesi. Tuliambiwa kwamba, gesi ya Mtwara, utawekwa mtambo wa umeme Mtwara ili ueneze umeme Mkoa wa Mtwara. Namwomba Mheshimiwa Waziri; juzi, wiki iliyopita nilikwenda Liwale. Liwale, imechukuliwa jenereta kutoka Kibiti, Ikwiriri, inakwenda Liwale. Watu wa Liwale, wameagiza kwamba, hatutaki tena umeme wa jenereta, tunataka umeme wa gesi ufike Liwale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri, Mkoa wa Lindi na Mtwara, kila Tarafa na kila Kata, lazima umeme wa gesi ufike katika eneo hilo. Hayo ndiyo manufaa yetu ya kwanza, kwa umeme wa gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina mengi zaidi, na huwa sisemi sana. Lakini namwomba Mheshimiwa Waziri afike Kilwa - Songosongo, akaonane na watu ambao wameathirika na gesi ya Songosongo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Sina maneno mengi sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kumezuka tabia ya kutokuheshimu Kiti. Kanuni ya 60 (9) inasema hivi: “Kila Mbunge, atalisemea jambo ambalo liko katika Mjadala tu.”

Sasa maneno aliyokuwa anayasema Mheshimiwa Selemani, ingekuwa wakati ule wa Hotuba ya Waziri Mkuu, yale yangekuwa yanakubalika kwa sababu, ilikuwa ni hotuba ya kisiasa. Lakini inapokuja kwenye suala la *energy,* ni lazima useme mambo ya *energy.*

Wako wengine wanasema atoe mawazo yake. Jamani mimi ni Spika wa Bunge, nafuata taratibu zilizopo ndani ya Kitabu hiki cha Kanuni za Kudumu za Bunge. Kwa hiyo, napenda tuzishike, tuheshimiane.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Rachel Mashishanga, halafu tunaweza kumfikia na Mheshimiwa Murji.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Madini na Nishati.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi mpaka hii leo. Lakini sitakuwa mwingi wa fadhila, kama sitatoa shukrani kwa Baba yangu Mzee Stephen Mashishanga, ambaye leo hii anatimiza miaka 78, toka amezaliwa. Sitakuwa Mwingi wa fadhila vilevile, nisipoishukuru Timu yangu ya Yanga, kwa kushinda jana. *Message delivered. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina michango katika Sekta hizi mbili. Nikianza na madini, kumekuwa na migogoro mingi sana kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa. Wachimbaji wadogo, kimsingi na sekondari, ndiyo wanaovumbua madini katika maeneo husika. Leo hii

wachimbaji hao wakivumbua hayo madini, Serikali inaleta wachimbaji wakubwa. Matokeo yake sasa, wachimbaji hawa wadogo wanatolewa, wananyanyaswa na wananyimwa haki zao. Nilikuwa nataka Kauli ya Serikali: Je, hawa wachimbaji wadogo ni lini sasa Serikali itawaangalia kwa kuwapatia vifaa ambavyo vitaweza kutumika katika uchimbaji wao mdogo ili waweze kuendelea na shughuli zao za kila siku? Wengine wanategemea hayo madini kwa ajili ya shughuli zao za kila siku, kupeleka watoto shule, pamoja na chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la makampuni ya madini kusafirisha mchanga kupeleka kwenda kupima huko nje. Nataka nijue, ni kweli, makampuni haya yanasafirisha michanga kwenda nje kupima hayo madini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kwa akili yangu ndogo, hawa Wazungu, wana akili sana, inawezekana kabisa wanachukua huu mchanga, wanakwenda kuupanda huko kwao; mwisho wa siku wanamaliza madini yetu, kwao yanaota. Tunabaki na mashimo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana kwa hesabu ya kawaida hatujui, tunaona kawaida, tunawaruhusu kuchukua mchanga. Sasa nataka nijue, kama ni kweli wanachukua michanga wanapeleka huko, wanakwenda kupanda mbegu, au wanakwenda kupima, au wanakwenda kuchambua kama ni dhahabu, au almasi? Kama wanachambua, ni akina nani wanaohusika kujua ni kiwango gani cha madini

kinachokwenda kuchukuliwa kule? Akina nani wako kule kwa ajili ya kujua *interest* za Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Shinyanga, tunalala, tunaamka juu ya madini. Hatuna kiwanja cha ndege, kila siku njaa, hatuna kitu chochote ambacho tunaweza kusema Mkoa huu ni Mkoa ambao una madini.

Mheshimiwa Spika, mimi nimezaliwa Mwadui miaka kadhaa iliyopita. Nimesoma Mwadui. Sasa hivi Mwadui, hakufai, hata aliyeanzisha Mgodi wa Mwadui, William akizinduka leo hii akauona Mgodi wa Mwadui ulivyo, anaweza akazimia mara 20. Sasa hivi Mwadui hakufai. Niliingia mwaka 2010, nilitamani kutoa machozi. Tulikuwa tunakwenda shule, pamoja na kuwa kulikuwa kuna shule moja ya *private* ya *primary,* ilikuwa inaitwa *English Medium,* tumesoma sisi shule hizi wanaita za “Kanumba”, lakini kulikuwa kuna A, B, na C, tulikuwa tunakwenda na mabasi, tunapitiwa nyumbani kwa mabasi, tunarudishwa nyumbani kwa mabasi. Lakini sasa hivi hakuna hicho kitu. Uwanja wa ndege ulikuwepo, sasa hivi umebomolewa, watu wamechimba; nyumba zimebomolewa, watu wanachimba madini.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua, hiyo Kampuni sijui ya Petra, sijui ni ya nini, inafanya nini pale? Sisi tunafaidika nini? Wale wanaoishi pale wanafaidika nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha sana na linasikitisha kwa kweli. Ule mgodi jinsi ulivyoanza, yaani

mimi toka baba yangu anamwoa mama yangu, ule mgodi ulikuwa unazalisha almasi, ni huko Mkoa wa Shinyanga. Lakini Shinyanga, mpaka sasa hivi ni njaa, hakuna maendeleo, miundombinu hovyo, Hospitali hakuna, yaani kila kitu ni balaa. Halafu ni Mkoa ambao Serikali inapata kura, yaani ndiyo inapotegemea kura nyingi, lakini angalia ni ajabu, kwa nini wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, wameachwa? Hatuna maji, ila tunashukuru mradi umekuja wa Ziwa Vcktoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kuihoji Serikali, madini yanachangia pato la Serikali kwa asilimia 3.8. Nataka Serikali inijibu, kuna mkakati gani sasa wa kuongeza hilo pato la Serikali kupitia kwenye madini, ilhali wananchi wakibaki wanahangaika na kuwaacha wakiteseka? Nilikuwa nataka majibu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoke kwenye madini sasa, niingie kwenye nishati. Nasikitika kuona Wizara inaiachia *TANESCO* kuagiza miti, nguzo za umeme kutoka nje ya nchi, tuna kiwanda Mufindi kinachotengeneza nguzo za umeme, kwa nini Serikali inakubali kuingia hasara kwa kuagiza miti kutoka nje ya nchi? Hii miti ya kwetu, wapo wanaoiona inafaa na inasafirishwa nje ya nchi. Nataka majibu ya Serikali, ni kwa nini wanaachia *TANESCO* inaagiza hizo nguzo kutoka nje na kuziacha nguzo zetu zikitoka nje, na sisi tunaagiza kutoka nje? Wanadai kuwa bei ni kubwa, kutoka Mufindi mpaka Dar es Salaam jamani, au kutoka *South Africa,* kipi kina gharama? Nilikuwa nataka Serikali, inijibu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri, amesema amepunguza bei ya uunganishaji wa umeme. Mwaka 2011 Waziri Ngeleja, nafikiri wakati anasoma bajeti yake alisema wamepunguza siku za kufunga umeme kutoka siku 270 mpaka 109 kwa wateja walioko ndani ya mita 30. Sasa hivi tunaambiwa tumepunguziwa umeme, sijui kimetoka kiasi fulani, kimekwenda kiasi fulani. Lakini hajatuambia huo umeme tunafungiwa kwa muda wa siku ngapi? Wengine wiki moja, wengine siku mbili, wengine siku siku, unalipa siku hiyo hiyo unafungiwa. Sasa tunataka Serikali ituambie, inachukua muda gani kwa Mtanzania anayeomba kufungiwa umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi juzi tumeona kwenye vyombo vya habari, kuna Kampuni inaitwa *Segus Electric Contractor,* ilikuwa inakusanya pesa kwa wananchi Shinyanga Vijijini, ikidai inawafanyia *wiring* pamoja na kuchora ramani. Walikamatwa na wananchi na wakataka kupigwa. Nataka Serikali iniambie, mpaka leo hao wananchi wanafanywa nini? Hiyo Kampuni pamoja na hao wafanyakazi wake sita, wamekamatwa? Hizo hela za wananchi walizochukua, zinarudishwa au inakuwaje? Kwa sababu, *TANESCO* imekiri kuwa, hiyo Kampuni iliomba isambaze, ipate tenda ya ku-*supply,* kufanya *wiring* kwenye majumba, pamoja na kufanya *wiring* kwenye nyumba. Sasa nataka nijue, na *TANESCO* imesema haihusiani, yaani waliomba tenda lakini hawajakubaliwa, lakini bado wakaingia kwa wananchi na kuwadanganya, kuwachukulia pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nijue hatma za hawa wananchi waliochukuliwa hizo hela, watarudishiwa? Hiyo Kampuni na wafanyakazi wake, wamechukuliwa hatua gani mpaka sasa hivi? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Pole sana. Nakushukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Murji.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Spika, nami naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika bajeti hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, nami naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wake wa *RC* makini, maridadi, ambaye alituletea Mtwara. Kwa kweli kwa muda mfupi aliokaa kwa kweli ametupa matumaini makubwa. Mimi naomba kusema kwamba tunamwahidi tutampa ushirikiano wa hali na mali na aendelee na moyo huu aliokuwa nao.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine tena nami naomba nichukue nafasi kuishukuru Ofisi ya Mkuu wa Mkoa pamoja na Wizara ya Nishati na Madini. Wiki iliyopita, tuliandaliwa *RCC* ya dharura Mtwara na katika *RCC* ile kulikuwa na semina inayotueleza kuhusu bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. Miongoni mwa watu ambao walikuwa wanakataa bomba la gesi Mtwara kwenda Dar es Salaam ni pamoja na mimi, na niliapa kabisa kwamba bomba lile

tutafanya kila njia hata kwa dua au kwa jambo lolote lisitoke Mtwara kwenda Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya ile semina, kwa kweli tuliridhika na tumeelewa nini faida ya bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muda mfupi uliopita kuna Mbunge ambaye anatoka maeneo ambayo bomba la gesi limetoka. Lakini ukishaanza kutoa bomba la gesi, yaani limeshaanza kutoa gesi kutoka Songosongo hadi Dar es Salaam, amesimama na kusema hatakubali na atafanya kila njia kuhakikisha bomba lile halijengwi Mtwara, sasa aende kwenye lile bomba la kutoka Songosongo kwenda Dar es Salaam, siyo la Mtwara. *(Makofi)*

Nilitegemea kwamba yeye mwenzangu ameshaanza tayari, kwa hiyo angetuambia faida na kutokuwa na bomba lile la gesi, lakini leo akija Mtwara hatutamwelewa na sisi tunampokea na tutamshughulikia. Ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba tumeandaliwa semina, mimi naona bado. Naomba Wizara ya Nishati na Madini, hii semina bado iendelee kuwepo kwa wakazi wa Mtwara, imefanya semina kwenye *RCC,* sisi viongozi tumeambiwa tumejua, lakini kuna watu wa Mtwara wanahitaji, kuna wazee wa Mtwara wapo pale wanalalamika nao kwamba nini watapata? Watanufaikaje na bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam? Naiomba Wizara ije iandae semina kwa wazee, akina mama na vijana ili

wajue faida ya bomba la gesi kama tulivyojua sisi na sasa tumekubali bomba hili litoke Mtwara kuja Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, lakini ni kweli tumeambiwa kuna faida nyingi ambayo tunanufaika na bomba la gesi la kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam, ila bado naomba Mheshimiwa Waziri, tuna ahadi nyingi ambayo watu wa Mtwara waliahidiwa, kabla ya mradi huu, kulikuwa na mradi huo wa gesi ambao sisi tunaupata ambao mgao ulikuwa unaendeshwa, na *ATMAS* iliwaahidi wananchi wa Mtwara kuwapa umeme kwa gharama nafuu. Iliawaahidi kuwaingizia umeme kwa *freight rate* ya Sh. 70,000/=.

Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Waziri, sisi tulikwenda kwa wananchi tukawaahidi, tunaomba kura zenu na tutawapa umeme kwa bei nafuu, ambapo ahadi ile ilitolewa na *ATMAS,* lakini mpaka leo ahadi ile haijatekelezwa. Leo ukitaka kuingiza umeme ni Sh. 491,000/= Mtwara. Je, ahadi yetu ambayo kampuni ya *ATMAS* ambayo sasa imefilisika na sasa imeikabidhi kwa *TANESCO* ahadi ile ikoje? Tunaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind-up*, basi atuambie ahadi ya umeme ya *freight rate* ya Sh. 70,000/= imeishia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeahidiwa kutupa umeme kwa kilomita nne katika Mji wa Mtwara na maeneo ya kilometa nne, hakuna kitu Mheshimiwa Waziri! Mmetupa umeme kwa kuingiza kwa gharama nafuu, wa Sh. 90,000/= na kilomita nne, lakini maeneo mengi Mtwara hakuna umeme, lakini hamtufanyii hisani. Huu

ni wajibu wetu kutupa umeme kwa gharama nafuu. Yaani kutupa umeme wa gharama nafuu sasa Mtwara ni haki yetu kwa sababu ndiyo inakotoka gesi pale, leo tunaambiwa umeme uingizwe Sh. 491,000/=! Tunakuomba Mheshimiwa Waziri ahadi ambayo ilikuwepo ya *ATMAS* ile kwanza mtekeleze ili wananchi wa Mtwara mtupe hata miezi sita kwamba ndani ya miezi sita wananchi wa Mtwara ingizeni umeme kwa ahadi ile ambayo ilitolewa na *ATMAS* ya Sh. 70,000/=. Wananchi wengi wameshafanya *wiring*, wananchi wengi wameshajiandaa tayari kwa kuingiza umeme, lakini wanashindwa kutokana na gharama kubwa ya umeme.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alikuja Mtwara, na kuna Mjumbe mmoja wa Kamati ya Nishati na Madini aliuliza swali kwa mtaalam ambaye alikuwa pale kwenye mitambo kwamba nini gharama ya uzalishaji wa umeme wa gesi? Akajibu kwamba, gharama ya uzalishaji wa umeme kwa *unit* moja ni Sh. 127/=. Akamwuliza, nini gharama ya uzalishaji wa umeme kwa mafuta? Akaambiwa, ni Sh. 700/= mpaka Sh. 800/=.

Kwa hiyo, uzalishaji wa umeme kwa kupitia mafuta, ni ghali zaidi kuliko gharama ya gesi, lakini sisi watu wa Mtwara tunatumia umeme wa gharama nafuu wa Sh. 127/=, lakini tunaingizwa kwenye *tariff* ya mchanganyo wa pamoja ambao pamoja na wale wanaotumia umeme wa mafuta, wanachanganya. Sasa hamtutendei haki. Tunaomba na sisi mtupe nafasi yetu pia. Kwa sababu umeme unaopatikana Mtwara ni gharama nafuu, ni Sh. 127/= kwa *unit* moja na

*TANESCO* inauza umeme Sh. 198/=, kwa hiyo, bado mna faida kubwa sana *TANESCO* katika hili. Sasa tunaomba faida hii inayopatikana, basi angalau mtupe *incentive* kwa wananchi wa Mtwara kuingiziwa umeme kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengi kama Mbezi, Mangowela, Mbaye na kuna eneo la Kilimanjaro hakuna umeme na watu wa pale wameshajiandaa. Juzi juzi tumeshagawa viwanja karibu 2000 Mtwara na ujenzi unaanza na panahitajika umeme. Kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri mtusaidie ahadi ile ya kuingiza umeme kwa gharama nafuu, iwepo. Mmetupa kilomita nne, ni ndogo sana ambayo haitakidhi haja ya wananchi wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, lingine tena leo Mwenyezi Mungu ametujalia tumepata gesi na gesi hii inatoka Mtwara, inakuja Dar es Salaam, lakini bado mrahaba wa watu wa Mtwara haujulikani ni nini. Kutupa umeme kwa kilomita nne, mkatupa kilomita tano kwamba tutawapa umeme, bado sana. Lakini hebu tujue mrahaba wetu ni nini? Tunashukuru juzi pale katika kijiji cha Madimba, mmewaambia mtawapa uwanja wa mpira, wanakijiji wote watakuwepo, wataingiziwa umeme bure, sawa. Lakini wapo wangapi wale? Bado sisi watu wa Mtwara hatuoni kama tunanufaika, na gesi ile lazima ifike sehemu tuone kwamba na sisi gesi hii tunanufaika nayo. Tuna Shule nyingi za Sekondari, hakuna umeme Mtwara. Tunaomba Waziri atoe kauli yake atakapo-*wind-up* kwamba atatuingizia umeme bure katika shule zote za sekondari Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mrahaba ni mkubwa na unaposikia kelele ya wananchi na unaposikia kelele ya kila mtu kwamba leo wanataka kujua ni nini, sasa kwa usalama wa bomba la gesi litakalotoka Mtwara mpaka Dar es Salaam ili mtueleze mtakapokuwa mna-*wind-up*, ni kwa vipi tutanufaika na bomba la gesi?

Lingine, kuna hii kampuni ya kichina inakuja kujenga bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. Tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri ajira kwa vijana wa Mtwara. Kuna hizi kampuni za nje zilizokuja zote, nyingine zile zilizochimba gesi baharini, hakuna hata vijana asilimia 0.1 *percent* iliyopata ajira, vijana wa Mtwara, hakuna! Leo wakitaka kununua hata mkate, wakitaka hata maziwa, wakitaka kitu chochote, wanaagiza chata kutoka Dar es Salaam ndiyo inashusha mikate pale Mtwara. Siyo kwamba hatuna viwanda vya mikate, vipo; sio kwamba watu hawana ng'ombe wa maziwa, wapo lakini hata kama wanavyosema wao kwamba maziwa haya na ya kule hayafanani, siyo kweli. Kwa hiyo, tunakuomba sana, vijana wa Mtwara wako tayari, vijana wengi wa Mtwara wana ujuzi huu, wameshajisomesha pamoja na nafasi mlizotupa 50 ni chache, lakini bado kuna vijana Mtwara wana uwezo mkubwa. Vile vile na uwezo wa kufanya zile kazi ndogo ndogo wanazo... *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Bahati mbaya sana kengele imegonga

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukirudi baadaye mchana Waheshimiwa wafuatao ambao watachangia wajiandae. Mheshimiwa Shaffin Sumar, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Joseph Selasini na Mheshimiwa Blandes. Wengine watatajwa baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, sina tangazo lingine, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni.

*(Saa 07.13 mchana Bunge liliahirishwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa Azzan Zungu) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumeingia *session* ya jioni ambayo ndiyo ya kumalizia siku ya leo na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar atafuatiwa na Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Anne K. Malecela ajiandae.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Lakini awali ya yote, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa uhai, afya na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuweza

kuchangia. Naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini, lakini pia ni mfanyabiashara ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Manaibu na Katibu Mkuu kwa kufanya kazi nzuri ya kutuletea maslahi. Kazi wanayofanya ni ya ujasiri, kazi ambayo inatueleza kwamba tuna uwezo wa kuziba mianya ya ufisadi, na tumedhamiria kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Serikali kwa kuamua kuwekeza katika bomba la mafuta la kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. Hapo nyuma, vikwazo mbalimbali vilitokea, lakini hatimaye tumeweza kufaulu na ushindi huu uliopatikana ni ushindi wa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala la *TANESCO. TANESCO* imekithiri uozo na ufisadi. Kwa mwezi mmoja Shirika la *TANESCO* lina uwezo wa kukusanya Shilingi bilioni 60 mpaka 70 na gharama za uendeshaji ni kama Shilingi bilioni 11, lakini fedha zinazobaki haieleweki zinakokwenda. Hali hii ni hali ya hatari sana, tusipoichunguza *TANESCO* tutajikuta inaiingizia Serikali hasara kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo, bado *TANESCO* imeendelea kutuchakachua katika manunuzi ya mita za Luku. Lakini taarifa niliyonayo ni kwamba, mita moja ya Luku inauzwa kwa Dola za Kimarekani 42 lakini pamoja na *TANESCO* kulijua hilo, wamekuwa wakinunua Luku kwa Dola za Kimarekani

100, hawana hata chembe ya huruma kwa Watanzania. Naiomba sana Serikali ichunguze vizuri kabisa *TANESCO* na wale watakaopatikana na makosa wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguzo za nyaya tunazotumia sisi zinatoka nje ya nchi, na maisha ya nguzo hizo haizidi miaka 15, lakini wenzetu wa Thailand pamoja na kwamba wameweza kupeleka umeme kwa asilimia 85 katika nchi yao, wana utaratibu wa kutumia nguzo hizi ambazo zimetengenezwa kwa nondo, *Cement* na kokoto na zinadumu kwa kipindi cha miaka 50. Kwa nini sisi tusiige mfano kama huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 katika Bunge hili Tukufu tulipitisha bajeti na tulikubaliana kwamba bei ya mafuta ya taa iongezwe ili kupunguza uchakachuaji, jambo ambalo tumelifanikisha kwa kiasi kikubwa. Lakini pia tulikubaliana kwamba ongezeko litakalopatikana kwa kuongeza bei ya mafuta ya taa lipelekwe *REA* ili umeme uweze kusambazwa vijijini. Nataka majumuisho atakapotoa Waziri atueleze ni kwa nini *REA* haijapokea fedha hizo. Tunahitaji umeme vijijini, lakini pia tunahitaji kuokoa mazingira, tukipeleka umeme vijijini hata mazingira tutakuwa tunayaokoa kwa sababu leo Mkoa wa Dar es Salaam unatumia takriban magunia 40,000 ya mkaa kwa siku na magunia yote haya yanatoka mikoani. Athati ya kuharibu mazingira ni kubwa mno, tunaomba tuiongezee *REA* uwezo ili itupelekee umeme, watu wanufaike na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini licha ya kuongeza bei ya mafuta ya taa, kinachonishangaza ni kwamba *EWURA* bado wameendelea kutumia vinasaba ambavyo vimetugharimu sana. Hali ya uchakachuzi imepungua, lakini tunapoteza fedha nyingi sana kwa ajili ya kununua na kuweka vinasaba. Kwa nini fedha hizi zisielekezwe *REA* ili tuweze kupata umeme vijijini? Kama kweli mafuta bado yanahitaji kuwekewa vinasaba, basi tuangalie utaratibu kama tukiweza tuweke mafuta ambayo yanakwenda *transit* yawe na vinasaba kwa sababu mafuta yanayokuwa kwenye *transit* ni machache kuliko mafuta yanayotumika hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vijiji vingi sana nchini ambavyo havina umeme na vipo mbali na gridi ya Taifa. Naiomba *REA* iangalie uwezekano wa kupeleka umeme mbadala kwenye maeneo ambayo gridi ya Taifa iko mbali kuwafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishauri *REA* kwamba tuna vijiji vingi ambavyo umeme umepita kwa juu, ni umeme wa kupungia mkono tu. Tuwe na utaratibu wa vijijini vyote hivi vishushiwe umeme kwa sababu wana haki ya kupata umeme. Hata Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Aden Rage ana Kata 14 za vijiji ambavyo vyote umeme umepita juu kwa juu, hawana umeme. Tunaomba umeme ushuke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Jimbo langu, nina Kituo kimoja tu cha Afya Kata ya Upuge ambacho kipo umbali wa kilomita sita tu kutoka

kwenye *grid* inapopita. Naomba umeme katika Kituo changu cha Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kwa kupitia Wakala wa Jiolojia Tanzania iharakishe mchakato wa upimaji na uchoraji wa ramani kwa nchi nzima, maana hata mimi katika Jimbo langu eneo la Bukumbi kuna viashiria vya kutosha kabisa kwamba dhahabu inaweza ikawepo. Mchakato huu ukiharakishwa, vijana wetu wengi watapata fursa ya kuchimba dhahabu, watapata matumaini na maisha yao, wataweza kujiajiri na hili wimbi la vijana wasiokuwa na ajira tutaweza kulipunguza kwa kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushuru sana Mheshimiwa Shaffin na sasa mchangiaji wetu anayefuata ni Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilollo na Mheshimiwa Ole-Sendeka ajiandae.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie nafasi hii ya awali kwanza nikupongeze wewe mwenyewe kwa nafasi hiyo kwa muda mfupi umeonyesha uwezo wa hali ya juu sana na hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba niingie kwenye mada ambayo tunaijadili leo ambayo ni hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwanza kwa jinsi ambavyo anawatambua watu wake ambao wanaweza wakamsaidia. Ni ukweli usiofichika kwamba, kwa muda mfupi Mheshimiwa Prof. Mhongo ameonyesha uwezo wa hali ya juu sana. Mimi nampongeza sana na namwomba Mwenyezi Mungu amtie nguvu ili aendelee na kazi yake ya kuhakikisha Wizara hiyo inarudisha heshima ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niendelee kuwapongeza Waheshimiwa Manaibu Waziri, nikianza na Mheshimiwa George Simbachawene - Naibu Waziri anayeshughulikia suala Nishati. Kwa kweli nina hakika ni jembe ambalo lina uwezo mkubwa wa kumsaidia Mheshimiwa Waziri kufanya kazi ya kuhakikisha kwamba sasa Wizara hiyo inaleta tija kwa Watanzania kwa vyote ambavyo vipo kwenye Wizara hiyo kwa maana ya Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimpongeze Naibu Waziri Kijana wangu Stephen Masele kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri anayeshughulikia masuala ya Madini. Nina hakika wote wawili, vijana hawa watafanya kazi nzuri ya kumsaidia Waziri kama ambavyo tumeanza kuona kwa muda mfupi sana. Nataka tu mtambue kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na ni Makamu Mwenyekiti kwa muda mfupi ambao nimefanya nao kazi, nimetambua kazi zao na ushirikiano wao katika kuhakikisha kwamba Wizara hiyo inaleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitumie nafasi hii kumpongeza mtani wangu, Ndugu yangu Eliakim Maswi, kwa kweli ndugu yangu huyu ameonyesha uwezo wa juu sana, ameonyesha uungwana wa hali ya juu sana. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, mimi sikatai Waheshimiwa Wabunge kupata *information* kwa njia mbalimbali, kwani ni kazi ya Mbunge kutafuta *information* na kuzifanyia kazi. Lakini nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tunapopata taarifa, basi hebu taarifa hizo tuzifanyie kazi, tuzitafakari mara mbili au tatu ili tuweze kuona ni jambo gani la kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa niliposoma magazeti mpaka kwenye televisheni, wanasema eti Maswi kwamba amekiuka Sheria ya Manunuzi. Nikiwa kwenye Kamati, tumefanya kazi ya kumwita Maswi, tumemsikiliza kwa makini sana na tumemsikiliza Waziri kwa makini sana, lakini kwa uelewa wangu kama Diana, Ndugu Maswi sijaona alipokiuka. Ndiyo kwanza amefanya kazi kubwa ya kuokoa fedha za nchi hii. Serikali hii ilikuwa itumie Shilingi bilioni 18, lakini imetumia Shilingi bilioni 15, imeokoa Shilingi bilioni tatu. Ukinililetea Shilingi bilioni tatu Singida, hatujambo! Mambo yetu yatanyooka!

Hivi jamani ndugu zangu, hivi kweli ndiyo tuseme ule msemo wa kusema kwamba mti uzaao matunda ndiyo unaorushiwa mawe? Tunamrushia mawe mtendaji ambaye ameamua kuinusuru nchi, ameamua kurudisha heshima ya Serikali! Hivi kweli mtu unamwita Mtendaji Mkuu, lakini leo unampa mipaka kwamba hapa usifike na hapa usiende! Hivi kweli huyo

mtu unataka afanye kazi, ama unataka aende kwa ubabaishaji tu? Ifike mahali tupige kelele, tumwambie kaa pembeni.

Ndugu zangu naomba tuwe waungana. Mtendaji akifanya jambo ovu na akikosea mimi nitaunga mkono, tutapiga kelele kwa nguvu zetu zote na Serikali itatusikia na huyo mtendaji atawajibishwa, lakini kwa hili la Maswi, mimi namuunga mkono asilimia mia moja, kwani ameonyesha uwezo wa hali ya juu sana, ameonyesha busara za juu sana, ameonyesha uzalendo wa juu sana kwa kuhakikisha kwamba mali ya nchi hii inafanya kazi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuangalie namna ya kuwakosoa Watendaji wetu, la sivyo, tutawakatisha tama, watashindwa kufanya kazi na wataingia kigugumizi na watakuwa waoga. Naomba sana tumwache huyu mwenzetu aendelee kutusaidia katika eneo hilo alilokabidhiwa na Mheshimiwa Rais tutakapoona kuna tofauti, mimi sikatai tutasema kwa sababu duniani aliyekamilika hayupo, bali aliyekamilika ni Mwenyezi Mungu peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa kama tutataka hao watendaji wawe wa Mangimeza. Mtendaji ni lazima utembee na ni lazima aangalie Taasisi zake, ni lazima aangalie kuna kasoro gani ili aweze kuzisahihisha na ili aweze kumpa taarifa Waziri wake na ninaamini hakuna mtendaji ambaye anaweza akafanya jambo lolote bila kuwasiliana na

Waziri wake, ninamini katika hilo  alikuwa na baraka zote za Waziri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo naomba nihame kwenye mada hiyo, ninaamini na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamenielewa na tutashirikiana katika hili na tutaendelea kuikosoa Serikali, lakini pia tutaendelea kuipongeza Serikali na kuwapongeza Watendaji pindi watakapofanya jambo jema kama hili alilofanya ndugu yangu Maswi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyofanyika *TANESCO* mimi sina mjadala katika hilo, bali naiomba Serikali ichukue mkondo wake, endapo itajiridhisha kwa jambo lolote lile, sina sababu ya kutia neno na niiombe Serikali iende kwa umakini wa juu ihakikishe haimwonei mtu, ihakikishe inatenda haki katika kufuatilia uharibifu ama yoyote mabovu yaliyofanyika *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, naomba niongelee juu ya Umeme Vijijini ambao unasimamiwa na *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishaongea asubuhi wakati nafanya majumuisho mimi mwenyewe kwenye taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini katika Bunge la mwezi wa Nne, Serikali ilishamaliza tatizo la uchakachuaji wa mafuta na tukagundua kwamba baada ya tatizo hilo kwisha, Serikali itakuwa imeshaokoa Shilingi bilioni 600 kwa ajili ya mafuta ya taa kupandishwa kodi. Tukaiomba Serikali kwamba kwa kuwa Watendaji wetu robo tatu ya wananchi wetu wanaishi gizani, wanatumia taa, wanatumia

vibatari, lakini tunataka watumie umeme. Nikaiomba Serikali na Bunge likaunga mkono kwamba jamani, tunaomba nusu ya pesa hizi zipelekwe *REA,* lakini tunaona kwenye maandishi mmepeleka Shilingi bilioni 140. Tunaomba nusu ya pesa hizi, ninaamini Wabunge wote hawa wanahitaji umeme kwenye Majimbo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tulishauri na mimi mwenyewe nilishauri kwamba hivi vinasaba havina kazi tena suala la uchakachuaji limeshajifunga. Kwa hiyo, tunaomba ile Shilingi bilioni 10 iliyokuwa inakusanywa na *EWURA* sasa iende kwenye umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu na Mheshimiwa *Professor* utusikilize sisi ndugu zako, sisi ndiyo washauri wako, basi chukua hiyo Shilingi bilioni 10 peleka *REA*, chukua na nusu, Shilingi bilioni 600 peleke *REA*, hawa Wabunge watakupigia makofi na bajeti yako itapita juu kwa juu. Utakuwa umesaidia wananchi wetu kuondoka kwenye giza, akina mama wanapikia kuni na mkaa, wana macho mekundu mpaka wanaambiwa wachawi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chilolo, nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Christopoher Ole Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Nishati na Madini jioni ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kunifikisha saa hii ya sasa ambapo nina afya njema na akili timamu ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia hotuba ya Mheshimiwa Prof. Mhongo kwenye hotuba ambayo inatoa matumaini, kama hujampongeza kwa matumaini hayo utakuwa ni mwizi wa fadhila kwa sababu inatoa dira na matumaini kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu kwa mara ya kwanza nimeshuhudia Waziri wa Serikali yetu akieleza ahueni watakayopata Watanzania masikini katika kuunganisha umeme katika nyumba zao kwa asilimia karibuni 70. Hilo ni punguzo kubwa sana ambalo Serikali yetu imekuwa sikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Prof. Mheshimiwa Muhongo ya kuhakikisha kwamba Watanzania wananufaika na rasilimali za nchi yao, mimi naiona kama ni dhamira njema inayostahili kuungwa mkono. Nami nataka nimwambie Mheshimiwa Prof. Muhongo, nilikuandika barua asubuhi baada ya hotuba yako kukupongeza kutokana na hotuba yako niliyoiona na siyo kwa unafiki, ni kwa dhati

kabisa. Hofu yangu ni changamoto utakazokutana nazo kaka yangu. Una nia njema ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanapungukiwa na mzigo, nikianza na sekta hii ya umeme. Lakini nataka nikuhakikishie, ni vizuri ukawasaidia Watanzania wajue hali halisi iliyopo ili baada ya mwaka mmoja wasije wakakushangaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu Wizara unayoiongoza inanunua umeme kutoka kwenye mitambo ya watu binafsi kwa senti za Marekani kwa wastani wa senti 23 kwa *unit* moja na inauza umeme huo kwa senti za Kimarekani senti 12 na hivyo kuwa na hasara ya senti 11 kwa kila *unit* ya umeme itakayotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye nitaeleza msingi wa mzigo huu unaobebwa na Watanzania, maana senti hiyo 11 ambayo ni hasara inabebwa na Watanzania masikini kwa Serikali yao kutoa ruzuku kwa *TANESCO* ili iweze kumudu kulipa mitambo ya Aggreko, kulipa mitambo ya *Symbion*, kulipa mitambo mingine ya kukodi kama *IPTL*, Songas na huu unakuwa ni mzigo kwa Watanzania wote na bahati mbaya sana wakati ruzuku hii inatolewa kutoka kwenye makusanyo madogo ya Watanzania walio masikini, ni kwamba ruzuku hiii inatolewa hata kwa makampuni au kwa umeme utakaotumika na makampuni tajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ni hatari kwa nchi masikini kama sisi, tutaendelea kutoa ruzuku hata kwa umeme utakaotumika na Barrick, hata kwa umeme utakaotumika na Tanzania *Breweries*, hata kwa umeme

wote utakaotumika na matajiri, kwa sababu ni sawa sawa na maskini kumsaidia tajiri kwa sababu makampuni haya ni ya kigeni na Watanzania wanaendelea kuumia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema kaka yangu, Mheshimiwa Prof. Muhongo ana kazi kubwa, na msingi wake ni nini? Msingi wa mzigo huu wanaoubeba ni mikataba ya kifisadi, Mikataba iliyopo katika Sekta ya gesi ambayo inawafanya wageni wanaosimamia makampuni hayo ya kigeni waweze kunufaika kwa fedha nyingi wakati Watanzania wanaendelea kusinyaa au wanaendelea na umaskini uliotopea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye sekta ya gesi utakuta mtu yeyote ukiambiwa leo uwashe mtambo kati ya mtambo wa Songas na mtambo wa Wartsira ambao ni wa Serikali utalazimika kuwasha ule mtambo wa Songas kwa sababu umeme wake ni bei ndogo kutokana na wao kuuziwa gesi kwa bei ndogo na kwa maana ule wa Serikali, Serikali inauziwa gesi yake kwa bei kubwa. Nami nataka niwaambie, ni vizuri watu wote wakajifunza na kujua kwamba hata mikataba ya visima vyetu vya gesi kule Songosongo sasa hivi tunasema ni ya kwetu, lakini tayari imekabidhiwa kwa makampuni ya kigeni. Mikataba hii ya kifisadi 21 iliyopo kwenye sekta hiyo ya gesi mikataba ambayo inapswa tena kupitiwa na Serikali na mimi Waziri ninakutakia kila kheri katika mapambano hayo ili dhamira yako njema na dhamira ya chama chetu iweze kuonekana kwa vitendo kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba pamoja na rasilimali ya gesi, madini na sasa matumaini pengine ya kuwa na mafuta huko tunakokwenda kama rasilimali hizi za nchi yetu hazitasimamiwa vizuri itakuwa ni laana na inaweza kuwa ndiyo mwanzo wa machafuko katika nchi yetu. Lakini iwapo itasimamiwa kwa umakini na mikataba ikaingiwa kwa namna ambayo itasaidia nchi yetu itakuwa baraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nawaambieni, juzi tulipokuwa *Norway* wenzetu kwenye sera yao ya petroleum wamesema *the right to sub petroleum deposits is invested in the state*. *The petroleum deposits shall be administered for benefit their Norwegians society as whole.* Nataka niwaambie ndugu zangu, ningependa na sisi tutamke na wao wanasema *gas for the development and oil for development,* maana yake ni nini? Ni kwamba gesi iliyopo huko Norway, mafuta yaliyopo huko yanatumika kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa *Norway* kwa ujumla wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu yangu na ambapo Kamati ya Nishati na Madini ilikuwa nayo ni: Je, gesi kubwa tuliyoipata leo ambayo tunamshukuru Mwenyezi Mungu, mikataba yake itakuwa ni kwa manufaa ya Watanzania au itakuwa sawasawa na madini ya dhahabu ambayo sehemu kubwa inahamishiwa kwenda Ughaibuni na Watanzania wanaendelea kuachwa na mashimo na umaskini na kiwango kidogo cha makusanyo ambayo hayalingani hata wakati mwingine na misamaha tunayoitoa kwa makampuni haya ya kigeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamtakia sana kila kheri Mheshimiwa Prof. Muhongo katika jitihada za kuendelea kutaka safu ya uongozi katika Wizara yake, nami nataka kusema lililo wazi katika hili iwapo Kamati mliyoiunda ya kuchunguza *TANESCO* itakapobaini haya ambayo yamezungumzwa na Mheshimiwa John Mnyika kuhusu mtendaji wao Mkuu. Naiomba Wizara yako ichukue hatua kwa mafisadi wote wa *TANESCO*, lakini pia kwa mafisadi wote wa Wizara hii. Hakuna mashaka, kuna kiongozi wa umma ambaye amejiundia kampuni na kufanya biashara na Taasisi anayoingoza huko ni kukiuka Sheria ya Maadili ya Uongozi na anapaswa kuchukuliwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema pia hakuna mashaka kwamba kitendo cha ununuzi wa mafuta nje ya utaratibu wa manunuzi ya umma uliofanywa kwa kisingizio cha nia njema, nao unapaswa kuchunguzwa na nina imani sana Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Pinda, na Mheshimiwa Rais Mrisho Jakaya Kikwete hao nao watendewe haki ili kuhakikisha kwamba mafisadi wote bila kuangalia wanatoka wapi wanachukuliwa hatua zinazostahili. Hili msilionee huruma. Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu ninakuomba sana mjue kwamba mitambo ya kuzalisha umeme ya kukodi ndiyo kichaka kinachoneemesha mifuko ya mafisadi waliopo kwenye Wizara ya Nishati na Madini na walioko huko TANESCO. Naomba sana, ulitupie jicho lako huko ili kusaidia sana nchi yetu kuondokana na fedheha hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza tena Mheshimiwa Prof. Muhongo kupitia kwa Naibu Waziri Masele kwamba alikwenda pale Mererani kwangu na kuhakikisha kwamba anamaliza matatizo na migongano ya kumwagiliana maji kati ya Kampuni ya *Tanzanite one* na wachimbaji wangu wadogo wadogo wa Mererani. Lakini ombi langu, na hili naliomba sana na Bunge Tukufu lisikilize na Mheshimiwa Waziri Mkuu anisikilize sana na Waziri Muhongo, leseni ya *Tanzanite one* inakwisha kesho kutwa na tulipitisha sheria hapa ya kuhakikisha kwamba madini ya vito yanachimbwa na Watanzania kwa asilimia mia moja, na sasa hivi mchakato wa ku-*renew* leseni umeanza na kuna *lobbing* kubwa inafanyika. Nataka kuiomba Serikali iheshimu sheria iliyopitishwa hapa Bungeni na kwamba eneo hilo ligawanywe kwa wachimbaji wadogo ili kuhakikisha kwamba madini ya vito yanachimbwa na Watazania kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelipigia kelele jambo hili kwa miaka saba ya Ubunge wangu, Kamati ya Nishati na Madini imelipigia kelele sana, Kamati ya Bomani ililipigia kelele, ripoti ya Jaji Mark Bomani ilitoa mapendekezo mazuri, sasa leseni hiyo imekwisha, na muda wake umekwisha, ligawanywe eneo hilo, kwa wachimbaji wadogo kama ombi ambalo walilitoa mbele ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Mkifanya hivyo, imani ya wananchi kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi na chini hasa ya Wizara yako Mheshimiwa Waziri Prof. Muhongo itarejeshwa kutokana na kutanguliza mbele maslahi ya nchi na

usihofu maana sheria ipo upande wako katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu pia kwamba ni vizuri niitumie nafasi hii kwa ufupi sana, nimezungumzia kuhusu gesi, lakini pia nataka nigusie mikataba yetu katika suala zima la uchimbaji wa *urani. Urani* hii itatusaidia kama tutaingia mikataba yake kwa uzuri, na nchi yetu inaweza ikaneemeka. Lakini kama tutayaachia makampuni ya kigeni yakaja kuchukua urani hapa. Nataka niwambie inaweza kugeuka kuwa laana pia katika nchi yetu maana inaweza kuanzisha vurugu. Mlisikia rafiki yangu Mbunge mmoja akiongea pale akizungumzia habari ya gesi kwamba ingetakiwa iwanufaishe na watu wa Mtwara na mimi ninaungana naye. Hata ule mradi wa megawati 300 wa Mtwara, ule wa Mnazi Bay, mimi bado naomba sana kama Bodi ya *TANESCO* ilivyopendekeza waendelee kuendeleza mradi huo wa Mnazi Bay ili umeme unaoweza kuzalisha huko nao uweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufisadi wa Kiwira, nataka niseme kama kuna mahali ambapo Serikali yetu inatakiwa kuliangalia kwa jicho ambalo kwa kweli halitakuwa na huruma na fisadi yeyote. Ni mkataba uliokuwa umeingiwa katika uchukuaji wa eneo la Kiwira na katika uchukuaji wa Kabulo. Haiwezekani wala haiingii akilini mtu ambaye una dhamana ndani ya Ofisi ile ile, ukiwa ni Waziri unajiandikia wewe na familia yako unajiandikia mgodi wenye hazina kubwa kiasi hicho, halafu unaachwa uendelee kwenda kutamba Mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu kwamba Waziri aliyetumia nafasi hiyo siku ya mwisho ya ofisi yake Serikali hii huko huko aliko achukuliwe hatua za kisheria na eneo hilo liweze kuchukuliwa kwa maslahi ya mapana ya nchi yetu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ya pili iulilia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru Mheshimiwa Ole – Sendeka ni kengele ya pili hiyo.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi ya kuongea kwa dakika 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nimuunge mkono ndugu yangu Mheshimiwa Diana Chilolo kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wake mzuri, ametupatia Waziri wa Madini, ametupatia Katibu Mkuu mzalendo, ametupatia Manaibu Mawaziri wazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 25 saa 3.00 mpaka saa 6.00 usiku, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tulikuwa na *Party Caucus,* tulizungumza mengi sana ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kumpongeza na Katibu Mkuu kwa maamuzi mazuri sana waliyoyachukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake kuanzia ukurasa 13, 14, 15 na 16. Naomba nimpongeze kwa kuweza kukopi yale tuliyoongea ndani ya *Party Cancus* akayaingiza ndani ya kitabu hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote yaliyoandikwa kwenye kitabu hiki ni yale tuliyoyazungumza ndani ya *Party Caucus* yetu. Kwa hiyo, katika hilo nampongeza sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa kuchukua yote tuliyoongea, maamuzi yote tuliyopitisha kwamba katika hili sasa tunazungumza kwamba maslahi ya Taifa kwanza, na siyo kundi dogo, na kwa hiyo wote kwa pamoja tunaupinga ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote kwa pamoja tunazungumzia kitu kimoja. Maamuzi ya Katibu Mkuu na Waziri yaliyokuwa maamuzi ya hekima, maamuzi yaliyojaa uzalendo. Hakuna Wizara mbaya kama Wizara ya Nishati na Madini. Wizara ya Nishati na Madini ikikutana na Katibu Mkuu ambaye ni fisadi, Waziri ambaye ni fisadi, Manaibu Mawaziri ambao ni mafisadi, ndipo tunapoingia kwenye matatizo. Lakini siku ile kwenye *Party caucus* saa 3.00 mpaka saa 6.00 za usiku tulikuwa tunawapongeza hao. Nasikia na nyie mkayapatapata mkayaingiza hapa, hongereni sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge kaa chini. Waheshimiwa Wabunge nimemwomba mtoa taarifa akae chini na aniheshimu. Sasa nashangaa kelele

wengine za nini tena? Endelea Mheshimiwa Anne. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nije kwenye madini ya vito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo nimelizungumza kipindi cha tatu sasa cha Ubunge wangu. Nikizungumza kwamba madini ya vito hayahitaji kwamba lazima yapate mitambo mizito sana, kwa hiyo, sisi wazalendo tuna uwezo wa kuyachimba yale madini. Muda wote nimekuwa nikizungumza *Tanzanite one* nikiwa namuunga mkono Mheshimiwa Mbunge wa Simanjiro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa dunia ya sasa hivi uko kwenye hali mbaya. Kila Taifa linakumbatia rasilimali yake na sisi Watanzania tukumbatie *Tanzanite one* yetu wenyewe. Kama alivyozungumza Mheshimiwa Ole- Sendeka Mkataba wa *Tanzanite one* umekwisha. Nahisi Serikali katika hili kama mnataka ugomvi mtetereke sasa. Sifa zote tulizotoa hapa tutakuwa wakali. Mtetereke katika hili la *Tanzanite one*, wafunge virago waondoke, watuachie na sisi wachimbaji wadogo, wachimba ile *Tanzanite* ili jina letu la *Tanzanite* liwe ni la Tanzania peke yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutakataa ile sheria inayosema anaweza akamkaribisha na mgeni, lakini siyo kwamba *Tanzanite one* aendelee kushikilia lile neno lote hapana. Kuhusu lile eneo, hapana. Katika hilo Mheshimiwa Waziri naomba niseme umenielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye hili la gesi. Gesi inatoka Kilwa, inatoka Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi ulipokuwa umekaa huku, ulipochangia nlikuunga mkono sana katika hili la gesi. Serikali tunaomba Watanzania hebu tuliangalieni vizuri, tudhibiti hii gesi sisi wenyewe, mbona tuna uwezo, tuidhibiti sisi wenyewe. Hata kama mtaona awepo mtu, awepo kidogo sana, lakini mbona tuna uwezo na pia tuangalieni hili. Mtwara na Lindi tusiwaache hivi hivi, nao waifaidi ile gesi kwamba gesi isije ikawa inatoka Mtwara na Lindi wao wakiona ikipita tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la msingi, hii gesi itusaidie kupunguza bei ya umeme. Hii gesi iwe ndiyo chanzo cha kupunguza bei ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyektii, lakini kabla sijaunga mkono hoja, nirudi kwa uzito, nimpongeze Katibu wa Wizara ya Nishati na Madini kwa mara nyingine. Msiogope hata siku Serikali kufanya jambo ambalo mtaambiwa, ooh, mmekiuka kanuni. Kama mtaambiwa mmekiuka kanuni kwa maslahi ya Watanzania, sisi tutakuwa tunawapa nguvu, mtakuwa mko salama kuliko mkikiuka kanuni kwa mslahi ya mafisadi. Tutawatoa, lakini kama mtafanya jambo mkiona hapa hapana, kuna kasoro mkienda kule ambako mnasaidia nchi yetu, mnawasaidia Watanzania, mnapunguza umasikini, Serikali tutawapigia vigelegele kama tulivyowapigia vigegele leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Anne Malecela. Sasa namwita Mheshimiwa David Kafulila.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nishukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hoja hii muhimu ambayo kimsingi inahusu mustakabali wa Taifa letu katika malengo ya aina zote, yawe malengo ya Milenia, yawe ya MKUKUTA na yale ambayo yanahusu malengo ya Dira ya Taifa ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara muhimu sana kuweza kufanya mapinduzi yawe ya viwanda, yawe ya kilimo na yawe ya huduma huwezi kufanya mapinduzi ya viwanda kama ambavyo mahitaji ya malengo ya Dira ya Taifa ya mwaka 2025 kwamba tujenge tabaka lenye uchumi wa kati kama huna nishati ya umeme wa kutosha, na ndiyo msingi wangu wa kupata kuuliza swali la tumefika wapi katika uzalishaji wa umeme ukilinganisha na malengo ya Dira ya Taifa ya mwaka 2025?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana kwamba katika kutekeleza ajenda hii ya kuhakikisha Taifa letu linakuwa na umeme wa kutosha. Tumekwama kwa muda mrefu, ambapo kimsingi inatosha kabisa Watanzania kuchoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka 1994 Tanzania tuliingia kwenye mgogoro wa umeme, tukaingia mikataba mibovu, mfano wa ule wa *IPTL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukiingia kwenye mikataba mibovu kutokana na mgogoro wa umeme mwaka 1994 ndiyo mwaka huo huo ambao nchi ya Malaysia ilikuwa na mgogoro wa umeme. Leo wenzetu wana ziada ya umeme wa zaidi ya megawati 10,000, sisi bado tunacheza na megawati 1,000, megawati 800, hii ni aibu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sababu nyingine yoyote ile hata ukimwuliza mwanafunzi wa Darasa la Kwanza ambaye ametoka kujifunza kuandika, hakuna sababu yoyote ya Taifa hili kuhangaika na ajenda ya umeme kwa miaka 50 ya uhuru tofauti na ufisadi. Nchi imebakwa, nchi imetekwa na ufisadi ndiyo sababu Serikali katika miradi ya umeme kwa miaka mingi ime-*paralise*. Haiwezekani! Hii ni nchi ya pili katika Afrika kuwa na vyanzo vingi vya umeme, baada ya Kongo ni sisi. Sababu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia taarifa za *TANESCO* kuangalia ni kiasi gani cha umeme unaozalishwa na Makampuni haya ambayo tunayakodi na kiasi cha umeme ambao unazalishwa na *TANESCO* yenyewe. Kwenye Makampuni ya kukodi kuna kitu kinaitwa *capacity charge.* Nimefanya mahesabu na taarifa ninayo hapa, kutoka mwaka 2002 mpaka mwaka 2011 *capacity charge* peke yake imekwenda zaidi ya shilingi trilioni moja. Juzi nilikuwa

nazungumza kwenye bajeti ya kilimo shilingi bilioni 14, Waziri anasema mkanda umefika tundu la mwisho, lakini kuna wanyama ambao wananyonya kila mwezi kupitia mikataba mibovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu hiyo siku zote...

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kaa. Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1), hii ni kwa faida ya Bunge hili. Hotuba anayoitoa Mheshimiwa Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, amesema nchi hii imebakwa. Sasa nilikuwa naangalia Kamusi hapa neno kubakwa ni matusi na Kanuni hii inakataza kutumia lugha ya kuudhi na pia inakataza kutumia lugha ya matusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge anayo maneno mengi sana anayoweza kufikisha ujumbe huo, atoe hilo neno la “kubakwa” ambalo tumelitungia sheria katika Bunge hili, mbakaji yeyote anafungwa kifungo cha maisha au zaidi ya miaka 30. Kwa hiyo, naomba tu atoe neno hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, lengo kuu la sisi kukaa humu ndani ni kuwatetea wananchi, sidhani kama tutawatetea wananchi kwa lugha ambazo sio nzuri au sio za kistaarabu. Tukija humu ndani hatuna vyama bali tuna msimamo mmoja wa kusaidia wanyonge wetu ambao wako nchini mwetu.

Mheshimiwa Kafulila hilo neno ulilotumia sio zuri. Nakuomba ulitoe na uendelee ili upate umeme Kigoma.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Chief Whip* amesema kwamba neno kubaka ni tusi ambapo adhabu yake ni miaka 30 jela lakini mimi nawaambia Uchina ufisadi adhabu yake ni kunyongwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafulila, haiku-*cost* jambo lolote kutoa neno hilo, wewe toa tu hilo neno kubaka, unalifuta, unaendelea na Waziri ana mapesa hapa, Kigoma umeme uwake kesho. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokizungumza hapa labda pengine tumwombe Prof. Kahigi mtaalamu wa Kiswahili atusaidie hapa. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ndiyoo!

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Taifa limetekwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafulila hebu kaa. Meza inapokuheshimu na wewe jaribu kuheshimu Meza, Mheshimiwa Kafulila endelea.

**MBUNGE FULANI:** Atoe!

**MBUNGE FULANI:** Atoe nini?

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma taarifa hii kutoka *TANESCO,* Makampuni ukichukua *Aggreko*, *Songas...*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Kafulila hebu kaa. Usitake Meza iwe na ugomvi na wewe. Nimekuomba hilo neno la kubaka si neno la kiungwana na wewe ukiwa mfano wa vijana utakapoanza kuzoea neno kama hilo litakuharibia maisha yako vilevile. Kwa hiyo, naomba litoe hilo neno halafu endelea na mchango wako.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuheshimu sana Mwenyekiti wangu. Kule nyumbani kijijini huwa tunabaka panzi. Sasa ukichukua kubaka kama ni tusi sijui tafsiri yako ni nini? Ndiyo maana nikasema pengine mtaalamu wa Kiswahili asaidie. Nimezungumza tafsiri ya kubaka sio tafsiri ya tusi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafulila unajua unatupotezea muda humu ndani. Wakati watu wanakuheshimu, jaribu na wewe kuwaheshimu. Nakuomba ulitoe neno hilo kwa sababu ukiendelea kubishana na Meza ujumbe wako hautawafikia watu huko na wewe una lengo la kuwafikia wananchi wako.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nakubali hayo uliyoyataka yawe hivyo ili niweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa mifano kuna Kampuni ya *Aggreko, Songas, IPTL* ukijumlisha kwa miaka 10 tu *capacity charges* ambazo tumezitoa ni takriban shilingi trilioni moja. Kwa hiyo, namwomba Waziri, Mheshimiwa Profesa, miongoni mwa mambo ambayo tungependa kuondokana nayo ni hii biashara ya umeme kwenye Makampuni ya kukodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwenye hotuba yake ametuonyesha ni kwa namna gani tuna nafasi ya kupata umeme kupitia gesi lakini biashara ya kupata mitambo hii wakati mwingine inachukua mwaka mmoja au miwili. Napenda kuishauri Wizara ianze mapema mchakato wa kupata mitambo ili kusudi tusije kufika mwisho wa siku tunapata gesi halafu tunaendelea na Makampuni hayahaya ya kukodi ambayo yana *formula* mbovu ya *capacity charge,* hilo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ya umeme Mkoa wa Kigoma. Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba mradi wa Igamba III ambao utazalisha takriban megawati 43 umekwishafanyiwa upembuzi wa kutosha na kwamba tupo tayari kwa ajili ya uzalishaji wa umeme ule. Napenda kushauri kwa msisitizo kwamba Mkoa wa Kigoma ni Mkoa ambao ni *very strategic* kama kweli tunataka kuongeza uchumi wa Taifa hili. Tukipata umeme Kigoma, tunao uwezo

wa kufanya mapinduzi ya kilimo, tukipata umeme Kigoma, tunao uwezo wa kufanya mapinduzi ya viwanda kutokana na mazao ya Ziwa Tanganyika na mazao ya Mto Malagarasi. Pale Kigoma kuna *reserve*, kuna *limestone* ambayo inatosha kuzalisha saruji. Walikuja wawekezaji pale kutoka Marekani, wanao uwezo wa kuzalisha kiasi cha kutosha cha saruji kwa soko la Tanzania, Zambia, Congo na Burundi lakini wanahitaji megawati 24 ili waweze kuzalisha kiasi hicho cha saruji, umeme ukawa mgogoro. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri, naomba Kigoma uitazame kwa umaarufu kwamba ni Mkoa ambao uko *very strategic,* ni Mkoa wa mkakati kuweza kuchochea mapinduzi ya uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii zaidi ya umeme inahusika na eneo moja ambalo ni muhimu sana, eneo la madini na gesi. Kuna makosa mengi yamefanyika kwenye eneo la madini na ni aibu kwamba Makampuni haya ya madini tangu yaingie nchi hii bado Watanzania hatufaidiki kwa kiasi cha kutosha. Mtaalamu mmoja anaitwa Sigris, alisema kwamba kuna nguzo tatu kwenye *role of state* katika ku-*govern* masuala haya ya gesi, mafuta na madini. Tunahitaji vitu vitatu, lazima mikataba yao na taratibu zao ziwe *transparency,* ziwe za uwazi, mikataba yao na taratibu zao ziwe *fair.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa tunazungumzia gesi, mpaka sasa hakuna anayejua ni gharama kiasi gani haya makampuni ambayo tumeyakubalia yaanze kufanya utafiti wa gesi yanatumia lakini mwisho wa siku gharama hizi

wanatumia wenyewe kutafuta hiyo gesi, wanagusa kiasi cha gharama ambazo wanazitumia, mwisho wa siku wakianza uzalishaji wataingiza gharama kubwa na itachukua muda mrefu sasa kuanza kupata *cooperate tax*. Kwa hiyo, napenda nishauri, ni lazima Serikali iwe na mkono wake kwenye tafiti hizi. Kuna makampuni leo yanatafuta gesi wanasema wanatumia dola milioni moja kwa siku. Wakienda miaka miwili tafsiri yake ni kwamba watatumia zaidi ya dola 600 na hizi dola milioni 600 watakuja kuziingiza kwenye kukokotoa gharama zao za *expenditure* ili kupunguza kodi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, najua wewe ni msomi, naomba tafadhali, makosa tuliyoyaingia kwenye madini, kuna kila dalili kwamba tunakwenda kuyaingia kwenye gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hoja ya madini, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kutokana na mifumo ya rushwa, mwaka 2004 Juni, ndani ya Bunge hili Tukufu iliwahi kuwasilishwa taarifa ya Kamati ya *PAC* ambayo ilichunguza ufisadi kwenye Mgodi wa Mwadui. Ukitaka kujua nguvu za mafisadi, ile taarifa mpaka leo nilikuwa nafanya utafiti kwenye mtandao haijawahi kujadiliwa kwenye Bunge lako Tukufu. Taarifa ninayo hapa, nimefanya utafiti nimeipata, hii hapa. Ukisoma taarifa hii, ndani yake Mwadui hawafai, wanasema hawapati faida pale Mwadui hawa Dibias ambao walikuwa wamiliki wa Mwadui walikuwepo Lesotho, walipoona biashara hailipi Lesotho wakaacha, lakini Tanzania miaka nenda miaka rudi wanasema hawapati faida mbona hawaendi kwao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi sio lazima tuchimbe madini ndio tuendelee, sio lazima, madini tutapata fedha kidogo sana, ni akili tu. Ndiyo maana Mwalimu Nyerere alisema kwamba kama hatujapata akili ya kuchimba madini tuyaache, watakapokuja wenye akili wayachimbe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusikaririshane kwamba bila madini hatuwezi kuendelea, hakuna kitu! Unasema kwamba kodi ya madini inaongezeka mwaka hadi mwaka, lakini taarifa hapa haionyeshi ni kiasi gani cha kodi tunawasamehe hawa watu, ni kiasi gani cha *exemption* ambacho tunawapa? Ukifanya utafiti, utagundua kwamba faida ambayo tunaipata kwenye eneo la madini, ni kidogo sawasawa na afadhali kuacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tuanze makubaliano ya kupitia au kukubaliana na taarifa za Kamati mbalimbali ambazo zimewahi kuchunguza kuona ni kwa namna gani tufanye biashara na nani. Kwa mfano huu mgodi wa Williamson Diamond, mimi nimesoma, hakuna kitu pale Serikali inapata na ukiangalia mchakato mzima wa uchimbaji hakuna mzawa pale... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Sasa umeona mchango wako kama huo wa kuelimisha ungeusemea wapi?

**MBUNGE FULANI:** Aaaah! *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mara nyingine msibishane na Meza, inakupa nafasi useme vitu *constructive, objective* kusaidia Serikali na umma. Sasa unapoleta mambo mengine ya ajabuajabu, haya tunaendelea na Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na niseme ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunijalia afya njema. Nitajaribu kujieleza lakini katika hali ya udhaifu, mtaniwia radhi kama sitaweza kujieleza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge la Saba, Bunge hili lilimshauri Mheshimiwa Rais kufanya mabadiliko ya uongozi katika Wizara hii na Mheshimiwa Rais alikubali ushauri wa Bunge, akafanya mabadiliko na sasa tuna uongozi wa Wizara chini ya Mheshimiwa Profesa Muhongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marehemu Shabaan Robert aliwahi kusema kwenye kitabu chake cha Kusadikika kwamba:-

*"Msemakweli ni mpenzi wa Mungu, sitaiacha kweli, nikichelea upweke wa kitambo, nikajinyima ushirika wa milele unaotazamiwa baada ya kushindwa kwa uongo".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wa wiki nzima hapa Dodoma Profesa Muhongo pamoja na Katibu

Mkuu wa Wizara hii walikuwa wanadhalilishwa kama watu waliovunja sheria, watu ambao hawana uwezo. Mkakati ambao ulikuwa unaandaliwa, eti kumshauri Rais awaondoe katika Wizara! Nitasema ukweli, mkakati huu ulikuwa unaandaliwa na pande zote, upande wa Chama cha Mapinduzi na vilevile wakauleta mpaka upande huu mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa haina chama, rushwa haina dini, rushwa haina kabila. Makampuni ya Mafuta yalikuwa hapa Dodoma yakigawa fedha na lazima niseme, kuna wenzetu wanasema kwa sauti kubwa, kuna wenzetu wanasema kwa mbwembwe lakini sasa naamini wanasema kwa nguvu ya chochote ambacho kiko mfukoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, jioni hii Profesa Muhongo utapongezwa sana kwa sababu inawezekana *caucus* ya Chama cha Mapinduzi imepunguza makali, lakini inawezekana yanayosemwa hayatoki moyoni bado watu wana uchungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia zinazofanywa na baadhi ya Wabunge zinalidhalilisha Bunge na zinalidhalilisha Taifa letu. Tulishuhudia katika Bunge la Saba, tunashuhudia katika Bunge hili, hatutaki, mnadhalilisha Taifa, mnadhalilisha Bunge, kama Wabunge acheni. Watanzania wanafikiri mnawapenda, mnawatetea, kumbe mnawatetea kwa nguvu ya kitu cha mfukoni, tumegundua! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa Profesa Muhongo na Wizara kununua mafuta, umeokoa shilingi bilioni sita (6) kwa mwezi za Taifa hili. Shilingi bilioni sita (6) sio shilingi 6,000/=. Rombo shule hazina madawati, Rombo shule hazina madarasa na maabara, Rombo hatuna umeme, shilingi bilioni sita zilizookolewa, zinaweza zikasaidia Serikali ikatusaidia!

**MBUNGE FULANI:** Huyo kasema ukweli.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo watu wanakuja na hoja ya sheria. Sheria hizi tumetunga wenyewe, hata Bwana Yesu alipoponya siku ya Sabato, Wayahudi walimwuliza kwa nini unaponya siku ya Sabato? Akasema, mimi ndio bwana wa Sabato. Lakini sisemi kwamba alivunja sheria kwa sababu mimi nimechunguza baadaye walikwenda *PPRA* kuomba utaratibu na wakapewa, wakafanya maamuzi. Ndio sababu hii, mimi nataka nimpongeze kwa dhati Professa Muhongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumtia moyo, inawezekana Mheshimiwa Muhongo wewe ulikuwa *academician* huko, wanasiasa huwajui. Jipe moyo, utatuzoea, fanya kazi yako. Nampongeza Katibu Mkuu wako Bwana Maswi. Bwana Maswi ametishwa, sisi tunajua. Bwana Maswi ametumiwa hata meseji za kumtisha, sisi tunajua. Bwana Maswi anafuatwa na baadhi ya Wabunge kwenda kumuomba rushwa, sisi tunajua. Wako baadhi…

**WAJUMBE FULANI:** Wataje hao!

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Wako baadhi ya Wabunge wanafanya biashara na *TANESCO*, wako humu! Leo wanataka kuliyumbisha Bunge, wanataka kuiyumbisha nchi kwa sababu ya maslahi yao, hatutaki! Mimi nawaambia, washindwe na wamekwishashindwa kwa jina la Yesu. (*Vifijo/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawezaje kuisifu *TANESCO* au kuitetea *TANESCO* tunayoambiwa kwamba kwa muda mfupi wa Profesa Muhongo pamoja na Bwana Maswi wamegundua kwamba ilikuwa inakusanya shilingi bilioni 60 kwa mwezi, mishahara shilingi bilioni 11, shilingi bilioni 49 hazijulikani zilipo? Utateteaje jambo hili? Tena tunazo habari kwamba walikuwa wanatuzimia umeme wakidai kwamba maji ni pungufu kumbe ni geresha yao ili wanunue mafuta.

**MBUNGE FULANI**: Waambie!

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina napendekezo, Sheria ya Wahujumu Uchumi ibadilishwe kwa sababu adhabu zao ni ndogo sana. Napendekeza turekebishe Sheria, mafisadi wote wahukumiwe katika Sheria ya Uhaini. Maana tumezoea kunyoshea kidole Serikali na Mawaziri, hata mafisadi ni Wabunge vilevile.

**MBUNGE FULANI:** Semasema baba! *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo limeeleweka, ujumbe umefika, *message sent and*

*delivered*. Watu tunapiga makofi, tunataka kupasua mbao kushangilia watu, kumbe wenzetu wameshiba, sisi hapa tunapiga makofi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie Jimbo langu la Rombo. Jimbo la Rombo tulipata umeme mwaka 1984 lakini Rombo ni kama hatuna umeme, umeme unapatikana kwa bahati, kwa wiki siku moja ama siku mbili. Unakatwakatwa hovyo hatujui ni kwa sababu gani. Nimekwishapiga kelele, nikaambiwa kwamba *transmission line* inayokwenda Rombo ni ndefu sana, inatoka *TPC* inakwenda Boma Ng'ombe ndiyo inakuja Rombo. Nikaahidiwa kwamba itajengwa *transmission line*. Mheshimiwa Waziri, sikusikia kwenye hotuba yako. Naomba sana uwape matumaini watu wa Rombo kwa sababu kwa mfano eneo la Tarakea tuna viwanda vingi sana vya mbao. Watu wanachukua *order* za mbao, wanashindwa kutimiza ahadi zao, wanaingia hasara kubwa. Pale Rombo Mjini kuna mjasiriamali mmoja, Bwana Shanaeli Ngowi, ameanzisha kiwanda kwa ajili ya *juice* na maji na hivi ni viwanda muhimu kwa sababu vinasadia kujenga ajira vijijini, lakini umeme umekuwa ni tatizo. Nawaomba sana, mtakapofanya majumuisho, Mheshimiwa Waziri nakuamini, Manaibu wako ni vijana wachapakazi, hebu tupeni wananchi wa Rombo matumaini ya kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ambayo yameomba umeme miaka mingi hayapati, tena wametapeliwa. Nitatoa mfano kuna Kata moja inaitwa Ubetukahe, kijiji cha Ngaseni, kijiji cha Ubetu, kijiji cha Kahe, wameomba umeme na wamelipia na

wamelipishwa miaka mingi. Nimeshaleta barua Wizarani, nimeshapeleka barua kwa Meneja pale Rombo kwamba watu hawa wametapeliwa, mpaka leo umeme haujaingia. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri tusaidieni. Tuna matatizo ya *transformer* wafanyabiashara kwa mfano pale Tarakea Kikelelwa, wanaomba miaka nenda rudi, tunaomba mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwashauri, jamani tunapiga kelele kuhusu nguzo hizi. Mimi nakaa pale Holili, nguzo ambazo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwanza kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Karagwe lakini pia kwa niaba ya Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumpongeza mtani wangu Mheshimiwa Profesa Muhongo, Naibu wake Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Masele na Katibu Mkuu wa Wizara, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Nawapongeza, nasema mkalie kiti vizuri kwa matako yote mawili, yaenee vizuri, msiwe na wasiwasi, sisi tunawaunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kipekee sana, kumshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Umeme Vijiji, Ndugu yangu Mwakayesa, kwa kazi nzuri anayoifanya kusambaza umeme vijijini pamoja na bajeti ndogo. Pia nishukuru sana utafiti wa gesi unaoendelea unaongozwa na Bodi ya *TPDC,* nawapongeza sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii, kutoa dukuduku langu kwamba kuna utafiti wa madini ya urani unafanyika kule Namtumbo, Mkoa wa Ruvuma lakini nasikia kuna wizi unajitokeza kwamba kuna madini ya urani yanavushwa kutoka Namtumbo kuelekea Nairobi na pia kuelekea nje ya nchi yetu. Nasema ni tetesi, kwa hiyo, naomba Serikali ifanyie kazi tetesi hizi ili ione kama ni kweli ama si kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa sita nilibahatika kutembelea Bunge la Senate la Canada na nilizungumza na baadhi ya Masenata kuhusiana na mrahaba mdogo unaotolewa na Kampuni ya Madini ya Barrick na nilikuwa najaribu kujenga hoja kwamba kwa nini Barrick hatupi mrahaba wa asilimia 50 kwa 50 na badala yake tunapata mrahaba wa asilimia tatu? Maseneta wote walinishangaa, kwanza walisikitishwa sana kusikia taarifa hizo kwamba ni kwa nini mlitengeneza mkataba mdogo kiasi hicho. Kwa hiyo, pengine nimwombe Profesa Muhongo na timu yake waangalie uwezekano wa kufanya majadiliano makubwa sana na Barrick na wachimbaji wengine ku-*review* ile mikataba kwa sababu imetupunja kiasi cha kutosha mpaka na nchi zao zinatushangaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa sana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri na hasa katika ukurasa wa 86 pamoja na 87. Pamoja na kwamba hotuba nzima imejaa mambo mazuri sana lakini kwa kweli ukurasa huu mimi ndiyo umenivutia zaidi na ukurasa huu unazungumzia kuendeleza usambazaji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya na Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya hizi, sisi Karagwe tumepata Wilaya mpya ya Kyerwa, kwa mwenzangu Mheshimiwa Katagira hawana umeme lakini nimeona mkakati wa kupeleka umeme katika Wilaya hii ya Kyerwa pamoja na vijiji vyake, napongeza sana na naomba mkakati huu uendelezwe na ufanyike haraka. Sambamba na hili, mimi niipongeze Serikali imeamua kupeleka umeme vijijini kwa sababu kwa Wilaya au Jimbo ambalo lipo pembezoni kabisa, mpakani mwa nchi yetu, ukiona nguzo ya umeme ikianza kufika huko ni jambo la kumshukuru Mungu. Nawashukuru sana *REA* wamefanya kazi nzuri, kuna mradi mzuri wa umeme unaotoka kijiji cha Bisheshe kwenda Nyaishozi, kwenda Ihembe mpaka Hembetua ambako mimi ndiyo natokea. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishasema hapa kwamba mradi huu umekwepa baadhi ya vijiji, kuna kijiji maarufu cha Urusimbi kwa Mchungaji Aligawesa, kimesahaulika. Vingine ni kijiji cha Rukale, Misha, Kibogoizi, Ruhita, Rubale na vinginevyo katika ukanda huu wa Nyaishozi. Kwa hiyo, naomba vijiji hivi navyo viangaliwe, vipewe umeme. Mheshimiwa Rais wetu amekuwa akitoa ahadi mbalimbali hasa wakati ule wa

kampeni. Alipokuja kwenye Jimbo langu la Karagwe katika Mji mdogo wa Nyakaiga, alitoa ahadi ya kupeleka umeme katika vijiji vyote vya Tarafa ya Nyabionza na ninaimani kabisa Profesa Muhongo, Katibu wake na timu yake na Wakala wetu wa Umeme Vijijini, kazi hii wataifanya na nimekuwa nikipata ahadi kwa sababu mimi kazi yangu ni kufuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda kusema kwamba Jimbo la Karagwe, ni kati ya Majimbo ambayo yapo mpakani kabisa na pembezoni mwa nchi yetu, linapakana na Uganda na Rwanda. Kwa hiyo, ni Jimbo ambalo linahitaji kuangaliwa kwa jicho la huruma sana na Jimbo la Karagwe limepata misukosuko mingi sana. Idd Amin alipigana vita huko, wakimbizi wanaendelea kutuvamia, tulipata tatizo la ugonjwa wa UKIMWI ulianzia huko, meli yetu MV Victoria ikazama na wananchi wetu ambao wangeweza kuendeleza Wilaya yetu hiyo. Kwa maana hiyo, ni Jimbo ambalo kwa kweli linahitaji kuangaliwa kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijiji ambavyo viko pembezoni mwa Uganda na Tanzania, vinashuhudia wenzao wa Uganda wanapata umeme sisi kwetu upande mwingine ni giza. Kwa mfano, tuna vijiji ambavyo viko mpakani kama kijiji cha Chamchuzi, kiko mpakani mwa Tanzania na Rwanda, kijiji cha Kayo, Kanyomagana, Kamagambo, Bukangara, Kijumbura, Kafunjo na vinginevyo. Kwa hiyo, nashauri na kumwomba Mheshimiwa Waziri, mimi kazi yangu hapa ni kuja kuomba umeme kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Karagwe na ndiyo kazi waliyonituma.

Utakuwa umetutendea haki wananchi wa Karagwe kama vijiji vyetu hivi vitafanikiwa kupata umeme ikiwa ni pamoja na vijiji vya Kanoni, Kigarama Chini, Kigarama Juu, vijiji vya Ruhwanya, Chanika, Kituntu na sehemu zingine. Nimeona niviseme hivi vijiji kwa sababu ndiyo kazi ambayo watu wa Karagwe walinituma nifanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama nilivyosema, naendelea kuwashukuru sana Wakala wa Umeme Vijijini, wanafanya kazi nzuri. Tatizo ni moja tu, hawana fedha za kutosha. Mimi naomba Serikali ifanye linalowezekana Wakala wa Umeme Vijijini apate fedha ya kutosha kwa sababu wameonyesha nia ya kupeleka umeme vijijini isipokuwa wanapungukiwa na fedha. Mimi natamani ninapomaliza kipindi changu cha Ubunge 2015 basi angalau Jimbo langu asilimia 95 liwe linawaka umeme tu yaani umeme uende Kibwera, Mshabaiguru, Rugera na sehemu zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nilitaka nizungumze hayo kuhusiana na Jimbo langu, nakushukuru, nitafurahi Mheshimiwa Waziri wakati ana-*wind up* akinijibu kwamba anapeleka umeme sehemu zote nilizozitaja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nipate fursa ya kutoa maoni yangu kuhusu hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya, uzima salama na kuniwezesha kufunga Swaumu hii ya Ramadhan lakini niwapongeze na kuwatakia kila la kheri Waislam wote ambao wanafunga katika mfungo huu mwezi wa Ramadhan, *inshallah,* Mungu awajalie wafunge salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri pamoja na Manaibu wake, Katibu Mkuu wake na wote wale ambao wamesaidia katika kuipamba hotuba hii ambayo imewasilishwa kwetu na kama unavyoona wewe mwenyewe, imezua mjadala mzuri na watu wengi wanaifurahia. Mheshimiwa Waziri ameanza vizuri na yale matumaini yaliyowekwa kwake na Mheshimiwa Rais wetu, ninahakika sasa anadhirisha kwa matendo. Naomba nimwombee kila la kheri ili aendelee kutimiza azma ya kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau, uniruhusu niwapongeze sana *Dar es Salaam Young African* kwa kazi nzuri waliyoifanya jana ya kuiokoa nchi na kuhakikisha kwamba nchi inabaki na kikombe cha Kagame. Kama wasingeshinda jana, tusingekuwa na uhakika kwamba Tanzania kama Tanzana tunapata kikombe cha Kagame lakini sasa tunapata kikombe, Yanga wapo, Azam wapo. Kwa hiyo, nawapongeza sana Yanga kwa mafanikio hayo lakini kwa kuisaidia nchi na naomba wasituangushe siku ya fainali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuwapongeza sana *REA*. Mwaka 2005 sisi ambao tulikuwepo wakati ule tulipokuwa tunapitisha Sheria hii ya *REA* maneno yalikuwa mengi sana lakini kubwa zaidi, matazamio ya wananchi na hasa sisi Wabunge kwa *REA* yalikuwa makubwa sana na kwa muda mfupi walioanza kufanya kazi, nafikiri mwaka 2008 ndiyo wameanza kufanya kazi mpaka sasa wamefanya kazi nzuri sana. Naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Dkt. Mwakahesya na wenzake wote wanaomsaidia kwa kazi nzuri ambayo wameonyesha kuifanya hadi sasa ya kutupatia umeme. Nalazimika kumpongeza zaidi kwa sababu mimi nilikuwa na tatizo la umeme wa Sepuka kwa miaka mingi sana lakini sasa ninavyosema *REA* wameshamteua mkandarasi, nguvu zimeshapelekwa kwenye *site* kule Sepuka na wakati wowote kuanzia sasa wananchi wa Sepuka ambao wamehangaika karibu miaka mingi sasa wanapata umeme. Pongezi sana kwa Mheshimiwa Waziri lakini pongezi sana kwa Dkt. Mwakahesya pamoja na wenzake kwa kuhakikisha kwamba Sepuka tunapata umeme. Naomba uwasimamie wale makandarasi ili kusudi umeme upatikane katika muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *REA* wangefanya vizuri zaidi kama tungewawezesha, ni bahati mbaya sana tunataka wafanye vizuri zaidi, watupelekee umeme vijijini lakini kwa kweli fedha wanayopata kwa ajili ya kazi hiyo ni ndogo sana. Mimi nashauri kwamba maadam sasa tumeamua kupeleka umeme vijijini na maadam tumeanzisha Wakala huu wa *REA*, hebu basi tutafsiri hiyo nia yetu nzuri kwa vitendo kwa kuhakikisha kwamba *REA* wanapata fedha ya kutosha ili waweze

kufanya kazi hiyo. Namwamini sana Dkt. Mwakahesya na wenzake, sina wasiwasi nao, fedha yoyote itakayopelekwa kule itatumika vizuri, wala hakuna haja ya kuwa na wasiwasi. Kwa hiyo, niombe tuwaongezee fedha ndugu zetu wa *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile Sheria ya *REA* ya mwaka 2005 inasema tozo iwe asilimia tano lakini ni bahati mbaya kwamba toka wakati wameanza mpaka sasa, tozo inayotolewa kwa *REA* ni asilimia tatu, kwa hiyo hata kile kiwango ambacho kimewekwa kwa mujibu wa Sheria ya REA hakijafikiwa. Kwa hiyo, mahali pa kuanzia kuwasaidia *REA* ni kutekeleza Sheria ambayo tayari ipo ya kutaka wapewe asilimia tano na sio asilimia tatu. Kwa hiyo, naomba nishauri kwamba Serikali ifike mahali itekeleze Sheria ambayo tumeitunga kwenye Bunge hili la kuwapa *REA* tozo ya asilimia tano badala ya asilimia tatu. Hiyo itakuwa njia mojawapo ya kuwaongezea *REA* mfuko wao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, tulizungumza hapa mwaka juzi, mwaka jana kwamba tuangalie uwezekano wa kuwapa pesa kupitia ile habari ya mafuta, baada ya uchakachuaji wa mafuta ya taa lakini vilevile tulizungumzia uwezekano wa kuwapa pesa kupitia kampuni hizi za simu. Mawazo yalikuwa mazuri na mimi nilifikiri Serikali inaenda kutekeleza hayo. Sasa sijui kigugumizi gani kimetokea mpaka sasa mawazo hayo hayajatekelezwa? Tukiwapa *REA* asilimia tano, tukawapa *REA* mchango wa fedha kutoka kwenye makampuni ya simu na ile nyingine ambayo ilikuwa inatokana na mauzo ya mafuta ya taa, mimi

ninahakika kwamba wenzetu hawa wataweza kufanya kazi vizuri. Kwa hiyo, nashauri Serikali iwape wenzetu hawa fedha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri alitamka suala ambalo mimi lilikuwa linanipa taabu, la gharama za kuunganisha umeme kule vijiji. Sasa nafurahi kwenye ukurasa wa 89 ameeleza kwamba gharama kwa vijijini zimepunguzwa ingawa kwa mjini ziko juu, *tariff* ya vijiji iko tofauti na *tariff* ya mijini. Lakini nina tatizo kidogo katika ukurasa wa 89, kwa yale yaliyoandikwa pale, imeandikwa shilingi 337,740/- kwa ajili ya vijijini lakini yeye kwa kauli yake aliyoitoa hapa Bungeni ni shilingi 170,000 au 130,000 na kitu. Naomba Mheshimiwa Profesa atakapokuwa ana-*windup* hoja yake, arekebishe hiyo kwamba tuchukue kauli yake aliyoitoa hapa Bungeni kwamba sasa ni shilingi 170,000 au 130,000/- na sio hiyo shilingi 337,740/- kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 89.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yanayosemwa kuhusu *TANESCO*, mimi kwanza nilikuwa na tatizo na uongozi wa *TANESCO* hata kabla hayajatokea kwa sababu ni aibu Shirika kama la *TANESCO* linakaa bila mita za kuunganisha umeme, zaidi ya miezi sita hakuna mita! Wananchi wanalipa lakini wanaambiwa mita hakuna, inakuwaje kitu kama mita ambalo ni jambo muhimu kwa upande wa *TANESCO* hazipatikani na wananchi wanalipa lakini hawapati umeme wakati yupo Mkurugenzi Mkuu, yupo Mkurugenzi wa Ugavi na Ununuzi yaani Wakurugenzi na kila kitu wote wapo lakini *item* kama mita ambayo mimi ninadhani ni *stock*

*item* haipo. Sasa anapokuja mtu na kutaka kusafisha ule uongozi wa *TANESCO,* naweza hata kumchinjia mbuzi akala kwa kazi nzuri ambayo anafanya kwa sababu kama wameshindwa kuweka mita wataweza vipi kufanya mambo mengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, naomba *REA* wapewe pesa ili kusudi tupate umeme zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushuru Mheshimiwa Missanga na muda mwingi ulikuwa unashangilia Yanga. Ninamwita Mheshimiwa Vicky Kamata na pia ajiandae Mheshimiwa Amar.

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mungu kwa kunijalia afya njema hata nimeweza kusimama na mimi nichangie kama walivyofanya wenzangu. Ninawashukuru wananchi wa Geita hususani akina mama wenzangu wa UWT kwa kunichagua na mimi ninawaahidi kuwa sitawaangusha, nitafanya kazi kwa uwezo wangu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kumpongeza Waziri Muhongo kwa uwezo mkubwa aliouonyesha na kwa juhudi kubwa anazozifanya. Napenda kuwapongeza Manaibu wote wawili, kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Masele, Rais Jakaya Kikwete hakukosea kabisa

kuwapa nafasi hizi, wameonyesha uwezo wa hali ya juu na sisi tuko pamoja na ninyi, tunawaunga mkono sana. Napenda sana pia kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kwa uzalendo wake, kwa nguvu zake anazoonyesha na jinsi anavyowathamini Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuleta salamu nilizotumwa na wachimbaji wadogo wa Geita, wamesema wanakushukuru sana Mheshimiwa Muhongo, Manaibu wako na Katibu Mkuu kwa kuwaita na kukaa nao, mkawasikiliza shida zao, kero zao na mkawaahidi jinsi gani mtashirikiana nao kuwasaidia. Walichosisitiza, mara bajeti hii itakapopita basi mfanye haraka kufanya yale ambayo mmekubaliana nao ili waweze kufanya shughuli zao vizuri, waweze kujikwamua kimaisha na waweze kuipenda zaidi Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuipongeza tena Wizara hii ya Nishati na Madini, kwa juhudi kubwa inazozifanya. Kwa kweli naona kama nimefilisiliwa maneno na Mheshimiwa Selasini, nimefilisiwa maneno na Mheshimiwa Mama Kilango na Wabunge wenzangu waliotangulia, wameongea mengi sana ya msingi. Mimi labda nikazie tu na niwatie moyo sana Mawaziri hawa nikianza na Mheshimiwa Profesa Muhongo, Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Masele na Katibu Mkuu. Niwaambie hivi, fanyeni kazi, msimwogope mtu yeyote. Watanzania wana imani kubwa nanyi, mmeonyesha njia, mnaondoa uovu, ninawakubali, nawaunga mkono mimi na wananchi wote wa Geita na Wabunge kwa asilimia tisini na kitu

wanawaunga mkono, msiogope. Nasema, Mungu akiwa upande wenu, ni nani atakayekuwa juu yenu? Hakuna kabisa! *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fanyeni kazi kwa kujiamini, Watanzania kumbe tumeonewa, tumekandamizwa na tumeumizwa na mafisadi ambao baadhi ya Wabunge wenzetu wanawatetea, ninasikitika sana. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshtuka sana na siyo peke yangu, tumeshtuka watu wengi kuona kwamba kumbe siku zote tunaingia kwenye mgao feki, mgao wa kutengeneza...

**MBUNGE FULANI:** Giza la kutengeneza!

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Yaani giza la kutengenezwa! Kwa kweli, nashindwa hata niseme nini? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Semaa!

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Hawa watu wanajua kuwa kwa kukosa umeme siku moja tu tunapoteza bilioni ngapi? Kumbe wenzetu wanaamua tu kwamba leo tukae, tukate umeme, tutengeneze shilingi bilioni tatu sisi *management* ya *TANESCO* tugawane, Bodi tugawane, tule kuku, tutanue hapa mjini, haya Matanzania majinga yaendelee kupayuka, wananchi waendelee kuichukia Serikali yao, kumbe ni hujuma! Nimesikitika sana na imeniuma sana na nashangaa

sana kuona baadhi ya Wabunge wanawa-*support* watu hawa eti wameonewa. *(Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Hawafai!

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anasimama kwa ujasiri kabisa anasema *TANESCO* inaonewa jamani, wanabana na sauti, kweli! Aah jamani, hebu tuache, tumwogope Mungu basi. *(Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Waambie, waambie! Wataje majina!

**MBUNGE FULANI:** Zitto!

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika sana, naomba Watanzania wenzangu tusiichukie Serikali yetu ambayo inatupenda, isipokuwa kuna watu wachache wanatugombanisha na Serikali yetu wanakata umeme, tunapata hasira na tunaona kwamba hatuzalishi, saluni zinafungwa, wenye mashine za kusaga wanashindwa kufanya kazi, wanatujengea hasira na chuki kwa Serikali yetu ambayo inatupenda sana, kumbe ni watu wachache wanatengeneza pesa jamani*. (Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Taja majina wewe!

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina sababu ya kutaja majina, wanajulikana, lakini kikubwa zaidi niwaombe, Watanzania sasa wameujua ukweli kumbe mgao unapotokea ni dili la watu binafsi.

Kwa hiyo, sisi tutasimama kidete, tutapigana, tutapambana, tutawatetea wale ambao wanaokoa hela ya Watanzania, tutawatetea wale wote ambao wanajali maslahi ya Watanzania ambao hawajali maslahi yao binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza kuona mtu anashikilia kwa kusema Sheria ya Manunuzi imekiukwa, imekiukwa kwa jambo jema! Kwa nini usiwapongeze watu kama hawa? Mbona watu wanapokiuka sheria kwa kufanya mambo maovu hamsemi? Kwanza hawajakiuka, wamefuata utaratibu. Wameokoa shilingi bilioni tatu (3) kwa wiki mbili sasa tunaokoa bilioni, ina maana kwa mwezi tunaokoa shilingi bilioni (6), Mheshimiwa Selasini kaongea vizuri sana hapa na mimi sina sababu ya kurudia kuongelea hizi shilingi bilioni sita (6) kwa mwezi zitasaidia mambo mangapi. Leo hii mtu anasimama kabisa mpaka mishipa ya shingo inamtoka anasema wamekosea, hawa watu washindwe na kulegea kwa jina la Yesu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Taja majina wewe! *(Kicheko)*

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona nimeshafilisika maneno lakini nachoomba, kwa kuwa tumeshaijua *TANESCO*, tumeshajua hila za hawa watu, naomba mara baada ya bajeti hii kupita, *management* ya *TANESCO* ifumuliwe kabisa, Bodi ipanguliwe, tunataka watu watakaokuwa na uzalendo, watakaokuwa na mapenzi na nchi hii, watakaokuwa na mapenzi ya dhati na Watanzania wanaoteseka, watakaoshirikiana vizuri na Wizara kwa maana ya Mheshimiwa Muhongo, Manaibu wake na Katibu

Mkuu, watakaofanya kazi itakayoweza kuleta tija, tumechoka kuonewa, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi/Vigelegele)*

**MHE. NASSOR H. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu. Pia napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya ya kuweza kusimama tena ndani ya Bunge hili Tukufu ili kuweza kutetea na kuwapigania Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu leo ni machache. La kwanza, naipongeza sana Wizara hii kwa mikakati yake ya kuweza kuboresha na kuweza kujenga bomba la gesi ili kuweza kupunguza tatizo la umeme. Mheshimiwa Waziri Profesa Muhongo nakupongeza sana kwa ujasiri wako pamoja na Manaibu wako, kwa kweli kazeni buti na msiogope, tuko nyuma yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie Jimbo la Nyang'hwale. Jimbo la Nyag'hwale tumeahidiwa umeme muda mrefu sana tangu mwaka 1998 mpaka leo hii umeme huu haujawaka. Ahadi hizi zimekuwa ni za muda mrefu tena zikiwa zinatolewa na viongozi wa ngazi za juu. Kwa kweli tuwe na aibu kwa ahadi ambazo zinatolewa na hazitekelezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri amefanya ziara hivi karibuni kwenye Jimbo langu, tumezunguka naye, ninampongeza sana kwa ujasiri wake kwa sababu alizungumza maneno mazito na kuwaahidi wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale kwamba umeme sasa utawashwa na kwa kweli

wanategemea ahadi yake hiyo kutekelezwa. Mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri tuliweza kuzunguka na kuona zile nguzo ambazo zimesambazwa maeneo mengi katika Jimbo la Nyang'hwale takribani leo miezi minane hakuna ambacho kinaendelea mpaka sasa. Lakini alivyoona na tukafanya mkutano wa hadhara, akawaambia wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale kwamba sasa umeme utawashwa na ahadi hii ninaahidi mimi mbele yenu na mimi ndiye nitakayekuja kuzindua mradi huu wa umeme. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakukumbusha ahadi yako ambayo uliahidi katika Jimbo la Nyag'hwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nataka nizungumzie suala ambalo nilizungumzia mwaka jana kuhusu uchimbaji ambao unafanywa na Kahama *Minning* au Bulya'hulu *Gold Minning.* Uchimbaji huu umeleta madhara makubwa sana katika Jimbo la Nyang'hwale. Serikali na Mgodi huu kwa nini hauangalii madhara ambayo yamepatikana katika Jimbo letu na kutafuta ufumbuzi? Hivi karibuni, kuna mlipuko ambao umelipuliwa, ardhi imeweza kupasuka na kuna baadhi ya nyumba zimepasuka. Tarehe 24, saa kumi na mbili asubuhi, mlipuko mwingine ulijitokeza, umeweza kupasua nyumba, madarasa matano na zahanati ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri amekuja kuweka jiwe la msingi tarehe 6/7. Nyumba hizo zimefikia kwenye linta na baruti hizo zimelipuliwa majuzi tarehe 24 na nyumba hizo tayari zimepasuka. Je, Serikali ina mpango gani kuweza kulipa fidia na kuangalia madhara makubwa ambayo yanaweza kuja kujitokeza hapo baadaye? Kwa nini milipuko hii inapofanywa, ardhi na majumba yanapasuka?

Tunaiomba Serikali na Wizara hii iweze kuangalia kwa makini sana, inawezekana hapo baadaye Jimbo la Nyang'hwale likazama. Kwa nini mipasuko inapotokea, inatokea mpaka juu ya ardhi? Naomba Wizara yako Mheshimiwa Muhongo, jaribuni kulifuatilia kwa makini, ikiwezekana maeneo yale wananchi wapewe fidia na kuhamishwa ili wasiwe na maisha ya hofu. Leo wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale hususani kijiji cha Ihenze, Nyamikonze, Mwasabuka na Stamico wanaishi kwa wasiwasi, kila mlipuko unapolipuka, ardhi inachanika. Hebu wahurumieni wananchi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sitakuwa na michango mingi, mambo yangu yalikuwa ni mawili kwamba Wizara hii itekeleze ahadi ambayo tumeahidiwa wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale kuwashiwa umeme na la pili, Wizara hii iangalie kwa makini milipuko inayolipuliwa na *Bulyanghulu Gold Mining* kwa kuwa inaharibu mazingira, nyumba zinapasuka na kuhatarisha maisha ya wananchi na kuwafanya waishi kwa wasiwasi. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anipe majibu yaliyo sahihi kwa ajili ya waanchi wa Jimbo langu la Nyang'hwale. Ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichuke nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kabisa, nimshukuru Waziri wa Nishati na Madini kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika Wizara hii. Vilevile

niwashukuru Manaibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara muhimu sana kwa ajili ya maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kushukuru kwa umeme hasa katika Jimbo la Busanda ambapo tayari wamekwishaweka nguzo katika kijiji cha Bukoli, Nyarugusu, Katoro, Rwamgasa, Bukondo, Chigunga na Chikobe. Kwa kweli hatua hii imewatia moyo wananchi wa Jimbo la Busanda pamoja na Geita kwa ujumla na wanasema kuwa wamebahatika kwa sababu wanapata umeme wa gridi ya Taifa. Nachoomba wakati wa majumuisho wananchi wasikie kuwa ni lini sasa umeme huu unawaka? Kwa sababu tayari nguzo tumeziona na nyaya zimewekwa lakini tunahitaji kusikia kwamba ni lini umeme unawaka ili wananchi waweze kujiandaa kwa ajili ya uwekezaji. Napenda niombe kuwa wakati wanapowasha umeme, tuhakikishe umeme huu katika sekta muhimu kama vituo vya afya na shule za sekondari zinapata meme huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala la madini. Mara nyingi suala la madini ni suala muhimu sana katika Wilaya ya Geita na Jimbo langu la Busanda. Wananchi wa Geita wanategemea shughuli za uchimbaji wa madini. Kwa siku ya leo, wananchi wa Geita wako makini kabisa kusikiliza bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini inasema nini kuhusu wachimbaji wadogo wa madini. Nimesoma katika kitabu hiki cha bajeti, nimeona jinsi ambavyo Serikali itaanzisha Kituo cha Uwekezaji cha Wachimbaji Wadogowadogo, Rwamgasa. Naishukuru sana Serikali lakini niombe suala

hili lisiwe tu kwenye maandishi liwe katika utekelezaji maana toka bajeti ya mwaka jana suala hili lilizungumziwa lakini utekelezaji wake sijauona. Niiombe Serikali mwaka huu watekeleze suala hili, kianzishwe hicho kituo cha Rwamgasa na wananchi wa Rwamgasa pamoja na Geita kwa ujumla wanategemea kituo hiki ili waweze kufanya kazi zao vizuri haswa wale wachimbaji wadogowadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, niiombe Serikali kwa wale wananchi ambao hawajapata maeneo ya uchimbaji wa madini hasa wananchi wa Nyarugusu, ni kilio kikubwa na cha muda mrefu na Mheshimiwa Naibu Waziri alipotembelea katika ziara yake ya hivi karibuni, alisikiliza kilio cha wananchi hawa katika mkutano pale Nyarugusu, Mheshimiwa Waziri alinipa taarifa kuwa walieleza kero zao. Naomba sasa kero hizi Wiziara izifanyie kazi ili wananchi hawa wapate maeneo ya uchimbaji hasa wale wa Nyarugusu hawana maeneo ya kuchimba, wale wachimbaji wa Nyaruyeye nao wapewe maeneo ya uchimbaji na Buziba, Bingarifu na *Tembo Minning* na Kaseme pia wapate maeneo ya uchimbaji madini. Maeneo mengi ni ya *STAMICO*, maeneo mengi yamechukuliwa na wawekezaji wakubwa, nimeona tamko katika hotuba kuwa kwa wale ambao hawajaendeleza maeneo yao watanyang’anywa na Serikali. Naomba niombe rasmi kuwa maeneo haya wapatiwe wachimbaji wadogo ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na kuweza kujipatia uchumi wao hasa kwa kuwa wanategemea shughuli za uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi sana ya kusema lakini niiombe Serikali kuwa huu mpango wa kuwakopesha wachimbaji wadogowadogo na kuwapa mitaji. Katika bajeti nimeona jinsi ambavyo Serikali imetoa shilingi bilioni 1.19 ambapo wamepewa wananchi wa Geita – Rwamgasa. Nimejiuliza sana katika kipengele hiki kwa sababu sijaona watu waliopata! Niombe sasa Serikali iniambie ni akina nani wamepata hizi fedha kwa sababu mara nyingi wanalalamika kuwa hawapati hizi fedha. Wakati wa kufanya majumuisho mnieleze ni wachimbaji gani hawa ambao wamepata fursa ya kupata mikopo hii kwa kiasi kikubwa namna hii? Naomba Serikali iongeze mikopo kwa wachimbaji wadogo ili waendelee kunufaika na shughuli zao za uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naishukuru sana Serikali na naomba iendelee kuwahudumia wananchi hawa, hasa kwa maeneo niliyoyataja, iwape maeneo ya uchimbaji wa madini, lakini vilevile iwawezeshe kimtaji ili waweze kufanya kazi zao vizuri na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGWALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kunifikisha kwenye mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na nitumie fursa hii kuwapongeza na

kuwatakia Ramadhani Karim Waislam wote walio katika Mfungo Mtukufu wa Mwezi wa Ramadhani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuweka kumbukumbu sahihi kwamba leo hii mimi ninafanya tukio la kihistoria, kwa mara ya kwanza katika Bunge lako Tukufu nasimama na ninaunga mkono hoja ya Wizara ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninaunga mkono hoja na ninazo sababu za msingi. Sababu ya kwanza ni uteuzi wa viongozi mahiri uliofanywa na Rais Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na sababu ya pili, ni mafanikio ambayo wameyapata katika kipindi kifupi walichokuwepo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nitende haki na nionekane najenga hoja vizuri, naomba niseme mambo machache ambayo ni mafanikio yaliyojitokeza kwa uwepo wa viongozi hao wateule katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ni kupatanisha na kuwezesha makampuni makubwa yanayochimba dhahabu katika nchi yetu kuanza kulipa mrabaha kwa kiwango kipya kilichopitishwa kwenye Sheria mpya ya mwaka 2010. Sheria ya zamani ilikuwa inawataka walipe mrabaha wa asilimia tatu kwenye *net profit* lakini Sheria mpya inawataka walipe asilimia nne kwenye *gross*. Viongozi hawa wapya wamewezesha hilo kufanyika na mimi naona ni sababu kubwa ya mimi kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili ni kutulia kwa umeme, sasa hivi umeme unawaka muda wote hakuna mgawo na hii mimi naona ni sababu ya kuunga mkono hoja ya Wizara ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya tatu na hii inawahusu ndugu zangu Wananzega, ni mafanikio tuliyoyapata juzi kwa kukaa kikao cha pamoja na watu wa Mgodi wa *Resolute* chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Waziri lakini zaidi na kwa nafasi ya kipekee Naibu Waziri Stephen Masele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge hili, kama kuna jambo moja ambalo nimeliongea kwa muda mrefu na kwa hasira katika Bunge hili, basi ni suala la haki ambazo watu wa Nzega tunastahili kuzipata kutokana na uwepo wa mgodi wa uchimbaji wa dhahabu wa *Golden Pride Project*. Siku nyingi nimekuwa nikitaka tukae mezani na watu wa *Resolute* tuzungumze, ili tuweze kupata mafanikio yanayotokana na mgodi ule sisi kama Wananzega, lakini pia watu ambao walinyang'anywa ardhi yao wakati mgodi ule unaingia, wapewe fidia ya mali iliyoharibiwa na uwepo wa ule mgodi. Kilio changu kimefikia mahali pazuri na juzi tumekaa chini na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya *Resolute* na tumekubaliana mambo kadhaa ambayo nadhani Wananzega watayafurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitambue ushirikiano tulioufanya kwa pamoja mimi na Mbunge

mwenzangu Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Jimbo la Bukene, lakini pia Mwenyekiti wa Halmashauri, Mheshimiwa Patrick Gululi Mbozu pamoja na Madiwani wengine wote ambao waliambatana naye kwenye msafara ambao ulipelekea sisi kukaa juzi pale Wizara ya Nishati na Madini na kuamua na hatimaye kufikia makubaliano kwamba ushuru wa huduma (*service levy)* wa asilimia 0.3 ni haki ya msingi ya Halmashauri ya Wilaya ya Nzega na pengine sasa tuwa-*issue Demand Note* ili waweze kutulipa fedha hizo ambazo zita-*amount* kufikia takribani shilingi bilioni nane, pesa ambayo itakwenda kwenye Halmashauri yetu, pesa ambayo imekosekana kupatikana kwa kipindi kisichopungua miaka kumi na tatu, leo hii tumefikia mafanikio ya kuzipata. Naomba niwaunge mkono watu hawa kwenye Wizara hii kwa sababu wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda si rafiki sana, naomba nipendekeze yafuatayo; kwamba Ndugu yangu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Shinyanga Stephen Masele, nakuomba sana usimamie kuhakikisha kwamba watu wa *Resolute* wana-*deliver to their promises*. Uhakikishe kwamba watu wa *Resolute* wanaleta hizo pesa kwenye Halmashauri yetu kama tulivyokubaliana na kama wakikiuka makubaliano hayo, ninakuomba sana wewe na wakubwa wako katika Wizara hiyo, uhakikishe hawapati kibali cha kusafirisha dhahabu kupeleka nje ya nchi mpaka watakapotulipa. Kama wasipotulipa hizo pesa, uhakikishe hawaendi kuwekeza kwenye mradi mpya wa Nyakafuru ambapo wanatarajia kuhamisha mitambo Nzega kuipeleka

huko kwa ajili ya kuendelea kuchimba dhahabu. Nakuomba sana uhakikishe watu hawa wanatupa hizo fedha ili makubaliano hayo yawe na maana kwa watu wa Nzega na Watanzania kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha sisi kupata asilimia 0.3 ya *turn over* ya mgodi wa *Resolute,* ni kitendo cha kihistoria kwa sababu tutakuwa ni Halmashauri ya kwanza katika nchi yetu kupata ushuru wa huduma kutokana na machimbo ya dhahabu katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa hoja hii imekuwepo katika Bunge hili kwa zaidi ya miaka kumi na tano toka migodi imeanza kuingia katika nchi yetu. Leo hii kwa uongozi mahiri wa Profesa Muhongo na Manaibu wake Mheshimiwa Stephen Masele na Mheshimiwa George Simbachawene, watu wa Nzega tunaelekea kupata asilimia 0.3 ya ushuru wa huduma katika Halmashauri yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini ni rasilimali iliyopo ardhini na kwa bahati mbaya sana kama rasilimali zingine zilivyo, madini ni *depletable type of resources*, ni rasilimali ambazo zinakwisha, hazioti, zikiisha zimeisha. Basi ni muhimu sasa Watanzania tukafaidika na rasilimali hizi ili tuweze kukuza uchumi wetu lakini pia tuweze kutoa huduma kutokana na pesa inayopatikana kwenye rasilimali hii ambayo ni urithi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu wakati *Resolute* wanaingia katika nchi yetu kuanza

kuchimba dhahabu waliwekeza fedha za Kitanzania zipatazo shilingi bilioni hamsini na nane tu, lakini leo hii tunavyoongea hapa watu wa *Resolute* wameweza kuvuna dhahabu zaidi ya *ounce* milioni moja na laki tisa ambazo ukizitafsiri kwa fedha zinafikisha jumla ya shilingi trilioni 1.8 karibu shilingi trilioni mbili lakini toka waingie mpaka leo hii kodi tuliyoipata, ukijumlisha na mrabaha, haizidi shilingi bilioni mia moja tu. Hivi tunavyoongea, watu hawa wanaelekea kufunga mgodi huo, hatutegemei kupata kingine chochote zaidi ya hicho, hii ni fedheha na haya ni matusi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tumeamua kuendelea kuchimba dhahabu katika nchi yetu, naomba nitoe ushauri kwa viongozi hawa mahiri waliopewa dhamana na Mheshimiwa Rais ya kusimamia sekta hii nyeti, basi watazame upya namna Tanzania inavyoingia katika kuwekeza kwenye migodi ili na sisi tuweze kufaidika na kama haiwezekani ni bora tukaacha kuendelea kuwekeza kuliko kuwekeza huku tukipata faida kidogo sana kutokana na rasilimali hii ambayo haioti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kushauri ni uwazi katika sekta ya madini.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dokta Kigwangwalla, nakushukuru sana, ni kengele ya pili.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGWALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Lugola atumalizie kipindi cha jioni.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya upendeleo ya mwisho kabisa ili na mimi niweze kutoa mchango wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wa Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, leo nina furaha kubwa na ya ajabu kwa kushuhudia toka niingie humu ndani kuwa na Bunge ambalo ni moja…

**MBUNGE FULANI:** Eeeh!

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Bunge ambalo limeamua kutotumika na mafisadi wanaotafuna nchi hii. *(Makofi/Vigelegele)*

Nami nawaambieni Wabunge wenzangu, watu wanaotaka kutumia Bunge hili kwa njia za kifisadi, wamenikumbusha miaka ya nyuma pale Dar es Salaam kulikuwa na mtu mmoja ametengeneza Mwanasesere anamwita 'Joyce Wowowo'. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasesere yule alikuwa anachezeshwa wimbo unaitwa '*mama inde, mami indii*' … *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwa anamchezesha yeye na anavyotaka ule wimbo umchezeshe Joyce Wowowo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili halitaki na hatutaweza kukubali kuchezeshwa na mafisadi kwenye ajenda zao eti kwa sababu wana pesa za kuhonga Wabunge wa Bunge hili. *(Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Waambie!

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo imedhihirika kwamba Mheshimiwa Rais alipowateua Profesa na Manaibu Mawaziri wake, Katibu Mkuu, ameteua *gate valve* ya kwenda kuziba mianya ya ufisadi ndani ya *TANESCO* na kwa mara ya kwanza sasa Bunge hili limeweza kusigina mirija yote ya mafisadi ndani ya *TANESCO*. *(Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Wengine wapo humu Bungeni!

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama inaruhusiwa nije hapo mbele nionyeshe namna tunavyosigina mirija ya mafisadi, kama inaruhusiwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposhuhudia kwa mara ya kwanza ndani ya *TANESCO*, Katibu Mkuu ambaye Wabunge walisema kwamba ni fisadi ndani ya Wizara ya Nishati na Madini gari lake linasukumwa, pale ndipo nilijua kwamba ufisadi ndani ya *TANESCO* hautaisha katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tumempata Katibu Mkuu na Waziri wake na Manaibu wamekwenda, wameziba mianya yote, ndipo tunaanza kusikia watu wanasema Kanuni na Sheria ya Manunuzi imekiukwa, walikuwa wapi wakati Watanzania tunauziwa giza, walikuwa wapi kusema Sheria ya Manunuzi inakiukwa? Kwa nini waseme kwamba Sheria ya Manunuzi imekiukwa baada ya watendaji wa *TANESCO* kusimamishwa kutokana na ufisadi wao? *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mkataba hapa na wale wote wanaosema kwamba Wizara imekiuka Sheria ya Manunuzi, wajue kuna mkataba baina ya *IPTL* na Wizara ya Nishati na Madini kwamba ni Wizara peke yake ndiyo inayoruhusiwa kuwanunulia *IPTL* mafuta au kuwapatia fedha na siyo *TANESCO*, hawajakiuka Sheria ya Manunuzi! Ndugu zangu ninao mkataba hapa, hawajakiuka Sheria ya Manunuzi, Mheshimiwa Mwenyekiti nitaomba nikupatie ili uusome vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeokoa shilingi bilioni sita kwa mwezi, imeokoa shilingi bilioni 72 kwa mwaka, Madaktari walikuwa wanagoma hawana vifaa kama *CT-SCAN* ya shilingi milioni mia sita ambapo tungeweza kutumia fedha hizi kujaza *CT-SCAN* kwenye hospitali zote, lakini leo zinachukuliwa na wajanja wachache halafu wanakuja kutaka kutumia Wabunge kwa sababu ya kubariki ufisadi wao, Bunge hili halitakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nchi gani ambayo utaruhusiwa, ni nchi gani Wabunge wenzangu, kulia, kushoto, kusini na kaskazini ambapo wewe ni Mtendaji Mkuu wa Shirika la *TANESCO* utaliendesha na mke wako kwa kumpatia tenda za zabuni? Ni nchi gani utakwenda? Ni lazima kupitia Bunge hili tabia hii tuikomeshe. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mnisikilize vizuri Waheshimiwa Wabunge, niliwahi kusema, pale DRC–Congo wanaendelea na vita na machafuko kwa sababu wanatengeneza mgogoro ili waweze kuiba madini na ili waweze kuuza silaha. Tanzania ndani ya *TANESCO,* mafisadi wanatengeneza mgogoro, wanatengeneza mgao ili watengeneze giza ili waendelee kuiba fedha za Watanzania, Bunge hili halitakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanatusikiliza, wanataka kuanzia leo kupitia kauli ya Waziri kwamba kwa kuwepo kwake pale hatutashuhudia mgawo, ni lazima kauli hii iungwe mkono na Bunge hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti na Ndugu Waheshimiwa Wabunge, kama tutagawanyika, hatutaweza kuunga mkono kauli hii na itaonekana kwamba Waziri alikuwa hasemi kweli. Naomba tuunge mkono kauli hii kwa kuhakikisha wale wote ambao Serikali sasa inawachunguza waweze kubainika, lakini hawa ambao wana mkataba ambao ni wa kifisadi wa mke wake Eva sijui Mhando na William, hao lazima

wachukuliwe hatua hata kabla ya kesho. *(Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Wawekwe ndani!

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Inakuwaje watu ambao wana mkataba unaoonekana wa kifisadi na wenyewe mnataka kuchunguza, mnataka kuchunguza nini, hamjui kwamba mke wake anaitwa Eva, nani asiyejua? Mnachunguza nini? *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wameanza kutumia Bunge kuhakikisha kwamba wanapokuja kuishi Dodoma wanadhani Wabunge tuna njaa, tutakimbilia peremende na vipesa vyao ili tuweze kuifanya Serikali, kwa kauli ambazo zimekuwa zikitolewa kwamba nchi haitatawalika maana yake nchi ikiwa giza, ndugu zangu, kutokuwa na umeme, hizo ndizo dalili za kutotawala nchi. Wote wanaosukuma hiyo kete ya kuhakikisha tunakuwa kwenye giza ili nchi isitawalike, Bunge hili halitakubali ndugu zangu. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafuteni maeneo mengine ya kwenda kuwaambia kwamba eti tutangaze Tanzania mgawo wa umeme ni janga, hatuwezi kukubali kutangaza kuwa janga wakati ni mafisadi ndiyo wanaosukuma kete hii. Nashukuru Mwenyezi Mungu mafisadi wote ndani ya *TANESCO* tunawafahamu kwa majina na tunawafahamu kwa nguo wanazovaa kila wakati na tunawafahamu kwa sura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, naomba tukubaliane mambo mawili ya mwisho, endapo itafikia hatua Wabunge tunatishana kwa sababu ya kutetea mafisadi, kizazi kitatuhukumu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lugola, nakushukuru sana, muda umekwisha.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ili tuendelee kuwa na umeme wa uhakika katika nchi hii. *(Makofi/Vigelegele)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa wachangiaji wetu wa leo. Naomba kuwataarifu wachangiaji wa kesho wajiandae panapo uhai. Mheshimiwa Moza Abedi, Mheshimiwa Magalle John Shibuda, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir na Mheshimiwa James Daudi Lembeli, wengine atakayekaa Mezani atawataja.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja, kwa niaba ya Wabunge Waislamu hapa Bungeni, Mwenyekiti wa Wabunge hawa anapenda kuwaalika Wabunge wote waliofunga na wasiofunga pamoja na Wafanyakazi wa Bunge waliofunga kuhudhuria futari ya pamoja itakayofanyika leo saa kumi na mbili na

nusu katika ukumbi wa Bunge wa *Basement*, tangazo hili vilevile linahusisha na Madereva.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hili, sina matangazo mengine, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.02 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumamosi, Tarehe 28 Julai, 2012, Saa Tatu Asubuhi)*